# RIPOTI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI

## Kuhusu Ukaguzi wa Taarifa za Fedha za Mamlaka ya Serikali za Mitaa kwa Mwaka ulioishia Juni 30, 2011

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

## OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI

Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi, Barabara ya Samora/Ohio, S.L.P. 9080, DAR ES SALAAM.
Simu ya Upepo : "Ukaguzi", Simu: 255(022)2115157/8, Nukushi: 255(022)2117527, Barua pepe: ocag@nao.go.tz, Tovuti: www.nao.go.tz

Unapojibu tafadhali taja;

Kumb. Na.CFA.27/249/01 Tarehe 28/3/2012

Mh. Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete,
Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,
Ikulu,
S.L.P. 9120,
**DAR ES SALAAM.**

**Yah: Kuwasilisha Ripoti Kuu ya Mwaka ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali Juu ya Taarifa za Fedha za Mamlaka ya Serikali za Mitaa kwa Mwaka wa Fedha ulioishia Juni 30, 2011**

Kwa mujibu wa Ibara ya 143 (4) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 (iliyorekebishwa 2005) na Kif. 48 cha Sheria ya Fedha za Mamlaka ya Serikali za Mitaa Na.9 ya mwaka 1982 (iliyorekebishwa 2000), pamoja na Kif. 34 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na.11 ya mwaka 2008, ninawasilisha Ripoti Kuu ya mwaka ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali za Mitaa kwa mwaka wa Fedha ulioishia Juni 30, 2011 kwa taarifa yako na hatua zinazopaswa kuchukuliwa.

Nawasilisha,

Ludovick S.L. Utouh
**MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI**

# Yaliyomo

Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ........................................ vii
Orodha ya Vifupisho ........................................................................................ viii
Dibaji xi
Shukrani ........................................................................................................ xiii
Muhtasari wa Mambo Muhimu katika Taarifa ya Ukaguzi ........................................ xiv vii

SURA YA KWANZA ............................................................................................ 43
1.0 Utangulizi wa Mambo ya Jumla ........................................................................ 43
1.1 Mamlaka na Umuhimu wa Ukaguzi ................................................................... 43
1.2 Viwango na taratibu zinazotumika kutoa taarifa ................................................. 45
1.3 Idadi ya Halmashauri zinazokaguliwa na mpangilio wa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ......... 47
1.4 Majukumu ya kisheria ya Mamlaka ya Serikali za mitaa katika kuandaa Taarifa za Fedha 49
1.5 Uwasilishwaji wa Taarifa za Fedha .................................................................... 50

SURA YA PILI ................................................................................................... 53
2.0 Maana, Aina, Vigezo na Mwelekeo wa Hati Za Ukaguzi ........................................ 53
2.1 Hati za Ukaguzi .............................................................................................. 53
2.2 Maana ya Hati za Ukaguzi ................................................................................ 53
2.3 Aina ya Hati za ukaguzi .................................................................................... 53
2.4 Mchanganuo wa Hati za Ukaguzi katika Halmashauri ........................................... 56
2.5 Orodha ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa zilizopata Hati zenye Mashaka na Hati Isiyoridhishana sababu Zilizopelekea kupata Hati hizo ........................................ 58

SURA YA TATU ................................................................................................. 61
3.0. Ufuatiliaji wa Utekelezaji wa Mapendekezo ya Ukaguzi kwa Miaka Iliyopita .. 61
3.1 Ufuatiliaji wa Utekelezaji wa Mapendekezo ya Ukaguzi kwa Miaka Iliyopita Katika Ripoti Ya Kuu Ya Ukaguzi ........................................................................................ 61
3.2 Ufuatiliaji wa Utekelezaji wa Mapendekezo ya Ukaguzi kwa Miaka Iliyopita Katika Ripoti Ya Kila Halmashauri ................................................................................... 67
3.3 Ufuatiliaji wa Utekelezaji wa Mapendekezo ya Ukaguzi katika Ripoti za Kaguzi Maalum 69
3.4 Ufuatiliaji wa Utekelezaji wa Mapendekezo ya Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC) ........................................................................................... 70

SURA YA NNE ................................................................................................... 73
4.0 Tathmini ya Hali ya Fedha za Halmashauri ......................................................... 73
4.1 Ukaguzi wa Bajeti ............................................................................................ 73
4.2 Mwenendo wa Mapato kutoka Vyanzo vya Ndani ya Halmashauri ikilinganishwa na Ruzuku kutoka Serikali Kuu ............................................................................... 78
4.3 Ruzuku ya Matumizi ya Kawaida Isiyotumika ........................................................ 79
4.4 Matumizi ya ziada zaidi ya ruzuku ya matumizi ya kawaida iliyotolewa .................. 79
4.5 Ruzuku ya Miradi ya Maendeleo Isiyotumika ........................................................ 80
4.6 Makusanyo Pungufu ya Kodi ya Majengo ............................................................. 61

SURA YA TANO ................................................................................................. 83

5.0 Mambo Muhimu Yaliyojiri Katika Ukaguzi wa Hesabu na Udhibiti na Ndani ................83
5.1 Tathimini ya Mifumo ya Udhibiti wa Ndani na Maswala ya Utawala Bora katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa ........................................................................................83
5.2. Usimamizi wa Maduhuli ...........................................................................90
5.3 Usimamizi wa Fedha ..............................................................................93
5.4 Usimamizi wa Rasilimali watu ...................................................................97
5.5 Usimamizi wa Mali Katika Halmashauri ........................................................109
5.6 Ukaguzi Wa Miradi Iliyopata Fedha Toka Kwa Wahisani ....................................116
5.7 Usimamizi wa Matumizi ..........................................................................126
5.8 Madeni na Mihadi ..................................................................................132
5.9 Masuala Mengine ...................................................................................133

SURA YA SITA ..........................................................................................137
6.0 Mapitio ya mikataba na uzingatiaji wa taratibu za manunuzi ..............................137
6.1 Ufuataji wa Kanuni za manunuzi ..............................................................137
6.2 Ufanisi wa Utendaji kazi wa Kitengo cha Usimamizi wa Manunuzi (PMU) ................137
6.3 Mapitio ya Mikataba na Uzingatiaji wa Taratibu za Ununuzi katika Halmashauri .....138
6.4 Mapungufu Katika Kuhesabu Mali/Vifaa Mwisho wa Mwaka ..................................143

SURA YA SABA ..........................................................................................145
7.0 Kaguzi Maalum ......................................................................................145
7.1 Muhtasari wa Masuala yaliyojitokeza katika Kaguzi Maalumu .............................145
7.2 Mafunzo yaliyopatikana kutokana na Kaguzi Maalum zilizofanyika katika mwaka.....154

SURA YA NANE ..........................................................................................157
8.0 Hitimisho na Mapendekezo .......................................................................157

VIAMBATISHO .............................................................................................167

## Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

| *Imeanzishwa kwa mujibu wa Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania* |
|---|

Wajibu na majukumu ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali zimeainishwa katika Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 (iliyorekebishwa 2005) na kama ilivyofafanuliwa zaidi katika Vif. Na.45 na Na.48 ya Sheria ya Fedha za Mamlaka ya Serikali za Mitaa Na.9 ya mwaka 1982 (iliyorekebishwa 2000) na Kif. Na.10 (1) ya Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na. 11 ya mwaka 2008.

**Dira ya Ofisi**
Kuwa kituo bora katika ukaguzi wa hesabu katika sekta za umma.

**Lengo la Ofisi**
Kutoa huduma za ukaguzi wenye ufanisi ili kuongeza uwajibikaji na thamani ya fedha katika kukusanya na kutumia raslimali za umma.

**Ofisi inaongozwa na Maadili ya Msingi ambazo ni:**

| | |
|---|---|
| **Kutopendelea:** | Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ni taasisi isiyopendelea, inayotoa huduma kwa wateja wake kwa malengo na kwa haki. |
| **Ubora:** | Tunatoa huduma za ukaguzi zenye ubora wa hali ya juu kwa kuzingatia viwango vya kitaaluma. |
| **Uadilifu:** | Tunazingatia na kudumisha maadili ya tabia kwa kiwango cha juu na kuheshimu sheria. |
| **Zingatio kwa wadau** | Tunalenga matakwa ya wadau wetu kwa kujenga utamaduni wa kutoa huduma bora kwa wateja na kuwa na watumishi wenye uwezo na ari ya kazi. |
| **Ubunifu:** | Tuna ubunifu ambao wakati wote inaimarisha utamaduni wa kuendeleza na kukaribisha mawazo mapya toka ndani na nje ya taasisi. |

*© Taarifa hii ni kwa ajili ya matumizi ya Serikali. Hata hivyo, baada ya taarifa hii kuwasilishwa Bungeni, taarifa hii itakuwa ni kumbukumbu ya umma na usambazaji wake hautakuwa na kikomo.*

## Orodha ya Vifupisho

| | |
|---|---|
| **AFROSAI - E** | Muungano wa Asasi Kuu za Ukaguzi katika nchi za Afrika zinazotumia lugha ya Kiingereza |
| **ASDP** | Programu ya Maendeleo ya Kilimo na Mifugo |
| **BoQ** | Mchanganuo wa Gharama za Kazi |
| **CAG** | Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali |
| **CDCF** | Mfuko wa Maendeleo ya Majimbo |
| **CDG** | Mfuko wa Maendeleo ya Jamii |
| **CHF** | Mfuko wa Afya ya Jamii |
| **DADPS** | Mpango wa Maendeleo ya Kilimo Wilayani |
| **GPSA** | Wakala wa Huduma ya Manunuzi Serikalini |
| **HBF** | Mfuko wa Afya |
| **IFAC** | Shirikisho la Kimataifa la Wahasibu |
| **IFMS** | Mfumo Funganifu wa Usimamizi wa Fedha |
| **INTOSAI** | Shirika la Kimataifa la Asasi Kuu za Ukaguzi. |
| **IPSASs** | Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu kwa Sekta ya Umma |
| **ISA** | Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu |
| **ISSAIs** | Viwango vya Shirika la Kimataifa la Asasi Kuu za Ukaguzi |
| **LAAC** | Kamati ya Bunge ya Hesabu za Mamlaka ya Serikali za Mitaa |
| **LAFM** | Memoranda ya Fedha za Mamlaka ya Serikali za Mitaa, 1997 |
| **LAAM** | Kitabu cha Mwongozo wa Uhasibu wa Mamlaka ya Serikali za Mitaa, 1993 |
| **LAPF** | Mfuko wa Pensheni ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa |
| **LGDG** | Ruzuku ya Miradi ya Maendeleo ya Serikali za Mitaa. |
| **LGFA** | Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, 1982 (iliyorekebishwa 2000) |
| **LGLB** | Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa |
| **LGRP** | Mpango wa Kuboresha Serikali za Mitaa |
| **MMAM** | Mpango wa Maendeleo wa Afya ya Msingi (PHSDP) |
| **MTEF** | Mpango wa kati ya Matumizi ya Fedha za Umma |
| **NAO** | Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi |

| | |
|---|---|
| **NHIF** | Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya |
| **NMSF** | Mkakati wa Taifa wa Kudhibiti UKIMWI |
| **NSSF** | Mfuko wa Huduma ya Jamii |
| **PEPFAR** | Mpango wa Raisi wa Marekani Kupambana na UKIMWI |
| **PFM** | Usimamizi Shirikishi wa Misitu |
| **PFMRP** | Mradi wa Mpango wa Maboresho katika Usimamizi wa Fedha za Umma |
| **PMG** | Mlipaji Mkuu wa Serikali |
| **PMU** | Kitengo cha Usimamizi wa Manunuzi |
| **PPR** | Kanuni za Manunuzi ya Umma, 2005 |
| **PPRA** | Mamlaka ya Udhibiti wa Manunuzi ya Umma |
| **Kif.** | Kifungu |
| **SIDA** | Wakala wa Maendeleo ya Kimataifa ya Sweden |
| **SNAO** | Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ya Sweden |
| **TACAIDS** | Tume ya Kudhibiti UKIMWI |
| **TASAF** | Mfuko wa Maendeleo ya Jamii Tanzania |
| **TRA** | Mamlaka ya Mapato Tanzania |
| **UDEM** | Usimamizi wa Maendeleo ya Mazingira Mijini |
| **UNHCR** | Umoja wa Mataifa ya Wakimbizi |
| **VAT** | Ongezeko la Thamani |
| **WSDP** | Mpango wa Maendeleo wa Sekta ya Maji |
| **OPRAS** | Usimamizi wa Upimaji wa Utendaji Kazi wa Watumishi |
| **PSPF** | Mfuko wa Pensheni wa Watumishi wa Umma |
| **PPF** | Mfuko wa Pensheni wa Watumishi wa Mashirika ya Umma |
| **MMEM** | Mpango wa Maendeleo wa Elimu ya Msingi |
| **HSDP** | Ruzuku ya Maendeleo ya Sekta ya Afya |
| **MMES** | Mpango wa Maendeleo wa Elimu ya Sekondari |
| **OWM - TAMISEMI** | Ofisi ya Waziri Mkuu – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa |
| **NRWSSP** | Mpango wa Maji Safi na Maji Taka Vijijini |
| **JRF** | Mfuko wa Pamoja wa Ukarabati wa Vituo vya Afya |
| **CUIS** | Mfumo wa Manunuzi wa Vifaa Vinavyotumika Mara kwa Mara |

## Dibaji

Ripoti hii ni majumuisho kwa muhtasari, ya taarifa za kina za ukaguzi zilizotolewa kwa uongozi wa Mamlaka husika ya Serikali za Mitaa.

Kwa mujibu wa Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 (iliyorekebishwa 2005), Kifungu cha 48 cha Sheria za Fedha za Serikali za Mitaa Na.9 ya 1982 (iliyorekebishwa 2000) pamoja na Kif. 34 (1) cha Sheria za Ukaguzi wa Umma Na. 11 ya 2008 ambacho kinamtaka Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu kutoa maoni ya kitaalam juu ya kila hesabu na matokeo ya ukaguzi, kuandaa taarifa juu ya kaguzi za hesabu hizo na kuwasilisha taarifa hiyo kwa Mheshimiwa Rais.

Ninayo heshima kuwasilisha Ripoti ya mwaka ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali za Mitaa kwa mwaka wa Fedha ulioishia Juni 30, 2011 kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa, Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete na hatimaye kuwasilishwa katika Bunge la Muungano la Tanzania kupitia yeye.

Nia ya Ripoti hii ni kuwajulisha wadau wetu ambao ni Mamlaka za Serikali za Mitaa, Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC), Serikali, Mahakama, Wahisani, Taasisi zisizo za Kiserikali na Jamii yot kwa ujumla kwa muhtasari wa matokeo ya ukaguzi wa Mamlaka ya Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha ulioishia Juni 30, 2011.

Ripoti hii inatoa tathmini kwa ujumla ya ukaguzi kuhusu utayarishaji wa taarifa za fedha kama zinafuata Sheria na Kanuni na masuala ya uwajibikaji na utawala zinazohusiana na uendeshaji wa Serikali za Mitaa. Pia kutoa majumuisho na mapendekezo kutokana na tathmini ya mambo yanayozihusu Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Mamlaka za Serikali za Mitaa zilipewa nafasi ya kupitia na kujadiliana na wakaguzi kuhusu matokeo ya ukaguzi kwa kupitia Taarifa za ukaguzi zilizotolewa kwa Mamlaka zote za Serikali za

Mitaa katika kikao cha mwisho baada ya ukaguzi. Ningependa kukiri kuwa majadiliano na Wakaguliwa yalikuwa na umuhimu mkubwa. Ofisi yangu inatarajia kufuatilia katika muda muafaka juu ya maamuzi yatakayotolewa na Serikali kupitia Mlipaji Mkuu wa Serikali kuhusuana na mapendekezo yaliyotolewa katika Ripoti hii.

Mamlaka za Serikali za Mitaa zina majukumu mbalimbali katika utoaji wa huduma muhimu na utawala bora kwa wananchi wa maeneo yao. Ili kutimiza majukumu haya, wanapaswa kukusanya mapato kwa njia ya kodi, leseni, ada na vyanzo mbali mbali vya mapato. Katika suala hili, usimamizi wa fedha ni muhimu ili Serikali za Mitaa ziweze kuleta ushawishi kwa Umma kuwa mapato hayo yamepokelewa kwa kufuata sheria na kutumika ipasavyo kwa matumizi yaliyokusudiwa.

Mwisho, napenda kutoa shukurani zangu za dhati kwa wote walioniwezesha kutekeleza majukumu yangu Kikatiba na kuweza kukamilisha kwa wakati Ripoti Kuu ya Ukaguzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2011.

Ludovick S.L. Utouh
**MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI**

---

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali,
Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi,
**Dar es Salaam,**
28 Machi, 2012

## Shukrani

Kwanza kabisa, kwa umuhimu wa pekee, napenda kutoa shukrani za dhati kwa Mwenyenzi Mungu kwa kunipa neema, uwezo na afya njema iliyoniwezesha kukamilisha Ripoti hii ya Ukaguzi.

Kuna wadau wengi ambao wameshiriki katika kufanikisha ukamilishaji wa Ripoti hii.

Napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete na Serikali yake yote, Bunge na Kamati za Bunge kwa kuisaidia Ofisi yangu na kuyafanyia kazi kwa umakini masuala yaliyojitokeza kwenye ripori zangu za ukaguzi kwa lengo la kuboresha uwajibikaji katika masuala ya fedha nchini na mgawanyo ulio sawa wa Mali za Umma.

Napenda pia kutoa shukrani zangu za dhati kwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda kwa kusisitiza kuhusu kuboresha uwajibikaji katika matumizi ya fedha za Umma kwa kutoa maelekezo kuwa kila Mkuu wa Mkoa, Meya, Mwenyekiti wa Halmashauri na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri kuhakikisha kuwa hoja za ukaguzi zinajibiwa wakati wa ukaguzi, pia kuwasisitizia wakaguliwa kuwa wanatakiwa wafuate kalenda ya mwaka ya Ukaguzi.

Vilevile, shukrani zangu za dhati ziende kwa jumuiya ya Wafadhili hasa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ya Sweden. Serikali ya Sweden kupitia mradi wa SIDA, Benki ya Dunia kupitia mradi wa PFMRP, Secretarieti ya AFROSAI-E na wote waliochangia katika kufanikisha mabadiliko ndani ya Ofisi yangu. Michango yao katika kuendeleza Watumishi, mifumo ya tekinolojia ya mawasiliano na ununuzi wa vitendea kazi vingine kama magari imekuwa msaada mkubwa sana katika maendeleo ya Ofisi yetu.

Kwa pamoja ninapenda kuwashukuru wadau wengine wote ikiwa ni pamoja na Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mlipaji Mkuu wa Serikali na Maafisa Masuuli

wote wa Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa  ushirikiano wao mkubwa wa kutoa taarifa muhimu zilizohitajika kuandaa taarifa hii.

Nitakuwa mchache wa shukurani kwa kutovitambua vyombo mbalimbali vya habari katika kuujulisha umma wa Tanzania juu ya matokeo na mapendekezo yaliyopo katika Ripoti yangu mara tu ninapowasilisha Bungeni.

Natoa pia shukurani kwa watumishi wa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa kutumia utaalamu wao katika ukaguzi na kujituma wakati wote wa ukaguzi na kuweza kufanikiwa kukamilisha Ripoti hii. Juhudi kubwa katika kazi imewezesha Ripoti hii kukamilika na kuwasilishwa Bungeni kwa wakati.

Mwisho kabisa, napenda kuwashukuru Umma tunaowahudumia nchini. Nawasisitizia kwamba waendelee kufanya kazi kwa uwazi na kusimamia matumizi mazuri ya fedha za Umma na uwajibikaji katika kutumia rasilimali za Umma.

Mwenyezi Mungu awabariki wote, nasi tunaahidi kuendelea kuchangia katika kukuza uwajibikaji na uzingatiaji wa thamani ya fedha katika ukusanyaji wa mapato na matumizi ya rasilimali za umma.

**Muhtasari wa Mambo Muhimu katika Taarifa ya Ukaguzi**

Taarifa hii inatoa muhtasari na majumuisho ya matokeo ya ukaguzi wa taarifa za fedha za Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2011. Ukaguzi wa taarifa za fedha ni upitiaji huru wa masuala ya uhasibu na utayarishaji wa taarifa za fedha katika taasisi za Sekta ya Umma.

Sehemu hii ya ripoti inatoa maelezo ya jumla ya matokeo ya ukaguzi wa hesabu za Mamlaka ya Serikali za Mitaa na kufuatiwa na mambo muhimu yaliyobainika wakati wa ukaguzi pamoja na muhtasari wa mapendekezo.

**1. Maelezo ya matokeo ya ukaguzi**

Ukaguzi wa hesabu za jumla ya Halmashauri 133 kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni 2011 umekamilika. Ukaguzi wa hesabu za Halmashauri ya Manispaa ya Tabora bado haukukamilika hadi ilipofikia tarehe 31 Disemba, 2011 hivyo matokeo ya ukaguzi huo yatatolewa peke yake. Muhtasari wa masuala muhimu yaliyoonekana wakati wa ukaguzi yapo katika ripoti hii na masuala haya kwa kirefu yamefafanuliwa katika taarifa zilizopelekwa kwa Uongozi na Wenyeviti wa Mamlaka za Serikali za Mitaa husika.

**Mwelekeo wa jumla wa hati za Ukaguzi zilizotolewa**

Sehemu hii inaonyesha tathmini ya mwelekeo wa hati za ukaguzi kwa miaka ya fedha ya 2007/2008, 2008/2009, 2009/2010 na 2010/2011. Madhumuni ya mwelekeo huu ni kuonesha kiwango cha utendaji na uwajibikaji katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa miaka husika.

**Mwelekeo wa Hati zilizotolewa katika miaka ya fedha ya 2007/08, 2008/09, 2009/10 na 2010/11**

| | Hati zinazoridhisha | | Hati zenye shaka | | Hati zisizoridhisha | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Miaka** | **Jumla** | **%** | **Jumla** | **%** | **Jumla** | **%** | **Jumla ya Halmashauri** |
| **2007/08** | 72 | 54 | 61 | 46 | 0 | 0 | **133** |
| **2008/09** | 77 | 58 | 55 | 41 | 1 | 1 | **133** |
| **2009/10** | 66 | 49 | 64 | 48 | 4 | 3 | **134** |
| **2010/11** | 72 | 54 | 56 | 42 | 5 | 4 | **133** |

Jedwali hapo juu linaonesha kuwa, hati zinazoridhisha zimeongezeka kwa 4% kutoka mwaka 2007/2008 hadi 2008/2009, zimepungua kwa 9% toka mwaka 2008/2009 hadi 2009/2010 na kuongezeka kwa 5% toka mwaka 2009/2010 hadi 2010/11.

Hati zenye shaka zimepungua kwa 5% toka mwaka 2007/2008 hadi 2008/2009 na kuongezeka kwa 7% toka mwaka 2008/2009 hadi mwaka 2009/2010 na kupungua kwa 6% toka 2009/2010 hadi mwaka 2010/2011.

Hati zisizoridhisha zimeongezeka kwa 1% toka mwaka 2007/2008 hadi 2008/2009, zimeongezeka kwa 2% toka mwaka 2008/2009 hadi 2009/2010 na pia kuongezeka kwa 1% toka mwaka 2009/2010 hadi mwaka 2010/2011.

**Mwelekeo wa Hati zilizotolewa katika Mamlaka za Serikali za Mitaa**

Hati zilizotolewa katika kipindi cha miaka minne katika Mamlaka za Serikali za Mitaa zinaonesha mwelekeo ufuatao:-

(i) Halmashauri kumi na moja (11) zimeendelea kupata hati zinazoridhisha kwa kipindi chote cha miaka minne.

(ii) Halmashauri thelathini na sita (36) zimeonesha utendaji mzuri ukilinganisha na miaka ya nyuma kwa kupata hati zinazoridhisha kwa mwaka huu wa fedha badala ya hati zenye shaka na hati zisizoridhisha.

(iii) Halmashauri kumi na moja (11) zimendelea kupata hati zenye shaka kwa miaka minne mfululizo.

(iv) Halmashauri ishirini na tisa (29), utendaji wake umeshuka ukilinganisha na miaka ya nyuma ambapo zilikuwa zikipata hati zinazoridhisha lakini mwaka huu zimepata hati zenye shaka na hati zisizoridhisha.

Kwa ujumla utendaji wa Serikali za Mitaa kwa mwaka 2010/2011 umeboreka kutokana na sababu zifuatazo:

- Maelekezo ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mizengo Pinda kwa kutaka uongozi wa Mikoa kuchukua jukumu la kuhakikisha kwamba, hatua madhubuti zinachukuliwa juu ya mapendekezo yaliyomo katika ripoti ya Mkaguzi inayotolewa kwa Halmashauri husika
- Ushiriki wa Wakuu wa Mikoa kwa kufanya ufuatiliaji na usimamizi wa karibu kwa Halmashauri juu ya maendeleo kuhusu utekelezaji wa mapendekezo ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Hii ni pamoja na kuongoza vikao vya baraza la Madiwani kujadili ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.
- .Kuwepo kwa uboreshaji wa taarifa za fedha zilizotolewa na Halmashauri kulingana na viwango vya Kimataifa.
- Maboresho haya pia yamechangiwa na msukumo uliotoka katika Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC). Kamati hii inafanya kazi nzuri katika kuhakikisha kuwa, Maafisa Masuuli wanawajibika ipasavyo katika kusimamia rasilimali za Halmashuri husika.
- Uboreshaji wa mifumo ya udhibiti wa ndani na kufuata kanuni na sheria za usimamizi wa rasilimali za umma.

## 2. Muhtasari wa mambo muhimu yaliyojitokeza katika ukaguzi wa Hesabu za mwaka 2010/2011 wa Mamlaka za Serikali za Mitaa

Makosa na madhaifu yaliyoonekana wakati wa ukaguzi ni pamoja na yafuatayo:-

**Mapendekezo ambayo hayajatekelezwa**

**(i) Ripoti Kuu**

Nimepokea majibu ya Ripoti Kuu kwa mwaka wa fedha wa 2009/2010 kutoka Serikalini kupitia Mlipaji Mkuu wa Serikali kwa barua yenye Kumb. Na.EB/AG/485/01/VOL.III/31 ya tarehe 28 Juni, 2011. Mapitio na uhakiki wa majibu umebaini kuwa, kati ya mapendekezo 12, pendekezo 1 limetekelezwa kikamilifu, 1 limetekelezwa kwa kiasi na 10 hayakutekelezwa kabisa.

**(ii) Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Hesabu za Mamlaka ya Serikali za Mitaa (LAAC)**

Katika kutoa majibu ya Serikali kuhusu ripoti ya ukaguzi juu ya taarifa za fedha kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2010, Mlipaji Mkuu wa Serikali hakuweza kuleta majibu ya mapendekezo saba (7) yaliyotolewa katika taarifa ya Kamati ya Bunge ya Hesabu za Mamlaka za Serikali za Mitaa (LAAC) iliyowasilishwa Bungeni mwezi Aprili, 2011. Muhtasari wa mapendekezo ya Kamati hiyo ni kama ifuatavyo:

- Serikali inapaswa kuwa na mpango madhubuti ili kuhakikisha kwamba mishahara ya kiasi cha Sh. 792.2 milioni iliyolipwa kwa wafanyakazi hewa inarejeshwa.
- Kamati ilipendekeza kwamba, Serikali inatakiwa kuchukua hatua madhubuti ili kuimarisha mifumo ya Udhibiti wa Ndani kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa.
- Kamati ilipendekeza kuwa, Maafisa Masuuli wote na Wakuu wa Idara lazima wawajibike katika utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo chini ya Mamlaka yao. Pia Kamati ilipendekeza kuanzishwa kwa ukaguzi wa kijamii ili kuongeza uwajibikaji na uwazi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa.
- Zaidi ya hayo Kamati ilipendekeza kwamba, ukaguzi wa thamani ya fedha katika Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ni lazima uimarishwe kwa kuongeza idadi ya wakaguzi

na kupanua wigo wa ukaguzi huo ili uweze kufanyika katika Mamlaka za Serikali za Mitaa nyingi zaidi.

- Kamati ilipendekeza kwamba, uongozi wa Halmashauri husika unapaswa kuzingatia kanuni na Sheria za manunuzi ya Umma ya mwaka, 2004 pamoja na Kanuni zake za mwaka 2005. Serikali pia inapaswa kutumia kwa ufanisi ripoti na miongozo iliyotolewa na Mamlaka ya Usimamizi wa Manunuzi ya Umma (PPRA) katika taratibu za kila siku kuhusu manunuzi ya umma.
- Kamati ilipendekeza kwamba, Serikali itafute njia maalumu ili kudhibiti matumizi mabaya ya fedha za umma kutokana na ununuzi wa mafuta na vipuri vya magari.
- Kamati ilipendekeza kwamba, Serikali inapaswa kupitia upya Miongozo ya matumizi ya fedha katika baadhi ya miradi kama TASAF, TACAIDS, DADPS, CDG na UDEM ambayo hulipa posho nyingi ukilinganisha gharama za utekelezaji wa miradi husika.

  Kamati ilipendekeza kwamba, Serikali itekeleze mapendekezo yaliyotolewa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali katika ripoti mbalimbali za ukaguzi maalum.

**iii) Ripoti za Halmashauri**

Kati ya Halmashauri 133, Halmashauri 130 hazikutekeleza masuala mbalimbali ya ukaguzi wa miaka ya nyuma yenye jumla ya kiasi cha cha Sh.105,263,165,967.

**iv) Ripoti za Kaguzi Maalum**

Jedwali hapa chini linaonyesha jumla ya masuala ambayo bado kutekelezwa yaliyopendekezwa katika ukaguzi maalum kwa miaka ya fedha 2008/2009, 2009/2010 na 2010/2011.

| Mwaka wa Fedha | Thamani ya Masuala ambayo bado kutekelezwa (Sh.) | Idadi ya Masuala ambayo bado kutekelezwa na yasiyokuwa na thamani | Halmashauri zinazohusika |
|---|---|---|---|
| 2008/09 | 2,533,956,821 | 11 | 7 |
| 2009/10 | 44,415,697,227 | 43 | 11 |
| 2010/11 | 27,615,658,694 | 69 | 19 |

Kutotekelezwa na kutojibiwa kwa mapendekezo ya ukaguzi kunaweza kusababisha kujirudia kwa mapungufu yaliyoonekana wakati wa ukaguzi. Hii inarudisha nyuma juhudi za kuboresha mazingira ya udhibiti wa ndani na usimamizi wa fedha katika Mamlaka za Serikali za Mitaa.

**(v) Matokeo ya ukaguzi wa mwaka huu**

(a) **Mapungufu katika Maandalizi na uwasilishaji wa taarifa za fedha**

Rasimu za taarifa za fedha kutoka Halmashauri 60 zilizowasilishwa zilikuwa na makosa mbalimbali kama vile baadhi ya taarifa kutoonyeshwa kabisa, baadhi ya tarakimu kuonyeshwa pungufu na baadhi kuonyeshwa zaidi, kutoonyeshwa kwa taarifa muhimu na mapungufu katika kuonyesha taarifa muhimu.

Jumla ya makosa na kutoonyeshwa kwa taarifa katika rasimu ya taarifa za fedha ilikuwa pungufu kwa Sh.187,064,788,252 ambao ni 16% ya jumla ya matumizi na zaidi kwa Sh.118,967,438,259 ambao ni 10% ya jumla ya matumizi. Kutokana na ukubwa wa makosa haya, Halmashauri zilifanya marekebisho ya taarifa za fedha na kuziwasilisha tena kwa ajili ya ukaguzi, kitu ambacho kiliongeza muda wa kukamilika kwa ukaguzi. Idadi ya mabadiliko mengi yaliyofanywa yanaonyesha kuwa, Wahasibu wa Halmashauri wana uwezo mdogo katika uandaaji wa taarifa za fedha.

**(b) Udhaifu katika mfumo wa udhibiti wa ndani na kitengo cha Ukaguzi wa Ndani**

- **Mfumo wa Uhasibu usiotumia mtandao wa Kompyuta**
  Mapitio na tathmini yetu katika mfumo wa uhasibu inaonyesha kwamba sampuli ya Halmashauri 36 zinachanganya mfumo unaotumia kompyuta na Mfumo usiotumia kompyuta katika uhasibu. Mfumo Funganifu wa Usimamizi wa Fedha (IFMS) unatumika kutayarishia hati za malipo na kuingiza taarifa za malipo katika kitabu cha fedha. Leja za taarifa za awali, Leja urari, taarifa za mizania ya hesabu na taarifa za mapato na matumizi yanaandaliwa bila kutumia Mfumo Funganifu wa Usimamizi wa Fedha (IFMS).

- **Kutotumika kikamilifu Mfumo Funganifu wa Usimamizi wa Fedha**
  Wakati wa tathmini ya mfumo wa uhasibu ilibainika kwamba, Katika Halmashauri nyingi Mfumo Funganifu wa Usimamizi wa Fedha aidha haufanyi kazi au matumizi yake bado yako katika kiwango cha chini. Pia, ilibainika kuwa, watumiaji wa mfumo huu hawana mafunzo ya kutosha, Mfumo haupo kama unavyotakiwa na Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu kwa Sekta za Umma (IPSASs) na utekelezaji wa Mfumo toleo la 7.2 haukukidhi kikamilifu mahitaji ya Serikali za Mitaa.

- **Mapungufu katika Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani na Kamati ya Ukaguzi**
  Ukaguzi unaonyesha kwamba pamoja na juhudi za kuimarisha Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani bado kuna mapungufu ya uwezo ambayo yanahitaji kushughulikiwa ili kufanya kitengo cha ukaguzi wa ndani kiwe na ufanisi zaidi.

Pia Kamati za Ukaguzi hazina ufanisi wa kutosha, hakuna miongozo ya ukaguzi inayoweza kutoa mikakati ya mwelekeo wa kazi. Pia ilibainika kuwa vitengo vina miongozo iliyopitwa na wakati inayowaongoza wakaguzi wa ndani juu ya mbinu na taratibu za kazi.

Pia tuliona kwamba katika baadhi ya ripoti za ukaguzi wa ndani za Serikali za Mitaa hushughulikiwa na uongozi wakati katika Halmashauri nyingine taarifa za ukaguzi hazitolewi mara kwa mara. Katika baadhi ya Halmashauri, wafanyakazi wa ukaguzi wa ndani ni wachache sana na hivyo hawatoshelezi kukidhi mahitaji ya Serikali za Mitaa ukizingatia ukubwa na hali ya kijiografia ya nchi.

Kutokana na uanzishwaji wa mfumo wa kutunza kumbukumbu za uhasibu kwenye komputa na kuanzishwa kwa toleo jipya la mfumo huu yaani toleo la 9.05, kuna haja ya Kuwa na ukaguzi wa ndani imara ili kupunguza hatari zinazohusiana na mazingira ya kiuhasibu katika kompyuta.

- **Menejimenti ya vihatarishi**

  Halmashauri zinatarajiwa kuangalia vihatarishi ambavyo madhara yake ni makubwa katika mazingira ya halmashauri husika ambayo ni pamoja na udhibiti wa vihatarishi vinavyohusiana na hatari ambazo zinaweza kuwa na athari katika taarifa za fedha za Halmashauri.

  Mapitio ya ukaguzi wa sampuli 73 za Serikali za Mitaa ulibaini kuwa, hapakuwa na

mwongozo wa menejimenti ya vihatarishi na kutofanywa kwa tathmini ya hivi karibuni ya vihatarishi ili kutambua vihatarishi vilivyopo na vile vinavyojitokeza kutokana na matokeo ya mabadiliko ya Mazingira na mbinu za utoaji wa huduma, sera na taratibu za menejimenti ya vihatarishi ambavyo vilikuwa havijaanzishwa.

- **Kuzuia na kudhibiti udanganyifu**
  Tathmini ya kuzuia na kudhibiti udanganyifu uliofanywa katika sampuli 68 za Serikali za Mitaa unaonyesha kuwa uongozi wa Halmashauri hizo hazina kumbukumbu na mipango iliyopitishwa kwa ajili ya kutambua na kukabiliana na hatari ya udanganyifu katika Halmashauri . Aidha, viashiria kama vile kukosekana kwa ufanisi wa utendaji wa kamati za Ukaguzi, ufanisi wa kitengo cha ukaguzi wa ndani, kukosekana kwa hati za malipo, makusanyo ya mapato kutopelekwa benki, malipo yasiyo na viambatanisho, upotoshwaji wa taarifa za fedha, kukosekana kwa vitabu vya stakabadhi za mapato, malipo ya mishahara kwa wafanyakazi hewa ambayo yanatazamwa kama dalili za udanganyifu yalibainishwa. Asili ya viashiria vya udanganyifu vilivyobainishwa hapo juu vinaharibu mifumo ya udhibiti wa ndani hivyo kuna hatari kubwa ya udanganyifu katika ngazi mbalimbali za uendeshaji wa Halmashauri. Mapungufu katika udhibiti wa udanganyifu unaweza kusababisha udanganyifu husika kutodhibitiwa na uongozi wa Halmashauri.

**(c) Ulegevu katika Usimamizi wa Mapato**

- Jumla ya vitabu 682 vya stakabadhi za mapato

kutoka Halmashauri 36 vilikosekana na hivyo havikuwasilishwa kwa ajili ya ukaguzi. Hivyo, wakaguzi hawakuweza kujua ukamilifu wa ukusanyaji wa mapato.

- Wakati wa ukaguzi wa mwaka wa fedha husika, kati ya Halmashauri zilizochaguliwa na kukaguliwa, Halmashauri 47 zilikuwa na jumla ya Sh.4,227,984,618 ikiwa ni mapato yaliyokusanywa na mawakala ambayo yalikuwa bado hayajawasilishwa kwenye Halmashauri husika.
- Ulegevu katika udhibiti wa ndani na ufuatiliaji wa makusanyo ya mapato ulisababisha kutokusanywa kwa mapato kutoka kwenye vyanzo vya ndani yenye jumla ya Sh.8,332,985,545 kutoka kwa wadaiwa wa kodi mbalimbali katika sampuli ya Halmashauri 22.
- Jumla ya Sh.2,328,276,795 ikiwa ni kodi ya Majengo sawa na 44% ya makisio ya Sh.5,085,350,996 hazikukusanywa na Halmashauri 14.

**(d) Udhaifu katika Usimamizi wa Fedha**

Usimamizi na udhibiti wa fedha ni muhimu ili kuhakikisha fedha zote zinazotokana na mapato zinakusanywa, kupelekwa benki na kuweka kumbukumbu zake. Mapungufu yafuatayo yalibainika katika ukaguzi wa mwaka 2010/2011:

- Suluhisho za benki ni msingi wa kudhibiti hatari na ulaghai wa taarifa za kifedha zinazofanyika kupitia akaunti za halmashauri. Udhaifu katika suluhisho za benki ulibainika katika Halmashauri 88. Hizi ni pamoja na Sh.4,662,975,016 ikiwa ni jumla ya mapato katika vitabu vya fedha vya Halmashauri lakini hayapo katika taarifa za benki. Jumla ya Sh.425,988,778 kutoka katika Halmashauri mbalimbali yalionyeshwa kama mapato yaliyomo njiani kupelekwa benki. Pia, jumla ya Sh.1,002,195,882 zilikuwa zimelipwa benki kutoka katika akaunti za Halmashauri bila ya kuonyeshwa

katika vitabu vya fedha vya Halmashauri. Mapungufu mengine katika suala la usimamizi wa fedha ni pamoja na:

- o Kaguzi za kushtukiza za fedha taslimu zilikuwa hazifanyiki katika Halmashauri 38
- o Kulikuwa na upotevu wa fedha taslimu wa jumla ya Sh.34,436,525 ukihusisha Halmashauri 3

**e) Mapungufu katika Usimamizi wa Matumizi**

Udhibiti wa mifumo ya matumizi ni muhimu ili kuhakikisha kwamba gharama zote zilizotumika zimelipwa kwa usahihi na kurekodiwa. Baadhi ya mapungufu katika usimamizi wa matumizi mwaka 2010/2011 ni pamoja na:

- Halmashauri 32 kati ya 133 zilizokaguliwa zilifanya malipo yenye jumla ya Sh.1,080,519,637 ambayo hayakuwa na hati za malipo zilizotolewa kwa ajili ya ukaguzi, na hivyo kupunguza wigo wa ukaguzi.
- Malipo ya jumla ya Sh.5,668,730,107 yenye hati pungufu yalibainika katika Halmashauri 63.
- Uhamisho wa fedha za Halmashauri kutoka akaunti moja kwenda nyingine kwa njia ya mikopo yenye jumla ya Sh.677,556,900 haikurejeshwa.

**(f) Mapungufu katika Udhibiti wa Mishahara**

- Suluhisho za mara kwa mara na kaguzi zilikuwa hazifanywi na uongozi wa Halmashauri ili kuthibitisha uhalali wa maingizo yote ya malipo ya mishahara, matokeo yake, malipo ya mishahara kwa wastaafu, watoro, waliojiuzulu, walioachishwa kazi yalikuwa yakilipwa kupitia akaunti zao za benki bila kugundulika. Malipo hayo ni vigumu sana kurejeshwa hata yakigundulika kwani fedha hizo tayari zimechukuliwa na kutumiwa na wahusika. Malipo kwa wastaafu, watoro, na walioachishwa kazi yenye jumla ya Sh.961,394,959 yalibainika katika Halmashauri 36

- Mishahara yenye jumla ya Sh.1,468,085,615 inayohusiana na watumishi waliofariki, wastaafu na watoro katika Halmashauri 46 haikuwasilishwa Hazina kinyume na maelekezo yaliyotolewa na wizara ya fedha kwa barua yenye Kumb.Na.EB/AG/5/03/01/Vol.IV/36 ya tarehe 31 Agosti 2007. Kuna uwezekano kwamba kiasi hicho kimetumika vibaya kwa sababu Halmashauri bado hazijarejesha hata baada ya hoja za ukaguzi kutolewa.
- Ukaguzi wa malipo ya mishahara kwa watumishi 22 katika Halmashauri 3 zilizochaguliwa uligundua kuwa, watumishi hawa walilipwa mishahara ambayo ilikuwa ni zaidi ya viwango vyao vya mishahara yenye jumla ya Sh.42,869,832, bila kupata kibali kutoka kwa Katibu Mkuu Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma.
- Ukaguzi wa nyaraka za udhibiti wa mishahara kwa miezi ya Februari na Machi, 2011 uligundua kuwa jumla ya Sh.65,007,802 zilikatwa na Hazina kutoka kwenye mishahara ya wafanyakazi wa Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara Sh.37,185,550 na Halmashauri ya Mji wa Njombe Sh.27,822,252 na kulipwa katika taasisi mbalimbali ikiwa ni pamoja na marejesho ya mikopo. Hata hivyo, ilibainika kuwa, kiasi kama hicho pia kilikatwa na Halmashauri na kulipwa katika taasisi hizohizo na hivyo kusababisha malipo mara mbili ya makato.
- Wakati wa ukaguzi wa mfumo wa malipo ya mishahara, imebainika baadhi mishahara ya watumishi wa Halmashauri ilikatwa hadi kufikia kiasi kinachozidi theluthi mbili (2/3) ya mishahara yao kwa sababu ya ukopaji unaozidi kiasi kutoka kwenye taasisi za fedha na nyinginezo. Katika Halmashauri nyingine idadi ya wafanyakazi walikuwa hawalipwi chochote kabisa kutokana na makato hayo. Ukaguzi uliofanyika katika Halmashauri 55 umeonyesha kuwa, zaidi ya watumishi 8827 walikuwa wakipokea

pungufu ya 1/3 ya mishahara yao. Hii ni kinyume na matakwa ya Waraka No.CCE.45.271/01/87 wa tarehe 19 Machi, 2010 uliotolewa wa na Ofisi ya Rais – Menejimenti ya Utumishi wa Umma ambao unakataza makato ya mshahara wa mtumishi wa serikali zaidi ya 2/3 ya mshahara wa kila mwezi.

**(g) Ruzuku isiyotumika**

Matokeo ya ukaguzi wa fedha za maendeleo na misaada ulionyesha kuwa Halmashauri 130 zilikuwa na jumla ya Sh.542,339,143,645 kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo ya Halmashauri hizo. Hata hivyo, hadi kufikia Juni 30, 2011 Sh.353,449,871,684 zilikuwa zimetumia na kubakia Sh.160, 518,294,140 sawa na 29.6% ya jumla ya fedha za maendeleo.

Aidha, katika mwaka husika, Halmashauri 128 zilitumia jumla ya Sh.1,978,117,478,839 ikiwa ni matumizi ya kawaida ya dhidi ya jumla ya ruzuku ya matumizi ya kawaida ya Sh.2,105,926,241,086 hivyo kusababisha kuwa na bakaa ya Sh.146,774,839,643 ambao ni sawa na 7%.

**(h) Mapungufu katika Usimamizi Rasilimali Watu**

Michakato ya usimamizi wa rasilimali watu unajumuisha usimamizi na utawala wa siku hadi siku wa haki za watumishi na mishahara. Vipengele vikuu katika gharama za watumishi vinajumuisha mishahara, likizo na madai mengine, michango ya kila mwezi ya mwajiri kwa ajili ya mafao ya uzeeni na gharama za fidia kwa wafanyakazi. Vitu hivi vinawakilisha uwiano muhimu wa matumizi ya Halmashauri zilizo nyingi. Kwa ujumla, madeni ya wafanyakazi, hasa kuhusiana na likizo ya kila mwaka na madai mengine ni moja ya madeni makubwa katika taarifa za mizania ya hesabu za Halmashaauri.

Ukaguzi katika Serikali za Mitaa unaonyesha kwamba baadhi ya Halmashauri zilikuwa na udhaifu mkubwa katika usimamizi wa rasilimali watu. Katika matukio kadhaa, iligundulika kuwa ajira hazifanyiki matokeo yake baadhi ya idara zinawatumishi wachache na hivyo kudhoofisha utoaji wa huduma. Pia, ilibainika kuwa baadhi ya Serikali za Mitaa zina matatizo katika kutunza kumbukumbu muhimu za watumishi. Maafisa rasilimali watu wameonekana kuweka uzito kidogo juu ya mapungufu ambayo yanaweza kuleta usumbufu endapo kuna uachishaji kazi au ustaafishaji wa mtumishi. Idadi ya Serikali za Mitaa zimeonyesha udhaifu mkubwa katika tathmini ya utendaji wa wafanyakazi.

**(i) Sheria na Kanuni za Manunuzi Kutofuatwa**

- Mapitio ya usimamizi wa manunuzi na mikataba ya mwaka uliomalizika ilionekana kuwa baadhi ya mikataba haikuwa na kumbukumbu za kutosha. Mfano nyaraka muhimu zilibainika kukosekana katika mafaili ya mikataba husika ikiwa ni pamoja na makubaliano ya mikataba, orodha ya manunuzi ya vifaa, makadirio ya Wahandisi, vyeti ya awali na manunuzi yaliyofanywa nje ya mpango wa manunuzi. Kiasi kinachohusika na mapungufu haya kinafikia Shs.4,452,071,069 kikihusisha sampuli ya Halmashauri 2.
- Ulegevu wa uongozi wa Halmashauri katika udhibiti wa malipo ya mkataba na usimamizi wa miradi ya Halmashauri unasababisha utekelezaji mbaya wa miradi na kuchelewa kukamilika kwa miradi ndani ya muda wa makubaliano.
- Manunuzi yenye thamani ya Sh.397,571,968 katika Halmashauri 20 yalifanyika kutoka kwa wauzaji mbalimbali wa bidhaa na huduma bila ushindani wa bei kinyume na matakwa ya Kanuni Na. 63 ya Kanuni za Manunuzi ya mwaka 2005.
- Manunuzi ya vifaa na Huduma yenye thamani ya

Sh.195,983,847 ulifanyika bila kibali cha Bodi ya Zabuni katika Halmashauri saba (7).

- Ukaguzi wa usimamizi wa vifaa ulionyesha kwamba, Halmashauri 22 hazikuingiza vifaa vilivyonunuliwa vyenye thamani ya Sh.594,164,665 katika leja. Hii inapingana na Agizo Na. 207 ya Memoranda ya Fedha za Serikali za Mitaa ya mwaka 1997.
- Vifaa vyenye thamani ya Sh.833,707,405 ziliagizwa na kulipwa na Halmashauri 13 lakini havikupelekwa kwenye Halmashauri husika kinyume na Kanuni Na.122(1) ya Kanuni za Manunuzi (Vifaa, ujenzi, Huduma zisizo za ushauri na uuzaji wa mali za Umma kwa Zabuni) ya mwaka 2005. Aidha, udhaifu katika taratibu za kuhesabu mali na vifaa ulibainika katika sampuli ya Halmashauri 28.

Kutofuata kwa taratibu za manunuzi zilizopendekezwa kunadhoofisha kanuni ya ushindani na thamani ya fedha.

**(j) Mapungufu katika Uendeshaji wa Mifuko**

- **Mfuko wa kuchochea maendeleo ya Jimbo**

  Jumla ya kiasi cha Sh.2,683,368,422 zilizotengwa kwa ajili ya shughuli za Mfuko wa kuchochea Maendeleo ya Jimbo hazikutumika katika sampuli ya Halmashauri 51. Hii ilisababishwa na usimamizi duni wa Mfuko kwa Kamati za maendeleo ya mfuko wa jimbo. Hivyo, malengo ya kuanzisha Mfuko ikiwa ni pamoja na utoaji wa rasilimali za nyongeza kwa ajili ya jamii kutumia katika maeneo ya kipaumbele kama maji, elimu, miundombinu afya, au kilimo na fursa kwa wananchi wa kawaida kuwa na nguvu katika kuamua vipaumbele na kugawanya fedha na rasilimali kufikia vipaumbele hivyo hayakufikiwa kikamilifu kama ilivyotarajiwa.

Aidha, Halmashauri nyingi hazikuandaa na kuwasilisha kwa Waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa taarifa ya kiasi kilichopokelewa na kutumiwa kwa kila Kamati ya kuchochea Maendeleo ya jimbo.

- **Mfuko wa Afya ya Jamii**

  Katika kipindi cha mwaka husika, ukaguzi uliofanyika juu ya usimamizi wa Mfuko wa Afya ya Jamii katika Halmashauri 33 ilibainika kuwa kulikuwa na bakaa ya Sh.2,963,900,725 ambayo hasa ilisababishwa na kutofungua na kuendesha akaunti tofauti kwa ajili ya Mfuko wa Afya ya Jamii na kuchelewesha kutolewa kwa ruzuku zinazolingana.

  Wakati wa ukaguzi ilionekana kuwa, fedha za Mfuko wa Afya ya Jamii zenye jumla ya Sh.44,086,650 katika Halmashauri 4 ambazo ni Halmashauri ya Manispaa ya Songea, Manispaa ya Dodoma, Halmashauri ya Wilaya ya Ulanga na Halmashauri ya Wilaya ya Iramba zilitumika katika kutekeleza shughuli zisizohusiana na uendeshaji wa mfuko huo kinyume na Miongozo ya Mfuko wa Afya ya Jamii.

- **Mfuko wa Wanawake na Vijana**

  Ukaguzi uliofanyika katika Halmashauri 23 umebaini kuwa Sh.1,587,780,350 zipo katika akaunti ya benki za Halmashauri bila kutolewa kama mikopo kwa vikundi vya Wanawake na Vijana.

**(k) Usimamizi wa Miradi**

Sampuli ya miradi mitatu ya maendeleo ya wafadhili ambayo ni NMSF na MMAM ilionyesha kasi ndogo

katika utekelezaji kwa kuwa na kiasi kikubwa kisichotumika cha Sh.1,104,364,692 kwa NMSF (Halmashauri 41) na Sh.5,848,929,864 kwa MMAM (Halmashauri 48).

Kutotumika kwa pesa zote ina maana kwamba idadi kubwa ya shughuli zilizopangwa hazikutekelezwa kikamilifu au hazikutekelezwa kabisa. Kwa maana hiyo basi, huduma/malengo yaliyotarajiwa na Halmashauri kwa ajili ya jamii husika yamecheleweshwa. Hii pia inaweza kupelekea marekebisho ya bajeti katika siku zijazo kwa sababu ya uwezekano wa kupanda kwa bei kutokana na athari za mfumuko wa bei.

**(l) Taarifa za Utekelezaji wa Miradi**

Kufuatia makubaliano kati ya Bunge, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi na Ofisi ya Waziri Mkuu-TAMISEMI na kwa mujibu wa barua yenye kumbukumbu Na.2/CA.26/215 ya tarehe 10/11/2010 kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu-TAMISEMI kwenda kwa Maafisa Masuuli, Halmashauri zinahitajika kuwasilisha taarifa za utekelezaji wa miradi pamoja na taarifa za fedha za mwaka kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu kabla ya au tarehe 30 Septemba, kila mwaka.

Ufuatiliaji wangu katika kujua uzingatiaji wa makubaliano ilibainika kuwa, kati ya Halmashauri 133, Halmashauri tano (5) hazikuwasilisha taarifa za utekelezaji miradi kinyume na maelekezo iliyotolewa na Ofisi ya Waziri Mkuu-TAMISEMI, Halmashauri kumi na tano (15) hazikuwasilisha taarifa za utekelezaji wa mradi ndani ya tarehe ya kisheria (kabla au 30 Septemba, 2011) na kuchelewa kwa kipindi cha kati ya siku 67-108. Pia Halmashauri kumi na tano (15) ziliwasilishwa taarifa za utekelezaji wa Mradi zisizokidhi viwango.

**(m) Mgawanyo wa mapato kati ya Halmashauri na Serikali za Vijiji/Mitaa**

Mgawanyo wa mapato kati ya Halmashauri na Vijiji/Mitaa ulikuwa duni kutokana na kwamba:

- Halmashauri nyingi hazikupeleka Vijijini au kwenye kata 20% ya kodi iliyofutwa kinyume na maelekezo ya Serikali. Ukaguzi wa Halmashauri 50 ulibainisha kuwa Halmashauri hizi hazikulipa Sh.1,556,830,464 kwa ajili ya mgao wa vijiji.
- Halmashauri nyingi hazikuzingatia matakwa ya kugawana mapato yanayotokana na vyanzo vyake na Vijiji/Mitaa.

**(n) Ukaguzi wa Bajeti**

- Kulikuwa na upungufu katika ruzuku iliyotolea na Serikali kuu. Katika baadhi ya vifungu vya bajeti Bunge liliidhinisha Sh.163,361,311,033 katika sampuli ya Halmashauri 18. Hata hivyo, ni Sh.130,326,225,146 tu ndizo zilizopokelewa na Halmashauri husika na kuacha upungufu wa Sh.33,035,085,889.
- Malipo yenye jumla ya Sh.444,367,001 yanayohusiana na Halmashauri 25 yalitakiwa kulipwa katika mwaka wa fedha 2009/2010, lakini yalilipwa katika mwaka wa fedha 2010/2011 kinyume na Agizo Na.46 ya Memoranda ya Fedha za Mamlaka ya Serikali za Mitaa ya mwaka1997.
- Ukaguzi wa bajeti iliyopitishwa pamoja na matumizi halisi ulionyesha kuwa, Halmashauri 18 zilikuwa zimetumia zaidi katika baadhi vifungu vya matumizi vyenye jumla ya Sh.24,880,254,344 ikilinganishwa na bajeti iliyopitishwa katika vifungu hivyo ya Sh.116,967,975,198.
- Matumizi yenye jumla ya Sh.4,673,316,247 yanayohusiana na Halmashauri 19 yalilipwa nje ya bajeti iliyopitishwa bila kuomba idhini yoyote kinyume na kifungu Na.10 (3) cha Sheria ya

Fedha za Serikali za Mitaa Na. 9 ya mwaka 1982 (iliyorekebishwa 2000).

**(o) Madeni Tarajiwa**

Halmashauri 10 zilikuwa na kesi mbalimbali zikisubiri uamuzi wa mahakama. Jumla ya Sh.5,852,750,556 zikiwa ni madeni tarajiwa zilionyeshwa katika taarifa za fedha kuhusiana na kesi hizo. Hata hivyo, ilibainika kwamba idadi watumishi wa idara ya sheria bado haitosherezi ili kuziwezesha Serikali za Mitaa kumudu kushughulikia masuala yote ya kisheria. Hali hii mara nyingine ilisababisha Serikali za Mitaa kutokuwa na wawakilishi katika mahakama wakati kesi ikiendelea. Serikali za Mitaa zinakabiliwa na hatari yakushindwa kesi mahakamani na kupata hasara zisizo za lazima. Hali hii inahitaji kuimarisha idara ya Sheria katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa.

**(p) Matokeo ya Ukaguzi Maalum**

Kuna masuala mengi yaliyojitokeza wakati wa ukaguzi maalum uliofanywa katika Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema, Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa, Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu, Halmashauri ya Wilaya ya Kilindi, Halmashauri ya Wilaya ya Moshi, Halmashauri ya Wilaya ya Monduli, Halmashauri ya Wilaya ya Longido na Halmashauri ya Maniapaa ya Ilala. Masuala hayo ni kama ifuatavyo:

- Hati za malipo za Sh.1,171,735,534 za Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu na Sh.31,245,700 za Halmashauri ya Wilaya ya Kilindi hazikuwasilishwa wakati wa ukaguzi kwa maana hiyo uhalisia wa matumizi ya fedha zilizotumika haukuweza kuthibitishwa.
- Kulikuwa na malipo ya fedha ya zuio iliyolipwa kimakosa mara mbili na Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa kwa mkandarasi kiasi cha Sh.11,796,685
- Baadhi ya wafanyakazi wa Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa walilipwa mishahara ya juu ya stahili

zao kwa jumla ya Sh.48,148,000 na kulikuwa na ulipwaji mishahara kwa wafanyakazi ambao si waajiriwa tena wa Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu jumla ya Sh.66,325,162.

- Katika Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu, kulikuwa na ubadhilifu wa fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo ya jumla ya Sh.551,3049,264 kupitia njia mbalimbali kama vile kughushi hundi, taarifa za benki za kughushi na benki kulipa kwa walipwaji wasiojulikana
- Nyaraka za mikataba za Sh.4,258,312,634 hazikuonekana katika mafaili husika ya mikataba wakati wa ukaguzi katika Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu.
- Kulikuwa na malipo yaliyolipwa zaidi ya Sh.4,846,715 kwa mkandarasi aliyehusika na ujenzi wa mabweni mawili na vyoo katika Shule ya Sekondari ya Nyampulikano.
- Kutokana na Ukaguzi uliofanyika tarehe 21/9/2011 na mapitio ya taarifa ya tarehe 5/10/2011 kutoka kwa mkandarasi aliyehusika na ujenzi wa skimu ya umwagiliaji ya Faru na Ndekombeka iliyoko Halmashauri ya Wilaya ya Moshi, mradi ulikuwa umefikia 49% sawa na Sh.8,303,030. Hata hivyo, Mkandarasi alikuwa amelipwa kiasi chote fedha kilichoko katika mkataba yaani Sh.17,000,000.
- Kulikuwa na makusanyo na malipo ambayo hayakuwa na viambatisho ya Sh.9,207,000 kwa mwaka 2005/2006 na Sh.10,029,880 kwa mwaka 2006/07 katika Halmashauri ya Wilaya ya Monduli
- Katika Halmashauri ya Wilaya ya Longido kulikuwa na jumla ya Sh.270,460,200 ambazo zilikuwa ni kodi ya ongezeko la thamani(VAT) zinazohusiana na mikataba mbalimbali ambazo wakandarasi hawakulipa kwenye Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA).

- Katika Halmashauri ya Wilaya ya Kilindi, aina ya Bati zilizotumika katika ujenzi wa jengo la Utawala la Halmashauri zenye thamani ya Sh.44,250,000 zilikuwa si sawa na zile zilizoainishwa katika mkataba.
- Halmashauri ya Wilaya ya Ilala ilishindwa kukusanya kiasi cha Sh.45,728,700 kilichokuwa kwenye bajeti. Hii ilitokana na Halmashauri kutokufatilia usahihi wa mifugo inayotoka kwenye mnada wa Pugu.

Masuala ya ulaghai na rushwa yanashughuliwa kwa mujibu wa Kifungu cha 27 cha Sheria Namba 11 ya Ukaguzi wa Umma ya 2008 kwa kuripoti katika vyombo vya kutekeleza sheria kwa ajili ya uchunguzi zaidi.

## 3. Muhtasari wa Mapendekezo

Mbali na mapendekezo ya kina yaliyotolewa kwa Uongozi wa Halmashauri kwa njia ya taarifa za ukaguzi, kwa mwaka huu wa fedha nina mapendekezo mbalimbali na muhtasari wake ni kama ifuatavyo:

### (i) Ufuatiliaji wa mapendekezo ya ukaguzi ya miaka ya nyuma

Kulikuwa na masuala muhimu yaliyo katika ripoti yangu ya ukaguzi ya mwaka uliopita ambayo aidha kwa sehemu yalitekelezwa au hayakutekelezwa kabisa kama ilivyoonyeshwa katika sura ya tatu (3) ya taarifa hii.

Serikali za Mitaa lazima ziongeze juhudi zaidi ili kuhakikisha mambo yaliyohojiwa katika miaka ya nyuma yanatekelezwa ili kuleta ufanisi katika utendaji wa Serikali za Mitaa.

### (ii) Usimamizi wa Mapato

Mamlaka ya Serikali za Mitaa zinapaswa kuhakikisha kuwa mapato yanakadiriwa vizuri, yanakusanywa kwa wakati na

kwa usahihi na yanaingizwa katika vitabu vya hesabu kwa usahihi. Pia, Halmashauri zihakikishe kuwa mikataba ya kukusanya mapato inasimamiwa vizuri ili kuongeza mapato ya Halmashauri na kuepuka mianya kwa mapato hayo kupotea au kufujwa kwa matumizi mabaya ya fedha za umma.

**(iii) Usimamizi wa Matumizi**

Maafisa Masuuli wanatakiwa kuhakikisha kwamba sheria zote zinazoongoza matumizi ya rasilimali za umma zinazingatiwa, hii ni pamoja na kuhakikisha kwamba rasilimali hizo zinatumika katika namna bora ya kukidhi malengo kwa ufanisi, kwa gharama nafuu na kwa uwazi. Wajibu huu ni pamoja na kuhakikisha Halmashauri inatunza nyaraka husika vizuri ikiwa ni pamoja na hati za malipo na viambatanisho vyake na pia ziwekwe katika hali ambayo ni rahisi kupatikana zikihitajika kwa ajili ya uhakiki.

**(iv) Usimamizi Wa Rasilimali Watu na Udhibiti wa Mishahara**

Rasilimali watu ni mali muhimu katika Halmashauri, kwa hiyo Maafisa Masuuli wa Serikali za Mitaa wanapaswa kuhakikisha kuwa swala la rasilimali watu linapewa umuhimu mkubwa ili kusaidia kufikia malengo ya Serikali za Mitaa.

Serikali za Mitaa kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI zinatakiwa kuhakikisha kuna mfumo endelevu wa ufuatiliaji wa viwango vya wafanyakazi na kuchukua hatua muafaka na kwa wakati kwa kujaza nafasi wazi ili kuboresha utoaji wa huduma katika sekta ya umma.

Maafisa Masuuli kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma wanatakiwa kuhakikisha kuwa taarifa za mishahara ya watumishi ni sahihi. Hili linaweza kufanyika kwa kuwahusisha Wakuu wa Idara kuthibitisha usahihi wa taarifa za mishahara na kuhuisha taarifa za watumishi. Usahihi wa

taarifa za mishahara utasaidia Serikali kuwa na bejeti sahihi za mishahara ya watumishi.

Tatizo la kukopa kupindukia kwa wafanyakazi wa Halmashauri bado ni sugu. Kukopa kupindukia si tu uvunjaji wa sheria halali lakini pia kunaondoa motisha kwa wafanyakazi kufanya kazi kwa ufanisi. Halmashauri lazima zipewe maelekezo ya kuhakikisha kwamba maombi yote ya mikopo yanapitishwa na Maafisa Masuuli na kwamba kila mwezi makato yasizidi 2/3 ya mshahara wa mfanyakazi kwa mwezi. Menejimenti zisaidie kuwa na utaratibu wa kuhakikisha kwamba wafanyakazi wana ufahamu kuhusiana na madhara ya kukopa kupita kiasi na hivyo kukiuka miongozo.

**(v) Kuzingatia Sheria ya Manunuzi**

Taasisi za umma zinazofanya manunuzi zinatakiwa kufuatilia na kutumia njia bora katika kufanya manunuzi ya vifaa, huduma na kazi ili kupata thamani ya fedha katika mchakato wa manunuzi.

Mamlaka ya Serikali za Mitaa kwa kushirikiana na PPRA na TAMISEMI wanapaswa kuendelea kufanya mafunzo ya mara kwa mara kwa wafanyakazi wa vitengo vya manunuzi (PMU), wajumbe wa Bodi za Zabuni za Halmashauri, Wakuu wa Idara, Maafisa wa Masuuli na Madiwani ili kuongeza maarifa yao kuhusu sheria ya manunuzi na majukumu waliyonayo katika kusimamia manunuzi ya umma.

**(vi) Kuboresha Mifumo ya Uhasibu na Udhibiti wa Ndani**

Udhaifu katika mifumo ya uhasibu na udhibiti wa ndani ni kati ya mambo yaliyoonekana wakati wa ukaguzi ambapo inaweza kuathiri uwezo wa uingizaji na utengenezaji wa taarifa za fedha. Kama juhudi za makusudi huzitachukuliwa inaweza kusababisha kukosekana kwa taarifa muhimu za fedha zinapohitajika. Baadhi ya masuala ya kuzingatiwa katika eneo hili ni pamoja na yafuatayo:

- **Kuimarisha Utayarishaji wa Taarifa za Fedha**
  Taarifa za fedha za Halmashauri ni sehemu muhimu ya uwajibikaji kwa ajili ya utoaji taarifa za rasilimali za Halmashauri. Malengo ya kutoa taarifa ni pamoja na kusaidia katika kuongoza na kutoa maamuzi na kuwezesha watumiaji wengine kama vile Bunge, vyombo vya fedha, wawekezaji, wafanyakazi, walipa kodi na Jumuiya za Kiraia kupata taarifa muhimu za Halmashauri.

  Idadi ya makosa katika rasimu ya taarifa za fedha zilizowasilishwa kwa ajili ya ukaguzi ilikuwa haikubaliki. Idadi ya makosa yaliyohitaji marekebisho katika hesabu hizo imeongezeka kwa kiasi kikubwa, marekebisho yaliyohitajika kwa kiasi kikubwa yameongeza wingi wa kazi zisizo za lazima kwa upande wa uongozi wa Halmashauri na pia timu za ukaguzi kuhusiana na taarifa za hesabu za mwaka wa fedha 2010/2011. Kwa hiyo, kuna haja ya kuboresha michakato yote inayohusiana na utayarishaji wa taarifa za fedha katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa.

- **Uhuru wa Vitengo vya Ukaguzi wa Ndani**
  Ukaguzi wa ndani ni chanzo muhimu cha ushauri ndani ya Halmashauri na lengo likiwa ni kushauri juu ya mambo yanayoweza kuathiri utekelezaji wa kazi za Halmashauri.

  Wakaguzi wa ndani wana jukumu muhimu katika kuchunguza na kushauri juu ya uimarishaji wa mifumo ya kusimamia masuala ya fedha na ambayo ni msingi katika utayarishaji wa taarifa za fedha zilizo sahihi. Ukaguzi wa ndani utaimarika kama kiutendaji wakaguzi wa ndani watakuwa huru toka katika mfumo wanao ukagua.

  Hivyo ili kuimarisha vitengo vya ukaguzi wa ndani, mfumo wa uwajibikaji upitiwe upya kwa kuwafanya

Wakaguzi wa ndani waweze kuwajibika kwa Mkurugenzi wa Halmashauri juu ya masuala ya Utawala na kwa Kamati ya Ukaguzi juu ya masuala ya kiukaguzi.

- **Mfumo wa Udhibiti wa Vihatarishi**

  Serikali za Mitaa zinahitajika kufuatilia mara kwa mara vihatarishi vinavyokabili mfumo wa usimamizi wa Serikali za Mitaa na utaratibu wa kutoa huduma kwa jamii yake. Halmashauri zikishirikiana na Kamati za ukaguzi zinatakiwa kuwa na ufahamu kwamba wakaguzi wa nje wanakagua juu ya umadhubuti wa udhibiti wa vihatarishi katika Halmashauri lakini hii haimanishi kwamba ukaguzi huu ni toshelevu na hivyo kuondoa jukumu la uongozi wa Halmashauri kufanya mapitio yake katika eneo linalohusiana na mfumo wa udhibiti wa vihatarishi.

  Halmashauri zinapaswa kuhakikisha kuwa zinakuwa na mipango ya udhibiti wa vihatarishi na taarifa kuhusiana na utekelezaji wa mipango hiyo zinaandaliwa mara kwa mara. Kutokana na kukosekana kwa mipango madhubuti, Halmashauri zinakuwa haziko katika nafasi nzuri ya kudhibiti athari ya vihatarishi vinapotokea na hivyo kuathiri utoaji wa huduma. Kamati za Ukaguzi ni muhimu kwani zina jukumu la kufuatilia na kutathmini shughuli za Halmashauri kuhusiana na udhibiti wa vihatarishi. Jukumu hili la Kamati za Ukaguzi linaweza kutekelezwa vizuri kwa kuwa na Ukaguzi wa ndani ulio madhubuti

- **Kamati za Ukaguzi**

  Katika utekelezaji wa IPSASs kuna mabadiliko muhimu katika utoaji wa taarifa za fedha. Kamati za Ukaguzi zipewe fursa ya kutosha katika kupitia taarifa za fedha zisizokaguliwa kabla ya kuwasilishwa kwa wakaguzi wa nje. Aidha, mafunzo yanapaswa kutolewa kwa wanakamati ili wawe na nafasi nzuri ya kutoa changamoto kwa uongozi wa Halmashauri ulioandaa

taarifa za fedha. Kuna haja ya kuboresha wigo na ufanisi wa Kamati za Ukaguzi na kuongeza uwazi zaidi katika majukumu waliopewa.

- Kwa ujumla, masuala haya ya udhibiti wa vihatarishi yanahitaji usimamizi makini kwa sababu yanaashiria hatari kubwa ambazo zinaweza kuzuia Serikali za Mitaa kufikia malengo yake.
- Halmashauri kwa kushirikiana na Idara ya Mkaguzi Mkuu wa Ndani na Ofisi ya Waziri Mkuu-TAMISEMI ni muhimu kuweka mpango thabiti wa kushughulikia maswala ya udhibiti wa ndani na mfumo wa utawala katika Halmashauri.

**(viii) Taarifa za Utekelezaji wa Miradi**

Taarifa za utekelezaji wa miradi ambazo zinaandaliwa kulingana na muundo unaohitajika na LAAC zinatakiwa ziwasilishwe Ofisi ya Ukaguzi kabla au tarehe 30 Septemba kila mwaka zikiwa pamoja na taarifa za fedha ya mwaka. Hii itawawezesha wakaguzi kufanya tathmini kuhusu taarifa za fedha zilizowasilishwa na taarifa nyingine kwa mwaka husika. Pia kutoa fursa kwa wakaguzi kukagua uwepo na thamani ya fedha kwa miradi mbalimbali iliyotolewa taarifa ya kutekelezwa.

**(ix) Matumizi ya Fedha za Maendeleo ya Mfuko wa Jimbo (CDCF)**

Mfuko wa Jimbo unatoa fursa kwa jamii husika kutekeleza miradi ya maendeleo katika majimbo yao kama miradi ya maji, elimu, afya na kilimo. Pia Mfuko wa Jimbo unatoa fursa kwa wananchi kuweza kuamua vipaumbele vya maendeleo ndani ya Jimbo na hivyo kutenga rasilimali ili kufikia malengo yaliyopangwa.

Halmashauri inapaswa kuwa makini ili kuhakikisha kwamba zinawajibika na kutumia fedha za Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo kwa mujibu wa Sheria Namba 16 ya Mfuko wa Jimbo ya mwaka 2009 na sheria zilizopo za kusimamia rasilimali za umma. Kwa majimbo ambayo

hayakutengeneza wala kuwasilisha taarifa za mapokezi na matumizi ya fedha hizo, OWM-TAMISEMI inashauriwa kusimamia ipasavyo utekelezaji wa Sheria ya Mfuko wa Jimbo kwa kuhakikisha kwamba hakuna fedha itakayotolewa kwa mwaka unaofuata kabla ya kuandaa taarifa ya mwaka uliotangulia kwa mujibu wa kifungu Na.7(3) cha Sheria ya Mfuko wa Jimbo ya 2009.

**(x) Uimarishaji wa Usimamizi wa Mradi**

Usimamizi wa miradi unahusisha uwepo wa miundombinu, michakato na vifaa ambavyo kwa pamoja hujulisha muda wa kufanya mradi, gharama za mradi na ubora na kisha kuhakikisha malengo hayo yanafikiwa.

Matokeo ya usimamizi wa miradi yanaonyesha kwamba usimamizi na utekelezaji wa miradi haukuwa mzuri kwani baadhi ya miradi yalitekelezwa katika viwango visivyostahili, pia kulikuwa na ucheleweshaji wa kukamilisha miradi ndani ya muda uliopangwa na vile vile baadhi ya miradi iliyokamilika haitumiki.

Kama kuna usimamizi duni wa miradi, gharama za ziada zinaweza kuongezeka katika utekelezaji wa miradi hiyo, hivyo:

- Uongozi wa Halmashauri unatakiwa kuimarisha Usimamizi na Tathmini (M & E), utaratibu ambao utahakikisha kwamba ufuatiliaji unaimarika na changamoto zilizobainika zinatatuliwa kwa haraka ili kuwepo na utekelezaji mzuri wa miradi iliyopangwa na matumizi mazuri ya miradi hiyo itakapokamilika kwa wakati muafaka.

- Taarifa juu ya fedha zilizopelekwa Serikali za Mitaa lazima itolewe Halmashauri na taasisi husika (mfano Hazina). Taarifa hii ipelekwe Halmashauri mara tu fedha hizo zinapotumwa. Taarifa hii lazima iwe na ufafanuzi wa wazi juu ya lengo la fedha zilizotumwa. Utoaji wa fedha zilizoidhinishwa kwa wakati, ni

muhimu ili kuhakikisha kwamba shughuli zilizopangwa zinatekelezwa kwa wakati muafaka.

**(xi) Haja ya kuwa na mwongozo sahihi juu ya uendeshaji wa akaunti sita (6) za Benki katika Halmashauri.**

Serikali imefanya uamuzi sahihi wa kupunguza idadi ya akaunti za benki za Serikali za Mitaa kutoka wastani wa akaunti 33 hadi 6 kwa kila Halmashauri. Inatarajiwa kwamba, hii itapunguza gharama za uendeshaji na kuimarisha usimamizi wa fedha ndani ya Serikali za Mitaa kwa:

(a) Kuwa na akaunti chache za benki zinazoweza kusimamiwa vizuri ikiwa ni pamoja na kufanya usuluhisho wa benki angalau mara moja kila mwezi.
(b) Kuondoa akaunti za benki ambazo zilikuwa hazifanyi kazi na hivyo kupunguza changamoto ya kuwa na fedha benki ambazo zilikuwa hazijafanyiwa kazi iliyokusudiwa.
(c) Kuondoa matumizi mabaya ya fedha za halmashauri ambazo zilikuwa zinakuwepo benki kwa muda mrefu bila kutekeleza kazi zilizokusudiwa.

Ili kuleta matokeo mazuri ya mabadiliko hayo, nina mapendekezo yafuatayo ambayo yanazingatia matarajio ya wadau wa Serikali za Mitaa:

- Kuna haja ya kuimarisha matumizi ya fedha kwa kuwa na daftari la kudhibiti matumizi ya fedha kwa kila kasma au mfumo wowote mwingine ambao utadhibiti na kuimarisha matumizi ya fedha ambapo miradi tofauti itatumia akaunti moja ya benki.
- OWM – TAMISEMI itengeneze mfumo thabiti wa namba wa kutambulisha kila kasma na ambao utaboresha otoaji wa kila taarifa inayohitajika kama taarifa za kila siku, kila wiki, kila mwezi, kila baada ya miezi mitatu na taarifa za mwaka.

- Jambo lingine la kuzingatia ni mabadiliko katika Mfumo Funganifu wa Usimamizi wa Fedha (IFMS). Mfumo huu unabadilika kutoka katika toleo la 7.35 na kwenda katika toleo la 9.05, hivyo ni muhimu katika kutekeleza matumizi ya akaunti 6 za benki, Halmashauri zikazingatia uwepo wa mfumo mpya (toleo la 9.05) ambao utaendeshwa na kudhibitiwa na OWM – TAMISEMI. Hii itasaidia kufanya kwa urahisi usuluhisho wa benki kwa fedha za kasma mbalimbali ambazo ziko katika akaunti moja ya benki.

## SURA YA KWANZA

## 1.0 UTANGULIZI WA MAMBO YA JUMLA

### 1.1 Mamlaka na Umuhimu wa Ukaguzi

#### 1.1.1 Mamlaka ya kufanya Ukaguzi

Ripoti hii imetolewa kwa mujibu wa Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Kifungu Na.45 cha Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa Na.9 ya mwaka 1982 (iliyorekebishwa 2000) pamoja na Kifungu Na.10 (1) cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na.11 ya mwaka 2008 ambavyo kisheria vinamtaka Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuwa ndiye Mkaguzi wa mapato na matumizi yote ya Serikali ikiwa ni pamoja na Mapato na Matumizi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Kwa mujibu wa Ibara ya 143 (2) (c) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anatakiwa kukagua na kutoa taarifa, angalau mara moja kila mwaka, juu ya ukaguzi wa hesabu za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, taarifa za fedha zilizoandaliwa na maafisa wote wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; taarifa za fedha za Mahakama zote za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na taarifa za fedha zinazotayarishwa na Katibu wa Bunge.

Kwa upande mwingine, kifungu 45 (1) cha Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa Na.9 ya mwaka 1982 (iliyorekebishwa 2000) kinabainisha kuwa Mkaguzi wa nje wa hesabu za Mamlaka za Serikali za Mitaa ni Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Pia Kifungu Na. 10(1) cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma ya mwaka 2008 kinampa mamlaka Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kukagua Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Zaidi ya hayo, kifungu cha 45 (5) cha Sheria Na.9 ya Fedha za Serikali za Mitaa ya mwaka 1982 (iliyorekebishwa 2000) kinampa mamlaka Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu kukagua fedha, uwekezaji au mali nyingine ambazo zinamilikiwa au zilizo chini ya udhibiti wa Halmashauri, kuwa na fursa kwa muda wowote ya kukagua hesabu, vitabu, hati za malipo na nyaraka zote zinazohusiana.

Aidha, kifungu cha 48 (1), (2) na (4) cha Sheria Namba 9 ya Fedha za Serikali za Mitaa ya mwaka 1982 kinamtaka Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuandaa na kusaini ripoti ya Ukaguzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa ambazo ni Mizania ya hesabu za mwaka na taarifa nyingine zinazohusiana nazo, ambapo nakala moja ya kila ripoti pamoja na mizania ya hesabu na taarifa nyingine zinazohusiana zitapelekwa kwa Waziri, Mkuu wa Mkoa na Mkurugenzi Mtendaji ambaye anatakiwa kuziwasilisha kwenye kikao cha Baraza la Madiwani.

Kifungu hicho pia kinamtaka Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kubainisha kila kifungu cha matumizi ambacho kimetumika bila kufuata Sheria

au kuidhinishwa na Mamlaka ya Serikali za Mitaa. Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu pia anapaswa kubainisha mapungufu au hasara ambayo imetokea aidha kwa uzembe au mtu yeyote kushindwa kutoa taarifa ya matumizi ya fedha alizokabidhiwa. Pia suala linguine ni kuthibitisha kiasi cha matumizi yaliyofanyika kinyume na sheria, matumizi yenye upungufu au hasara ambayo haijaoneshwa vitabuni.

Huu ni mwaka wa tatu ambapo taarifa za fedha za Mamlaka za Serikali za Mitaa zimetayarishwa kwa kuzingatia Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu kwa Sekta za Umma (IPSASs), pamoja na sehemu ya (iv) ya Sheria Na.9 ya Fedha za Mamlaka ya Serikali za Mitaa mwaka 1982 (iliyorekebishwa 2000) , na pia kulingana na Agizo Na.53 la Memoranda ya Fedha za Serikali za Mitaa ya mwaka, 1997 kama msingi wa utayarishaji wa taarifa za Fedha za Mamlaka za Serikali za Mitaa. Mamlaka za Serikali za Mitaa zilianza kutayarisha kwa mara ya kwanza Taarifa za fedha kwa kuzingatia viwango vya kimataifa vya uhasibu kwa Sekta ya Umma mwaka 2008/2009.

Seti kamili ya taarifa za hesabu zinazotayarishwa kwa kutumia viwango vya Kimataifa vya Uhasibu wa Sekta ya Umma ambayo inatakiwa kuwasilishwa kwa ajili ya ukaguzi inajumuisha:

(a) Taarifa ya Mizania ya hesabu
(b) Taarifa ya mapato na matumizi
(c) Taarifa kuhusu mabadiliko ya mtaji;
(d) Taarifa ya mtiririko wa fedha;
(e) Taarifa ya uwiano wa bajeti na kiasi halisi cha matumizi kama yalivyojitokeza;
(f) Taarifa ya uwiano wa bajeti na kiasi halisi cha matumizi kwa kila idara;
(g) Maelezo ya ziada yanayohusiana na taarifa za hesabu.

Kwa uwazi na uwajibikaji, Kifungu Na. 49 cha Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa Na.9 ya mwaka 1982 (iliyorekebishwa 2000) na kama ilivyosisitizwa kwenye Agizo Na. 90 la Memoranda ya Fedha za Serikali za Mitaa ya mwaka 1997, kila Mamlaka ya Serikali za Mitaa inatakiwa kutangaza katika Ofisi zake au kwa kadri itakavyoelekezwa na Mkuu wa Mkoa kutangaza taarifa zifuatazo katika eneo lake:

(i) Taarifa jumuifu ya Mizania ya hesabu na taarifa ya mapato na matumizi (muhtasari wa hesabu) zilizokaguliwa na

(ii) Ripoti yoyote inayohusu hesabu husika na kusainiwa na Mkaguzi katika kipindi cha miezi sita baada ya kufungwa kwa mahesabu ya mwaka au katika kipindi cha miezi sita baada ya kupata taarifa ya ukaguzi au kadri itakavyokuwa.

Nimeridhia kwa kufuatwa kwa msingi wa utaarishaji wa taarifa za Hesabu na kuchapishwa kwa hesabu na ripoti za ukaguzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa kuwa ni fursa nyingine kwa Mamlaka hizo kuongeza mawasiliano kwa upana zaidi na kuongeza uwajibikaji katika matumizi ya rasilimali za Umma.

### 1.1.2 Madhumuni ya ukaguzi

Lengo kuu la kufanya ukaguzi ni kumwezesha Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuwa na uhuru wa kutoa maoni ya ukaguzi kuhusiana na hesabu za Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2011 na kubainisha endapo kama zimetayarishwa kwa kuzingatia ubora unaotakiwa kulingana na misingi ya utayarishaji wa hesabu, ikiwa ni pamoja na:

| | |
|---|---|
| Uidhinishaji wa bajeti | •Kuhakikisha kuwa fedha zote zimepokelewa na kutumiwa kwa matumizi halali kama ilivyoidhinishwa na Bunge kwa kufuata Kanuni zinazosimamia matumizi ya fedha za Serikali kwa kuzingatia bajeti iliyopitishwa. |
| Uingizaji taarifa kwenye vitabu | •Kuhakikisha iwapo mapato yote yaliyokusanywa yameingizwa vema katika vitabu |
| Utunzaji nyaraka | •Kuhakikisha kuwa nyaraka zote muhimu, vitabu, regista, taarifa za fedha na taarifa mbalimbali zimetayarishwa vizuri zikionesha miamala yote na bakaa husika. |
| Uwasilishaji na utoaji taarifa | •Kuhakikisha kwamba vitu vyote muhimu vilivyo kwenye taarifa za fedha vinawasilishwa na kutolewa taarifa vizuri |
| Ufanisi katika udhibiti | •Kufanya tathmini na kupima mifumo mbali mbali katika Mamlaka za Serikali za Mitaa ili kubaini uimara na ubora wa Uthibiti wa Mfumo wa ndani ikiwa ni pamoja na uthibiti wa tekinologia ya mawasiliano. |
| Tathmini ya majanga | •Kutathmini hatari inayoweza kutokea kutokana na makosa ya kiukaguzi |
| Matokeo yanayotarajiwa | •Kuhakikisha kuwa malengo yaliyo tegemewa au mafanikio yamepatikana na kwamba malengo yaliyowekwa na Bunge au chombo kingine kilichoidhinishwa yamefikiwa |
| Kufuata sheria | •Kufanya tathmini ili kuona kama Mamlaka za Serikali za Mitaa zinafuata taratibu za manunuzi kama zilivyoelezwa katika Sheria ya Manunuzi ya Umma Na.21 ya mwaka 2004, pamoja na Kanuni zake za mwaka, 2005. |
| Utawala bora | •Kuhakikisha kuwa utawala bora umejengeka katika kufanikisha shughuli za kila siku za Halmashauri na katika kutekeleza malengo yote kwa ujumla na jinsi menejimenti inavyosimamia masuala ya kijamii na mazingira. |

## 1.2 Viwango na taratibu zinazotumika kutoa taarifa

### 1.2.1 Viwango vinavyotumika wakati wa Ukaguzi

Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ni mwanachama wa Shirika la Kimataifa la Asasi za Ukaguzi (INTOSAI) kwa kupitia Shirika la Afrika la Asasi Kuu za Ukaguzi - kwa nchi zinazozungumza lugha ya Kiingereza (AFROSAI-E) ambazo zinasaidiana katika kubadilishana mawazo na uzoefu kati ya nchi wanachama zinazozungumza lugha ya Kiingereza katika ukaguzi wa taasisi za Umma.

Ikiwa ni mwanachama wa Asasi hizo za kimataifa, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi inawajibika kutumia viwango vya ukaguzi vilivyotolewa na INTOSAI ambavyo ni viwango vya Shirika la Kimataifa la Asasi Kuu za Ukaguzi (ISSAI) na viwango vya Kimataifa vya Ukaguzi (ISA) vilivyotolewa na Shirikisho la Wahasibu la Kimataifa (IFAC) wakati wa ukaguzi wa Taarifa za Fedha za Mamlaka za Serikali za Mitaa.

### 1.2.2 Taratibu zinazotumika kutoa taarifa

Hatua mbalimbali zimechukuliwa ikiwa ni pamoja na kufanya mawasiliano na uongozi wa Halmashauri inayokaguliwa kabla ya kutoa ripoti hii ya mwaka. Kwa hiyo basi, ni vyema kubainisha hatua zote kwa watumiaji wa Ripoti hii ili waweze kufahamu juu ya ripoti hii ya mwaka na taratibu zinazotumika katika kukamilisha ripoti ya ukaguzi ya mwaka. Hatua hizo ni kama ifuatavyo:

1. Kutoa barua ya kuanza ukaguzi kwa mkaguliwa inayoeleza madhumuni na mawanda ya ukaguzi, na maeneo yanayotarajiwa kufanyiwa ukaguzi na kuelezea kazi na majukumu ya mkaguzi na uongozi wa Halmashauri inayokaguliwa.
2. Kuandaa mpango mkakati wa ukaguzi unaoonyesha mwelekeo mzima wa ukaguzi, vigezo vitakavyotumika katika hatua za mwanzo za kutathmini Halmashauri inayokaguliwa.
3. Kufanya kikao cha kwanza na uongozi wa Halmashauri inayokaguliwa kabla ya kuanza ukaguzi. Kikao hiki kinatoa nafasi ya kuueleza Uongozi madhumuni na malengo ya kufanya ukaguzi na kinampa nafasi mkaguliwa kuelezea maeneo ya ukaguzi.
4. Kuanza ukaguzi wa awali kwa kutathmini uthibiti wa ndani katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa husika na kujiridhisha kama inafanya kazi ipasavyo.
5. Kutoa ripoti kwa uongozi wa Halmashauri kwa kipindi cha kati inayoonesha matokeo ya ukaguzi ikiwa ni pamoja na hoja za ukaguzi na kutoa nafasi kwa uongozi wa mkaguliwa ili kuweza kujibu hoja hizo.
6. Kufanya ukaguzi wa taarifa za fedha kwa kujiridhisha kwamba zimeandaliwa kwa kufuata misingi ya utayarishaji wa taarifa za Hesabu za Mamlaka za Serikali za Mitaa.
7. Kufanya kikao cha mwisho na Uongozi wa Halmashauri inayokaguliwa baada ya kumaliza ukaguzi kwa kuwajulisha matokeo ya ukaguzi na kuwapa nafasi ya kutoa maoni yao kabla ya taarifa ya mwisho ya ukaguzi haijatolewa.
8. Kutoa taarifa ya mwisho ya ukaguzi kwa Uongozi wa Halmashauri inayokaguliwa kwa kuujulisha Uongozi wa Halmashauri iliyokaguliwa mambo yote yaliyojitokeza wakati wa ukaguzi na kutoa nafasi zaidi ya kuyashughulikia. Hatua hii pia ni ya msingi katika kutayarisha ripoti ya mwaka katika Mamlaka za Serikali za Mitaa.
9. Kuandaa ripoti kuu ya mwaka ya Mamlaka za Serikali za Mtaa na kuiwasilisha Bungeni kupitia kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mujibu wa Ibara ya 143(4) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

10. Kufuatilia matokeo ya ukaguzi yaliyotolewa katika ripoti kama ilivyoainishwa katika Kifungu Na.40 na Kifungu Na.10(1) cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma ya mwaka 2008 kwa kubainisha na kutoa taarifa kama kila Mkaguliwa ameandaa mkakati au ametekeleza mapendekezo yaliyotolewa katika ripoti pamoja na kuonesha hali ya utekelezaji wa mapendekezo ya Ukaguzi katika Ripoti ijayo ya Ukaguzi kama inavyotakiwa na Kifungu Na.40(4) cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma ya mwaka 2008.

Kwa kifupi mchoro ufuatao hapa chini unaonesha hatua zinazofuatwa wakati wa ukaguzi:




## 1.3 Idadi ya Halmashauri zinazokaguliwa na mpangilio wa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi

### 1.3.1 Idadi ya Halmashauri zinazokaguliwa

Katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2010/2011, kulikuwa na Mamlaka za Serikali za mitaa 134 katika Tanzania bara ambazo zilikaguliwa na kutolewa ripoti ya ukaguzi kwa kila Halmashauri husika. Mamlaka hizi za Serikali za Mitaa zina hadhi tofauti kuanzia Halmashauri za Wilaya hadi Halmashauri za jiji kama inavyoonekana katika jedwali hapa chini:

| Na. | Halmashauri | Jumla | Asilimia (%) |
|---|---|---|---|
| 1. | Halmashauri za Jiji | 4 | 3 |
| 2. | Halmashauri za Manispaa | 17 | 13 |
| 3. | Halmashauri za Miji | 7 | 5 |
| 4. | Halmashauri za Wilaya | 106 | 79 |
| | **Jumla** | **134** | **100** |

Takwimu zilizoonyeshwa hapo juu zinaweza kuonyeshwa kwa kutumia mchoro wa duara ulioonyeshwa hapa chini:




Mchoro duara uliopo hapo juu unaonesha kwamba, katika mwaka wa fedha 2010/2011 kulikuwa na Halmashauri za Wilaya 106 sawa na 79% ya Halmashauri zote, Halmashauri za Manispaa zilikuwa 13% ya Halmashauri zote wakati Halmashauri za Miji na Halmashauri za Majiji zilikuwa 5% na 3% ya Halmashauri zote.

Hata hivyo, katika mwaka ujao wa fedha, idadi ya Halmashauri zinatarajiwa kuongezeka na kufikia 162 baada ya uanzishwaji wa mikoa mipya minne na Halmashauri 19.

### 1.3.2 Mpangilio wa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi

Kuna jumla ya Halmashauri 134 ambazo zinakaguliwa na Ofisi 24 za Ukaguzi zilizopo mikoani kote Tanzania Bara. Kuna Wakaguzi 267 wanaokagua taarifa za fedha katika Mamlaka za Serikali za Mitaa na kufanya kuwa na wastani wa Wakaguzi 11 kwa kila Mkoa. Ofisi za Ukaguzi Mikoani zinaongozwa na Wakaguzi Wakazi ambao wanasimamiwa na Wakaguzi wa Kanda. Kwa madhumuni ya Ukaguzi unaofanyika katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa nchini, Ofisi hizo zimegawanywa katika Kanda tano. Ofisi za Kanda zinaongozwa za Wakaguzi wa Kanda ambao wanasimamiwa na Msaidizi wa Mkaguzi Mkuu wa Hesabu Divisheni ya Mikoa. Kwa mujibu wa Muundo wa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi , Msaidizi wa Mkaguzi Mkuu wa Hesabu Divisheni ya Mikoa anawajibika moja kwa moja kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kama inavyoonekana katika Sehemu ya Muundo wa Ofisi hapa chini:

**MUUNDO WA OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI KWA MAMLAKA YA SERIKALI ZA MITAA**




## 1.4 Majukumu ya kisheria ya Mamlaka za Serikali za mitaa katika kuandaa Taarifa za Fedha

Uongozi wa kila Halmashauri ina wajibu wa kuandaa na kuonesha kwa usahihi taarifa za fedha kwa kufuata udhibiti wa ndani ambao uongozi umejiwekea katika kuandaa taarifa za fedha ambazo hazina dosari kutokana na udanganyifu au makosa mengine.

Kifungu cha 40(1) cha Sheria ya Fedha za Mamlaka ya Serikali za Mitaa Na.9 ya mwaka 1982 (Iliyorekebishwa 2000) imeainisha kuwa kila Mamlaka ya Serikali za Mitaa ina wajibu wa kutunza vitabu vya hesabu na kumbukumbu zinazohusu:

(a) Mapato na matumizi za fedha na miamala mingine ya fedha za Mamlaka.

(b) Mali na Madeni za Mamlaka, na kutayarisha mizania kila mwaka wa fedha, inayoonesha maelezo ya mapato na matumizi ya mamlaka, mali na madeni yake yote.”

Kifungu kilichotajwa hapo juu kimehuishwa na Agizo Na.9 mpaka 16 la Memoranda ya Fedha ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa, 1997 inayotaka

Halmashauri kuanzisha na kusimamia udhibiti wa ndani wa shughuli za Halmashauri. Kwa nyongeza, Agizo Na.53 inazipa majukumu uongozi wa Halmashauri kuandaa taarifa za fedha kwa kuzingatia Sheria, Kanuni, miongozo inayotolewa na Waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa, Memoranda ya Fedha ya Serikali za Mitaa na kuzingatia Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu kwa Sekta ya Umma (IPSASs).

Pamoja na majukumu ya uaandaaji wa taarifa za hesabu, Kifungu cha 49 cha Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa Na. 9 ya 1982 (Iliyorekebishwa 2000) na Agizo Na.90 la Memoranda ya Fedha ya Serikali za Mitaa, 1997 inaitaka kila Mamlaka ya Serikali ya mtaa kuchapisha taarifa za fedha zilizokaguliwa ndani ya maeneo yao ya uwajibikaji.

## 1.5 Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha

Agizo Na. 82 na 88 la Memoranda ya Fedha za Serikali za Mitaa, 1997 na Kifungu 45(4) cha Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa Na.9 ya mwaka 1982 (iliyorekebishwa, 2000) inamtaka kila Afisa Masuuli kuandaa taarifa za mwisho za Hesabu na kuziwasilisha kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu kwa ajili ya ukaguzi tarehe 30 Septemba au kabla ya tarehe hiyo kila mwaka.

Katika mwaka husika wa ukaguzi ulioishia tarehe 30 Juni, 2011, Mamlaka zote za Serikali za Mitaa ziliweza kuwasilisha taarifa za Mahesabu yao katika muda iliokubalika kisheria tarehe 30 Septemba na wengine kabla ya tarehe hiyo.

Hata hivyo, wakati wa ukaguzi wa taarifa hizo za fedha imebainika kwamba kuna baadhi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa ziliwasilisha taarifa za fedha zikiwa na makosa makubwa na kutooneshwa kabisa kwa mambo mengine muhimu. Taarifa hizo za fedha ziliwasilishwa tu kwa lengo la kutimiza wajibu wa kisheria wa kuwasilisha taarifa za fedha kwa wakati kwa ajili ya ukaguzi.

Mamlaka za Serikali za Mitaa zipatazo sitini (60) ziliwasilisha taarifa za fedha zikiwa na makosa mbalimbali ikwa ni pamoja na kuonyesha tarakimu katika mahesabu ambazo ni zaidi au pungufu ikilinganishwa na tarakimu zilizotakiwa kuonyeshwa katika taarifa hizo za fedha. Kwa ujumla taarifa hizo zilizowasilishwa awali zilionyesha jumla ya kiasi cha Sh.187,064,788,252 pungufu ya kiasi ambacho kilitakiwa kuonyeshwa sawa na 16% ya matumizi yote na kiasi cha Sh.118,967,438,529 kilionyeshwa zaidi ambacho ni sawa na 10% ya matumizi yote ya fedha kama inavyoonyeshwa katika jedwali hapo chini. Orodha kamili ya Mamlaka za Serikali za Mitaa ambazo taarifa zake za fedha zilionyesha tarakimu zaidi au pungufu imeonyeshwa katika **Kiambatisho (i).**

| Maelezo | Kiasi kilichooneshwa pungufu (Sh.) | Kiasi kilichooneshwa zaidi (Sh.) |
|---|---|---|
| Jumla ya matumizi | 1,191,182,477,501 | 1,191,182,477,501 |
| Jumla ya makosa | 187,064,788,251 | 118,967,438,529 |
| **Asilimia (%)** | **16** | **10** |

Taarifa hiyo hapo juu inaonyeshwa pia katika Chati Mhimili ifuatayo:




Kutokana na Chati Mhimili hapo juu, inatafsiriwa kwamba, katika mwaka husika matumizi ya jumla katika Halmashauri sitini (60) yalikuwa ni Sh.1,191.2 bilioni kati ya hayo matumizi ya kiasi cha Sh.187.1 bilioni yalionyeshwa pungufu na kiasi cha Sh.119 bilioni yalionyeshwa zaidi.

Kwa kuzingatia makosa, mambo yaliyoachwa kuonyeshwa na mapungufu mengine ambayo yalipelekea mahesabu kuonyeshwa zaidi au pungufu, Mamlaka za Serikali za Mitaa husika zilirejeshewa taarifa za fedha zilizowasilishwa awali kwa minajili ya kuzifanyia marekebisho na baadaye ziliwasilishwa tena kwa ajili ya ukaguzi.

Idadi ya Halmashauri zilizoreshewa taarifa za fedha za awali na kuziwasilisha tena baada ya kufanya marekebisho zimeongezeka kutoka Halmashauri 44 mwaka wa fedha uliopita (2009/2010) hadi 60 katika mwaka husika (2010/2011). Mwelekeo wa taarifa za fedha zilizorekebishwa kwa kipindi cha miaka minne mfululizo ni kama ufuatao:

| Mwaka wa fedha | Idadi ya Halmashauri zilizokaguliwa | Idadi ya Halmashauri zilizoleta taarifa za fedha zilizorekebishwa | % |
|---|---|---|---|
| 2007/08 | 133 | 15 | 11 |
| 2008/09 | 133 | 24 | 18 |
| 2009/10 | 134 | 44 | 33 |
| 2010/11 | 133 | 60 | 45 |

Mchanganuo huo hapo juu unaonekana pia katika chati Mhimili kama ifuatavyo:




Mwelekeo wa taarifa za fedha zilizorekebishwa kwa kipindi cha miaka minne mfululizo hapo juu unaonyesha kuwa kuna ongezeko kubwa la Halmashauri ambazo zilirejeshewa taarifa za hesabu zilizowasilishwa awali na kuzifanyia marekebisho na baadaye kuziwasilisha tena kwa ajili ya ukaguzi. Hali hiyo imejitokeza kwa sababu ya kutokuwepo kwa mafunzo ya kutosha kwa watumishi ili waweze kuandaa hesabu kwa kutumia Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu kwa Sekta ya Umma (IPSASs) na uhamisho wa watumishi ambao wamebobea kwenye kuandaa taarifa kwa kufuata IPSASs.

Idadi kubwa ya makosa na marekebisho yaliyofanywa kwenye taarifa za fedha zilizowasilishwa kwa ajili ya ukaguzi na masuala ya uhasibu yanayohusiana nayo yanaashiria kutakiwa kuwepo kwa jitihada za dhati katika kuhakikisha taarifa zinazoletwa kwa ukaguzi zinakuwa sahihi na zinazoonyesha mambo yote yanayotakiwa.

Ninapendekeza kuwa, katika miaka ijayo, Mamlaka za Serikali za Mitaa zinatakiwa zianzishe mchakato wa uhakiki na udhibiti wa ubora kwa ajili ya maandalizi ya taarifa za fedha ili kuhakikisha usahihi wa taarifa hizo kabla hazijawasilishwa kwa ajili ya ukaguzi. Kwa kuongezea, OWM-TAMISEMI inatakiwa kuandaa mafunzo ya mara kwa mara katika kujenga uwezo wa watumishi wanaoandaa taarifa za fedha.

# SURA YA PILI

## 2.0 MAANA, AINA, VIGEZO NA MWELEKEO WA HATI ZA UKAGUZI

### 2.1 Hati za Ukaguzi

Katika kutekeleza matakwa ya Kisheria, ninawajibika kutoa uhakika kwa wadau wa Halmashauri kwamba taarifa za fedha zilizotayarishwa na Halmashauri zinatoa picha halisi ya matokeo ya shughuli zilizofanyika, mtiririko wa fedha pia mali na madeni ya Halmashauri kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2011. Maoni ya ukaguzi yanatolewa kwa wadau kama uhakikisho wa usahihi wa taarifa za fedha za Halmashauri pamoja na uzingatiaji wa taratibu zinazotakiwa.

### 2.2 Maana ya Hati za Ukaguzi

Hati ya ukaguzi ni maoni ya mkaguzi yanayoeleza kama taarifa za fedha zilizokaguliwa zimetayarishwa katika mambo yote muhimu, kwa mujibu wa misingi inayotumika katika uandaaji wa tarifa hizo. Hati ya ukaguzi pia inazungumzia kama taarifa za fedha zilizowasilishwa zina maelezo ya kutosha katika kuelezea vizuri na kwa upana zaidi tarifa hizo.

### 2.3 Aina ya Hati za ukaguzi

Kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Ukaguzi (ISA) na Viwango vya Shirika la Kimataifa la Asasi Kuu za Ukaguzi (ISSAIs), zifuatazo ni aina za Hati za Ukaguzi ambazo zimetolewa kama kipimo katika utayarishaji wa taarifa za fedha:

#### 2.3.1 Hati inayoridhisha

Hati ya aina hii inatolewa wakati nimeridhika kuwa, taarifa za fedha za Mamlaka za Serikali za Mitaa zimetayarishwa kulingana misingi ya utaarishaji wa taarifa za fedha za Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Hata hivyo, utoaji wa hati inayoridhisha haina maana kwamba Halmashauri ina mfumo safi kabisa wa udhibiti wa ndani. Hati hii ina maana kwamba hakuna jambo lolote nililoliona ambalo lingesababisha kutolewa kwa hati yenye shaka. Kila Halmashauri iliyopata aina hii ya hati imeandikiwa taarifa nyingine ya ukaguzi kwa ajili ya menejimenti inayoeleza masuala ambayo yasipoangaliwa, yanaweza kuisababishia Halmashauri kupata hati yenye shaka miaka ijayo.

#### 2.3.2 Hati inayoridhisha na yenye masuala ya msisitizo

Masuala ya msisitizo na masuala mengine yanawekwa kama mawasiliano ya ziada kupitia katika ripoti ambayo Mkaguzi anaona inafaa:

(a) Kuvuta dhamira ya watumiaji wa hesabu zilizoandaliwa katika suala au masuala yaliyoonyeshwa ndani ya taarifa za fedha, kwamba ni muhimu na ya msingi kwa watumiaji katika kuelewa taarifa za fedha.

(b) Kuvuta dhamira ya watumiaji wa hesabu katika suala au masuala yale yaliyo onyeshwa kwenye taarifa za hesabu ambayo ni muhimu kwa ajili ya kuuelewa vizuri ukaguzi, majukumu ya wakaguzi au ripoti ya ukaguzi.

### 2.3.2.1 Masuala yenye msisitizo

Katika baadhi ya mazingira, nimejumuisha aya inayohusu masuala yenye msisitizo ili kuweka bayana masuala ambayo hata kama yameoneshwa vema katika taarifa za fedha, kwa mtizamo wangu, yana umuhimu na ya msingi kwa watumiaji wa taarifa za fedha. Nyongeza ya aya ya masuala hayo yenye msisitizo hakuathiri maoni ya ukaguzi. Aya ya masuala yenye msisitizo inajumuishwa pale panapokuwa na mazingira yafuatayo:

- Kuweka angalizo juu ya mambo yanayoweza kuwa na athari ambapo ufumbuzi wake unategemea mambo ya baadaye yasiyo moja kwa moja ndani ya uwezo wa taasisi yenyewe na ambayo yanaweza kuleta athari katika taarifa za fedha, kwa mfano matokeo ya baadae yasiyo ya kawaida yanayohitaji kushughulikiwa mahakamani au kisheria.
- Kuweka angalizo juu ya mambo mengineyo yaliyoonyeshwa katika ripoti ya ukaguzi wa mwaka ambayo kuyafanyia marekebisho ni muhimu lakini Mkaguliwa amekataa kufanya marekebisho.
- Kuweka angalizo katika masuala yanayoathiri taarifa za fedha yaliyoonyeshwa katika taarifa za fedha ambayo ni muhimu kuleta karibu uelewa wa taarifa za hesabu kama vile janga kubwa lililotokea au linaendelea kutokea na kuleta madhara makubwa ya hali ya kifedha katika taasisi.

### 2.3.2.2 Masuala mengine

Aya ya masuala mengine inahusu mambo ambayo hayakuonyeshwa katika taarifa za fedha na kwamba kwa mtazamo wa mkaguzi ni muhimu mtumiaji wa taarifa za fedha kuelewa ukaguzi, majukumu ya mkaguzi na ripoti ya mkaguzi.

Endapo nitaona inafaa kuwasilisha masuala mengine kuliko yale yaliyoonyeshwa katika taarifa za hesabu, nitatumia aya ya masuala mengine kwa masuala hayo yenye kichwa cha masuala mengine, ambayo itakuwa baada ya aya ya hati ya ukaguzi na masuala yenye msisitizo kama yapo. Haya masuala mengine yapo katika sehemu tofauti ya ripoti ya mwaka ya ukaguzi ili kutenganisha wazi wazi kutoka katika majukumu ya mkaguzi, na hati ya ukaguzi juu ya taarifa za fedha na masuala mengine yaliyokuwa na angalizo katika aya zilizotangulia za msisitizo wa masuala. Mifano ya masuala mengine ni pamoja na kutofuata sheria na udhaifu katika udhibiti wa ndani.

### 2.3.3 Hati yenye shaka

Hati yenye shaka inatolewa iwapo ninaridhika kuwa, taarifa za fedha hazikuonyesha usahihi, kutokukubaliana na uongozi au kukwazwa kwa mawanda ambapo athari yake ni kubwa lakini si muhimu na kwamba ukiacha athari zilizopelekea kutoa hati yenye shaka, taarifa za hesabu zimetengenezwa

kulingana na misingi ya utaarishaji wa taarifa za fedha za Mamlaka za Serikali za Mitaa hivyo hazihitaji kutolewa hati isiyoridhisha.

Kwa maana nyingine Hati yenye shaka inatolewa endapo kuna kutoelewana na Uongozi katika sehemu moja au zaidi ya taarifa za fedha lakini makosa hayo hayaathiri eneo lililosalia la taarifa za fedha na halisababishi taarifa za fedha kwa ujumla kuonekana zina makosa.

### 2.3.4 Hati isiyoridhisha

Hati isiyoridhisha inatolewa pale ninapothibitisha kwamba, taarifa za fedha hazikutengenezwa kwa kufuata misingi ya inayokubalika ya utayarishaji wa taarifa za fedha au viwango vya uhasibu ambapo, kunakuwa na kiasi kikubwa cha kutokukubaliana na menejimenti na kuna madhara makubwa kwenye taarifa za hesabu kwa aidha kutofuata taratibu za fedha zilizowekwa au taarifa za hesabu zilizowasilishwa hazina maelezo ya kutosha ambayo yanawezesha taarifa za fedha kuelezekaka vizuri na kwa upana zaidi.

Kwa maana nyingine, aina hii ya Hati inatolewa kama nikiona kuwa taarifa za fedha zilizowasilishwa kwa ajili ya ukaguzi kama zimeonekana zimekosewa kwa kiwango kikubwa na zimetayarishwa bila kufuata misingi wa utayarishaji wa taarifa za Hesabu za Mamlaka za Serikali za Mitaa. Kwa ujumla, aina hii ya hati inatolewa wakati kumekuwa na mapungufu makubwa katika taarifa za fedha kiasi kwamba zinapotosha kabisa ukweli wa taarifa hizo.

### 2.3.5 Hati mbaya

Hati mbaya hutolewa wakati ninaposhindwa kupata uthibitisho wa ukaguzi wa kutosha na hivyo kushindwa kutoa maoni juu ya taarifa za fedha zilizowasilishwa. Hali hiyo inaathiri kwa kiasi kikubwa taarifa za hesabu kiasi ambacho ninashindwa kutoa maoni yangu juu ya hesabu husika. Endapo taarifa za fedha zitakuwa na mapungufu makubwa, sitaweza kutoa maoni yangu juu ya taarifa zilizowasilishwa.

Hati hii ya ukaguzi inatolewa endapo kumekuwa na mambo ambayo si rahisi kwangu kupata taarifa na nyaraka ambazo zimetumika kuandaa taarifa za fedha.

Kwa maana hiyo, hati mbaya inatolewa katika taarifa za fedha ambazo uwezekano wa kufanya ukaguzi umeshindikana ili kubaini kama kuna mapungufu yoyote au kubaini kwamba utayarishaji wa taarifa za fedha umefuata msingi wa utayarishaji wa taarifa za Hesabu za Mamlaka za Serikali za Mitaa.

### 2.3.6 Vigezo au mambo yanayopelekea kutoa hati yenye mashaka

Vifuatavyo ni vigezo au mambo ambayo yanaweza kumuwezesha Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kutoa hati yenye mashaka:

(a) Kukwazwa kwa mawanda ya Ukaguzi kwa kushindwa kupata taarifa na nyaraka za kutosha wakati wa ukaguzi.

(b) Mambo ambayo yanaendana na kutokufuata sheria:

- Utayarishaji wa taarifa za fedha ambao haukufuata misingi ya utayarishaji wa taarifa za Hesabu za Mamlaka za Serikali za Mitaa.
- Uingizaji wa taarifa katika vitabu vya fedha ambao haujafuata taratibu zinazostahili.
- Taarifa muhimu na za msingi zinazoathiri vitabu vya fedha na hivyo kusababisha kupata hati yenye mashaka.

## 2.4 Mchanganuo wa Hati za Ukaguzi katika Halmashauri

### 2.4.1 Mchanganuo wa ujumla wa hati za ukaguzi zilizotolewa katika Mamlaka za Serikali za Mitaa

Sehemu hii ya ripoti inaonyesha mwelekeo wa hati za ukaguzi zilizotolewa kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa mwaka 2007/2008, 2008/2009 2009/2010 na 2010/2011. Umuhimu wa taarifa hii ni kuonyesha mwelekeo wa hali ya utendaji na uwajibikaji katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa kipindi cha miaka minne. Orodha ya Mamlaka za Serikali za Mitaa na Hati za ukaguzi zilizopata kwa miaka minne imeonyeshwa katika **Kiambatisho (ii).**

Mchanganuo wa ujumla wa hati za ukaguzi zilizotolewa katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa miaka ya fedha 2007/2008,2008/2009,2009/2010 na 2010/2011 ni kama inavyoonekana katika jedwali lifuatalo.

| | Hati inayoridhisha | | Hati yenye shaka | | Hati isiyoridhisha | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Miaka** | **Jumla** | **%** | **Jumla** | **%** | **Jumla** | **%** | **Jumla ya Halmashauri** |
| **2007/08** | 72 | 54 | 61 | 46 | 0 | 0 | **133** |
| **2008/09** | 77 | 58 | 55 | 41 | 1 | 1 | **133** |
| **2009/10** | 66 | 49 | 64 | 48 | 4 | 3 | **134** |
| **2010/11** | 72 | 54 | 56 | 42 | 5 | 4 | **133** |

Mchanganuo wa Hati za ukaguzi ulioonyeshwa hapo juu umeonyeshwa pia katika grafu zifuatazo:




Kutokana grafu hapo juu, Hati zinazoridhisha zimeongezeka kwa asilimia nne (4%) kuanzia mwaka 2007/08 hadi 2008/09, zimepungua kwa asilimia tisa (9%) kuanzia mwaka 2008/09 hadi 2009/10 na kuongezeka kwa asilimia tano (5%) kuanzia mwaka 2009/2010 hadi 2010/2011.

Hati zenye mashaka zimepungua kwa asilimia tano (5%) kuanzia mwaka 2007/2008 hadi 2008/2009, zimeongezeka kwa asilimia saba (7%) kuanzia mwaka 2008/2009 hadi 2009/2010 na zimepungua kwa asilimia sita (6%) kuanzia mwaka 2009/2010 hadi 2010/2011.

Hati mbaya zimeongezeka kwa asilimia moja (1%) kuanzia mwaka 2007/08 hadi 2008/09, zimeongezeka kwa 2% kuanzia mwaka 2008/2009 hadi 2009/2010 na pia zimeongezeka kwa asilimia moja (1%) kuanzia mwaka 2009/2010 hadi 2010/2011.

### 2.4.2 Mchanganuo wa kipekee wa Hati za ukaguzi zilizotolewa kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa

Kutokana na mchanganuo wa hati za ukaguzi zilizotolewa katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa miaka minne, yafuatayo yamebainika:

i) Halmashauri kumi na moja (11) zimeendelea kuwa na hadhi ya kupata Hati zinazoridhisha kwa miaka minne. Orodha ya Halmashauri husika ni kama inavyonekana hapo chini:

| Na. | Halmashauri |
|---|---|
| 1 | H/W Kisarawe |
| 2 | H/W Mufindi |
| 3 | H/W Biharamulo |
| 4 | H/W Missenyi |
| 5 | H/W Siha |
| 6 | H/W Nachingwea |

| | |
|---|---|
| 7 | H/W Serengeti |
| 8 | H/W Kyela |
| 9 | H/M Shinyanga |
| 10 | H/W Maswa |
| 11 | H/W Singida |

ii) Halmashauri thelathini na sita (36) zimefanya vizuri ikilinganishwa na miaka ya nyuma ambapo zilipata Hati zenye mashaka na Hati isiyoridhisha na kwa mwaka huu wa fedha zimepata Hati zinazoridhisha. Orodha ya Halmashauri husika na Hati za ukaguzi zilizopata ni kama inavyonekana katika **Kiambatisho (iii).**

ii) Halmashauri kumi na moja (11) zimeendelea kupata Hati zenye mashaka kwa miaka mine mfululizo. Orodha ya Halmashauri husika ni kama inavyonekana hapo chini:

| Na. | Halmashauri |
|---|---|
| 1 | H/W Mvomero |
| 2 | H/W Kilosa |
| 3 | H/W Morogoro |
| 4 | H/W Monduli |
| 5 | H/W Ngorongoro |
| 6 | H/W Longido |
| 7 | H/W Makete |
| 8 | H/W Moshi |
| 9 | Jiji la Mwanza |
| 10 | H/W Namtumbo |
| 11 | H/Mji Korogwe |

iii) Halmashauri ishirini na tisa (29) ambazo zimeshuka ikilinganishwa na miaka ya nyuma ambapo zilipata Hati zinazoridhisha lakini katika ukaguzi wa mwaka husika zimeweza kupata Hati zenye mashaka na Hati zisizoridhisha. Orodha ya Halmashauri husika na Hati za ukaguzi zilizopata ni kama inavyonekana katika **Kiambatisho (iv).**

## 2.5 Orodha ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa zilizopata Hati zenye mashaka na Hati isiyoridhisha na sababu zilizopelekea kupata hati hizo

Katika mwaka husika wa ukaguzi, kulikuwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa zipatazo hamsini na sita (56) zilizopata Hati zenye Shaka na Mamlaka za Serikali zipatazo tano (5) zilizopata Hati isiyoridhisha. Mchanganuo wa mambo ambayo yalikuwa ni vigezo katika kutoa Hati isiyoridhisha na Hati yenye mashaka kwa

Mamlaka ya Serikali za Mitaa husika ni kama inavyoonekana katika **Kiambatisho (v).**

Kutokana na **Kiambatisho (v),** sampuli ya mambo yaliyokuwa ni kigezo cha kutoa Hati zenye mashaka na Hati zisizoridhisha kama yafuatayo:

- Mishahara iliyolipwa kwa watumishi ambao wamestaafu, kufariki, kuachishwa kazi, watoro na watumishi waliohamishiwa utumishi wao sehemu nyingine malipo haya yalifanyika kupitia kwenye akaunti zao binafsi za benki, Serikali haikunufaika kutokana na malipo ya jinsi hii.
- Mapitio ya hati za malipo na vyeti vya malipo kwa ajili ya ujenzi iligundulika kuwa, kulikuwa na ulipwaji zaidi kwa wakandarasi uliofanywa bila kuambatanisha vyeti vya malipo ya ujenzi.
- Halmashauri inamiliki 100% ya hisa katika kampuni ambapo haikutengeneza taarifa za fedha za fedha jumuifu ikiwa kama taasisi miliki ya hisa hizo.
- Kulikuwa na kutoonyeshwa kwa uwekezaji katika taarifa za fedha za Halmashauri ambako kulipelekea kuonyeshwa pungufu kwa thamani ya mali za Halmashauri.
- Hati za malipo pamoja na viambatanisho vyake havikupatikana kwenye makabrasha yake na hivyo kudhibiti mawanda ya ukaguzi.
- Baadhi ya hati za malipo hazikuwa na viambatanisho vya kutosha na hivyo kufanya ukaguzi kushindwa kuthibitisha uhalali wa malipo hayo.
- Kulikuwa na upotoshwaji na kutoonyeshwa kwa mali, madeni, mapato na matumizi ambayo hayaonyeshi ukweli na hali halisi ya taarifa za fedha zilizowasilishwa.
- Kutotayarishwa kwa majedwali ya viambatanisho na taarifa za ziada za taarifa za fedha kulikosababisha kutokamilika kwa kumbukumbu zinazohusiana na taarifa za fedha zilizowasilishwa.
- Idadi kubwa ya vitabu vya kukusanyia mapato havikuwasilishwa kwa ajili ya ukaguzi, hivyo kiasi cha mapato yaliyokusanywa kwa kutumia vitabu hivyo hayakuweza kuthibitika.
- Vifungu vya matumizi vililipiwa kimakosa kwenye vifungu vingine na hivyo kupotosha taarifa za fedha zilizoletwa.
- Malipo hayakuthibitishwa kupokelewa na walipwaji. Hakuna ushahidi wa mapokezi ya fedha hizo hivyo kudhibiti mawanda ya ukaguzi.
- Halmashauri zilifanya malipo ambayo hazikunufaika nayo na hivyo kufanya matumizi ambayo hayana manufaa kwa Serikali.

  Mapungufu yote yaliyoainishwa hapo juu yalisababishwa kwa kiasi kikubwa na sababu zifuatazo:

  - Mafunzo ya kutosha hayatolewi kwa ajili ya kuandaa taarifa za fedha kwa kutumia Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu kwa Sekta ya Umma.
  - Kuwepo kwa watumishi wa Halmashauri wanaokiukamaadili ya kazi zao na kujihusisha na ubadhilifu wa fedha za Halmashauri.
  - Kuna udhaifu katika mifumo ya udhibiti wa ndani kwaujumla katika Halmashauri.

- Kula njama baina ya watumishi wa Halmashauri na watumishi wa benki katika kufuja fedha za Halmashauri, inashauriwa kwamba likiwa ni jambo la haraka, OWM-TAMISEMI iandae miongozo sahihi ikijumuisha mwongozo wa uandaaji wa taarifa za fedha zinazoendana na mfumo wa IPSASs.

Pia, ninapendekeza kuwa, katika miaka ijayo, Halmashauri zinatakiwa zianzishe utaratibu wa kupitiwa kwa taarifa za fedha zilizoandaliwa na Wataalam wengine wa fani ya uhasibu na kuwe na ratiba kwa ajili ya kuandaa taarifa za fedha ili kusaidia uwepo wa usahihi wa rasimu kabla ya taarifa ya mwisho haijawasilishwa kwa ajili ya ukaguzi. Wakuu wa Idara wanatakiwa kushirikishwa kikamilifu kwa kutoa taarifa ambazo zinahitajika wakati wa utayarishaji wa taarifa za fedha.

Kwa kuongezea, uongozi wa Halmashauri unatakiwa kuchukua hatua zinazostahili kwa wafanyakazi wanaojihusisha na ubadhilifu na vile vile kuimarisha mfumo wa udhibiti wa ndani ili kuepukana na udhaifu unaojirudia.

## SURA YA TATU

## 3.0 UFUATILIAJI WA UTEKELEZAJI WA MAPENDEKEZO YA UKAGUZI KWA MIAKA ILIYOPITA

Sehemu hii inajumuisha ufuatiliaji wa utekelezaji wa mapendekezo ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) katika ripoti za miaka ya nyuma na muhtasari wa masuala yasiyo na tarakimu (qualitative) na yale yenye tarakimu (quantitative) ambayo yalionekana katika taarifa za ukaguzi za mwaka na taarifa za ukaguzi maalum ambayo ama hayakutekelezwa au yalitekelezwa kwa sehemu. Pia sehemu hii inajumuisha ufuatiliaji wa utekelezaji wa maagizo yaliyotolewa na Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC) kwa Halmashauri husika. Sura hii inamalizia na ufuatiliaji wa mapendekezo yaliyomo katika ripoti ya mwaka ya LAAC iliyopitishwa na Bunge.

### 3.1 Ufuatiliaji wa utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi kwa miaka iliyopita katika Ripoti ya jumla ya Ukaguzi

Kifungu 40 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na.11 ya mwaka 2008 kinatoa mwongozo juu ya kutoa majibu na/au mpango wa utekelezaji wa ripoti ya kila mwaka ya ukaguzi. Zaidi ya hayo, Kifungu 40 (4) kinamtaka Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu
za Serikali kujumuisha hali ya utekelezaji wa mpango kazi katika ripoti ya ukaguzi wa mwaka ujao. Aya hii inaonesha hali ya utekelezaji wa mapendekezo ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali juu ya taarifa za fedha za Mamlaka ya Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha 2009/10.

Kwa mujibu wa Kifungu Na. 40(2) cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma, 2008, Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG) anapaswa kupokea majibu kutoka kwa Maafisa Masuuli na baada ya hapo kuwasilisha kwa Waziri ambaye atapeleka mbele ya Bunge. Pia, Mlipaji Mkuu anawajibika kuwasilisha nakala jumuifu ya majibu na mpango wa utekelezaji kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Majibu juu ya masuala yaliyoibuliwa katika ukaguzi wa mwaka wa fedha uliomalizika Juni 30, 2010 yalitolewa na Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG) kwa barua yenye Kumb. Na. EB/AG/485/01/Vol.III/31 ya tarehe 28 Juni, 2011. Ningependa kutoa shukrani zangu za dhati kwa juhudi zinazofanywa na Serikali kupitia Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG) na Maafisa Masuuli wote kwa ajili ya kujibu masuala yaliyotolewa juu ya taarifa za ukaguzi na hatua zilizochukuliwa juu ya mapendekezo yaliyomo katika taarifa hiyo.

Hata hivyo, mapendekezo mengi katika ripoti ya mwaka ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa ajili ya Serikali za Mitaa kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2011 hayakushughulikiwa katika majibu yaliyowasilishwa. Masuala yaliyosalia ni pamoja na yafuatayo:

**(i) Ukosefu wa mwongozo kwa ajili ya Mfumo wa Udhibiti wa Ndani**

Kwa miaka kadhaa sasa, nimekuwa nikitoa mapendekezo juu ya udhaifu ulioonekana katika mifumo ya udhibiti wa ndani wa Halmashauri mbalimbali. Udhaifu huu ni pamoja na yale yanayohusiana na mfumo wa Teknolojia ya Habari, ukosefu wa mpango endelevu na mipango ya kujikinga na majanga na kutumia Mfumo funganifu wa usimamizi wa fedha/Epicor kwa kiwango kidogo au kutoutumia kabisa.

Nilipendekeza kwamba OWM-TAMISEMI inapaswa kuja na muundo sahihi wa udhibiti wa ndani ili kusaidia Halmashauri katika kuweka kumbukumbu za udhibiti wa ndani katika Halmashauri kwa ajili ya mafanikio ya malengo yao.

Hii ni pamoja na mwongozo wa ujumla katika maandalizi ya teknolojia ya habari, mfumo wa usimamizi wa majanga, mkataba wa utendaji wa kamati ya Ukaguzi, mkataba wa utendaji wa ukaguzi wa ndani na miongozo mingine muhimu katika kujenga mfumo madhubuti wa udhibiti wa ndani katika Halmashauri.

**(ii) Utofauti wa ripoti za fedha na kupitwa na wakati kwa Sheria za Serikali za Mitaa**

Ilitolewa taarifa kwamba, kumekuwa na utofauti wa taarifa za fedha zinazoandaliwa na uongozi wa Halmashauri kwa ajili ya kuwasilishwa kwa wadau mbalimbali na kwa madhumuni mbalimbali. Hii inatokea kwa sababu ya kutokuwepo kwa ushiriki na usimamizi wa kutosha wa uongozi wa Halmashauri katika uandaaji wa taarifa za fedha.

Pia ilibainika kuwa, miongozo iliyopo ambayo ni Mwongozo wa Uandaaji Hesabu za Serikali za Mitaa wa mwaka 1993 na Memoranda ya Fedha ya Mamlaka za Serikali za Mitaa, 1997 imepitwa na wakati na haina msaada katika kutoa ushauri wa kuridhisha unaoendana na misingi ya Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu kwa Sekta ya Umma. Miongozo hii miwili pamoja na mfumo mzima wa kisheria unaoongoza uendeshaji wa Serikali za Mitaa unatakiwa kuboreshwa kwa haraka.

Ilipendekezwa kwamba miongozo iliyopo ambayo ni Mwongozo wa Uandaaji Hesabu za Serikali za Mitaa wa mwaka 1993 na Memoranda ya Fedha ya Mamlaka za Serikali za Mitaa, 1997 inatakiwa kuboreshwa kwa haraka ili kuendana na Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu kwa Sekta ya Umma.

Pia Halmashauri ziandae taarifa za fedha za mwezi na robo mwaka ikiwa ni pamoja na leja kuu, Urari, taarifa za fedha, taarifa ya mapato na matumizi, taarifa ya mtiririko wa fedha, taarifa ya mlinganisho wa bajeti na matumizi na taarifa ya matumizi ya miradi ya maendeleo na ugharimiaji. Vile vile Uongozi wa Halmashauri unapaswa kutambua na kufahamu wajibu wa pamoja katika

kuandaa taarifa za fedha za Halmashauri na pia kuwapa mafunzo watumishi wanaohusika na uandaaji wa taarifa za fedha.

**(iii) Kutoandaliwa kwa Taarifa za Fedha na Ukaguzi wa Hesabu za Vijiji**

Ilitolewa taarifa kuwa usimamizi wa fedha zilizohamishiwa na zilizokusanywa katika ngazi ya chini ya serikali hasa katika Vijiji kwa kiwango kikubwa utunzaji wa vitabu vya fedha katika ngazi hizo si mzuri. Halmashauri ambazo zina wajibu wa kuanzisha mfumo wa usimamizi wa fedha kulingana na kifungu Na. 45 (3) cha Sheria za Fedha za Serikali za Mitaa ya mwaka 1982 hazitimizi wajibu wao inavyopaswa. Ilibainika katika matukio mbali mbali kuwa fedha zilizopelekwa katika ngazi za chini za serikali, taarifa za fedha hizo hazikutunzwa vema. Utunzaji mbovu wa taarifa za fedha katika ngazi ya Vijiji unavunja moyo wananchi kuchangia katika miradi ya maendeleo hivyo kucheleweshautekelezaji wa miradi ya maendeleo katika ngazi hiyo ya chini ya Serikali.

Katika suala hili, ilipendekezwa kwamba Uongozi wa Halmashauri unapaswa kuchukua jukumu la kuongoza kuhakikisha kuwa masharti ya Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa Na.9 ya mwaka 1982 yanazingatiwa. Hii ni pamoja na kuhakikisha kuwa uongozi wa kijiji husika unandaa taarifa za fedha na Halmashauri iwatumie ipasavyo wakaguzi wa ndani kwa ajili ya kufuatilia maandalizi ya taarifa hizo. Utaratibu huu unatarajiwa kuimarisha usimamizi katika ngazi ya Vijiji na kuboresha utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika ngazi ya chini ya Serikali (Vijiji na kata).

**(iv) Kujenga uwezo kwa uongozi wa ngazi za chini za Serikali**

Katika ripoti ya ukaguzi ya mwaka uliopita ilibainika kuwa viongozi wa Vijiji hawana mbinu za msingi na uelewa kwa ajili ya kusimamia miradi inayotekelezwa katika ngazi ya vijiji. Ukosefu wa uwezo imekuwa moja ya sababu kuu ya kutokufikia lengo la miradi, hivyo kuikosesha jamii husika kupata huduma iliyokusudiwa.

Ilipendekezwa kwamba Uongozi wa Halmashauri unapaswa kuanzisha mpango wa mafunzo ambayo yatasaidia viongozi wa Vijiji na Kamati za usimamizi wa Miradi ya Maendeleo kusimamia vizuri utekelezaji wa miradi ya maendeleo na wakati huo huo kuhakikisha kwamba kuna udhibiti sahihi juu ya ukusanyaji na matumizi ya mali za umma. Mpango wa mafunzo haya unaweza pia kusaidia kujenga uwezo wa Madiwani katika kusimamia rasilimali za Halmashauri.

**(v) Udhaifu ulioonekana wakati wa kaguzi maalum**

Katika kaguzi maalum zilizofanywa kwa mwaka uliopita wa ukaguzi, Niliripoti udhaifu katika udhibiti wa ndani hasa katika usimamizi wa mikataba na manunuzi. Pia nilibaini matukio mbalimbali yenye sura ya udanganyifu na rushwa katika usimamizi wa usimamizi wa mikataba na manunuzi.

Ilipendekezwa kwamba, pamoja na uimarishaji wa mfumo wa udhibiti wa ndani kama kipimo cha kurekebisha mapungufu yaliyoonekana katika ukaguzi wa kawaida na kaguzi maalum, Halmashauri zinashauriwa kuimarisha mfumo wa manunuzi katika kila Halmashauri husika. Hii inajumuisha utayarishaji wa taarifa za manunuzi kwa mujibu wa sheria, Halmashauri kutumia huduma zinazotolewa na Wakala wa Manunuzi wa Serikali (GPSA) ambao wana jukumu la kupanga na kusimamia manunuzi ya bidhaa za kawaida na huduma za manunuzi kupitia mfumo wa makubaliano.

**(vi) Fedha za Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo (CDCF)**

Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo ulianzishwa Julai mwaka 2009 kwa ajili ya miradi ya maendeleo katika kila Jimbo la uchaguzi.

Ilibainika kuwa, fedha za CDCF kwa mwaka wa ukaguzi uliopita hazikutumika kama ilivyokusudiwa. Katika baadhi ya Halmashauri, ukaguzi uligundua kuwa fedha hizo hazikutumika kabisa. Sababu zilizopelekea ni pamoja na kutofunguliwa kwa akaunti maalum katika baadhi ya Halmashauri, pia fedha zilitolewa mwisho wa mwaka wa fedha yaani kati ya mwezi Mei na Juni 2010.

Nilihitimisha kwa kusema kwamba lengo la kuwa na mfuko huu katika mwaka wa fedha wa 2009/10 halikutimia kikamilifu.

Katika maeneo machache ambapo fedha zilitumika, Halmashauri hazikuwa zikiandaa na kuwasilisha kwa Waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa rekodi ya kiasi kilichopokelewa na kutumika kwa kila Kamati ya Maendeleo ya Jimbo. Hii ni kinyume na matakwa ya kifungu na. 7 (3) cha sheria ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo, 2009.

Ilipendekezwa kwamba Halmashauri zinashauriwa kuhakikisha kuwa mfumo wa uwajibikaji unatekelezwa kwa mujibu wa Sheria Na.16 ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo ya mwaka 2009 na sheria zilizopo sasa kwa ajili ya kusimamia mali za umma.

Pia, kwa kutokutayarisha na kuwasilisha taarifa za mapokezi na matumizi ya fedha hizo, OWM-TAMISEMI inashauriwa kusimamia ipasavyo utekelezaji wa sheria ya Mfuko wa Jimbo kwa kuhakikisha kwamba hakuna matumizi yatakayofanyika kwa mwaka unaofuata kabla ya kuandaa taarifa ya mwaka uliotangulia, kuwasilisha tarifa hiyo na kuhakikisha kwamba imekubaliwa.

**(vii) Ucheleweshaji wa ukamilishaji wa miradi na miradi iliyokamilika ambayo haitumiki**

Ilitolewa taarifa kuwa, baadhi ya miradi ya ujenzi ilikuwa bado haijakamilika na idadi nyingine ya miradi ya ujenzi katika baadhi ya Halmashauri ilikamilika lakini ilikuwa haitumiki. Sababu zikiwa ni pamoja na ukosefu wa michango ya jamii hasa pale ambapo michango ya fedha taslimu na nguvu za wananchi zilihitajika, ukosefu wa wafanyakazi wa afya kwa ajili ya vituo vya

afya/zahanati zilizokamilika na ukosefu wa huduma kama vile maji. Katika matukio yote, thamani ya fedha iliyowekezwa haikuweza kufikiwa.

Yalitolewa mapendekezo kuwa, Uongozi wa Halmashauri uimarishe ufuatiliaji na tathmini ya mara kwa mara ambayo itahakikisha kwamba ufuatiliaji unaimarishwa na changamoto zinatatuliwa haraka kwa ajili ya utekelezaji wa miradi iliyopangwa. Pia Halmashauri zihakikishe kwamba mara tu baada ya miradi kukamilika itumike kutoa huduma zilizokusudiwa.

Pia ilishauriwa kuwa, wanasiasa wote katika ngazi zote waongeze mchango wao wa uhamasishaji katika kuhakikisha jamii inashiriki kikamilifu katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika maeneo yao. Hii si tu kuhakikisha kukamilika kwa miradi lakini pia kuwezesha jamii kujenga utamaduni wa kujitegemea.

**(viii) Uwajibikaji usioridhisha katika mfuko wa LGDG na NMSF**

Ilitolewa taarifa kuwa baadhi ya tofauti ambazo zilibainika wakati wa ukaguzi wa Ruzuku ya Maendeleo ya Serikali za Mitaa (LGDG) na fedha kwa ajili ya shughuli za Mkakati wa Kitaifa wa Kudhibiti UKIMWI (NMSF). Ukaguzi ulibaini kuwa kuna tofauti kati ya kiasi kilichotajwa kupokelewa katika ngazi ya Halmashauri na kiasi kilichorekodiwa kwamba kimelipwa kwa Halmashauri kwa mujibu wa hesabu za Mpango wa Maboresho wa Serikali za Mitaa (LGRP) chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu-TAMISEMI.

Tofauti hizo zilitokana na ukosefu wa mawasiliano sahihi, usimamizi na ufuatiliaji wa fedha zinazohamishiwa katika Halmashauri. Aidha, Halmashauri hazipati taarifa ya kutumiwa fedha katika akaunti zao za benki kwa wakati sahihi ili kuweza kujua kiasi walichotumiwa na madhumuni ya fedha hizo

Ilipendekezwa kwamba, taarifa juu ya fedha zilizopelekwa katika Mamlaka za Serikali za Mitaa lazima itolewe kwa Halmashauri mara tu pesa hizo zinapopelekwa. Taarifa hii lazima iwe na ufafanuzi wa wazi juu ya lengo la fedha zilizotumwa. Utoaji wa fedha zilizoidhinishwa kwa wakati, ni muhimu ili kuhakikisha kwamba shughuli zilizopangwa zinatekelezwa kwa wakati muafaka.

**(ix) Haja ya kuimarisha uratibu na usimamizi wa majukumu ya Sekretarieti ya Mikoa**

Eneo lililobainika kwa na udhaifu ni katika usimamizi wa fedha za Serikali za Mitaa. Msisitizo zaidi unawekwa kwa Ofisi ya Waziri Mkuu-TAMISEMI kuhakikisha hatua stahiki zinachukuliwa dhidi ya maofisa ambao ni wabadhilifu au ambao wameshindwa kusimamia vizuri rasilimali za Serikali za Mitaa. Hatua zitakazochukuliwa zitasaidia kuimarisha utamaduni wa nidhamu ya fedha ndani ya Halmashauri.

Ilipendekezwa kwamba, ili kuwa na matokeo yanayotarajiwa katika Serikali za Mitaa, Serikali inatakiwa kuimarisha uratibu na majukumu ya usimamizi wa

Makatibu Tawala wa Mikoa. Hii ni pamoja na kuhakikisha kwamba, Sekretarieti za mikoa zinakuwa na uwezo unaotakiwa katika suala la kuwezesha ukuaji, kuinua maendeleo na kuzisimamia Serikali za Mitaa na utambuzi wa malengo na shabaha ya Serikali za Mitaa kwa kuhusisha malengo ya maendeleo ya taifa.

**(x) Ukopaji uliokithiri kwa watumishi wa Halmashauri ambao haukudhibitiwa na uongozi**

Nilitolea taarifa udhaifu katika usimamizi wa kukopa ili kuhakikisha ustawi wa wafanyakazi unalindwa. Wakati wa ukaguzi wa mishahara, ilibainika kuwa idadi kubwa ya wafanyakazi wa Halmashauri wanalipwa mishahara yao ya kila mwezi chini ya 1/3 ya stahili zao kinyume na Waraka wa Utumishi wenye Kumb. Na.CCE.45/271/01/87 wa tarehe 19/03/2009 ambao unataka makato ya mishahara ya wafanyakazi yasizidi 2/3 ya mishahara yao. Zaidi ilibainika kuwa baadhi ya wafanyakazi walikuwa hawalipwi chochote (mshahara ulikuwa sifuri).

Nilipendekeza kwamba, Uongozi wa Halmashauri upewe maelekezo kuwa kila maombi ya mkopo ni lazima yapitishwe kwa Afisa Masuuli. Pia uongozi wa Halmashauri uwe na usimamizi na utaratibu wa kuhakikisha kwamba elimu inatolewa miongoni mwa wafanyakazi ili waelewe kwamba hairuhusiwi.

Kwa muhtasari, hali ya utekelezaji wa mapendekezo iliyotolewa inaweza kuonyeshwa katika jedwali hapa chini:

| Na. | Kiwango cha Utekelezaji | Idadi ya mapendekezo | Asilimia |
|---|---|---|---|
| 1 | Yaliyotekelezwa | 1 | 8 |
| 2 | Yaliyo katika hatua ya utekelezaji | 1 | 8 |
| 3 | Yasiyo tekelezwa | 10 | 84 |
| **Jumla** | | **12** | **100** |

Utekelezaji wa mapendekezo yaliyotolewa katika mwaka wa fedha 2009/2010, yanaweza kutolewa katika chati kama ifuatavyo:




Kutokana na chati mduara hapo juu unaonyesha wazi kwamba, majibu yaliyotolewa hayaridhishi, hii inatokana na kutokuwa na juhudi katika kuweka mikakati ya kutekeleza mapendekezo yaliyotolewa kwa lengo la kuboresha usimamizi wa fedha za umma kwenye Halmashauri. Majibu yaliyotolewa hayajaonyesha jitihaja za dhati za Serikali katika kutekeleza kikamilifu na kutatua mafungufu yaliyojitokeza. Mapendekezo mengi bado hayajatekelezwa na machache yapo katika hatua za utekelezaji. Ni maoni yangu kwamba, Serikali ichukue hatua madhubuti ili kuhakikisha kwamba mapendekezo yote yaliyotolewa miaka ya nyuma yanatekelezwa ipasavyo kwa ajili ya utendaji bora na uwajibikaji wa Mamlaka za Serikali za Mitaa.

## 3.2 Ufuatiliaji wa utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi kwa miaka iliyopita katika Ripoti ya kila Halmashauri

Madhumuni ya mapendekezo ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) yaliyotolewa kwa Mamlaka ya Serikali za Mitaa kuziwezesha Serikali za Mitaa husika ni kurekebisha mapungufu yaliyojitokeza wakati wa ukaguzi wa taarifa za fedha na mara moja kutekeleza mapendekezo yaliyotolewa ili kuboresha udhibiti wa ndani na usimamizi wa rasilimali za Halmashauri.

Katika mwaka wa ukaguzi uliopita, mapendekezo mbalimbali yaliyotokana na hoja za ukaguzi yalitolewa, mapendekezo hayo yalihitaji uongozi wa Serikali za Mitaa kuchukua hatua madhubuti za utekelezaji ili kuboresha utendaji na uwajibikaji wa Halmashauri. Baadhi ya Serikali za Mitaa zimefanya jitihada za kutekeleza mapendekezo ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Kati ya Hamashauri 133, Halmashauri 130 hazikutekeleza mapendekezo ya ukaguzi ya miaka ya nyuma yenye jumla ya Sh.105,263,165,967, katika kiasi hicho, Halmashauri ya Kishapu ilikuwa na mapendekezo yasiyotekelezwa yenye

kiasi kikubwa cha Sh.5,354,805,097, ikifuatiwa na Misungwi Sh.5,080,403,320, na Halmashauri ya Rugwe ambayo ilikuwa na mapendekezo yasiyotekelezwa yenye kiasi kidogo cha fedha Sh.1,020,000.

Hulka au tabia ya kutotekeleza mapendekezo ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali inapelekea kujirudia kwa hoja ambazo zimetolewa na wakaguzi kwa miaka ya nyuma. Hii inaashiria kuwepo kwa mapungufu katika uwajibikaji kwa uongozi wa Halmashauri husika.

Jedwali hapo chini linaonyesha kwa muhtasari hoja za ukaguzi ambazo hazijajibiwa katika kaguzi za miaka iliyopita kuanzia mwaka 2006/2007, 2007/2008, 2008/2009 na 2009/2010 kama ifuatavyo:

| Mwaka wa fedha | Hoja za ukaguzi ambazo hazijajibiwa (Sh.) | Idadi ya Halmashauri husika |
|---|---|---|
| 2006/07 | 32,903,395,306 | 112 |
| 2007/08 | 53,463,558,647 | 126 |
| 2008/09 | 122,128,377,615 | 129 |
| 2009/10 | 105,263,165,967 | 130 |

Mwelekeo wa masuala yasiyotekelezwa ni kama inavyooneshwa katika chati mstari ifuatayo:




Chati mstari hapo juu inaonyesha kwamba, jumla ya mapendekezo ya miaka ya nyuma ambayo hayakutekelezwa kwa mwaka 2007/2008 yalikuwa Sh.32.9 bilioni yakihusisha Halmashauri 112. Katika mwaka wa fedha 2008/2009 idadi ya Halmashauri ambazo hazikutekeleza mapendekezo ya ukaguzi ziliongezeka kutoka 112 hadi 126 zikiwa na jumla ya kiasi cha Sh.53.5 bilioni na kusababisha

ongezeko la Sh.20.6 bilioni. Pia katika mwaka wa fedha 2009/2010 idadi ya Halmashauri ambazo hazikutekeleza mapendekezo ya ukaguzi ziliongezeka kutoka 126 hadi 129 zikiwa na jumla ya kiasi cha Sh.122.1 bilioni na kusababisha ongezeko la Sh.68.7 bilioni. Zaidi katika mwaka wa fedha 2010/2011 idadi ya Halmashauri zimeongezeka kutoka 129 hadi kufikia 130 zikiwa na jumla ya kiasi cha Sh.105.2 bilioni na kusababisha kupungua mapendekezo ambayo hayajatekelezwa kwa Sh.16.8 bilioni.

Mwenendo hapo juu unaonyesha kwamba, Uongozi wa Serikali za Mitaa haukuchukua hatua madhubuti katika kushughulikia mapendekezo ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Muhsatari wa Mamlaka za Serikali za Mitaa zilizokuwa na hoja za ukaguzi ambazo hazijajibiwa ni kama inavyoonekana katika **Kiambatisho (vi).**

## 3.3 Ufuatiliaji wa utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi katika Ripoti za Kaguzi Maalum

Kifungu 36 (1) cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na.11 ya mwaka 2008 kinampa mamlaka Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kufanya kaguzi maalumu. Sheria hii inaeleza kuwa, iwapo Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ataona kuwa kuna jambo lolote lihusulo fedha au mali ya umma ambalo inabidi Bunge lijulishwe pasipo kuchelewa, ataandaa taarifa maalumu kuhusiana na jambo hilo na kuwasilisha taarifa hiyo Bungeni kupitia kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Katika mwaka wa ukaguzi uliopita, mapendekezo mbalimbali yaliyotokana na hoja za ukaguzi maalum yalitolewa, mapendekezo hayo yalihitaji uongozi wa Serikali za Mitaa kuchukua hatua madhubuti za utekelezaji ili kuboresha utendaji na uwajibikaji wa Halmashauri.

Orodha ya Halmashauri zilizo na hoja za ukaguzi ambazo hazijajibiwa ni kama inavyoonekana katika **Kiambatisho (vii)**

Jedwali hapa chini linaonyesha mapendekezo ya kaguzi maalum ambayo hayajatekelezwa kwa miaka mitatu kuanzia mwaka 2008/2009, 2009/2010 na 2010/2011.

| Mwaka wa fedha | Hoja za ukaguzi ambazo hazikujibiwa (Sh.) | Hoja za ukaguzi zilizosalia ambazo hazikuthaminishwa (Idadi ya Halmashauri) | Idadi ya Halmashauri |
|---|---|---|---|
| 2008/09 | 2,533,956,821 | 11 | 7 |
| 2009/10 | 44,415,697,227 | 43 | 11 |
| 2010/11 | 27,615,658,694 | 69 | 19 |

## 3.4 Ufuatiliaji wa utekelezaji wa mapendekezo ya Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC)

Sehemu hii inajumuisha ufuatiliaji wa utekelezaji wa mapendekezo ya Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC) yaliyotolewa katika ripoti ya Kamati ya Mwaka kama inavyohitajika katika Kifungu Na. 40(3) cha Sheria ya Ukaguzi wa Hesabu za Umma 2008.

Kifungu hicho kinamtaka Mlipaji Mkuu wa Serikali kuandaa majibu na mpango wa utekelezaji wa ripoti ya CAG yakizingatia udhaifu uliobainika na mapendekezo yaliyotolewa na Kamati ya Usimamizi.

Mwenyekiti wa LAAC aliwasilisha ripoti ya Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC) ikijumuisha mapendekezo juu ya Hesabu za Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2009. Ripoti hii iliwasilishwa Bungeni tarehe 4 Aprili 2011. Katika kuandaa majibu na mpango wa utekelezaji wa ripoti ya ukaguzi juu ya taarifa za fedha kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2010, Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG) hakuzingatia mapendekezo ya LAAC. Muhtasari wa mapendekezo ya LAAC yasiyojibiwa ni kama ifuatavyo:

### (a) Mshahara Kwa Watumishi hewa

Kuhusu Suala la mishahara kwa watumishi hewa Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa ilipendekeza kuwa, Serikali inapaswa kuwa na mpango sahihi utakaohakikisha kwamba mishahara yote iliyolipwa kwa watumishi hewa (Sh. Mil. 792.9) ikiwa ni pamoja na mishahara ambayo haikurejeshwa Wizara ya Fedha (Sh. Bil. 1.7) inarejeshwa.

Pia Kamati ilipendekeza kwamba Serikali itafute ufumbuzi wa kudumu juu ya malipo ya mishahara kwa watumishi hewa.

### (b) Udhaifu katika Mifumo ya Udhibiti wa Ndani

Kamati ilibaini kwamba, suala la udhaifu katika mifumo ya ndani lina uhusiano wa moja kwa moja na suala la kulipa mishahara kwa watumishi hewa pamoja na bei za kughushi katika manunuzi ya vipuri na mafuta ya magari.

Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa ilipendekeza kwamba Serikali ichukue hatua za makusudi za kuimarisha udhibiti wa mifumo ya ndani ya Halmashauri. Hii pia ni pamoja na kuimarisha kitengo cha ukaguzi wa ndani ili watende kazi kwa uhuru bila kuwa na vikwazo kutoka kwa Wakurugenzi Watendaji.

### (c) Usimamizi Mbovu wa Miradi ya Maendeleo

Miradi inayotekelezwa katika Serikali za Mitaa pia husimamiwa na Wakuu wa Idara wa mradi husika. Hivyo Kamati ilipendekeza kwamba, Maafisa Masuhuli pamoja na Wakuu wa Idara wote wahusike kikamilifu katika kusimamia utekelezaji wa miradi ya maendeleo iliyochini yao.

Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa ilipendekeza kuanzishwa kwa ukaguzi wa kijamii ili kuhakikisha kuwa uwazi na uwajibikajii unakuwepo. Hili pia litaimarisha utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Kamati ilipendekeza kwamba, kitengo cha Ukaguzi wa Serikali za Mitaa ambacho kipo chini ya OWM-TAMISEMI kiimarishwe ili kiweze kuwa na mifumo mizuri zaidi katika kupata habari za utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo katika Halmashauri.

Kamati pia ilipendekeza kuwa, kitengo cha Ukaguzi wa Ufanisi katika Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kiimarishwe kwa kuongezewa watumishi (idadi ya wataalam), pia kiongeze wigo na kasi zaidi ya ukaguzi ili kuzifikia Halmashauri nyingi katika ukaguzi wake.

Pia Kamati ilipendekeza kuwa, Madiwani hasa Kamati za Fedha, Mipango na Utawala zijengewe uwezo wa kusimamia miradi ya maendeleo inayotekelezwa na Halmashauri.

**(d) Kutozingatiwa kwa Sheria na taratibu za Manunuzi ya Umma**

Kamati ilipendekeza kwamba, Uongozi wa Serikali za Mitaa uzingatie Sheria na taratibu za Manunuzi ya Umma kama zinavyoelezwa katika Sheria za Manunuzi ya Umma za mwaka 2004 na Kanuni zake za mwaka 2005. Serikali inatakiwa kutumia ripoti zinazotolewa na Mamlaka ya Udhibiti wa Manunuzi ya Umma katika kufuata taratibu za manunuzi ya kila siku. Pia wakaguzi wa ndani wajielekeze zaidi katika kuangalia taratibu na uhalali wa manunuzi yanayofanyika katika Halmashauri zao.

**(e) Gharama za kughushi katika Matengenezo na Manunuzi ya vipuri na Mafuta**

Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa ilipendekeza kwamba Serikali itafute teknolojia maalum ya kudhibiti matumizi mabaya ya fedha za Umma yanayotokea kupitia katika manunuzi ya mafuta na vipuri vya magari.

**(f) Malipo ya posho kuwa makubwa kuliko gharama za kutekeleza Miradi**

Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa ilipendekeza kwamba Serikali irejee upya miongozo ya matumizi ya fedha katika baadhi ya miradi kama vile TASAF, UKIMWI, Miradi ya Kilimo (DADPs), Miradi ya maendeleo (CDG) na Miradi ya Uhifadhi wa Mazingira. Taarifa za matumizi ya miradi zinazoletwa na Halmashauri kuhusu utekelezaji wa miradi zinaonyesha kwamba fedha nyingi za miradi zinatumika kwa malipo ya posho zaidi kuliko kazi za msingi za utekelezaji wa miradi hiyo. Kwa mfano katika miradi ya mazingira Kamati ingependa kuona gharama za tafiti mbalimbali za masuala ya mazingira, gharama za upandaji miti, uhifadhi wa uoto na viumbe vingine vya asili nakadhalika kuliko kuona taarifa zinaonyesha malipo ya posho za mafunzo kwa watumishi.

**(g) Kuhusu Ripoti za Ukaguzi Maalum zilizotekelezwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali**

Kamati ilipendekeza kwamba Serikali itekeleze ipasavyo maoni ya yaliyotolewa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali katika Kaguzi maalum. Utekelezaji wa mapendekezo hayo utaimarisha nidhamu ya matumizi ya fedha katika Halmashauri.

## SURA YA NNE

# 4.0 TATHMINI YA HALI YA FEDHA ZA HALMASHAURI

## 4.1 Ukaguzi wa Bajeti

Uandaaji wa bajeti ni sehemu muhimu katika mchakato wa kuandaa mipango, kudhibiti na kutathmini hali ya fedha za Mamlaka ya Serikali za Mitaa. Kwa uhalisia wake, ni njia ya kugawa rasilimali ili kufikia malengo yaliyowekwa. Ni chombo kinachosaidia viongozi kupanga pamoja na kudhibiti fedha ili kuhakikisha kwamba, kwa kadri inavyowezekana malengo yaliyopangwa yanafikiwa.

Kif. 43(1) ya Sheria ya Fedha za Mamlaka ya Serikali za Mitaa Na.9, 1982 (iliyorekebishwa 2000) imeainisha kwamba, kila Mamlaka ya Serikali za Mitaa, kwa muda usiopungua miezi miwili kabla ya mwanzo wa kila mwaka wa fedha, katika mkutano maalum utakaoitishwa kwa lengo, ipitishe bajeti ya makadirio ya kiasi (a) inachotarajia kupokea na (b) inachotarajia kutolewa, na Mamlaka katika mwaka wa fedha husika, na wakati wowote itakapohitajika, Mamlaka inaweza kupitisha bajeti ya ziada katika mwaka wa fedha husika.

Katika kipindi cha ukaguzi wa mwaka uliomalizika, mapungufu yafuatayo yalionekana katika ukaguzi wa bajeti:

### 4.1.1 Ruzuku ya Serikali Pungufu ikilinganishwa na Bajeti Iliyoidhinishwa Sh.33,035,085,889

Katika mwaka wa fedha 2010/11, ukaguzi wa bajeti katika Halmashauri 18 ulibaini kuwa, kiasi cha Sh.163,361,311,033 kiliidhinishwa na Bunge la Tanzania kwa ajili ya matumizi ya mafungu mbalimbali na utekelezaji wa miradi. Hata hivyo kiasi cha Sh.130,326,225,146 ndicho kilichopokelewa na Halmashauri na kubakiza kiasi kisichopokelewa cha Sh.33,035,085,889 sawa na 20% ya bajeti iliyoidhinishwa kama inavyoonekana katika jedwali lifuatalo:

| Na | Jina la Halmashauri | Bajeti iliyoidhinishwa (Sh.) | Ruzuku iliyopokelewa (Sh.) | Ruzuku isiyopokelewa (Sh.) | % |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | H/W Bahi | 1,564,405,150 | 87,229,915 | 1,477,175,235 | 94 |
| 2 | H/W Ulanga | 4,350,771,000 | 1,313,319,000 | 3,037,452,000 | 70 |
| 3 | H/W Siha | 754,103,000 | 279,391,635 | 474,711,365 | 63 |
| 4 | H/W Kilosa | 4,155,700,467 | 1,664,156,000 | 2,491,544,467 | 60 |
| 5 | H/W Mbarali | 1,562,332,900 | 753,733,684 | 808,599,216 | 52 |
| 6 | H/W Mbozi | 1,562,332,900 | 753,733,684 | 808,599,216 | 52 |
| 7 | H/W Morogoro | 3,706,429,212 | 1,942,999,090 | 1,763,430,122 | 48 |
| 8 | H/M Morogoro | 6,179,183,118 | 3,287,788,354 | 2,891,394,764 | 47 |
| 9 | H/W Kilombero | 5,363,595,000 | 2,958,916,608 | 2,404,678,392 | 45 |
| 10 | H/W Mpwapwa | 21,640,041,266 | 15,813,383,562 | 5,826,657,704 | 27 |
| 11 | H/W Mbulu | 2,458,721,000 | 1,799,516,400 | 659,204,600 | 27 |
| 12 | H/W Chamwino | 21,004,013,050 | 17,765,134,760 | 3,238,878,290 | 15 |
| 13 | H/W Kongwa | 19,123,728,712 | 16,456,272,881 | 2,667,455,831 | 14 |
| 14 | H/W Babati | 16,798,491,000 | 14,590,120,000 | 2,208,371,000 | 13 |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 15 | H/W Iringa | 16,654,813,000 | 15,435,329,755 | 1,219,483,245 | 7 |
| 16 | H/W Simanjiro | 18,618,376,629 | 17,852,295,726 | 766,080,903 | 4 |
| 17 | H/W Kiteto | 9,184,375,629 | 8,987,102,091 | 197,273,539 | 2 |
| 18 | H/W Hanang' | 8,679,898,000 | 8,585,802,000 | 94,096,000 | 1 |
| | **Jumla** | **163,361,311,033** | **130,326,225,145** | **33,035,085,889** | **20** |

Hii ina maanisha kwamba, shughuli zilizopangwa na Halmashauri husika zenye thamani sawa na Sh.33,035,085,889 hazikuweza kutekelezwa kikamilifu na kwa sababu hiyo, malengo ya Halmashauri hayakuweza kufikiwa.

### 4.1.2 Madai ya miaka ya nyuma yaliyolipwa mwaka wa fedha 2010/11 Sh.412,414,001

Agizo Na. 46 la Memoranda ya Fedha ya Mamlaka za Serikali za Mitaa, 1997 linaelekeza kwamba, malipo yote yanatakiwa, ikiwezekana, yalipwe katika mwaka wa fedha husika kwa kuonesha orodha ya wadai wa Halmashauri ikilazimika na kwa hali isiyotegemewa malipo yasije yakaachwa kulipwa kwa sababu ya kukwepa kuonesha matumizi ya ziada katika taarifa za fedha.

Katika mwaka husika wa ukaguzi, ilibainika kwamba kiasi cha Sh.412,414,001 katika Halmashauri 24 kilitakiwa kilipwe katika mwaka wa fedha 2009/10, lakini malipo hayo yamefanyika katika mwaka wa fedha 2010/11 kinyume na Agizo lililotajwa hapo juu. Pia hakuna uthibitisho kuwa malipo hayo yalioneshwa katika orodha ya Wadai wa Halmashauri katika mwaka wa fedha 2009/10.

Jedwali lifuatalo laonesha Halmashauri zilizolipa madai ya miaka ya nyuma kama ilivyoelezwa hapo juu.

| Na. | Jina la Halmashauri | Madai ya yaliyolipwa (Sh.) |
|---|---|---|
| 1 | H/W Mpwapwa | 98,009,078 |
| 2 | H/W Chato | 42,155,809 |
| 3 | H/M Dodoma | 38,990,458 |
| 4 | H/W Sengerema | 34,635,368 |
| 5 | H/W Chunya | 30,237,600 |
| 6 | H/Mji Babati | 28,192,003 |
| 7 | H/W Muleba | 22,471,700 |
| 8 | H/W Mbulu | 19,425,000 |
| 9 | H/W Sumbawanga | 14,803,647 |
| 10 | H/W Pangani | 12,504,400 |
| 11 | H/W Bahi | 11,215,271 |
| 12 | H/W Kasulu | 9,985,000 |
| 13 | H/W Nzega | 7,247,729 |
| 14 | H/W Karatu | 5,783,620 |
| 15 | H/W Meatu | 5,741,880 |
| 16 | H/W Bukoba | 5,052,099 |
| 17 | H/W Tabora | 4,260,000 |
| 18 | H/Mji Kibaha | 4,148,400 |
| 19 | H/W Kilwa | 4,148,400 |

| | | |
|---|---|---|
| 20 | H/W Kahama | 4,000,000 |
| 21 | H/W Mpanda | 3,972,400 |
| 22 | H/W Rufiji/Utete | 2,022,000 |
| 23 | H/W Kondoa | 1,829,770 |
| 24 | H/W Rombo | 1,582,369 |
| **Jumla** | | **412,414,001** |

Bajeti ya mwaka katika Halmashauri husika zimeathirika kwa kiasi hicho na kusababisha baadhi ya miradi iliyopangwa katika mwaka husika kutotekelezwa.

Uongozi wa Halmashauri husika unashauriwa kuonesha madeni yote ya miaka iliyopita katika taarifa za fedha. Kwa kuongezea inashauriwa kuwa madeni yote ya miaka ya nyuma yawe yanaingizwa katika bajeti ya mwaka ujao wa fedha.

### 4.1.3 Matumizi ya Fedha zaidi ya Bajeti Iliyoidhinishwa Sh.10,633,138,935

Kif. 43(1) ya Sheria ya Fedha za Mamlaka ya Serikali za Mitaa Na.9, 1982 (iliyorekebishwa 2000) imeainisha kwamba, kila Mamlaka ya Serikali za Mitaa, kwa muda usiopungua miezi miwili kabla ya mwanzo wa kila mwaka wa fedha, katika mkutano maalum utakaoitishwa kwa lengo, ipitishe bajeti ya makadirio ya kiasi (a) inachotarajia kupokea na (b) inachotarajia kutolewa, na Mamlaka katika mwaka wa fedha husika, na wakati wowote itakapohitajika, Mamlaka inaweza kupitisha bajeti ya ziada katika mwaka wa fedha husika.

Ukaguzi wa bajeti ulibaini kuwa, Halmashauri 18 zilitumia Shs.10,633,138,935 zaidi ikilinganishwa na bajeti ya mafungu mbalimbali ya matumizi ya Sh.78,083,615,788 yaliyoidhinishwa na bunge bila kuandaa bajeti ya ziada kama inavyoonekana katika jedwali lifuatalo:

| Na. | Jina la Halmashauri | Bajeti iliyoidhinishwa | Matumizi | | % zaidi ya bajeti |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Matumizi halisi | Matumizi zaidi ya bajeti | |
| 1 | H/M Morogoro | 640,516,822 | 958,584,855 | 318,068,033 | 50 |
| 2 | H/W Musoma | 2,991,261,195 | 4,457,377,329 | 1,466,116,134 | 49 |
| 3 | H/W Kibondo | 14,487,081 | 21,566,477 | 7,079,396 | 49 |
| 4 | H/W Maswa | 2,587,049,719 | 3,509,360,519 | 922,310,800 | 36 |
| 5 | H/W Bukoba | 385,732,000 | 517,732,000 | 132,000,000 | 34 |
| 6 | H/W Morogoro | 12,148,485,000 | 16,097,882,307 | 3,949,937,307 | 33 |
| | H/M Mtwara | 3,872,822,000 | 4,794,450,000 | 921,628,000 | 24 |
| | H/Mji Masasi | 382,657,081 | 466,750,094 | 84,093,013 | 22 |
| 9 | H/W Kilosa | 19,505,416,319 | 21,695,486,945 | 2,190,070,626 | 11 |
| 10 | H/W Kishapu | 841,828,000 | 893,241,334 | 51,413,334 | 6 |
| 11 | H/W Tabora | 24,522,737,064 | 24,964,042,931 | 441,305,867 | 2 |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 12 | H/W Urambo | 10,190,623,507 | 10,339,739,932 | 149,116,425 | 1 |
| | **Jumla** | **78,083,615,788** | **88,716,214,723** | **10,633,138,935** | **14** |

### 4.1.4 Matumizi ambayo hayamo katika Bajeti Shs.4,673,316,247

Katika mwaka wa fedha 2010/11, Halmashauri 19 zilitumia kiasi cha Shs.4,673,316,247 ikiwa ni matumizi ambayo hayakuwa katika bajeti iliyoidhinishwa bila idhini yoyote kutoka mamlaka husika kinyume na Kif. 10 (3) ya Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa Na.9, 1982 (iliyorekebishwa 2000). Kiasi cha matumizi katika Halmashauri husika ni kama inavyoonekana katika jedwali lifuatalo:

| Na. | Halmashauri | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|
| 1 | H/W Bahi | 2,687,711,211 |
| 2 | H/W Iramba | 1,060,000,000 |
| 3 | H/W Mpwapwa | 236,995,838 |
| 4 | H/W Kinondoni | 204,207,523 |
| 5 | H/W Geita | 136,815,000 |
| 6 | H/M Arusha | 75,000,000 |
| 7 | H/M Shinyanga | 66,528,000 |
| 8 | H/W Chamwino | 46,532,500 |
| 9 | H/W Misungwi | 29,627,840 |
| 10 | H/W Tabora | 28,360,000 |
| 11 | H/W Bukombe | 24,453,000 |
| 12 | H/W Handeni | 17,604,590 |
| 13 | H/W Chato | 15,816,800 |
| 14 | H/W Bagamoyo | 12,719,945 |
| 15 | H/W Nanyumbu | 10,000,000 |
| 16 | H/W Namtumbo | 7,895,000 |
| 17 | H/W Kahama | 7,000,000 |
| 18 | H/W Rorya | 3,799,000 |
| 19 | H/W Bariadi | 2,250,000 |
| | **Jumla** | **4,673,316,247** |

### 4.1.5 Mwenendo wa Makusanyo katika Vyanzo vya Halmashauri ikilinganishwa na Bajeti iliyoidhinishwa

Mapato kutoka vyanzo vya ndani ni fedha zinazokusanywa katika vyanzo vya umma kama vile kodi, ada, leseni na fidia ya makosa mbalimbali. Matumizi ya kawaida ni matumizi katika kuendesha shughuli za kila siku za Halmashauri.

Wakati wa ukaguzi mwaka 2010/11, Mamlaka ya Serikali za Mitaa zilipanga kukusanya mapato kupitia vyanzo vyao vya ndani ya kiasi cha Sh.183,470,314,765. Hata hivyo Halmashauri ziliweza kukusanya kiasi cha Sh.184,344,284,252. Hii inamaanisha kwamba Halmashauri zilikusanya zaidi ya bajeti kwa Sh.873,969,486 sawa na 0.5% ya bajeti.

Maelezo ya ulinganisho kati ya bajeti na mapato yaliyokusanywa na Halmashauri umeoneshwa kwenye **Kiambatisho (viii)**

Muhtasari wa mwenendo kati ya bajeti na mapato yaliyokusanywa na Halmashauri kwa miaka minne mfululizo 2007/2008, 2008/2009, 2009/2010 na 2009/2010 ni kama ifuatavyo:

| Mwaka wa Fedha | Bajeti iliyoidhinishwa | Mapato yaliyokusanywa na Halmashauri | Mapato Zaidi/ (Pungufu) ya Bajeti | % |
|---|---|---|---|---|
| 2007/08 | 90,477,657,278 | 93,545,987,812 | 3,068,330,534 | 3.39 |
| 2008/09 | 111,327,810,815 | 110,852,341,512 | (475,469,303) | 0.43 |
| 2009/10 | 136,673,109,767 | 137,416,106,722 | 742,996,955 | 0.54 |
| 2010/11 | 183,470,314,765 | 184,344,284,252 | 873,969,486 | 0.48 |

Mwenendo kati ya bajeti na mapato yaliyokusanywa na Halmashauri kwa miaka minne mfululizo yanaweza kuoneshwa kwa kutumia chati ifuatayo:




Chati hapo juu inaonyesha kwamba, kwa mwaka wa fedha 2007/08, Halmashauri zilikusanya mapato ya ndani zaidi ya bajeti kwa 3.39%, wakati kwa mwaka wa fedha 2008/09 kulikuwa na makusanyo pungufu ya bajeti kwa 0.43%. Vile vile kwa miaka ya fedha 2009/2010 na 2010/2011 Halmashauri zilikusanya mapato yao ya ndani zaidi ya bajeti kwa 0.54% na 0.48% katika mtiririko wa miaka husika.

Mamlaka za Serikali za Mitaa zinashauriwa kuandaa bajeti yenye uhalisia vile vile kuwa na mikakati imara katika ukusanyaji wa mapato kwa lengo la

kuongeza wigo wa vyanzo vya mapato na hatimaye kuwezesha Halmashauri kujiendesha zenyewe kwa ufanisi zaidi.

### 4.2 Mwenendo wa Mapato kutoka Vyanzo vya Ndani ya Halmashauri ikilinganishwa na Ruzuku kutoka Serikali Kuu

Wakati wa ukaguzi katika mwaka husika, Mamlaka za Serikali za Mitaa zilikusanya jumla ya Sh.184,344,284,251 kutoka vyanzo vyao vya ndani na kutumia jumla ya Sh.2,153,971,770,095 katika matumizi ya kawaida. Hata hivyo, ulinganisho kati ya mapato na matumizi ya fedha ya Serikali za Mitaa umebaini kuwa Serikali za Mitaa, kwa kutumia mapato yake ya ndani zinaweza kugharimia matumizi ya shughuli za kawaida kwa 8.6% bila kutegemea fedha kutoka serikali kuu na wafadhili. Maelezo kwa asilimia ya uwezo wa Halmashauri ni kama yanavyoonekana katika **Kiambatisho (ix)**

Kama inavyoonekana katika **Kiambatisho (ix),** Halmashauri yenye asilimia kubwa ya makusanyo ya mapato dhidi ya matumizi ya kawaida ni Halmashauri ya Mji wa Masasi kwa 102%, ikifuatiwa na Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam kwa 73%.

Kwa wastani, Halmashauri haziwezi kujiendesha kwa kutumia mapato kutoka vyanzo vya ndani ya Halmashauri husika na hivyo wigo wa vyanzo vya mapato ni lazima vipitiwe upya ili kujumuisha pamoja na mapato ambayo hayajakusanywa kutoka vyanzo vingine vya mapato vya ndani.

Muhtasari wa mwenendo kati ya mapato yaliyotokana na vyanzo vya ndani vya Halmashauri na ruzuku toka Serikali kuu kwa miaka minne mfululizo 2007/2008, 2008/2009, 2009/2010 na 2009/2010 ni kama ilivyooneshwa katika jedwali lifuatalo:

| Mwaka wa Fedha | Mapato toka vyanzo vya ndani (Sh.) | Matumizi ya Kawaida (Sh.) | % |
|---|---|---|---|
| 2007/08 | 93,545,987,812 | 1,140,847,566,087 | 9.2 |
| 2008/09 | 110,852,341,512 | 1,437,216,933,939 | 8 |
| 2009/10 | 137,416,106,722 | 1,823,788,009,947 | 7.5 |
| 2010/11 | 184,344,284,252 | 2,153,971,770,095 | 8.6 |

Mwenendo kati ya mapato yaliyotokana na vyanzo vya ndani ya Halmashauri kulinganisha na ruzuku kutoka Serikali Kuu kwa miaka minne (4) mfululizo yanaweza kuoneshwa kwa kutumia grafu ifuatayo:




Grafu hapo juu inaonyesha kwamba, kiwango cha Halmashauri kutegema ruzuku toka Serikali Kuu kinaongezeka kila mwaka ukilinganisha na mapato ya ndani yanayokusanywa. Pia inaonyesha kwamba, Halmashauri haziwezi kujiendesha kutokana na vyanzo vya mapato yake bila kutegemea ruzuku toka Serikali Kuu.

## 4.3 Ruzuku ya Matumizi ya Kawaida Isiyotumika Sh.146,774,839,643

Ruzuku ya matumizi ya kawaida ni ruzuku toka Serikali Kuu kwa ajili ya matumizi ya kawaida katika kuendesha shughuli za kila siku za Halmashauri.

Kwa mwaka wa fedha 2010/11, Jumla ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa 127 zilitumia kiasi cha Sh.1,978,117,478,839 katika shughuli za kila siku ukilinganisha na Ruzuku kutoka Serikali Kuu ya Sh.2,105,926,241,086 hivyo kupelekea baki la Sh.146,774,839,643 sawa na 7% ya Ruzuku kutoka Serikali Kuu ambacho hakikutumika. Mchanganuo umeoneshwa katika **kiambatisho (x)**

## 4.4 Matumizi ya ziada zaidi ya ruzuku ya matumizi ya kawaida iliyotolewa Sh. Sh.4,041,504,154

Wakati wa ukaguzi, halmashauri sita (6) zilitumia kiasi cha Sh.92,477,645,440 katika shughuli za kila siku ukilinganisha na Ruzuku kutoka Serikali Kuu ya Sh.88,436,141,286 na hivyo kufanya matumizi ya ziada kwa Sh.4,041,504,154. Mchanganuo ni kama unavyoonekana katika jedwali lifuatalo:

| Na. | Halmashauri Husika | Ruzuku ya matumizi ya kawaida (Sh.) | Matumizi ya kawaida (Sh.) | Matumizi ya ziada (Shs.) | % |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | H/W Ludewa | 11,728,301,656 | 13,851,856,856 | 2,123,555,200 | 18 |
| 2 | H/W Mvomero | 18,565,175,752 | 19,541,702,512 | 976,526,760 | 5 |
| 3 | H/W Musoma | 19,062,654,006 | 19,514,686,923 | 452,032,917 | 2 |
| 4 | H/W Iringa | 16,121,233,007 | 16,372,459,871 | 251,226,864 | 2 |
| 5 | H/W Hanang' | 14,012,493,000 | 14,186,175,000 | 173,682,000 | 1 |
| 6 | H/W Ngara | 8,946,283,865 | 9,010,764,278 | 64,480,413 | 0.7 |
| **Jumla** | | **88,436,141,286** | **92,477,645,440** | **4,041,504,154** | **4.6** |

## 4.5 Ruzuku ya Miradi ya Maendeleo Isiyotumika Sh.177,360,574,367

Ruzuku ya miradi ya maendeleo hutolewa kwa Halmashauri kwa ajili ya kujenga miundombinu au kufanya ukarabati wa miundo mbinu iliyopo kulingana na maeneo yaliyopewa kipaumbele kwa lengo la kujenga uwezo katika jamii, kuboresha huduma na kupunguza umaskini.

Ruzuku ya miradi ya maendeleo hutumika katika maeneo yanayohusu kupunguza umaskini kama vile Afya, Elimu, Maji, Barabara na Kilimo.

Kwa mwaka wa fedha 2010/11, kiasi cha Sh.542,339,143,645 kilichotolewa katika Halmashauri 130 (isipokuwa Halmashauri ya Mji wa Masasi, Halmashauri ya Manispaa ya Tabora na Jiji la Dar es salaam) ikiwa ni ruzuku ya fedha za maendeleo kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali.

Hata hivyo hadi kufikia Juni 30, 2010 kiasi cha Sh.367,778,247,642 kilitumika, na kubakia kiasi cha Sh.174,560,896,003 sawa na 32% ya fedha zote zilizotolewa.
Mchanganuo wa Halmashauri zilizokuwa na fedha za maendeleo zilizobaki bila kutumika ni kama unavyoonekana katika **Kiambatisho (xi)**

Mwenendo wa fedha za ruzuku za miradi ya maendeleo za Serikali zisizotumika kwa miaka minne mfululizo 2007/2008, 2008/2009, 2009/2010 na 2010/2011 ni kama ilivyooneshwa hapa chini:

| Mwaka | Ruzuku iliyotolewa | Kiasi kilichotumika | Kiasi kilichosalia (Shs.) | % | Idadi ya Halmashauri |
|---|---|---|---|---|---|
| 2007/08 | 270,547,629,434 | 171,791,488,611 | 98,756,140,823 | 37 | 111 |
| 2008/09 | 328,203,178,845 | 239,482,549,650 | 88,720,629,195 | 27 | 118 |
| 2009/10 | 507,866,599,666 | 332,092,443,562 | 175,774,156,104 | 35 | 133 |
| 2010/11 | 542,339,143,645 | 367,778,247,642 | 174,560,896,003 | 32 | 130 |

Mwenendo wa maelezo hayo hapo juu ni kama inavyoonyeshwa kwa kutumia grafu ifuatayo:




Grafu hapo juu inaonyesha kwamba, kwa mwaka wa fedha 2007/08 hadi 2008/09 ruzuku ya miradi ya maendeleo isiyotumika ilipungua kwa 10% ukilinganisha na jumla ya ruzuku iliyotolewa, wakati kwa mwaka wa fedha 2008/09 hadi 2009/10 ruzuku ya miradi ya maendeleo isiyotumika iliongezeka kwa 8% ya jumla ya ruzuku iliyotolewa. Hata hivyo kwa mwaka wa fedha 2009/10 hadi 2010/11 kiasi cha fedha ambacho hakikutumika kilipungua kwa 3% ya jumla ya ruzuku ya maendeleo iliyopokelewa.

Kuwepo kwa fedha za ruzuku za miradi ya maendeleo isiyotumika ni ushahidi kwamba miradi ya maendeleo ambayo ilitengewa ruzuku hizi haikutekelezwa kikamilifu kama ilivyopangwa na hivyo huduma au faida zinazotokana na miradi hiyo kwa jamii husika hazijafikiwa. Hii pia inaweza ikasababisha mabadiliko ya bajeti ili kuweza kufidia mapungufu yaliyojitokeza kutokana na mfumuko wa bei.

## 4.6 Makusanyo pungufu ya kodi ya majengo

Mamlaka ya Mapato Tanzania imekuwa ikikusanya kodi ya majengo kwa niaba ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa tokea mwaka 2008. Kwa mwaka wa fedha 2010/11, jumla ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa 11 zilipanga kukusanya mapato ya kiasi cha Sh.5,085,350,996 kutokana na kodi ya majengo. Hata hivyo Halmashauri ziliweza kukusanya mapato ya Sh.2,757,074,201. Hii inamaanisha kwamba Halmashauri zilikusanya pungufu ya bajeti kwa Sh.2,329,686,795 sawa na 46% ya bajeti.

Muhtasari wa ulinganisho kati ya bajeti na mapato ya kodi ya majengo yaliyokusanywa na jumla ya Halmashauri 14 ni kama inavyoonyeshwa katika jedwali lifuatalo

| S/N | Jina la Halmashauri | Kodi ya Majengo | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | Bajeti iliyoidhinishwa | Makusanya halisi | Tofauti | % |
| 1 | H/M Kigoma/Ujiji | 135,309,000 | 25,889,000 | 109,420,000 | 81 |
| 2 | H/Mji Babati | 11,250,000 | 3,138,200 | 8,111,800 | 72 |
| 3 | H/W Urambo | 1,090,000 | 1,795,000 | 705,000 | 65 |
| 4 | H/M Temeke | 2,139,373,294 | 786,866,155 | 1,352,507,139 | 63 |
| 5 | H/J Tanga | 300,000,000 | 128,808,764 | 171,191,236 | 57 |
| 6 | H/Mji Lindi | 36,000,000 | 19,306,800 | 16,693,200 | 46 |
| 7 | H/J Mwanza | 1,384,520,650 | 808,645,863 | 575,874,787 | 42 |
| 8 | H/M Shinyanga | 50,000,000 | 30,244,443 | 19,755,557 | 40 |
| 9 | H/M Singida | 104,791,500 | 83,995,246 | 20,796,254 | 20 |
| 10 | H/M Morogoro | 384,616,552 | 312,090,588 | 72,525,964 | 19 |
| 11 | H/M Songea | 77,000,000 | 69,582,987 | 7,417,013 | 10 |
| 12 | H/M Moshi | 288,000,000 | 277,952,240 | 10,047,760 | 3 |
| 13 | H/M Iringa | 110,000,000 | 117,758,215 | (7,758,215) | -7 |
| 14 | H/Mji Kibaha | 63,400,000 | 91,000,700 | (27,600,700) | -44 |
| | **Jumla** | **5,085,350,996** | **2,757,074,201** | **2,329,686,795** | **46** |

Hii inadhihirisha kwamba Halmashauri tajwa hapo juu hazikukusanya kodi ya mapato kama zilivyo bajetiwa kwa 46%.

Mamlaka za Serikali za Mitaa zinashauriwa kuandaa bajeti yenye uhalisia na ukweli na vile vile kuwa na mikakati imara katika ukusanyaji wa kodi za majengo kwa lengo la kuongeza wigo la mapato na hatimaye kuwezesha Halmashauri husika kujiendesha zenyewe kwa ufanisi zaidi.

## SURA YA TANO

## 5.0 MAMBO MUHIMU YALIYOJIRI KATIKA UKAGUZI WA HESABU NA UDHIBITI NA NDANI

### 5.1 Tathmini ya Mifumo ya Udhibiti wa Ndani na Masuala ya Utawala Bora katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa

Udhibiti wa Ndani ni mpangilio ulioundwa katika kuhakikisha kuwa malengo yanafikiwa kwa ufanisi na ustadi katika utendaji, taarifa za fedha ni za kuaminika, na sheria na kanuni husika zinafuatwa. Kwa madhumuni ya ripoti hii, udhibiti wa ndani ni jinsi Mamlaka ya Serikali za Mitaa zinavyojihakikishia zenyewe kwamba taarifa zao za fedha ni za kuaminika, ufanisi na ustadi katika utendaji vinazingatiwa na pia wanafuata sheria na kanuni husika.

Sehemu hii ya ripoti inaonyesha matokeo ya ukaguzi yanayohusiana na baadhi ya vipengele vya udhibiti wa ndani katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa ikiwa ni pamoja na; mifumo ya kihasibu, udhibiti wa mazingira, tathmini za vihatarishi, udhibiti wa utendaji, teknolojia ya habari na mawasiliano, ufuatiliaji wa udhibiti, na kuzuia na kudhibiti udanganyifu.

Mfumo wa Udhibiti wa ndani wenye ufanisi ni kama unavyoonyeshwa katika umbo lifuatalo:




Katika mwaka wa ukaguzi, baadhi ya mapungufu yaliyoonekana kutokana na ukaguzi wa mfumo wa udhibiti wa ndani kwenye Mamlaka ya Serikali za Mitaa ni kama ifuatavyo:

#### 5.1.1 Mapungufu katika Mifumo ya Kihasibu

Waraka wa Fedha Na.1 wa 1999/2000 unataka shughuli zote za kihasibu za Serikali kufanyika katika Mfumo Funganifu wa Usimamizi wa Fedha (IFMS). Mfumo huu una baadhi ya vipengele vinavyoshughulika na; maandalizi ya bajeti, fedha kutoka Serikali Kuu na hati za kuidhinisha uhamisho wa fedha, usimamizi wa mali, kudhibiti manunuzi, miadi na matumizi, malipo ya wadai/usuluhisho wa taarifa za kibenki, usimamizi wa fedha za maendeleo, vitabu vya majumuisho na taarifa za fedha.

Katika mwaka wa ukaguzi ilibainika kwamba, jumla ya halmashauri 67 kama zilivyoonyeshwa katika **kiambatisho (xii)** hazikutumia ipasavyo Mfumo Funganifu wa Usimamizi wa Fedha (IFMS) katika kuandaa ripoti. Mapungufu haya ni kama yafuatavyo:

- Vipengele vya usimamizi wa mali, manunuzi pamoja na malipo ya mishahara havikuboreshwa katika mfumo ili viweze kutumika.
- Taarifa za mizania ya hesabu, taarifa za mapato na matumizi, urari na taarifa za mtiririko wa fedha kutozalishwa kupitia katika mfumo.
- Mfumo hautengenezi ripoti kuu za mapato na matumizi; hivyo ukaguzi haukuweza kuthibitisha mapato na matumizi ya kila mwezi ya Halmashauri husika.
- Udhibiti wa miadi haujaimarishwa katika mfumo, hii inamaanisha kuwa, hakuna miadi katika vifungu vya matumizi vilivyomo kwenye mfumo, hivyo matumizi zaidi yanawezekana kufanyika katika mafungu ya matumizi.
- Mfumo hautumiki katika kuchapisha hundi.
- Chati ya hesabu inayotengenezwa na mfumo haikidhi matakwa ya Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu katika Sekta ya Umma (IPSASs)

Kutokana na mapungufu yaliyoainishwa hapo juu inadhihirisha kuwa, baadhi ya watumiaji wa Mfumo Funganifu wa Usimamizi wa Fedha (IFMS/Epicor) katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa hawana uwezo mkubwa kuhusu matumizi sahihi ya Mfumo katika kuandaa baadhi ya taarifa za fedha.

Inashauriwa kuwa, OWM-TAMISEMI ihakikishe kuwa vipengele vyote vya Mfumo Funganifu wa Usimamizi wa Fedha vinaboreshwa na Mfumo unatumika kikamilifu.

Zaidi ya hayo, uongozi wa Mamlaka ya Serikali za Mitaa kwa kushirikiana na OWM-TAMISEMI wanatakiwa wahakikishe kuwa, watumiaji wa Mfumo wanapata mafunzo katika matumizi sahihi ya Mfumo ili kuongeza ufanisi katika matumizi ya Mfumo.

### 5.1.2 Mfumo wa Uhasibu nje ya Mfumo Funganifu

Wakati wa ukaguzi ilibainika kuwa, jumla ya Halmashauri 36 kama zilivyoonyeshwa katika **kiambatisho (xii)** hawatumii Mfumo Funganifu wa Usimamizi wa Fedha katika kuandaa taarifa za fedha.

Vihatarishi vinavyohusiana na kutotumia Mfumo Funganifu wa Usimamizi wa Fedha katika kuandaa taarifa za fedha ni pamoja na kwamba, taarifa za fedha zinakabiliwa zaidi na makosa na zinaweza kufanyiwa mabadiliko na mtu yeyote hivyo kupunguza uaminifu wa taarifa za fedha zinazoandaliwa

nje ya mfumo. Kutotumia mfumo pia kunaathiri umakini na kasi na inasababisha utata wa utoaji taarifa za fedha katika ngazi zote.

Kutokana na masuala yaliyobainika hapo juu, ninashauri kwamba, kuna haja kwa kila Halmashauri kuhakikisha kuwa watumishi walioko katika Idara ya Fedha, wanapatiwa mafunzo ya kutosha kuhusiana na matumizi sahihi ya Mfumo wa /IFMS Epicor toleo jipya la 9.05.

Kwa kuongezea, OWM-TAMISEMI pamoja na Wizara ya Fedha zinatakiwa kuhakikisha kuwa, utumiaji wa mfumo wa IFMS/Epicor toleo la 9.05 unapewa kipaumbele katika Halmashauri zote ili kuandaa na kutoa taarifa za fedha pamoja na taarifa zingine zinazohusiana na hizo kwa wakati. Utumiaji wa mfumo huu unatakiwa uwe ni wa lazima kwa kila Halmashauri, vilevile OWM-TAMISEMI na Wizara ya Fedha wanatakiwa wasimamie utekelezaji wa matumizi ya mfumo huo.

### 5.1.3 Mapungufu katika Utendaji wa Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani

Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani ni kitengo kinachojitegemea katika kutoa ushauri ili kuongeza ufanisi katika utendaji wa Taasisi. Inawezesha Taasisi kufikia malengo kwa kuleta utaratibu uliopangwa katika kutathmini na kuongeza ufanisi wa usimamizi na udhibiti wa vihatarishi na katika utawala bora.

Kif. 45 (1) cha Sheria ya Fedha za Mamlaka ya Serikali za Mitaa, 1982 na Agizo Na. 12 la Memoranda ya Fedha za Mamlaka ya Serikali za Mitaa, 1997 zinamtaka Afisa Masuuli katika kila Halmashauri kuanzisha na kuendeleza kitengo imara cha ukaguzi wa ndani kama sehemu ya mfumo wa udhibiti wa ndani wa Halmashauri. Kitengo imara cha ukaguzi wa ndani kinatakiwa kutoa tathmini juu ya usalama na matumizi ya kihasibu, fedha na udhibiti wa utendaji ndani ya Halmashauri kwa kufanya mapitio kwa utaratibu, kutoa taarifa katika ufanisi wa kiutendaji, fedha, mifumo ya uendeshaji na udhibiti wa bajeti.

Kinyume na mahitaji ya kisheria hapo juu, kutokana na tathmini za utendaji wa kitengo cha ukaguzi wa ndani, mapungufu yafuatayo yamebainika katika Halmashauri 116 kama inavyoonyeshwa katika **kiambatisho (xii)**

- Vitengo bado vina upungufu wa watumishi, baadhi wana mtumishi mmoja au wawili na baadhi hawajawezeshwa kifedha. Kwa kuzingatia shughuli mbalimbali za Halmashauri, mkaguzi mmoja au wawili hawatoshi katika mawanda ya ukaguzi yaliyojitosheleza.
- Wakati wa ukaguzi katika mwaka wa fedha 2010/11, mawanda na ukaguzi uliojitosheleza katika kitengo cha ukaguzi wa ndani yalizuiwa kwasababu ya upungufu wa rasilimali watu na fedha. Hivyo udhibiti wa fedha na utendaji haukuweza kufanyiwa tathmini kama

ilivyotakiwa, hivyo sikuweza kutegemea kazi za kitengo cha ukaguzi wa ndani ili kupunguza kiwango cha vipimo vya ukaguzi.

- Nafasi ya ukaguzi wa ndani katika mfumo wa utawala bora pamoja na majukumu na wajibu wake hayakubainishwa wazi katika mkataba wa ukaguzi wa ndani.
- Ukosefu wa nyaraka zinazoonesha taarifa ya maeneo yaliyokaguliwa ambayo yangewezesha mchakato wa mapitio na kutengeneza msingi wa matokeo ya ukaguzi na mapendekezo yaliyomo katika taarifa ya ukaguzi wa ndani.

Uongozi wa Mamlaka ya Serikali za Mitaa kwa kushirikiana na OWM-TAMISEMI na Kitengo cha Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Serikali chini ya Wizara ya Fedha zinashauriwa kuwa, kuna umuhimu wa kuimarisha kazi za ukaguzi wa ndani kwa kuongeza rasilimali fedha na rasilimali watu. Aidha wakaguzi wa ndani lazima wapatiwe elimu na ujuzi ili waweze kuongeza wigo wa ukaguzi na kuboresha utendaji wao.

### 5.1.4 Mapungufu katika Kamati ya Ukaguzi

Kamati ya Ukaguzi ni sehemu muhimu katika mfumo wa utawala iliyoundwa kuimarisha mfumo wa udhibiti wa Halmashauri. Kamati imara ya ukaguzi ina uwezo wa kuimarisha udhibiti wa mazingira na hivyo kusaidia Maafisa Masuuli kutimiza wajibu wao katika uongozi na majukumu ya udhibiti na pia kuwezesha ufanisi wa kazi za ukaguzi wa ndani na kuimarisha utoaji taarifa za fedha.

Kwa kuongezea, kamati ya ukaguzi wa hesabu inapaswa kutoa usimamizi unaojitegemea wa kazi na matokeo za ukaguzi wa ndani na wa nje, kutathmini juu ya rasilimali zinazohitajika katika ukaguzi na kusuluhisha mahusiano kati ya wakaguzi na Mamlaka ya Serikali za Mitaa.

Kamati za ukaguzi wa hesabu zinatakiwa zihakikishe kuwa, matokeo ya ukaguzi yanawekwa wazi, na ushauri wa maboresho yoyote au hatua za marekebisho zinatekelezwa.

Kwa mujibu wa Waraka Na. CHA/3/215/01 wa 27/11/2007 uliotolewa na OWM-TAMISEMI, kila Mamlaka ya Serikali za Mitaa zinatakiwa ziunde Kamati imara ya Ukaguzi wa Hesabu.

Wakati wa kupitia mchakato wa utendaji wa Kamati za Ukaguzi, ilibainika kuwa, jumla ya Halmashauri 95 kama inavyoonekana katika **Kiambatisho (xii)** hazikuwa wa ufanisi kutokana na mapungufu yafuatayo:

- Udhaifu wa kiutendaji katika Vitengo vya Ukaguzi wa Ndani ambao unaashiria kwamba Kamati za Ukaguzi zilishindwa kusimamia majukumu ya wakaguzi wa ndani.

- Kamati za Ukaguzi hazikuweza kupitia taarifa za fedha na ripoti za Halmashauri.
- Katika baadhi ya matukio hakukuwa na ushahidi kuwa,
  ripoti za kamati za kila mwaka zimeandaliwa na kuwasilishwa kwa Maafisa Masuuli kwa ajili ya kuchukua hatua sahihi juu ya mapendekezo ya Kamati.
- Kamati za Ukaguzi zilizo nyingi hazikutani wala
  haziwaaliki wakaguzi wa nje katika vikao vyake ili kujadili kwa pamoja mambo yaliyokosa uvumbuzi kama ilivyoelekezwa na OWM-TAMISEMI.

Utendaji usio wa ufanisi wa Kamati ya Ukaguzi unaweza kusababisha udhaifu katika udhibiti wa mazingira na utawala bora katika Halmashauri kwa ujumla.

Ni muhimu kwa OWM-TAMISEMI kuongeza majukumu zaidi katika hadidu za rejea za Kamati za Ukaguzi kama vile mapitio ya taarifa za fedha na ripoti, usimamizi na udhibiti wa vihatarishi na udanganyifu ili kuifanya Kamati kuwa ni chombo imara katika ufuatiliaji wa udhibiti wa ndani.

### 5.1.5.1 Tathmini ya Usimamizi wa Vihatarishi

Usimamizi wa vihatarishi ni sehemu ya mfumo wa udhibiti katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa katika kusimamia vihatarishi kwa kuwa vinahusiana na ufahamu wa malengo ya Halmashauri, kutambua, kuchambua na kutathmini vihatarishi vinavyohusiana na kufikia malengo na mara kwa mara kuendeleza na kutekeleza mipango/taratibu kuwasilisha vihatarishi vilivyotambuliwa.

Mamlaka ya Serikali za Mitaa zinahitajika mara kwa mara kufuatilia na kuboresha mifumo ya usimamizi wa vihatarishi ili kujihakikishia kuwa, ni chombo imara kwa Halmashauri katika mchakato na utaratibu wa kutoa huduma kwa jamii

Ukaguzi uliofanyika katika sampuli ya jumla ya Halmashauri 73 kama zinavyoonekana katika **kiambatisho (xii)** unadhihirisha kuwa, Halmashauri husika hazina mfumo wa usimamizi wa vihatarishi na hawajafanya tathmini ya hivi karibuni ya vihatarishi hivyo ili kutambua vihatarishi vilivyomo na vile vilivyoibuka baada ya mabadiliko ya mazingira na jinsi ya kutoa huduma. Pia, ilibainika kuwa sera na taratibu za usimamizi wa vihatarishi havikuanzishwa.

Kukosekana kwa sera na mipango imara ya usimamizi wa vihatarishi, Halmashauri husika hazitakuwa katika nafasi ya kukabiliana kwa wakati kutokana vihatarishi ambavyo vinaweza kuleta madhara makubwa katika utendaji wa sasa na wa baadae wa Halmashauri.

Uongozi wa Mamlaka ya Serikali za Mitaa unatakiwa kuanzisha utaratibu unaojitosheleza kutambua na kutathmini vihatarishi, kuchambua madhara

yake pamoja na udhibiti wa utendaji katika ufuatiliaji na kukabiliana na vihatarishi husika kwasababu ni chombo imara kwa halmashauri katika mchakato na taratibu za utoaji huduma kwa jamii

### 5.1.6 Mazingira ya Udhibiti wa Teknolojia ya Habari

Wakati wa kufanya tathmini katika mazingira ya udhibiti wa teknolojia ya habari, mapungufu yafuatayo yalibainika katika jumla ya Halmashauri 108 kama zinavyoonyeshwa katika **kiambatisho (xii)**

- Mamlaka ya Serikali za Mitaa hazina sera ya teknolojia ya habari, kitu ambacho kinaweza kuashiria udhaifu katika usimamizi na utumiaji wa vifaa vya teknolojia ya habari ikiwa ni pamoja na vifaa na programu za kompyuta.
- Haikuwezekana kutathmini na kuthaminisha mpango wa teknolojia ya habari wa Halmashauri husika na mipango wa utekelezaji iliyosababishwa na kutowasilishwa kwa mpango mkakati wa teknolojia ya habari kwa ajili ya ukaguzi.
- Kutokuwepo kwa vizuizi vya ruhusa katika seva ya hifadhidata. Seva ya hifadhidata iko katika vyumba ambavyo shughuli zingine za kawaida zinafanyika kinyume na taratibu ambazo zinazohitaji seva za hifadhidata iwekwe katika chumba kilichotengwa, vyenye ulinzi, safi na isiyo na vumbi
- Kutokuwepo kwa sera na taratibu za teknolojia ya habari katika kuhakikisha usalama wa kumbukumbu ikiwa ni pamoja na taarifa inayosambazwa kwa kutumia mawasiliano ya simu, taarifa zilizopo katika mfumo na usafirishaji wa taarifa zilizohifadhiwa kwenda katika maeneo ya mbali
- Kuhifadhi taarifa katika vyombo kama kanda sio salama kwasababu kanda hizo zinawekwa katika makabati yenye vumbi. Baadhi ya taarifa zilizohifadhiwa katika kanda zilionekana kuharibika baada ya siku chache. Hii inaweza kusababisha upotevu wa taarifa husika.
- Kwa baadhi ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa, taarifa hazihifadhiwi katika Mfumo Funganifu wa Usimamizi wa Fedha (IFMS-Epicor), hivyo inaweza kusababisha kutowezekana kurejesha mfumo katika hali ya kawaida wakati wa majanga. Pia, kutokuwepo kwa vifaa vya kuhifadhi taarifa maeneo ya mbali na Halmashauri hali ambayo inaweza kusababisha upotevu wa taarifa wakati wa kuharibika kwa mfumo, kupasuka kwa hifadhidata au majanga mengine kama moto katika chumba kilichowekwa hifadhidata au majengo ya Halmashauri husika. Kutokana na hali hii, upotevu au kuharibika kwa data inaweza kupelekea kutopatikana kwa data hizo pindi zinapohitajika.
- Kutokuwepo kwa mpango wa kujikinga na majanga na vipimo vya kujikinga na majanga havijawahi kufanyika. Kukosekana kwa mpango wa kujikinga na majanga kunasababisha ugumu katika kurejesha mfumo kwa wakati na kukosekana kwa vyanzo vya vipimo vya data kwa ajili ya kurejesha data husika na hakuna atakayehusika na urejeshwaji wa

taarifa. Hii inasababisha hatari katika mpango endelevu wa Halmashauri husika.

Kutokana na haya ninashauri yafutayo yafanyike;

- OWM-TAMISEMI inatakiwa iwezeshe Mamlaka ya Serikali za Mitaa kuanzisha sera na taratibu za teknolojia ya habari ili kila mtumiaji aweze kuelewa majukumu na wajibu wake katika kutunza vifaa na programu za teknolojia ya habari.
- Mamlaka ya Serikali za Mitaa zinatakiwa zihakikishe kuwa, kumbukumbu za akiba zinachukuliwa mara kwa mara na kuhifadhiwa katika jengo lililo mbali na hifadhidata. Sehemu ya kuhifadhiwa ni lazima iwe na usalama na ya kufikika kwa urahisi. Vilevile kuwe na majaribio ya kuangalia kumbukumbu za akiba kwa kutumia hifadhidata na mabadiliko mapya katika Mfumo Funganifu wa Usimamizi wa Fedha (IFMS).
- Mamlaka za Serikali za Mitaa zinatakiwa ziwe na mpango wa kujikinga na majanga, hii ina maana ya kuandaa, kuandika, kujaribu na kutekeleza mpango wa kujikinga na majanga ambao unalenga mfumo funganifu wa usimamizi wa fedha (IFMS) pamoja na mifumo mingine muhimu katika kila Halmashauri.

### 5.1.7 Kuzuia na Kudhibiti Udanganyifu

Viwango vya Kimataifa vya Ukaguzi (ISA) 240 vinafafanua udanganyifu kama "kitendo cha makusudi kinachofanywa na mtu mmoja au zaidi ndani ya menejimenti, wale wanaohusika na utawala bora, wafanyakazi, au watu wa nje, wakishiriki kwa njia ya udanganyifu ili kupata faida kwa njia isiyo ya haki au haramu." Jukumu la msingi la kuzuia na kutambua udanganyifu ni la wale wanaohusika na utawala bora, wafanyakazi wa Halmashauri na uongozi.

Ni muhimu kuzuia na kudhibiti Udanganyifu katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa. Ni moja ya masuala mengi ambayo yanahitaji kusimamiwa kwa ufanisi na kuhakikisha kuwa Mamlaka ya Serikali za Mitaa zinafuata kanuni za utawala bora.

Lengo la kutathmini udanganyifu ni kulihakikishia Bunge kwamba Mamlaka ya Serikali za Mitaa zina mfumo sahihi katika kusaidia kuzuia na kupambana na udanganyifu na kutambua maeneo ya kufanyia maboresho.

Tathmini zilizofanyika katika jumla ya Halmashauri 68 kama inavyoonyeshwa katika **kiambatisho (xii)** inaonyesha kuwa, uongozi wa Halmashauri husika haukuwa na kumbukumbu za kimaandishi zilizoidhinishwa za mipango ya kuzuia udanganyifu. Pia, hapakuwa na mchakato iliyowekwa bayana kutoka katika uongozi wa Halmashauri husika ya kutambua na kukabiliana na vihatarishi vinavyohusiana na udanganyifu katika Halmashauri husika.

Aidha, viashiria hatari ambayo ni dalili ya udanganyifu ni kama vifuatavyo:

- Mapungufu katika Kamati ya Ukaguzi,
- Kukosekana kwa hati za malipo,
- Kuwepo kwa matukio ambayo mapato hayakuwasilishwa benki kwenye akaunti za Halmashauri.
- Hati za malipo kuwa na nyaraka pungufu,
- Taarifa za hesabu kuwa na makosa.
- Kutokuwepo kwa kamati ya ukaguzi na mapokezi wa mali zilizonunuliwa.
- Mapungufu katika usimamizi wa mali, utunzaji wa kumbukumbu na kufanya tathimini ya mali za kudumu.
- Mishahara ambayo haikulipwa kwa watumishi
- kutopelekwa Hazina.
- Ukosefu wa udhibiti ili kuhakikisha kuwa mapato yote ambayo hayajakusanywa yanakusanywa na yanaingizwa kwa usahihi katika taarifa za fedha.
- Kukosekana kwa stakabadhi za kukusanyia mapato.
- Malipo ya mishahara kwa watumishi hewa
- Mapungufu katika kamati ya ukaguzi

Asili ya viashiria vya udanganyifu vilivyoainishwa hapo juu, vinaathiri udhibiti wa ndani na hivyo kuficha udanganyifu unaofanywa na uongozi na/au wafanyakazi wa ngazi ya chini na unaweza kusababisha uongozi wa Halmashauri kutogundua na kushindwa kuzuia udanganyifu.

Kwa kuwa wajibu wa kugundua na kuzuia udanganyifu ni wa uongozi wa Halmashauri husika, mianya yaliyoainishwa ambayo yanaweza kuwa ni chanzo cha udanganyifu na ni lazima kizuiwe pamoja na kuandaa sera za kuzuia udanganyifu. Aidha, uongozi unatakiwa kuweka kumbukumbu na kuidhinisha mipango ya kuzuia udanganyifu na mara kwa mara kufanya tathimini za vihatarishi.

Udhibiti wa udanganyifu ni lazima uunganishwe na majukumu na mipango ya Halmashauri na ionekane kwamba ni jukumu la kila mtu katika Halmashauri. Ni wajibu wa kila mmoja kutambua na kufanya kila awezalo kuzuia na kugundua, kuepuka makosa yasitendeke na mafunzo ya ufahamu yatolewe kwa watumishi.

## 5.2. Usimamizi wa Maduhuli

Usimamizi wa maduhuli ni matumizi ya elimu ya uchambuzi ambao unabashiri tabia ya jamii na huduma bora na ongezeko la mapato. Lengo kuu la usimamizi wa maduhuli ni kutoa huduma inayotakiwa katika jamii sahihi kwa muda unaotakiwa na kwa kiasi kinachotakiwa.

Wakati wa ukaguzi wa mwaka 2010/11, baadhi ya mapungufu yalibainika katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa yanayohusiana na usimamizi wa maduhuli kama ifuatavyo:

### 5.2.1 Vitabu 682 vya Makusanyo ya Mapato Kutowasilishwa

Agizo Na. 101 na 102 la Memoranda ya Fedha za Mamlaka ya Serikali za Mitaa, 1997 imebainishwa kuwa, maafisa wote waliopewa vitabu vya makusanyo lazima wawasilishe taarifa ya vitabu vilivyotumika na vile ambavyo havijatumika kila mwisho wa mwezi na endapo kuna upotevu wowote wa vitabu, uripotiwe kwa afisa anayehusika mapema iwezekanavyo. Nakala ya taarifa hiyo iwasilishwe kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na msaidizi wa afisa anayehusika. Kinyume na maagizo haya, vitabu 682 vya makusanyo kutoka katika jumla ya Halmashauri 36 havikuwasilishwa kwa ukaguzi kama inavyoonekana katika **kiambatisho (xiii)**

Mwelekeo wa vitabu vya makusanyo visivyowasilishwa kwa miaka ya fedha ya 2006/07, 2007/08, 2008/09 2009/10 na 2010/11 unaweza kuainishwa kama ifuatavyo;

| Mwaka | Idadi ya vitabu vilivyokosekana | Idadi ya Halmashauri |
|---|---|---|
| 2006/07 | 996 | 8 |
| 2007/08 | 860 | 43 |
| 2008/09 | 1341 | 50 |
| 2009/10 | 948 | 48 |
| 2010/11 | 682 | 36 |

Taarifa zilizoainishwa hapo juu zinaweza kuonyeshwa kwenye grafu zifuatazo;




Tafsiri ya grafu hapo juu ni kwamba, hakuna mahusiano kati ya idadi ya vitabu vya mapato vilivyokosekana na idadi ya Halmashauri zilizohusika. Kwa wastani wa Halmashauri 37 katika miaka mitano (5) mfululizo, idadi ya vitabu vilivyokosekana ilipungua kwa vitabu 136 kutoka mwaka 2006/07 hadi 2008/09 na kuongezeka kwa vitabu 481 kutoka mwaka 2007/08 hadi 2008/09. Kutoka mwaka 2008/09 hadi 2009/10 mpaka 2010/11 idadi ya

vitabu visivyowasilishwa imepungua kwa vitabu 393 na 269 katika mfululizo huohuo.

Kwa kuwa vitabu hivi vilikusudiwa kukusanya mapato ya Halmashauri, kiasi kilichokusanywa kwa kutumia vitabu hivyo hakikiweza kujulikana. Hali hii inadhihirisha kuwa, kuna uwezekano mkubwa wa wizi wa mapato ya Halmashauri na kupotosha makisio ya mapato ya Halmashauri.

Hivyo inashauriwa kuwa, uongozi wa Halmashauri zinatakiwa kuweka mifumo imara ya udhibiti katika usimamizi wa vitabu vya makusanyo ili kuondoa uwezekano wa upotevu wa fedha za Halmashauri. Vilevile Halmashauri husika zinatakiwa kuwasilisha vitabu vilivyokosekana kwa ajili ya ukaguzi.

Hatua za haraka zichukuliwe ikiwa ni pamoja na kuwachukulia hatua za kisheria wale wote walioshindwa kuwasilisha makusanyo ya Halmashauri.

### 5.2.2 Maduhuli Yasiyorejeshwa na Mawakala Sh.4,360,299,618

Agizo Na. 110 la Memoranda ya Fedha za Mamlaka ya Serikali za Mitaa, 1997 imeainisha kuwa, makusanyo yote ya Halmashauri yawasilishwe kwa watunza fedha wa Halmashauri husika kwa usalama.

Kinyume na Agizo hilo, ukaguzi uliofanywa katika jumla ya Halmashauri 46 kama zinavyoonyeshwa katika **kiambatisho (xiv)** ulibaini kuwa, kiasi cha Shs.4,360,299,618 kilichokusanywa na Mawakala mbalimbali hakikuwasilishwa kwa mtunza fedha wa Halmashauri husika.

Mchanganuo wa maduhuli yasiyowasilishwa kwenye Halmashauri husika kwa miaka miwili ni kama inavyoonekana katika jedwali lifuatalo;

| Mwaka | Maduhuli yasiyowasilishwa (Sh) | Idadi ya Halmashauri husika |
|---|---|---|
| 2009/10 | 2,756,763,702 | 43 |
| 2010/11 | 4,360,299,618 | 48 |

Kutokana na jedwali hapo juu imedhihirika kuwa, kiasi cha makusanyo yasiyowasilishwa kimeongezeka kwa kiasi cha Sh.1,603,535,916 sawa na 58% kutoka Sh.2,756,763,702 katika mwaka 2009/10 hadi Sh.4,360,299,618 katika mwaka 2010/11. Hii inaonyesha udhaifu katika mfumo wa udhibiti wa ndani na mapungufu katika usimamizi wa mikataba ya makusanyo.

Menejimenti za Halmashauri zinatakiwa kuimarisha udhibiti wa ndani katika makusanyo ya maduhuli yatokanayo na vyanzo vya ndani ikiwa ni pamoja na kuboresha taratibu za kuingia mikataba na kufuatilia marejesho kutoka kwa mawakala wa makusanyo.

### 5.2.3 Fedha zisizokusanywa kutoka katika vyanzo vya ndani Sh.8,332,986,175

Agizo Na. 120 la Memoranda ya Fedha za Mamlaka ya Serikali za Mitaa, 1997 linaeleza kuwa, itakuwa jukumu la Mweka Hazina wa Halmashauri kuweka mipango thabiti ya kifedha na kihasibu ili kuhakikisha usahihi katika ukusanyaji na utunzaji wa fedha zote za Halmashauri ambazo hazijakusanywa. Kinyume na Agizo hili, ukaguzi umebaini kuwa, kiasi cha fedha cha Sh.8,332,986,175 kutoka vyanzo vya ndani vya Halmashauri hayakukusanywa kutoka kwa walipa kodi husika kama inavyoonyeshwa katika jedwali lifuatalo:

| Na | Halmashauri | Chanzo cha mapato | Kiasi kisichokusanywa (Sh |
|---|---|---|---|
| 1. | H/M Ilala | Mabango ya matangazo, ushuru wa huduma mbali mbali na kodi ya majengo | 1,382,625,902 |
| 2. | H/M Kinondoni | Mabango ya matangazo | 906,613,704 |
| 3. | H/M Dodoma | Mabango ya matangazo na ushuru wa maegesho | 327,842,806 |
| 4. | H/W Biharamulo | Minara ya mawasiliano | 35,000,000 |
| 5. | H/M Bukoba | Mabango ya matangazo | 315,642,595 |
| 6. | H/W Ngara | Leseni za uwindaji | 19,800,000 |
| 7. | H/W Chato | Fukwe za ziwa | 2,112,000 |
| 8. | H/W Mbeya | Ushuru wa huduma | 3,712,300 |
| 9. | H/W Kilombero | Ushuru wa miwa | 1,365,308,289 |
| 10. | H/W Kilosa | Ushuru wa miwa | 1,270,628,385 |
| 11. | H/W Morogoro | Ushuru wa huduma | 328,500,000 |
| 12. | H/W Ulanga | Minara ya mawasiliano | 19,200,000 |
| 13. | H/W Mvomero | Ushuru wa miwa | 375,826,802 |
| 14. | H/M Masasi | Ushuru wa mazao kutoka AMCOS | 25,356,960 |
| 15. | H/J Mwanza | Pango la vibanda vya soko | 13,483,000 |
| 16. | H/W Mpanda | Ushuru kutoka kwa mawakala wa zao la tumbaku | 252,739,447 |
| 17. | H/W Mbinga | Ushuru wa stendi ya basi, vibanda vinavyozunguka stendi na maeneo ya gereji za kutengeneza magari | 7,010,000 |
| 18. | H/W Manyoni | Ushuru wa nyumba za kulala wageni | 44,418,750 |
| 19. | H/W Singida | Ada ya kamisheni kutoka SUMATRA | 9,501,100 |
| 20. | H/W Pangani | Kodi ya nyumba na mauzo ya viwanja | 8,871,883 |
| 21. | H/W Nzega | Ushuru na pango la vibanda soko kuu. | 66,000,000 |
| 22. | H/W Urambo | Punjo kutokana na viwango pungufu vya ushuru wa tumbaku vilivyotozwa | 1,552,792,252 |
| | **Jumla** | | **8,332,986,175** |

Kutokana na jedwali hapo juu, inaashiria udhaifu katika kutumia fursa mbalimbali za ukasanyaji wa maduhuli na inaonesha jinsi Halmashauri zinavyoshindwa kuboresha vyanzo vya mapato vilivyopo. Kwa hiyo, ni jukumu la menejimenti za Halmashauri kuweka mipango thabiti ya kiuhasibu ili kuhakikisha ukusanyaji na utunzaji mzuri wa maduhuli.

## 5.3 Usimamizi wa Fedha

Usimamizi wa fedha kwa ujumla unahusisha makusanyo na mapokezi ya fedha za umma, pia usimamizi wa akaunti za benki za Halmashauri kwa lengo la kuweka fedha za kutosha kukidhi mahitaji ya kila siku ya Halmashauri na wakati huo huo kuongeza kiasi cha kutosha kwa ajili ya

uwekezaji kwa kuendeleza mifumo ya udhibiti ya ndani katika kupokea na kutoa fedha, kuanzisha taratibu endelezi kwa ajili ya ukusanyaji wa kodi, kuanzisha mawasiliano mazuri kati ya mweka hazina na wakuu wa idara na kuendeleza uhusiano imara wa kitaalamu kati ya benki za ndani na wawekezaji wengine.

Wakati wa ukaguzi katika usimamizi wa fedha katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa, baadhi ya mapungufa yalibainika kama yafuatayo:

### 5.3.1 Masuala ya Usuluhisho wa Kibenki Yasiyoshughulikiwa

Agizo Na. 68 la Memoranda ya Fedha za Mamlaka ya Serikali za Mitaa, 1997 linataka kila Mweka Hazina katika Halmashauri wahakikishe kuwa usuluhisho wa kibenki ukiwemo udhibiti kati ya kitabu cha mapato na hati za benki zinafanywa kila Mwezi na marekebisho ya hesabu zenye tofauti yanaingizwa katika vitabu vya hesabu.

Kinyume na Agizo hili, jumla ya Halmashauri 88 zilikuwa na masuala ya usuluhisho wa kibenki yasiyoshughulikiwa. Pia hakuna ushahidi unaoonyesha kuwa taarifa za usuluhisho wa kibenki zinahakikiwa na maafisa wafawidhi. Mchanganuo wa masuala ya usuluhisho wa kibenki yasiyoshughulikiwa kwa mwaka unaoishia Juni 30, 2011 ni kama yafuatayo:

- Kiasi cha Sh.4,662,975,016 kutoka Halmashauri 46 kiliingizwa kama mapato katika vitabu vya fedha vya Halmashauri bila kuingizwa katika taarifa za kibenki.
- Kiasi cha Sh.10,897,078,986 zilizolipwa kwa watu mbalimbali katika Halmasahuri 81 hazikuwasilishwa benki hadi mwaka wa fedha ulipoisha Juni 30, 2011.
- Hakuna jitihada zilizofanyika kuhakikisha kiasi cha Sh.425,988,776 kama fedha ambazo hazijafika benki kutoka Halmashauri 8 vimeingizwa katika taarifa za kibenki kama fedha ambazo hazijafika.
- Kiasi cha Sh.1,002,195,882 kilichukuliwa kutoka benki na jumla ya Halmashauri 21 lakini hazikuingizwa kwenye vitabu vya fedha.
- Kiasi cha Sh.401,528,675 kilipokelewa kwenye taarifa za benki mbalimbali za jumla ya Halmashauri 22 lakini hazikuingizwa kwenye vitabu vya fedha vya Halmashauri husika.

Jedwali lifuatalo linaonyesha mchanganuo wa masuala ya usuluhisho wa kibenki yasiyoshuhulikiwa kwa miaka ya fedha 2009/10 na 2010/11.

| Mwaka | Mapokezi katika vitabu vya fedha bila kuingiza katika taarifa za kibenki(Sh.) | Hundi ambazo Hazikupelekwa Benki (Sh.) | Fedha ambazo Hazijafika benki (Sh.) | Malipo benki hayajaingizwa katika vitabu vya fedha (Sh.) | Mapato Benki hayakuoneka katika daftari la fedha (Sh.) |
|---|---|---|---|---|---|
| 2009/10 | 9,612,413,862 | 28,792,732,991 | 805,665,694 | 2,586,187,823 | 1,257,775,757 |
| 2010/11 | 4,662,975,016 | 10,887,247,851 | 425,988,776 | 1,002,195,882 | 401,528,675 |

Taarifa katika jedwali hapo juu zinaweza kuonyeshwa katika mapiramidi yafuatayo:




Kutokana na mapiramidi hapo juu, inaonyesha kwamba;

- Kiasi kilichoingizwa katika vitabu vya fedha vya Halmashauri bila kuingizwa katika taarifa za kibenki yalipungua kwa Sh.4,949,438,846 kutoka mwaka 2009/10 hadi 2010/11.
- Kiasi kilicholipwa kwa watu mbalimbali ambacho hazikuwasilishwa benki zilipungua kwa Sh.17,895,654,005 kutoka Mwaka 2009/10 hadi 2010/11.
- Fedha ambazo hazijafika benki ambazo hazikuingizwa katika taarifa za kibenki kama fedha ambazo hazijafika zilipungua kwa Sh.379,676,918 kutoka Mwaka 2009/10 hadi 2010/11.
- Kiasi kilichochukuliwa kutoka benki bila kuingizwa kwenye vitabu vya fedha zilipungua kwa Sh.1,583,991,941 kutoka mwaka 2009/10 hadi 2010/11.
- Kiasi kilichopokelewa kwenye taarifa za benki mbalimbali ambazo hazikuingizwa kwenye vitabu vya fedha vya Halmashauri husika zilipungua kwa Sh.856,247,082 hadi 2010/11.

Makosa na ubadhirifu wa fedha za Serikali yanaweza yasibainike kwa muda mrefu na uongozi wa Halmashauri husika kama masuala yanayohusu usuluhishi wa benki hayatashughulikiwa mapema. Hali hii inaweza kusababisha hasara zisizohitajika kwenye Halmashauri husika na wakati mwingine inaweza kusababisha kuwa chanzo cha udanganyifu. Kwa hali hiyo, uongozi wa Halmashauri husika unatakiwa kuhakikisha kuwa usuluhisho wa benki unafanywa kila mwezi na kuidhinishwa na maafisa waandamizi, pia marekebisho yafanyike katika vitabu vya hesabu.

Mchanganuo wa masuala yanayohusu usuluhisho wa kibenki yasiyoshulikiwa na Halmashauri husika umeonyeshwa kwenye **Kiambatisho (xv)**.

### 5.3.1 Uhakiki na Ukaguzi wa Fedha wa Kushtukiza

**(i) Ukaguzi wa Fedha wa Kushtukiza**

Agizo Na.170 la Memoranda ya Fedha za Mamlaka ya Serikali za Mitaa, 1997 linamtaka Mkurugenzi au Mwakilishi wake kuratibu uhakiki wa fedha taslimu wa kushtukiza mara kwa mara. Kinyume na agizo hili, ukaguzi umebaini kuwa, Halmashauri 38 hazikufanya wala hazikuwa na utaratibu wa kuhakiki fedha na Mkurugenzi au Mwakilishi wake kama inavyoonekana katika **kiambatisho (xvi)**

**(ii) Kiwango cha juu cha kutunza fedha**

Agizo Na.352 la Memoranda ya Fedha za Mamlaka ya Serikali za Mitaa, 1997 imeainisha kwamba, kiwango cha juu cha kuhifadhi fedha kwa kila Halmashauri kikubaliwe na kamati ya Fedha na Mipango na kiwango hicho hakitakiwi kuzidi bila kibali cha kamati. Hatahivyo, ukaguzi wa kushtukiza uliofanywa katika Halmashauri 16 ulibaini kuwa, Halmashauri hizo hazikuwa na viwango maalumu vilivyoidhinishwa na kamati za fedha kinyume na Agizo kama inavyoonyeshwa katika **kiambatisho (xvi)**

### 5.3.2 Masurufu yasiyorejeshwa Sh.984,955,534

Agizo Na.134 na 136 la Memoranda ya Fedha za Mamlaka ya Serikali za Mitaa, 1997 limeainisha kuwa, masurufu maalumu au ya safari ni lazima yarejeshwe ndani ya wiki mbili (2) tangu mtumishi anapotoka safari au baada ya shughuli maalumu kukamilika. Kushindwa kufanya hivyo siyo tu kwamba kutalazimisha makato ya kiasi kisichorejeshwa yafanyike kutoka katika mshahara mtumishi husika katika kiwango ongezeko bali pia kunaweza kupelekea tozo lisilo chini ya asilimia 5% ya mshahara wa mtumishi huyo. Vilevile, masurufu yasiyorejeshwa kwa zaidi ya mwezi mmoja bila kujali kama tozo limetozwa au hapana kutapelekea tozo ya riba isiyopungua ile inayotumika benki kwa muda huo.

Kinyume na agizo hilo, masurufu ya Sh.984,955,534 yaligundulika kuwa hayajarejeshwa kutoka katika Halmashauri 33 hadi kufikia mwisho wa mwaka kama inavyoonyeshwa katika **Kiambatisho (xvii)**

Hata hivyo haikujulikana endapo kama maafisa masuuli wa Halmashauri hizo walichukua hatua kulingana na agizo hilo kuhusiana na ucheleweshaji wa marejesho ya masurufu kutoka kwa wahusika.

### 5.3.3 Upotevu wa Fedha/Vifaa Sh.34,436,525

Maagizo Na.134 na 136 ya Memoranda ya Fedha za Mamlaka ya Serikali za Mitaa, 1997 zimeainisha kuwa, endapo kutatokea upotevu wa fedha taslimu au vifaa, itabidi taarifa itolewe kwa Mkurugenzi Mtendaji.
Ripoti inatakiwa iwe na vifuatavyo;

- Asili ya upotevu, kiwango, tarehe ilipogundulika na ni nani mhusika.
- Jinsi upotevu huo ulivyotokea.
- Sababu ya kwa nini upotevu huo ulishindwa kuzuiliwa na mfumo wa udhibiti na usimamizi wa ndani.
- Hatua zilizochukuliwa kuzuia kutokea tena.
- Tarehe ya kutolewa kwa taarifa ya upotevu huu polisi.
- Endapo mtumishi anahusika, utaratibu upi uliopendekezwa ikiwa ni pamoja na urejeshwaji wa fedha hizo, hatua za kinidhamu au hatua za kisheria pamoja na uwezekano wa tozo.

Jumla ya Sh.34,436,525 ikiwa ni fedha taslimu na vifaa zimeripotiwa kuwa zimepotea zikihusisha Halmashauri tatu (3) kama inavyoonyeshwa katika jedwali lifuatalo:

| Na. | Halmashauri husika | Aina ya upotevu | Kiasi/thamani (Sh.) |
|---|---|---|---|
| 1. | H/W Kasulu | Fedha taslim | 17,810,000 |
| 2. | H/W Rombo | Vifaa | 3,239,025 |
| 3. | H/M Shinyanga | Fedha taslim | 13,387,500 |
| | **Jumla** | | **34,436,525** |

Hata hivyo, haikujulikana endapo kama kuna hatua zozote zilizochukuliwa dhidi ya wahusika wa matukio haya kama inavyoagizwa na Memoranda ya Fedha za Mamlaka ya Serikali za Mitaa hapo juu.

## 5.4 Usimamizi wa Rasilimaliwatu

Usimamizi wa Rasilimaliwatu katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa ni shughuli inayolenga uboreshaji wa Rejista ya taarifa zote zinazohusu watumishi wake zikiwemo mishahara, kupandishwa vyeo, uhamisho, vifo, kufukuzwa kazi, kuhakikisha kuwa taarifa zote muhimu za waajiriwa zinapatikana kwa wakati katika kitengo cha Mishahara, kujua wasio kuwepo kazini. Usimamizi wa rasilimaliwatu pia ni mfumo ambao inahakikisha tarifa zote zinazohusiana na mishahara na mabadiliko ya malipo yana pokelewa kwa wakati. Vilevile, Usimamizi wa rasilimaliwatu inahusiana na usimamizi wa upimaji wa utendaji kazi wa watumishi (OPRAS), mfumo ambao kila mtumishi anatakiwa kutimiza wajibu wake, na inaweka bayana misingi ya tathmini za kila mwaka.

Wakati wa Ukaguzi wa mwaka 2010/11, tathmini zilifanyika katika ufanisi wa usimamizi wa rasilimaliwatu na mishahara kwa mwaka ulioisha Juni 30, 2011. Baadhi ya mapungufu yaliyobainika ni kama yafuatayo:

### 5.4.1 Kutokuwepo/Mapungufu Katika Mfumo wa Kupima Utendaji Kazi wa Watumishi (OPRAS)

Ukaguzi katika sampuli ya Waajiriwa wa Mamlaka za Serikali za Mitaa imebaini kuwa, jumla ya Halmashauri 17 kama zilivyoorodheshwa katika jedwali lifuatalo hawakuwa na utaratibu wa kupima mara kwa mara utendaji kazi wa watumishi

kinyume na Kif. D (62-63) cha Taratibu za kudumu za utumishi wa umma, 2009. Tathmini nyingi zilifanyika kwa watumishi katika Makao Makuu na hasa wale ambao wanasubiri kupandishwa vyeo. Halmashari husika ni kama yafuatayo.

| Na. | Jina la Halmashauri |
|---|---|
| 1 | Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo |
| 2 | Halmashauri ya Wilaya ya Songea |
| 3 | Halmashauri ya Wilaya ya Kahama |
| 4 | Halmashauri ya Wilaya ya Bariadi |
| 5 | Halmashauri ya Wilaya ya Maswa |
| 6 | Halmashauri ya Wilaya ya Bukombe |
| 7 | Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu |
| 8 | Halmashauri ya Wilaya ya Meatu |
| 9 | Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga |
| 10 | Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga |
| 11 | Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa |
| 12 | Halmashauri ya Wilaya ya Kilombero |
| 13 | Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro |
| 14 | Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro |
| 15 | Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga |
| 16 | Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru |
| 17 | Halmashauri ya Manispaa ya Arusha |

Kukosekana kwa mfumo wa upimaji utendaji kazi wa watumishi, ni vigumu kuweza kutambua watumishi ambao wanastahili kupongezwa, kupandishwa vyeo au kuondolewa katika utumishi. Pia Halmashauri husika itashindwa kuelewa utendaji kazi wa watumishi wake waliopo katika ngazi mbalimbali.

Inashauriwa kuwa, uongozi wa Halmashauri husika zihakikishe kuwa mfumo wa upimaji wa utendaji kazi wa watimishi wake (OPRAS) unakuwepo ili iwe rahisi kutambua, kuchanganua na kuweka kumbukumbu za utendaji wa watumishi wake ili zisaidie katika kuchukua hatua za uboreshaji.

### 5.4.2 Kutokuwepo na Kutoboresha Rejesta za Watumishi

Agizo Na. 302 la Memoranda ya Fedha za Mamlaka ya Serikali za Mitaa, 1997 linamtaka mkuu wa Idara ya Rasilimaliwatu kutunza na kuboresha rejesta yenye orodha na kumbukumbu za watumishi wote. Pia Agizo Na. 307 la Memoranda hiyohiyo, linaagiza kuwa mishahara isiyolipwa kumbukumbu zake zitunzwe na kuingizwa kwenye rejesta ya mishahara isiyolipwa. Kinyume na maagizo hayo, ukaguzi ulibaini mapungufu katika jumla ya Halmashauri 15 kama ifuatavyo;

- Rejesta za mishahara isiyolipwa hazitunzwi na mara nyingi taarifa za namba za wafanyakazi na sababu za kutokulipwa mishahara havionyeshwi katika rejesta hizo.
- Hakuna mfumo maalum ya kuhakikisha kuwa, taarifa zote za muhimu zinapokelewa katika kitengo cha mishahara.
- Vitengo vya mishahara hawatunzi taarifa kudhibiti mishahara inayolipwa kwa wasiofika makazini.

Mapungufu haya yameonekana katika Halmashauri zifuatazo;

| Na. | Mkoa | Jina la Halmashauri |
|---|---|---|
| 1 | Mbeya | H/W Ileje |
| 2 | Shinyanga | H/W Kishapu |
| 3 | Kagera | H/W Bukoba |
| 4 | Dodoma | H/W Mpwapwa |
| 5 | Morogoro | H/W Kilombero |
| 6 | Morogoro | H/A Kilosa |
| 7 | Morogoro | H/W Morogoro |
| 8 | Morogoro | H/M Morogoro |
| 9 | Morogoro | H/W Mvomero |
| 10 | Morogoro | H/W Ulanga |
| 11 | Tabora | H/W Igunga |
| 12 | Tanga | H/W Kilindi |
| 13 | Tanga | H/W Lushoto |
| 14 | Coast | H/W Kibaha |

Mamlaka za Serikali za Mitaa zinatakiwa zihakikishe kwamba zinatunza kumbukumbu sahihi za watumishi wake ili kuepuka uwezekano wa kulipa watumishi hewa. Vile vile Idara za Rasilimaliwatu zinatakiwa kuanzisha na kuboresha rejesta za watumishi ili kuweza kusimamia masuala yote yanayohusu watumishi ikiwemo mishahara na stahili zao zingine.

### 5.4.3 Halmashauri Haziandai Usuluhisho wa Mishahara za kila Mwezi

Katika utaratibu mzuri, Mamlaka ya Serikali za Mitaa zinatakiwa kuandaa usuluhisho kati ya fomu za orodha ya walipwaji na kiasi cha mshahara na fomu ya makato ya kisheria kutoka Hazina (fomu Na.11 na Na.12) kwa minajili ya kuangalia kama fedha zilizotumwa kama mshahara kwa mwezi husika zinatosha ili kuepuka kulipa mshahara kwa kutumia hela za makusanyo ya Halmashauri.

Hata hivyo, wakati wa ukaguzi kulibainika kwamba, baadhi ya Halmashauri hazifanyi usuluhisho kati ya fomu za orodha ya walipwaji na kiasi cha mshahara na fomu ya makato ya kisheria na kiasi kinachopokelewa toka hazina. Uthibitisho huu ulionekana katika sampuli ya Halmashauri tano 5 zifuatazo;

| Na. | Mkoa | Halmashauri |
|---|---|---|
| 1 | Sindida | Halmashauri ya Manispaa ya Singida |
| 2 | | Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni |
| 3 | kilimanjaro | Halmashauri ya Wilaya ya Rombo |
| 4 | Ruvuma | Halmashauri ya Wilaya ya Songea |
| 5 | Manyara | Halmashauri ya Wilaya ya Hanang' |

Kukosekana kwa usuluhisho wa mishahara wa kila mwezi, malipo yanaweza kupunguzwa na Hazina bila Halmashauri husika kugundua. Hii itazisababisha Halmashauri husika kutumia fedha za makusanyo ya ndani kulipa mishahara na makato ya kisheria ambayo hayapo kwenye makisio.

Uongozi wa Mamlaka ya Serikali za Mitaa zinatakiwa zihakikishe kuwa, usuluhisho wa mishahara wa kila mwezi unafanyika kabla ya malipo, nyaraka za usuluhisho zihifadhiwe vizuri na mawasiliano na Hazina yafanyike mara moja pale inapobainika kuwa mishahara iliyoletwa ni pungufu ili kuepuka kutumia fedha za makusanyo ya Halmashauri kulipa mishahara.

**5.4.4 Mishahara Isiyolipwa ambayo Haikurejeshwa Hazina Sh.4,400,144,124**

Agizo Na. 307 la Memoranda ya Fedha za Mamlaka ya Serikali za Mitaa, 1997 linaagiza kwamba, mishahara isiyolipwa inatakiwa ipelekwe benki ndani ya siku kumi (10) za kazi. Pia maelekezo kutoka Wizara ya Fedha ambayo yalitolewa kwa barua yenye Kumb. Na.EB/AG/5/03/01/Vol.VI/136 ya Agosti 31, 2007 ambayo inaelekeza kwamba mishahara yote isiyolipwa inatakiwa kurejeshwa Hazina kupitia kwa Katibu Tawala wa Mkoa.

Kinyume na maagizo hayo, ukaguzi wa mishahara umebaini kwamba, kuna mishahara isiyolipwa kiasi cha Sh.4,400,144,124 katika Halmashauri 46 kama inavyoonyeshwa katika **Kiambatisho (xviii)** ambazo hazikuweza kurejeshwa Hazina**.** Hali hii inaweza kusababishwa na ukosefu wa uwajibikaji katika mishahara isiyolipwa ambayo inaweza kusababisha hasara katika Halmashauri husika.

Inashauriwa kuwa, Halmashauri husika zihakikishe kuwa mishahara isiyolipwa inarejeshwa Hazina haraka kupitia Ofisi za Makatibu Tawala wa Mikoa na Hazina ihakikishe kuwa kiasi husika kimerejeshwa kama inavyotakiwa.

**5.4.5 Mishahara Iliyolipwa kwa Watumishi Waliostaafu, Walioachishwa Kazi, Waliofariki Sh.961,394,959**

Wakati wa ukaguzi wa mfumo wa malipo ya mishahara na rejesta za mishahara isiyolipwa kwa mwaka wa fedha ulioishia Juni 30, 2011 ilibainika kwamba, kiasi cha Sh.961,394,959 kililipwa na Halmashauri 36 kama zinavyoonyeshwa katika **Kiambatisho (xix)** ikiwa ni mishahara kwa watumishi ambao aidha wamestaafu, wamejiuzulu, wameachishwa kazi au wametoroka na majina yao yameendelea kuonekana katika mfumo wa malipo ya mishahara.

Hii inaashiria udhaifu katika udhibiti wa ndani kwenye Mamlaka ya Serikali za Mitaa jambo ambalo linaweza kusababishia hasara serikali kwa kulipa watumishi hewa.

Uongozi wa Halmashauri husika unatakiwa ufanye uchunguzi na kuhakikisha kuwa mishahara iliyolipwa kwa wasiokuwa watumishi inarejeshwa na kupelekwa Hazina kupitia ofisi za Makatibu Tawala wa Mikoa kama ilivyoelekezwa kwenye barua yenye Kumb. Na. CA:307/334/01 iliyotolewa tarehe 15/01/2010.

Ninasisitiza kuwa, OWM-TAMISEMI, Ofisi ya Raisi - Menejimenti ya Utumishi wa Umma pamoja na Hazina wanatakiwa waanzishe uhusiano wa karibu na

kuchukua takwimu ya watumishi katika utumishi wa umma na baada ya hapo, waandae mfumo imara wa udhibiti wa ndani ili uweze kutumiwa na Mamlaka ya Serikali za Mitaa.

### 5.4.6 Mikopo kwa Watumishi Isiyodhibitiwa

Waraka wa utumishi Na. CCE.45/271/01/87 wa tarehe 19/03/2010 unaelekeza kwamba, makato katika mishahara ya watumishi yanatakiwa yasizidi 2/3 ya mishahara yao.
Hata hivyo imebainika kwamba kuna wafanyakazi wengi wa Halmashauri wanakatwa zaidi ya 2/3 ya mishahara yao. Pia kuna baadhi ya watumishi wamekuwa wakikatwa mshahara wote.

Katika jumla ya Halmashauri 55 zilizokaguliwa, kumebainika kuwepo kwa jumla ya watumishi 8827 ambao wanapokea chini ya 1/3 ya mishahara yao kama inavyoonekana katika **Kiambatisho (xx).**

Mikopo isiyodhibitiwa inaweza kuleta madhara makubwa kwa watumishi husika katika ufanisi wa kazi na katika Halmashauri husika. Matatizo hayo ya mishahara yanachangiwa na uongozi wa Halmashauri husika kutokuwa makini kwa kuhakikisha masilahi ya wafanyakazi ni salama.

Inashauriwa kuwa, udhibiti wa malipo ya mishahara unatakiwa kwamba, zaidi ya kuhakikisha kuwa watumishi husika wanalipwa mshahara unaotakiwa, pia usawa katika malipo lazima uangaliwe. Kufanya hivyo itazuia uwezekano wa kuwa na madhara katika ufanisi wa watumishi.

### 5.4.7 Tofauti Kati ya Fedha za Mishahara Zilizopokelewa toka Hazina na Fedha Zilizolipwa Sh.267,544,718

Ukaguzi umebaini fedha pungufu za mishahara zilizopokelewa kutoka Hazina kwenda katika Halmashauri. Katika kulinganisha fedha za mishahara kutoka Hazina na kiasi cha fedha kilicholipwa kwa watumishi kama mishahara kwa mwaka wa fedha 2010/11 imebainika kuwa, jumla ya Halmashauri 6 kama ilivyo changanuliwa katika jedwali lifuatalo zilikuwa na fedha za mishahara zilizopokelewa kutoka Hazina pungufu kwa cha Sh.267,544,718:

| Na. | Halmashauri | Kilichopokelewa (Sh.) | Kilicholipwa (Sh.) | Tofauti (Sh.) |
|---|---|---|---|---|
| 1. | H/W Kahama | 14,953,194,946 | 14,953,983,436 | 788,489 |
| 2. | H/W Bunda | 10,989,222,708 | 11,027,876,490 | 38,902,383 |
| 3. | H/W Njombe | 1,936,775,988 | 1,956,056,223 | 19,280,235 |
| 4. | H/W Chunya | 6,017,691,354 | 6,071,867,128 | 54,175,774 |
| 5. | H/W Mbeya | 8,303,441,870 | 8,402,202,979 | 98,761,109 |
| 6. | H/W Arusha | 11,410,698,661 | 11,452,491,359 | 55,636,726 |
| | | **Jumla** | | **267,544,718** |

Kwa kuwa kiasi kilichopokelewa na Halmashauri kutoka Hazina ni pungufu kuliko walicholipa, hii ina maana kuwa, Halmashauri husika zilitumia fedha nyingine ambazo hazikuwa zimekasimiwa kwa ajili ya kulipa mishahara.

Mamlaka ya Serikali za Mitaa zinashauriwa kufanya usuluhisho kati ya taarifa za mishahara ya watumishi na taarifa za fedha zilizopokelewa kutoka Hazina zinazotunzwa katika Ofisi za Makatibu Tawala wa Mikoa na kuwasiliana na Hazina haraka ili waweze kulipwa ikiwa itabainika kuwa kiasi cha fedha kilichotumwa ni pungufu kulinganisha na kiasi cha mishahara kinachotakiwa kulipwa.

### 5.4.8 Kutokuwepo kwa Usahihi wa Tarehe ya Kuzaliwa kwa Watumishi Katika Mfumo wa Malipo ya Mishahara

Mfumo wa malipo ya mishahara hauko imara. Ukaguzi uliofanyika katika tarifa kutoka katika mfumo wa malipo ya mishahara za watumishi wa Halmashauri za mkoa wa Mara kama inavyoonekana katika jedwali lifuatalo ilibaini kuwa, tarehe za kuzaliwa za jumla ya watumishi 3819 hazikuwa sahihi. Imeonekana kuwa tarehe za kuzaliwa ziliingizwa kama 1/1/1700 na 1/1/1900;

| Na. | Halmashauri | Idadi ya watumishi husika |
|---|---|---|
| 1 | Bunda DC | 935 |
| 2 | Musoma DC | 547 |
| 3 | Musoma MC | 524 |
| 4 | Rorya DC | 587 |
| 5 | Tarime DC | 815 |
| 6 | Serengeti DC | 411 |
| | **Jumla** | **3819** |

Hii ina maanisha kuwa tarehe za kustaafu za watumishi husika hazijulikani na kusimamiwa na Hazina.

Uongozi wa Halmashauri husika unashauriwa kuwa, taarifa za watumishi na taarifa katika mfumo wa kulipia mishahara kutoka Hazina zinasuluhishwa na terehe za kuzaliwa zinasahihishwa ipasavyo.

### 5.4.9 Watumishi Wasiochangia katika Mifuko ya Jamii, Bima ya Afya na Kodi ya Mapato

Ukaguzi katika sampuli ya Halmashauri 3 kwa mwezi wa Juni 2011 imebaini kuwepo kwa watumishi wasiochangia katika Mifuko ya Jamii (watumishi 366), Bima ya Afya (watumishi 44) na Kodi ya Mapato (watumishi 23) kama inavyoonyeshwa kwenye jedwali lifuatalo;

| Na | Halmashauri | Idadi ya Watumishi wasiochangia | | |
|---|---|---|---|---|
| | | Mifuko ya Jamii | Bima ya Afya | Kodi ya Mapato |
| 1 | H/W Ileje | 43 | 44 | 23 |
| 2 | H/W Ukerewe | 182 | | |
| 3 | H/W Mbozi | 141 | | |
| | **Jumla** | **366** | **44** | **23** |

Madhara ya kutokuchangia makato haya ya kisheria ni kwamba watumishi husika watakosa mafao yao wakati wa kustaafu, hawatapata huduma za afya na pia mapato ya serikali kupungua kutokana na kutokatwa kodi ya mapato.

Inashauriwa kwamba, wakaguzi wa ndani wa Halmashauri husika wafanye ukaguzi wa mishahara na pia kupitia mara kwa mara taarifa za watumishi ili kama kuna mapungufu yaweze kufanyiwa kazi mapema.

### 5.4.10 Makato Ya Kisheria ambayo Hayakuwasilishwa katika Taasisi Husika Sh.316,614,938

Wakati wa kupitia nyaraka mbalimbali za mishahara ikiwa ni pamoja na nyaraka za benki na fomu Na.11 kutoka Hazina ilibainika kuwa, kiasi cha makato ya kisheria cha Sh.316,614,938 katika jumla ya Halmashauri 4 hayakuwasilishwa katika taasisi husika kama vile LAPF, PSPF, NSSF, PPF na TRA kama ifuatavyo;

| Na. | Mkoa | Jina la Halmashauri | Kiasi(Sh.) |
|---|---|---|---|
| 1 | Dodoma | H/M Dodoma | 126,882,042 |
| 2 | Morogoro | H/W Kilosa | 165,019,277 |
| 3 | Tabora | H/W Nzega | 22,329,780 |
| 4 | Ruvuma | H/W Namtumbo | 2,383,839 |
| | | **Jumla** | **316,614,938** |

Kutokana na jedwali hapo juu, imedhihirika kuwa, kuna uwezekano wa Halmashauri husika kushtakiwa na taasisi husika kwa kutowasilisha makato ya kisheria. Pia, kiasi cha miadi katika taarifa za hesabu husika kimeingizwa pungufu kwa Sh.316,614,938.

Inashauriwa kuwa, Mamlaka ya Serikali za Mitaa zihakikishe kuwa makato yote ya kisheria yanalipwa katika Taasisi husika na kuwasilisha uthibitisho wa nyaraka kwa ajili ya ukaguzi.Vile vile kiasi cha madeni ambacho hakijawasilishwa katika Taasisi husika kionyeshwe katika taarifa za hesabu za mwisho wa mwaka.

### 5.4.11 Kutowasilishwa kwa Stakabadhi za Kupokelea Mishahara Isiyolipwa na Makato ya Kisheria Yaliyolipwa Sh.521,617,627

Kiasi cha Sh.521,617,627 zikiwa ni Sh.192,486,204 kama mishahara iliyorudishwa Hazina kupitia Ofisi za Makatibu Tawala wa Mikoa kutoka Halmashauri tano (5) na Sh.329,131,422 kama makato ya kisheria yaliyolipwa katika taasisi mbalimbali kutoka katika Halmashauri tisa (9) hayakuweza kuthibitika kama yamepokelewa na taasisi husika kwa vile stakabadhi ya kupokelea hazikuwasilishwa kuthibitisha kiasi cha fedha kilicholipwa kinyume na Agizo Na. 5 (c) la Memoranda ya Fedha za Mamlaka ya Serikali za Mitaa, 1997. Halmashauri husika ni kama zinavyoonyeshwa katika majedwali yafuatayo:

(h) Halmashauri zisizowasilisha stakabadhi za kupokelea mishahara iliyorejeshwa Hazina kupitia Ofisi za Makatibu Tawala wa Mikoa kiasi cha Sh.192,486,204.

| Na. | Mkoa | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh) |
|---|---|---|---|
| 1 | Morogoro | H/W Kilosa | 140,192,319.52 |
| 2 | Iringa | H/W Njombe | 16,238,333.19 |
| 3 | Rukwa | H/M Sumbawanga | 17,232,199.13 |
| 4 | Mtwara | H/W Nanyumbu | 5,246,592.00 |
| 5 | Shinyanga | H/W Maswa | 13,576,761.00 |
| | | **Jumla** | **192,486,204.84** |

(ii) Halmashauri zisizowasilisha stakabadhi za kupokelea makato ya kisheria yaliyolipwa kwenye taasisi mbalimbal kiasi cha Sh.329,131,422.

| Na | Halmashauri | Taasisi | Kiasi (Sh) |
|---|---|---|---|
| 1 | H/W Bukombe | Bima ya Afya na TALGWU | 9,528,143 |
| 2 | H/W Shinyanga | Bodi ya Mikopo Ya Elimu ya Juu (HESLB) | 4,364,760 |
| 3 | H/W Meatu | Mfuko wa Jamii wa Serikali Za Mitaa (LAPF) | 1,930,488 |
| 4 | H/W Urambo | Mifuko Mbalimbali ya Jamii na Taasisi za Fedha na Michango ya Hiari | 66,117,798 |
| 5 | H/W Iringa | Mifuko Mbalimbali ya Jamii na Taasisi za Fedha na Michango ya Hiari | 11,929,415 |
| 6 | H/M Iringa | Mifuko Mbalimbali ya Jamii na Taasisi za Fedha na Michango ya Hiari | 23,915,927 |
| 7 | H/W Mafia | Mifuko ya Jamii wa Serikali za Mitaa na Serikali kuu (LAPF na PSPF) | 73,518,099 |
| 8 | H/W Rufiji | Mifuko Mbalimbali ya Jamii na Michango ya Hiari | 56,441,591 |
| 9 | H/W Kibaha | Mifuko ya Jamii wa Serikali za Mitaa na Serikali kuu (LAPF na PSPF) | 81,385,201 |
| **Jumla** | | | **329,131,422** |

Kukosekana kwa stakabadhi za kupokea malipo hayo kutoka kwa walipwaji inadhihirisha kuwa, kuna uwezekano wa malipo hayo kufanyika kwa walipwaji wengine kimakosa.

Uongozi wa Mamlaka ya Serikali za Mitaa unatakiwa kuimarisha mfumo wa udhibiti wa ndani katika kufuatilia wahusika mara moja baada ya kuhakikisha kuwa malipo yote yamefanyika.

### 5.4.12 Watumishi Wanaotumia Akaunti Moja Ya Benki

Ukaguzi uliofanyika kwenye orodha ya walipwaji mishahara na nyaraka nyinginezo zilizotumwa na Wizara ya Fedha kwa mameneja wa mabenki kwa ajili ya kulipia mishahara umebaini kuwa, baadhi ya watumishi wanatumia akaunti moja ya benki. Kiasi cha Sh.79,809,738 katika Halmashauri ya wilaya ya Kilombero na kiasi cha Sh.28,923,897 katika Halmashauri ya wilaya ya Morogoro kililipwa kwa watumishi mbalimbali ambao walikuwa wanatumia akaunti moja ya benki.

Kutumia akaunti moja ya benki kunaweza kupelekea mtu mmoja kulipwa mara mbili kwa majina tofauti hivyo kusababisha ubadhilifu wa fedha za umma na kuzuia utekelezaji wa shughuli zingina za Serikali.

Hivyo, Halmashauri zinatakiwa zipitie kwa makini akaunti za benki za watumishi wake ili kama kuna mapungufu yaweze kufanyiwa kazi haraka. Pia, uongozi wa Mamlaka ya Serikali za Mitaa zihakikishe kuwa, kila mtumishi ana akaunti yake binafsi ya benki inayojulikana kabla ya kuwalipa mishahara yao ya kila mwezi.

### 5.4.13 Majina ya Watumishi yaliyoonekana zaidi ya mara moja katika Orodha ya Walipwaji Mishahara

Ukaguzi uliofanywa kwenye mfumo kulipia mishahara umebaini kuwa, kuna jumla ya watumishi 11 walioonekana kuwa na namba ya utambulisho (check number) zaidi ya moja kama inavyoonyeshwa katika jedwali lifuatalo.

| Na. | Mkoa | Halmashauri | Idadi ya Watumishi |
|---|---|---|---|
| 1 | Morogoro | H/W Kilombero | 4 |
| 2 | Morogoro | H/M Morogoro | 3 |
| 3 | Morogoro | H/W Ulanga | 1 |
| 4 | Ruvuma | H/W Namtumbo | 3 |
| **Jumla** | | | **11** |

Kutokuwepo kwa usuluhisho wa idadi halisi ya watumishi waliopo na wale wanaoonekana katika mfumo wa kulipia mishahara kunaweza kusababisha mishahara kulipwa zaidi ya kiasi kinachostahili.

Kwa mtumishi kulipwa zaidi ya mshahara mmoja kwa mwezi kunaashiria ubadhilifu wa fedha za umma hivyo kufanya fedha zilizolipwa zaidi kwa watumishi kushindwa kufanya kazi nyinginre za kimaendeleo.

Uongozi wa Halmashauri husika unatakiwa zipitie kwa makini hali iliyojitokeza ya ulipwaji wa mshahara zaidi ya mmoja kwa watumishi na kuhakikisha usuluhisho unafanywa haraka na vyombo vinavyohusika. Pia uongozi uhakikishe kuwa kiasi kilicholipwa zaidi kinarejeshwa Hazina kupitia ofisi za Makatibu Tawala wa Mikoa.

### 5.4.14 Mishahara Iliyolipwa Zaidi ya Viwango Vilivyoidhinishwa Sh.42,869,832

Ukaguzi uliofanyika katika malipo ya mishahara katika sampuli ya Halmashauri 3 umebaini kuwa, jumla ya watumishi 22 walilipwa mishahara ambayo ni zaidi kwa Sh.42,869,832 ya viwango vilivyoidhinishwa na Katibu Mkuu – Ofisi ya Raisi Menejimenti ya Utumishi wa Umma katika waraka wenye Kumb. Na.C/AC.45/257/01/C/14 wa tarehe 26/10/2006. Halmashauri husika ni kama zinavyoonyeshwa katika jedwali lifuatalo:

| Na. | Halmashauri | Watumishi Wanaohusika | Kiasi Kilicholipwa (Sh) |
|---|---|---|---|
| 1 | H/W Ludewa | 18 | 36,621,300 |
| 2 | H/Mji Njombe | 1 | 4,361,226 |
| 3 | H/W Meru | 3 | 1,887,306 |
| | **Jumla** | **22** | **42,869,832** |

Ninashauri kuwa, Maafisa wanaohusika na Rasilimaliwatu wanatakiwa kuhakikisha kuwa, Waraka na miongozo mbalimbali inayotolewa kuhusiana na malipo ya mishahara inazingatiwa. Vilevile kiasi kilicholipwa zaidi ya stahiki kwa watumishi hao kinatakiwa kirejeshwe kutoka kwa watumishi husika.

### 5.4.15 Makato mara mbili Kutoka Kwenye Mishahara ya Watumishi Sh.65,007,802

Ukaguzi wa mishahara kwa miezi ya Februari na Machi 2011 umebaini kuwa, kiasi cha Sh.65,007,802 ikiwa ni Sh.37,185,550 kama makato katika mishahara ya watumishi wa Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara na Sh.27,822,252 kama makato katika Halmashauri ya Wilaya ya Njombe. Hata hivyo ilibainika kuwa kiasi tajwa kilikatwa kwa mara mbili katika Halmashauri hizo kutoka katika mishahara ya watumishi hao na kulipa taasisi hizo hizo.

| Na. | Halmashauri | Miezi Husika | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|
| 1 | H/M Mtwara | Februari na Machi 2011 | 37,185,550 |
| 2 | H/Mji Njombe | Februari na Machi 2011 | 27,822,252 |
| | | **Jumla** | **65,007,802** |

Taarifa katika jedwali linaashiria kuwa, watumishi husika waliokatwa mara mbili katika mishahara yao wameathirika kifedha kwa kiasi tajwa.

Uongozi wa Halmashauri unatakiwa ihakikishe inafanya usuluhishi wa malipo na kiasi kilichozidi kirejeshwe kwa watumishi husika. Pia inatakiwa iwe sera kwa Mamlaka ya Serikali za Mitaa kufanya usuluhishi wa malipo ya mishahara kila mwezi.

### 5.4.16 Mikopo ya Mishahara Isiyorejeshwa Sh.32,875,432

Agizo Na. 137 la Memoranda ya Fedha za Mamlaka ya Serikali za Mitaa, 1997 inaeleza kuwa, Mkurugenzi anaweza kuidhinisha mkopo wa mishahara ya hadi miezi mitatu ambayo inatakiwa iwe imelipwa ndani ya miezi kumi na mbili kwa kukatwa kiasi kinacholingana kwa kila mwezi.

Hata hivyo, ukaguzi wa hati za malipo katika Halmashauri nne (4) ulibaini kuwa, kiasi cha Sh.32,875,432 kilitolewa kama mkopo kwa watumishi lakini hakikuwa kimerejeshwa hata mwisho wa mwaka. Halmashauri husika ni kama inavyoonekana katika jedwali lifuatalo.

| Na. | Halmashauri | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|
| 1 | H/W Hai | 14,475,503 |
| 2 | H/W Siha | 5,150,000 |
| 3 | H/W Makete | 9,630,294 |
| 4 | H/W Sumbawanga | 3,619,635 |
| | **Jumla** | **32,875,432** |

Kutokurejeshwa kwa mikopo tajwa kwa muda kunaweza kuathiri utekelezaji wa shughuli zilizopangwa na kukasimiwa kutokana na ukosefu wa fedha na pia kuna uwezekano wa mikopo hiyo kutokurejeshwa kabisa.
Uongozi wa Halmashauri husika unatakiwa uzingatie agizo Na. 137 la Memoranda ya Fedha za Mamlaka ya Serikali za Mitaa, 1997 na kuhakikisha kwamba mikopo hiyo inarejeshwa na kuwasilisha nyaraka za ushahidi kwa ukaguzi.

### 5.4.17 Majina ya Watumishi Waliostaafu Kutofutwa katika Mfumo wa Malipo ya Mishahara

Agizo Na. 302 la Memoranda ya Fedha za Mamlaka ya Serikali za Mitaa, 1997 linamtaka Mkuu wa Idara ya Rasilimaliwatu kutunza na kuboresha rejesta yenye orodha na kumbukumbu za watumishi wote ambao utaarifu Hazina kuhusiana na mambo yota yanayohusiana na walioajiriwa, waliojuizulu, waliofukuzwa, waliohamishwa na tarifa zingine muhimu ili kutunza taarifa hizo kwa ajili ya malipo ya kodi ya mapato, kuchangia mifuko n.k.
Kwa upande mwingine, Kif. Na. 57(1) cha Sheria Na. 8 ya Utumishi wa Umma, 2002 inaeleza kuwa, mtumishi atakayekuwa nje ya kituo chake cha kazi kwa siku zinazozidi tano bila ruhusa atachukuliwa hatua za kisheria na kuadhibiwa kwa kufukuzwa.

Kinyume na sheria zilizotajwa hapo juu, wakati wa kukagua mfumo wa malipo ya mishahara na pia ukaguzi wa daftari la mishahara isiyolipwa kwa kipindi kilichoisha Juni 30, 2011 ilibainika kuwa jumla ya watumishi 120 kutoka kwenye sampuli ya Halmashauri saba (7) zinavyoonyeshwa kwenye jedwali lifuatalo walikuwa aidha wamefariki, wamestaafu, wameacha au wamefukuzwa kazi lakini majina yao bado yalikuwa hayajafutwa katika mfumo wa malipo ya mishahara;

| Na. | Halmashauri | Idadi ya Watumishi |
|---|---|---|
| 1 | H/W Bunda | 7 |
| 2 | H/W Musoma | 18 |
| 3 | H/W Tarime | 3 |
| 4 | H/W Igunga | 57 |
| 5 | H/W Njombe | 5 |
| 6 | H/W Handeni | 17 |
| 7 | H/W Morogoro | 13 |
| | **Jumla** | **120** |

Kucheleweshwa kufutwa majina ya watumishi waliostaafu, waliofariki au kuacha kazi kunasababisha kuwepo na ongezeko makisio ya mshahara na pia kupoteza fedha za umma kwa kulipa watumishi hewa.

Uongozi wa Halmashauri husika wanatakiwa kuakikisha kuwa majina ya watumishi waliofariki, waliostaafu au kuacha kazi yanafutwa kwenye Mfumo wa kulipa mishahara na vile vile zifuatilie marejesho ya fedha zilizolipwa kama makato ya watumishi hao kutoka kwenye taasisi husika zilizolipwa.

### 5.4.18 Ubadhilifu wa Mishahara Isiyolipwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa Sh.20,893,662

Ukaguzi wa mishahara ya watumishi katika Hlmashauri ya Wilaya ya Kilosa ulibaini kuwa, kiasi cha Sh.95,688,250 ikiwa ni mishahara isiyolipwa kilichukuliwa kutoka benki na mtunza fedha wa Halmashauri katika Miezi ya Desemba 2010 na Januari 2011 kwa ajili ya kulipa watumishi ambao hawakuwa na akauti za benki. Hata hivyo, wakati wa kupitia nyaraka za malipo, nyaraka za benki na kitabu cha fedha ilibainika kuwa, kiasi cha Sh.63,797,588 kililipwa kwa wahusika na kiasi kingine cha Sh.11,000,000 kilirudishwa benki ya NMB Kilosa na kuingizwa kwenye akaunti ya amana yenye namba 218100003, kuacha baki ya Sh.20,893,662 ambacho hakikuwa kimelipwa wala kuthibitishwa kurejeshwa benki.

Hii inamaanisha kwamba, kiasi kilichobaki bila kulipwa au kurejeshwa benki kinaweza kuwa kimetumiwa vibaya na uongozi wa Halmashauri husika au na mtumishi/watumishi waliopewa dhamana ya kutunza fedha na hivyo kusababisha hasara ya kiasi tajwa. Pia hili limesababishwa na kutokuwepo kwa uthibiti na uwajibikaji katika malipo ya mishahara.

Menejimenti ya Halmashauri inatakiwa ifanye uchunguzi wa kina na kuhakikisha kuwa kiasi cha Sh.20,893,662 kinarejeshwa.

### 5.4.19 Malipo Holela ya Mishahara kwa Fedha Taslimu Sh.191,194,302

Wakati wa ukaguzi wa hati za malipo na vithibitisho vyake ilibainika kuwa, kiasi cha Sh.191,194,302 kama malipo ya mshahara kililipwa na Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro kama fedha taslimu kwa watumishi kupitia dirishani badala ya kuingiza mishahara hiyo kwenye akaunti binafsi za walipwaji. Madhara ya kulipa mishahara kwa kutumia fedha taslimu kupitia dirishani badala ya kutumia akaunti binafsi za walipwaji ni pamoja na;

- Kiasi kikubwa cha fedha katika ofisi ya mtunza fedha ambao ni kinyume na kiwango kilichowekwa na kamati kama inavyoainishwa katika Agizo Na. 352 ya Memoranda ya Fedha za Mamlaka ya Halmashauri za Serikali za Mitee, 1997.

- Utaratibu huu unaleta usumbufu kwa watumishi walio mbali na Halmashauri kutumia muda mwingi na gharama kufuata mishahara yao.

Uongozi wa Halmashauri unashauriwa kuwa waajiriwa wanahimizwa kufungua akaunti binafsi za benki ili zitumike katika kulipa mishahara yao.

## 5.5 Usimamizi wa Mali Katika Halmashauri
### 5.5.1 Usimamizi wa Mali za Kudumu
#### 5.5.1.1. Kutokutunzwa kwa Rejista ya Mali za Kudumu

Agizo Na. 366 na 367 la Memoranda ya Fedha ya Mamlaka za Serikali za Mitaa ya mwaka 1997 linaagiza Halmashauri kutunza daftari la mali za kudumu litakaloonyesha tarehe ya manunuzi, bei ya kununulia, maelezo kuhusu mali zilizouzwa au kununuliwa katika mwaka husika.

Kinyume na maagizo hayo, katika sampuli ya Halmashauri ishirini na mbili (22) Halmashauri mbili (2) hazikuwa na rejista ya mali za kudumu, Halmashauri kumi na tano (15) zilikuwa na rejista ambazo hazikuandaliwa ipasavyo ili kuimarisha udhibiti wa mali za kudumu. Halmashauri 6 zilizosalia zilikuwa hazikuandika namba za mali zake za kudumu na katika hizo Halmashauri moja ilikuwa haina rejista kabisa. Zaidi ya hayo baadhi ya rejista za mali za kudumu hazikuhuishwa ili kuonyesha mali zilizonunuliwa, kuuzwa au zilizohamishwa kwa kipindi cha mwaka husika.

Kulingana na hali hiyo hapo juu, inakuwa vigumu kuthibitisha usahihi wa mali za kudumu zinazomilikiwa na Halmashauri. Menejimenti za Halmashauri zinatakiwa kutunza rejista za mali za kudumu zinazoonesha taarifa zote muhimu za mali za Halmashauri.

Jedwali lifuatalo linaonyesha Halmashauri ambazo aidha hazitunzi rejista za mali au rejista zilizopo hazijaboreshwa ipasavyo:

| Na. | Halmashauri | Rejista ya mali za kudumu haitunzwi ipasavyo | Hakuna rejista ya mali za kudumu | Mali hazikuandikwa namba |
|---|---|---|---|---|
| 1. | H/M Arusha | | | √ |
| 2. | H/W Arusha | | | √ |
| 3. | H/W Monduli | | | √ |
| 4. | H/W Longido | | √ | √ |
| 5. | H/M Arusha | | √ | |
| 6. | H/W Mbinga | √ | | |
| 7. | H/W Namtumbo | √ | | |
| 8. | H/M Songea | √ | | |
| 9. | H/W Tunduru | √ | | |
| 10. | H/W Mbeya | √ | | |
| 11. | H/W Biharamulo | √ | | |
| 12. | H/Jiji Mwanza | | | √ |
| 13. | H/W | √ | | |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | sengerema | | | |
| 14. | H/W Shinyanga | √ | | |
| 15. | H/W Bahi | | | √ |
| 16. | H/M Dodoma | √ | | |
| 17. | H/W Mpwapwa | √ | | |
| 18. | H/W Iramba | √ | | |
| 19. | H/W Nzega | √ | | |
| 20. | H/W Urambo | √ | | |
| 21. | H/W Masasi | √ | | |
| 22. | H/ Mji wa Masasi | √ | | |
| | **Jumla** | **15** | **2** | **6** |

### 5.5.1.2 Mali za kudumu zisizotumika

Katika mwaka wa ukaguzi, Halmashauri kumi na saba (17) zilikuwa na Mali za kudumu ambazo zilikuwa hazitumiki na kutelekezwa kinyume na maagizo Na.159-161 ya Memoranda ya fedha za Serikali za Mitaa ya mwaka 1997 na aya Na.26 ya IPSAS 21 na 23. Hata hivyo, kati ya idadi ya Halmashauri iliyotajwa hapo juu, Halmashauri 15 zimetelekeza mali za kudumu zisizo onyesha thamani yake, wakati Halmashauri mbili (2) zimetelekeza mali za kudumu zenye thamani ya Shs.133, 157,150 kama inavyoonekana katika aya (i) na (ii) zifuatazo kwa mtiririko huo;

**(i) Mali za kudumu zilizotelekezwa zisizoonyesha thamani yake**

Mapitio ya taarifa za fedha za Halmashauri 15 ilionekana kuwa, kulikuwa na orodha ya mali ambazo zilionyeshwa bila thamani. Mapungufu haya yana athari ya kuonyeshwa kwa thamani ndogo za Halmashauri kama ilivyoripotiwa katika taarifa za fedha na kama inavyoonyeshwa katika **kiambatisho (xxi)**

**(ii) Mali za kudumu zilizotelekezwa Sh. 133,157,150**

| Na. | Halmashauri | Maelezo | Idadi | Kiasi (Sh) |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Halmashauri ya Wilaya ya Babati | Magari yasiyotumika; magari chakavu ambayo yametelekezwa katika eneo la Halmashauri kinyume na Agizo Na.159 ya Memoranda ya Fedha za Serikali za Mitaa ya Mwaka 1997 ni pamoja na STG 2154 Isuzu bodi refu, STJ 3454 Toyota Hilux (D/C0, 3488 CW | 4 | 124,000,000 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | Wheel Loader na CW 3480 greda | | |
| 2. | Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni | **Vifaa chakavu vyenye thamani ya Sh.9,157,150** Uhahakiki uliofanyika katika sehemu kulikotunzwa vitu hivyo ulibainisha vitu chakavu vyenye thamani ya Sh 9,157,150 ambavyo vipo stoo kwa muda mrefu bila kufutwa kwenye vitabu vya Halmashauri. | Vitu mbali mbali | 9,157,150.00 |
| | | **Jumla** | | **133,157,150.00** |

### 5.5.1.3 Mali za Kudumu Ambazo Hazikuthaminishwa

IPSASs Na.17 inaagiza kwamba, mali zinatakiwa kuthaminiwa na kutambuliwa katika taarifa za fedha zinazotolewa na kwamba zitaendelea kutambuliwa katika hesabu kwa kiasi ambacho kimethaminishwa. Thamani inayotambuliwa itazingatia kutolewa kwa thamani ya uchakavu na hasara inayotokana kwa mali isiyotumika.

Kinyume na muongozo huu, Uongozi wa Halmashauri 13 kama inavyoonekana katika **Kiambatisho (xxii),** haukuthaminisha mali zake ingawa baadhi ya mali hizo zilionyeshwa katika hesabu kama ni mali ambazo hazina thamani kabisa wakati katika hali halisi mali hizi ziliendelea kutumiwa na Halmashauri.

Kutokana na hali hii, thamani ya mali za kudumu zilizoonyeshwa katika taarifa za fedha za Halmashauri husika hazitoi taswira halisi ya Halmashauri.

### 5.5.1.4 Kukosekana kwa nyaraka zinazohusiana na umiliki wa mali za kudumu Shs.30,928,516,441

Agizo Na. 202 na 203 la Memoranda ya fedha za Serikali za Mitaa ya mwaka 1997 linaagiza kwamba Uwekezaji wa zaidi ya fedha taslimu utafanyika baada ya azimio la uongozi wa Halmashauri na utajumuishwa katika bajeti ya Maendeleo au bajeti ya Matumizi ya Kawaida. Uwekezaji kama huo utathibitishwa na kwa kuwa na hati au mkataba ambao utaingizwa katika rejista na kutunzwa katika sehemu ya usalama .

Kinyume na maagizo hayo hapo juu, wakati wa ukaguzi mali nyingi hazikuwa na ushahidi wa maandishi wa umiliki, kutokana na mazingira hayo ukaguzi ulizuiliwa kupata uhakika wa kuwepo, usahihi, umiliki, na uhalali wa mali iliyo katika taarifa za fedha. Mali hizo zenye thamani ya Sh. 30,928,516,441

zinazohusiana na Halmashauri kumi na nne (14) kama inavyoonekana katika **kiambatanisho (xxiii)**

### 5.5.1.5 Kukosewa kwa Thamani ya Mali za Kudumu Katika Taarifa za Fedha 5,574,172,011

Katika mwaka uliokaguliwa Halmashauri nane (8) kama zilivyoorodheshwa katika jedwali hapa chini, aidha zilizidisha au kupunguza thamani za mali za kudumu katika taarifa za fedha. Kukosewa kwa taarifa hii katika taarifa za fedha kulisababishwa na kufanya marekebisho ya kuthaminisha mali za kudumu kusikofaa, majedwali ya mali kutoonyesha mitambo na Vifaa kama ilivyoonyesha katika hesabu na makosa ya katika kukokotoa uchakavu. Pia, bakaa ya Mali za kudumu kutoka mwaka wa fedha uliopita kuhamishiwa katika mwaka huu kwa tarakimu tofauti. Hivyo kutokana na makosa haya, taarifa za fedha zimekosewa katika jumla ya Shs.5,574,172,011. Kukosewa huku kwa thamani ya mali kunapotosha watumiaji wa taarifa za fedha kutokana na ukweli kwamba taarifa zilizotolewa sio sahihi na wala hazionyeshi hali halisi, na kwamba sio za kutegemewa kwa ajili ya kufanyia maamuzi.

| Halma-shauri | Maelezo | Kiasi kilichozidishwa Kimakosa (Sh) | Kiasi kilichopunguzwa Kimakosa (Sh) | Jumla (Sh) |
|---|---|---|---|---|
| Halmashauri ya Wilaya ya Kilombero | Majedwali yanayoonyesha ongezeko la mali za kudumu na kazi zinazoendelea hayakuletwa | - | 719,485,138 | 719,485,138 |
| “ | Hasara iliyotokana na kuthaminisha mali za kudumu haikurekebishwa katika taarifa ya mtirirko wa fedha | 28,755,199 | - | 28,755,199 |
| Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro | Majedwali yanayoonyesha ongezeko la mali za kudumu na kazi zinazoendelea hayakuletwa | 3,868,065,392 | - | 3,868,065,392 |
| Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro | Makosa katika kutambua na kupima mali za kudumu | 720,241,285 | - | 720,241,285 |
| “ | Kuonyeshwa pungufu kwa thamani ya mali za kudumu | - | 13,253,505 | 13,253,505 |
| Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni | Kuonyeshwa zaidi kimakosa kwa thamani ya mali | 128,781,727 | - | 128,781,727 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema | Kuonyeshwa zaidi kimakosa kwa thamani ya mali za kudumu | 24,800,922 | - | 24,800,922 |
| Halmashauri ya Wilaya ya Kwimba | Kuonyeshwa zaidi kimakosa kwa salio anzia la thamani ya mali za kudumu | 48,631,991 | - | 48,631,991 |
| Halmashauri ya Wilaya ya Ngorongoro | Kuonyeshwa zaidi kimakosa kwa uchakavu wa mali zitokanazo na vyanzo vya Halmashauri | 22,156,851 | - | 22,156,851 |
| | **Jumla** | **4,841,433,367** | **732,738,643** | **5,574,172,010** |

### 5.5.1.6 kutoonyeshwa kwa Mali za Kudumu Katika Taarifa za Fedha Sh.41,456,500

Memoranda ya fedha za Serikali za Mitaa inasema kwamba Uwekezaji wote utafanywa na Mkurugenzi kwa jina la Halmashauri kwa Mujibu wa agizo Na. 200 na 203 na kuwa Uwekezaji huo utathibitishwa na hati au mkataba ambayo utaingizwa katika rejesta na kutunzwa katika sehemu ya usalama.

Ukaguzi wa mapitio ya taarifa za fedha umebaini matukio ambayo ni kinyume na maagizo yaliyotajwa na Memoranda hapo juu ambapo uwekezaji na Mali za Halmashauri nne (4) haukuonyeshwa katika taarifa za fedha kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2011. Kwa sababu hiyo taarifa za fedha zimekosa ushahidi kwa watumiaji wa taarifa hizo kutokana na ukweli kwamba, mali hizo aidha zimeonyeshwa pungufu kimakosa katika taarifa za fedha au mali hizo hazikuonyeshwa katika taarifa za fedha kama ifuatavyo:

| Halmashauri | Maelezo | Kiasi (Sh) |
|---|---|---|
| Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu | Mali za kudumu hazikuonyeshwa katika rejista | 8,956,500 |
| Halmashauri ya Manispaa ya Arusha | Uwekezaji kutoonyeshwa katika taarifa za fedha | 32,500,000 |
| Halmashauri ya Wilaya ya Mpanda | **Magari yaliyopokelewa kutoka shirika la wakimbizi duniani (UNHCR) hayakuonyeshwa katika taarifa za fedha** Toyota L/C Station wagon DFP 6728 (Iko katika hali nzuri), Toyota L/C Station wagon DFP 6753 (Iko katika hali nzuri), Lori-Scania 124 DFP 3769 (Hali ya wastani), Lori-Scania 124 DFP 2991 ( Iko katika hali mbaya) Pia zilikosekana nyaraka kuhusiana kuhalalisha uhamishaji wa umiliki wa mali | |

| | | |
|---|---|---|
| | hizi kutoka UNHCR kuja Halmashauri. | |
| Halmashauri ya Mji wa Mpanda | **Magari yaliyopokelewa kutoka shirika la wakimbizi duniani (UNHCR) hayakuonyeshwa katika taarifa za fedha**<br>Uhakiki uliofanywa kuhusiana na mali za kudumu uligundua kwamba Halmashauri ilipewa magari mawili (2) kutoka Shirika la wakimbizi duniani yenye namba za usajiri DFP 2872 na DFP 3768 ambayo hayakuonyeshwa katika taarifa za fedha kama mali za kudumu za Halmashauri. | |

### 5.5.2 Wadaiwa wasiolipa Sh. 37,795,747,360

Ukaguzi wa taarifa za fedha za Halmashauri mia moja na tisa (106) umeonyesha jumla ya Sh. 37,795,747,360 ikiwa ni madai mbalimbali ambayo hayajarejeshwa kama ilivyoainishwa kwenye K**iambatisho (xxiv).**

Aina za wadaiwa katika Halmashauri zilizo nyingi ni fedha zilizolipwa kabla ya huduma, Maduhuli kutoka kwa mawakala wa kukusanya mapato, Masurufu na karadha za watumishi na Mikopo ya Wanawake na Vijana

Jedwali hapa chini linaonyesha ulinganisho wa wadaiwa kwa miaka minne yaani 2007/08, 2008/09, 2009/2010 na 2010/2011.

| Mwaka | Kiasi (Shs.) | Idadi ya Halmashasuri |
|---|---|---|
| 2007/08 | 8,675,739,790 | 115 |
| 2008/09 | 35,644,785,554 | 113 |
| 2009/10 | 44,059,104,038 | 109 |
| 2010/11 | 37,795,747,360 | 106 |

Ulinganisho huo unaweza kuonyeshwa katika grafu kama ilivyo hapa chini:




Grafu hapo juu inaonyesha kuongezeka kwa wadaiwa kutoka mwaka 2007/08 kwenda mwaka 2008/09 na pia kwenda mwaka 2009/10 kwa sh. 26.8 bill. Na sh. 8.5 bill. kwa mfuatano.

Pia inaonyesha kwamba mwaka 2009/10 kwenda 2010/11 wadaiwa walipungua kwa sh.6.3bill.kutoka sh.44.1bill kwenda sh.37.8bill kama ilivyoonyeshwa katika hesabu za 2009/10 na 2010/11 kwa mfuatano.

Kuwa na rasilimali ambazo zimeshikiliwa kwa njia ya wadaiwa ni kinyume na Agizo Na 120 na 121 la Memoranda ya Fedha ya Mamlaka za Serikali za Mitaa, 1997 ambalo linaeleza wazi kuwa "litakuwa jukumu la mweka hazina kuweka mipango mizuri ya kiuhasibu ili kuhakikisha ukusanyaji, utunzaji na upelekaji wa fedha benki" pia Agizo linamtaka mweka hazina "pale inapowezakana kuhakikisha kuwa fedha zote zikusanywe kabla au wakati wa kutoa huduma".

Kushindwa kukusanya fedha za wadaiwa kwa wakati ni ishara ya udhaifu katika kusimamia madeni na ukosefu wa sera madhubuti juu madeni. Halmashauri zinashauriwa kuongeza juhudi katika usimamizi wa rasilimali ikiwemo kuanzisha kanuni na taratibu na kuweka kipaumbele katika usimamizi wa ukusanyaji wa madeni bila kuathiri utoaji wa huduma.

### 5.5.3 Wadai wasiolipwa Sh.52,132,811,928

Ulipaji wa madeni kwa wakati ni jambo muhimu na linaleta imani kati ya Halmashauri na wasambazaji wa vifaa na huduma na kuongeza hali ya kuaminiwa na jamii inayohudumia Halmashauri.

Hata hivyo, ukaguzi wa Hesabu za Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni 2011 ulibaini kuwa Halmashauri 111 zilikuwa na wadai wasiolipwa wenye jumla ya Sh. 52,132,811,928 ikiwa ni punguzo la Sh. 91,697,531 ikilinganishwa na Sh. 52,041,114,397 kwa mwaka uliopita.

Halmashauri zilizoripoti kiasi kikubwa cha wadai ni Manispaa ya Ilala Sh. 8,243,132,583, Halmashauri ya Wilaya ya Kilindi Sh. 1,857,102,452, Halmashauri ya Jiji la Mwanza Sh. 1,837,399,546 na Manispaa ya Dodoma Sh. 1,828,881,645

Jedwali lifuatalo linaonyesha ulinganisho wa wadai kwa mwaka wa fedha 2009/2010 na 2010/2011:

| Mwaka | Kiasi (Shs.) | Idadi ya Halmashsuri |
|---|---|---|
| 2009/10 | 52,041,114,397 | 113 |
| 2010/11 | 52,132,811,928 | 111 |

Wadai hao wanaweza kuonyeshwa katika mchoro duara kama ifuatavyo:




Kwa kuangalia Mchoro duara hapo juu, inatafsiriwa kuwa kiasi cha Wadai kwa miaka miwili mfululizo yaani mwaka 2009/2010 na 2010/2011 kwa wastani walikuwa wanadai kiasi cha Sh.52bilioni.

Mamlaka za Serikali za Mitaa zinashauriwa kulipa madeni yake haraka yanapofikia wakati wa kulipa na zianzishe udhibiti thabiti, kanuni na taratibu katika kuhakikisha kuwa uongozi wa Halmashauri unawajibika kwa madeni ambayo hayana faida kwa halmashauri.

Orodha ya Halmashauri zinazodaiwa imeonyeshwa kwenye **kiambatisho Na.(xxiv)**

## 5.6 Ukaguzi Wa Miradi Iliyopata Fedha Toka Kwa Wahisani

Mamlaka za Serikali za Mitaa, pamoja na kukusanya mapato kutoka kwenye vyanzo vyake pia hupata ruzuku kutoka Serikali Kuu na wafadhili mbambali kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Wakati wa ukaguzi nilifanya tathmini ya Ruzuku ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ya Serikali za Mitaa (LGDG); Mkakati wa Taifa wa Kudhibiti UKIMWI (NMSF), Mpango wa Maendeleo wa Elimu

ya Msingi (MMEM) na Mpango wa Maendeleo wa Afya ya Msingi (MMAM). Kwa kuongezea, Mamlaka za Serikali za Mitaa hupokea, ruzuku kutoka kwa wafadili wengine katika kuboresha hali ya kijamii kwa kupitia miradi ya Mfuko wa Jamii Tanzania (TASAF), Mfuko wa Afya ya Jamii (HBF), Programu ya Maendeleo ya Kilimo na Mifugo (ASDP) na Mpango wa Sekta ya Maendeleo ya Maji (WSDP). Hata hivyo matokeo ya ukaguzi wa miradi inayofadhiliwa kupitia mifuko hii imetolewa kwenye ripoti za pekee na kupelekwa kwenye uongozi wa Halmashauri husika na pia kuna taarifa ya jumla ya miradi inayofadhiliwa na wahisani.

### 5.6.1 Mkakati wa Taifa wa Kudhibiti UKIMWI (NMSF)

#### 5.6.1.1 Fedha za Mkakati wa Taifa wa Kudhibiti UKIMWI (NMSF) Ambazo Hazikutumika Sh.1,104,364,692

Katika mwaka wa ukaguzi, Tume ya Kudhibiti Ukimwi Tanzania (TACAIDS) kwa kupitia Wizara ya Fedha ilipeleka fedha kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa chini ya Mkakati wa Kitaifa wa Kudhibiti Ukimwi (NMSF) 2008-2012 ambao wafadhili wake wakuu ni Serikali ya Marekani kupitia USAID, PEPFAR, wafadhili wengine na Serikali ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia MTEF.

Hata hivyo, ukaguzi uliofanyika kuangalia mapato na matumizi ya fedha hizo katika sampuli ya Halmashauri 41 zilizochaguliwa ilibainika kuwa kiasi cha Sh. 1,104,364,692 kilikuwa hakijatumika kufikia tarehe 30 Juni, 2011 kama inavyooneshwa kwenye **Kiambatisho (xxv)**

Kiwango kikubwa cha salio la fedha kinaonesha kuwa kazi za mradi zilizolengwa hazikutekelezwa kama ilivyopangwa na hivyo kuchelewesha utoaji wa huduma kwa jamii.

#### 5.6.1.2 Ruzuku ya NMSF zilizoingizwa kimakosa Sh.859,163,571

Ulinganisho wa fedha zilizopokelewa katika sampuli ya Halmashauri 43 na taarifa zilizopatikana kutoka kitengo cha Taifa cha kudhibiti UKIMWI kilichopo TACAIDS umeonyesha kwamba fedha zilizotolewa kwa ajili ya shughuli za NMSF kwa mwaka ulioishia Juni 30, 2011 ilikuwa ni Sh.3,752,178,000 tofauti na Sh.4,611,341,571 zilizokuwa katika taarifa za Halmashauri husika. Hivyo kuna tofauti ya Sh.859,163,571 ikihusisha Halmashauri 25 kati ya 43 zilizochaguliwa. Hii inaonyesha kwamba, Halmashauri 18 ziliingiza kwa usahihi fedha zilizopokelewa katika vitabu vya fedha kama inavyoonekana katika **Kiambatisho (xxvi)**

Hii inaonyesha kwamba, kuna udhaifu katika mawasiliano na kufanya usuluhishi wa fedha zilizotumwa na kupokelewa kati ya kitengo cha Taifa cha kudhibiti UKIMWI na Halmashauri

### 5.6.2 Ruzuku ya Maendeleo ya Serikali za Mitaa (LGDG)

#### 5.6.2.1 Ufadhili

Ruzuku ya Maendeleo ya Serikali za Mitaa inafadhiliwa na michango kutoka kwa Wadau wa Maendeleo ambao ni pamoja na KFW, Ubalozi wa Ireland, Finland, Uholanzi, Ubalozi wa Sweden, Benki Kuu ya Tokyo-Japan, Ushirikiano wa Ubelgiji kupitia akaunti Na. 9931206651 iliyopo Benki Kuu na Shirika la maendeleo la Kimataifa (IDA) kupitia akaunti Na.87080-206,688-00 iliyopo katika benki ya "Standard Chattered".

Katika mwaka husika, Mpango huu ulikuwa na jumla ya kiasi cha dola za Kimarekani 74,137,084.14 sawa na Sh. 109,742,900,821 kiasi ambacho kimechangiwa na Wadau wa Maendeleo. Aidha kulikuwa na Mchango kutoka Serikali ya Tanzania wenye jumla ya Sh. 24,047,523,953 na kufanya jumla ya Shs.133,790,424,774 kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli zilizopitishwa katika Ruzuku ya Maendeleo ya Serikali za Mitaa (LGDG). Michango kutoka kwa wafadhili ilikuwa na jumla ya dola za Kimarekani 74,137,084.14 sawa na Sh.109,742,900,820.75 kama ilivyoonyeshwa hapa chini:

| Na. | Wadau wa Maendeleo | Kiasi katika dola za Kimarekani | Kiasi katika Shilingi za Kitanzania |
|---|---|---|---|
| 1. | KFW | 18,007,192.75 | 25,492,730 741 |
| 2. | Ubalozi wa Ireland | 4,588,844.00 | 6,276,646,521 |
| 3. | Finland | 9,635,136.49 | 13,851,294,931 |
| 4. | Uholanzi | 19,555,137.87 | 28,723,630,749 |
| 5. | Ubalozi wa Sweden | 2,942,258.18 | 4,312,663.180 |
| 6. | Benki Kuu ya Tokyo-Japan | 1,220,774.12 | 1,794,179,049 |
| 7. | Ushirikiano wa Ubelgiji | 10,381,021.00 | 15,384,012,889 |
| 8. | Shirika la maendeleo la Kimataifa | 7,806,719.73 | 13,907,742,761 |
| | **Jumla** | **74,137,084.14** | **109,742,900,821** |

Hata hivyo, katika akaunti hodhi Na.9931206651 kwa ajili ya fedha za ruzuku ya Maendeleo ya Serikali za Mitaa (LGDG), kulikuwa na salio anzia la dola 2,931,465.64 hadi kufikia tarehe 1 Julai 2010 sawa na Shs.4,003,441.064.

Aidha, ruzuku ya Maendeleo ya Sekta ya Afya (HSDG) ikiwa ni moja wapo ya Sekta ambatishi katika mfumo wa ruzuku ya Maendeleo ya Serikali za Mitaa (LGDG) ilipokea mchango wenye jumla ya Sh.12,647,302,763 kutoka wahisani mbalimbali na Sh.7,116,720,000 kutoka Serikali ya Tanzania,na hivyo kufanya kuwa na jumla ya Sh.19,764,022,764. Jedwali lililopo hapa chini linaonyesha wachangiaji na kiasi walichochangia:

| Na. | Mchangiaji | Akaunti Na. | Kiasi katika dola za Kimarekani | Kiasi katika Shilling za Kitanzania |
|---|---|---|---|---|
| 1. | KFW kupitia (LGDG) akaunti iliyoko benki kuu | 9931206651 | 5,383,840.40 | 7,908,053,972 |
| 2. | DANIDA | 011103000383 | | 2,732,680,529 |
| 3. | KFW | 011103000383 | | 2,006,568,263 |
| 4. | Serikali ya Tanzania | | | 7,116,720,000 |
| | **Jumla** | | | **19,764,022,764** |

Katika mwaka huo jumla ya dola za Kimarekani 45,658,149.46 sawa na Sh.67,259,547,500 zilihamishiwa katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa kwa ajili ya shughuli za maendeleo (LGDG).

### 5.6.2.2 Fedha kwa ajili ya ruzuku ya Maendeleo ya Serikali za Mitaa (LGDG) zilizotolewa pungufu Sh.153,943,547,023

Katika mapitio ya fedha kwa ajili ya ruzuku ya Maendeleo ya Serikali za Mitaa (LGDG) ilionekana kuwa jumla ya Sh.324,384,652,759 zilitengwa kwa ajili ya kuhamishiwa kwenye Halmashauri katika mwaka uliomalizika. Hata hivyo, hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2011 jumla ya Sh.170,441,105,736 pekee zilikuwa zimehamishwa na kusababisha tofauti ya Sh.153,943,547,023 kiasi ambacho kilitolewa pungufu kama muhtasari unavyoonyesha katika jedwali hapa chini:

| Na. | Mfuko | Kiasi kilichotengwa ( Sh.) | Kiasi kilichohamishwa (Sh.) | Kiasi kilichotolewa pungufu (Sh) |
|---|---|---|---|---|
| 1 | LGDG CORE | 175,248,000,200 | 109,295,521,453 | 65,952,478,747 |
| 2 | Afya | 30,284,700,000 | 17,401,420,000 | 12,883,280,000 |
| 3 | Kilimo | 55,645,745,550 | 43,744,164,283 | 11,901,581,267 |
| 4 | Maji Vijijini | 63,206,207,009 | 0.00 | 63,206,207,009 |
| | **Jumla** | **324,384,652,759** | **170,441,105,736** | **153,943,547,023** |

Hali hii inamaanisha kwamba shughuli zilizopangwa hazikutekelezwa kikamilifu na kwa sababu hiyo, malengo yaliyokusudiwa hayakuweza kufikiwa.

Hata hivyo, ukaguzi wa ruzuku ya Maendeleo ya Serikali za Mitaa (LGDG) katika ngazi ya Halmashauri bado unaendelea na taarifa ya kina itatolewa pekee baada ya kukamilika kwa ukaguzi.

### 5.6.3 Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo

Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo ulianzishwa kwa Sheria Na. 16 ya mwaka 2009 kwa malengo ya kuendeleza miradi ya maendeleo katika majimbo husika. Kwa

mujibu wa sheria hii mapato yote, matumizi na kiasi kinachobakia kwa kila mwaka kinatakiwa kitumike kwa shughuli za Maendeleo ya Jimbo kwa mwaka unaofuta.

Katika kupitia uendeshaji wa Mfuko wa Jimbo katika Halmashauri 51 tuliweza kubaini mapungufu yafuatayo:

**(a) Fedha za Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo kwenye Halmashauri zisizotumika Sh.2,683,368,422**

Katika ukaguzi kwenye baadhi ya Halmashauri iliweza kubainika kuwa kiasi kikubwa cha fedha za Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo bado kilikuwa katika akaunti za benki bila ya kutumika. Kwa mfano katika sampuli ya Halmashauri 51 zilizokaguliwa tulibaini kiasi cha sh. 2,683,368,422 bado kilikuwa hakijatumika kama inavyoonyeshwa kwenye **kiambatisho (xxvii)**

Hii inasababishwa na usimamizi mdogo wa fedha za Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo, jambo linaloifanya jamii iliyolengwa kuchelewa kupata matunda ya mfuko hivyo malengo tarajiwa kutokufikiwa.

Mipango thabiti lazima iwekwe na Halmashauri pamoja na Kamati za Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo ili kuhakikisha kuwa fedha zilizobaki zinatumika bila kuchelewa ili kufikia malengo yaliyokusudiwa.

**(b) Kutokuandaliwa kwa Taarifa ya Mfuko wa Maendeleo wa Jimbo na Kuwasilishwa TAMISEMI**

Hamashauri zilizo nyingi hazikuandaa taarifa ya fedha zilizopokelewa na Kamati za Maendeleo ya Jimbo na matumizi ya fedha hizo ili kupata picha halisi ya fedha zilizotolewa kwa ajili ya maendeleo ya majimbo. Hii ikiwa ni kinyume na kifungu cha 7(3) cha Sheria ya mfuko wa maendeleo ya Jimbo ya mwaka 2009

Tuanaishauri Ofisi ya Waziri Mkuu-TAMISEMI kuhakikisha kuwa haipeleki fedha nyingine kwenye Halmashauri ambazo hazikuandaa na kupeleka taarifa ya fedha zilizopokelewa na Kamati za Maendeleo ya Jimbo na matumizi yake kwa mwaka husika.

**(c) Matumizi ya Fedha za Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo kwa Miradi Isiyoibuliwa na Jamii**

Kifungu namba 19(1) cha Sheria ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo ya Mwaka 2009 kimeelekeza kuwa miradi yote itakayofanywa na fedha za mfuko huu iwe imeibuliwa na wananchi wa eneo husika. Kinyume na Sheria tajwa hapo juu, Halmashauri zimekuwa zikitumia fedha za Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo katika miradi ambayo haijaibuliwa na jamii kutoka katika eneo husika.

Ninazishauri Mamlaka za Serikali za Mitaa kuhakikisha kwamba fedha za Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo zinatumika kwa miradi iliyoibuliwa na wananchi na kwa kuzingatia vipaumbele vilivyoainishwa.

**(d) Kutokuwepo kwa Mhasibu wa Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo**

Kifungu namba 21(1) cha Sheria ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo ya Mwaka 2009 kinaelekeza kwamba kila Afisa Masuuli atamteua Mweka Hazina wa Halmashauri kuwa mhasibu wa Kamati ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo.

Kinyume ha sheria hiyo, Halmashauri hazikuteua Mhasibu atakayechukua majumu ya usimamiaji wa shughuli za kila siku za uendeshaji wa Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo.

Mamlaka za Serikali za Mitaa zinatakiwa zimteue Mhasibu atakayeshughulikia majukumu ya kifedha yahusuyo Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo.

### 5.6.4 Fedha za Mpango wa Maendeleo ya Afya ya Msingi (MMAM) Ambazo Hazikutumika Sh. 5,848,929,864

Ukaguzi uliofanyika katika baadhi ya Halmashauri kuhusu mwelekeo na utumiaji wa Fedha za MMAM ilibainika kuwa Halmashauri arobaini na nane (48) zilipokea fedha kwa ajili ya kuboresha huduma ya afya ambapo hadi kufikia tarehe 30 Juni 2011 zilikuwa zimebakia jumla ya Sh. 5,848,929,864 kama inavyooneshwa katika **kiambatisho (xxviii).**

Kuwa na bakaa ya kiasi cha sh. 5,848,929,864 inamaanisha kwamba kazi zilizokuwa zimepangwa kutekelezwa za kiwango cha hiyo bakaa hazikutekelezwa na hivyo jamii iliyolengwa hajapata manufaa ya miradi iliyopangwa kutekelezwa.

### 5.6.5 Bakaa katika Mfuko wa Wanawake na Vijana Sh.1,587,780,350

Halmashauri kwa kushirikiana na Serikali Kuu ilianzisha mfuko huu maalumu kwa ajili ya kusaidia vikundi vya wanawake na vijana kwa kuwapa mikopo midogo midogo katika maeneo wanayoishi.

Wakati wa Ukaguzi wetu wa kutaka kujua utendaji wa Mfuko huu tulibaini kuwa kulikuwa na bakaa kiasi cha Sh. 1,587,780,350 ambacho hakikuwa kimetumika katika Halmashauri 23 kama inavyoonyeshwa katika jedwali hapa chini, hii inaonyesha udhaifu upande wa Halmashauri hizo katika kuhakikisha kuwa fedha hizi zinakopeshwa kwenye vikundi vilivyokusudiwa.

| Na | Halmashauri | Kiasi kisichotumika (Sh.) |
|---|---|---|
| 1 | Halmashauri ya Manispaa Musoma | 243,844,404 |
| 2 | Halmashauri ya Wilaya Bunda | 160,070,931 |
| 3 | Halmashauri ya | 150,648,998 |

| | | |
|---|---|---|
| | Wilaya ya Tarime | |
| 4 | Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa | 120,356,124 |
| 5 | Halmashauri ya Wilaya ya Rorya | 110,869,620 |
| 6 | Halmashauri ya Manispaa ya Bukoba | 106,832,731 |
| 7 | Halmashauri ya Wilaya ya Muheza | 86,317,621 |
| 8 | Halmashauri ya Wilaya ya Musoma | 64,846,600 |
| 9 | Halmashauri ya Wilaya ya Serengeti | 63,801,189 |
| 10 | Halmashauri ya Wilaya ya  Karagwe | 56,539,109 |
| 11 | Halmashauri ya Wilaya ya Biharamulo | 54,883,194 |
| 12 | Halmashauri ya Wilaya ya Missenyi | 51,912,102 |
| 13 | Halmashauri ya Wilaya ya Korogwe | 44,379,747 |
| 14 | Halmashauri ya Wilaya ya Karatu | 43,003,602 |
| 15 | Halmashauri ya Wilaya ya Mkinga | 40,573,535 |
| 16 | Halmashauri ya Mji wa  Lindi | 34,778,547 |
| 17 | Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa | 34,767,300 |
| 18 | Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni | 27,930,020 |
| 19 | Halmashauri ya Wilaya ya  Singida | 27,930,020 |
| 20 | Halmashauri ya Wilaya Lindi DC | 22,226,200 |
| 21 | Halmashauri ya Wilaya Kasulu DC | 17,017,510 |
| 22 | Halmashauri ya Wilaya Ngara DC | 15,178,246 |
| 23 | Halmashauri ya Wilaya ya Bahi | 9,073,000 |
| | **Jumla** | **1,587,780,350** |

Utaratibu huu wa kuwa na salio kubwa la fedha katika akaunti ya akina mama na vijana unanyima haki kwa vikundi vilivyokusudiwa kuweza kufaidika na mfuko huu.

Ninazishauri Mamlaka za Serikali za Mitaa kuweka mikakati ya kuzitumia fedha zilizobaki kwenye akaunti kwa kutoa mikopo kwa vikundi vingi ili kuwawezesha kuboresha hali zao za maisha kwa kutumia fedha za mfuko huu kuliko kuacha kiasi kikubwa kwenye akaunti za benki bila ya kukitumia.

### 5.6.6 Fedha za MMEM Ambazo Hazikutumika Sh.997,528,258

Ukaguzi uliofanyika kuhusiana na utendaji wa kifedha na matumizi ya fedha za MMEM zilizopokelewa na Halmashauri kwa lengo la kuongeza ubora wa shule, upatikanaji wa shule na uboreshaji wa shule za msingi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa imebainika kuwa, hadi kufikia tarehe 30 Juni 2011 zilikuwa zimebakia jumla ya Sh. 997,528,258 katika sampuli ya Halmashauri 11 zilizokaguliwa kama inavyoonyeshwa katika jedwali hapa chini:

| S/N | Halmashauri | Kiasi kilichopo (Sh.) | Kiasi kilichotumika (Sh.) | Kiasi kilichobaki (Sh.) | % ya kiasi kilichobaki |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | H/W Liwale | 40,842,000 | 0 | 40,842,000 | 100.0% |
| 2 | H/W Shinyanga | 77,519,000 | 0 | 77,519,000 | 100.0% |
| 3 | H/W Kilwa | 224,761,500 | 113,434,500 | 111,327,000 | 49.5% |
| 4 | H/W Mufindi | 164,630,000 | 88,228,000 | 76,402,000 | 46.4% |
| 5 | H/W Rorya | 111,025,599.85 | 68,525,599.85 | 42,500,000 | 38.3% |
| 6 | H/W Kishapu | 145,850,000 | 95,000,000 | 50,850,000 | 34.9% |
| 7 | H/W Muleba | 512,339,617.96 | 366,159,484.96 | 146,180,133 | 28.5% |
| 8 | H/W Karagwe | 1,550,983,752 | 1,140,580,756.50 | 410,402,996 | 26.5% |
| 9 | H/W Missenyi | 171,127,221.46 | 152,191,502.47 | 18,935,719 | 11.1% |
| 10 | H/W Chato | 130,226,470.63 | 118,486,621.99 | 11,739,849 | 9.0% |
| 11 | H/W Karatu | 212,266,480 | 202,436,918 | 9,829,562 | 4.6% |
| 12 | H/W Musoma | 169,198,000 | 168,198,000 | 1,000,000 | 0.6% |
| | **Jumla** | **3,510,769,642** | **2,513,241,384** | **997,528,258** | **28.4%** |

Kuwepo kwa kiasi kikubwa cha fedha ambacho hakijatumika inamaanisha kuwa shughuli zilizopangwa kufanywa hazikutekelezwa kikamilifu na hivyo kusababisha jamii iliyolengwa kutokufaidika na fedha walizotengewa.

### 5.6.7 Fedha za Usimamizi wa Misitu (PFM) Ambazo Hazikutumika Sh.178,826,876

Ukaguzi uliofanyika kuhusiana na utendaji wa kifedha na matumizi ya fedha za Usimamizi wa Misitu (PFM) kwa mwaka wa fedha wa 2010/2011 umebaini kuwa kulikuwa na fedha za mradi kiasi cha Sh. 178,826,876 katika Halmashauri kumi na moja (11) ambazo hazikutumika hadi mwisho wa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2011 kama inavyoonekana katika jedwali hapo chini:

| Na. | Halmashauri | Kiasi kilichopo (Sh.) | Kiasi kilichotumika (Sh.) | Kiasi kilichobaki (Sh.) | % ya kiasi kilichobaki |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Kilwa DC | 28,232,045 | - | 28,232,045 | 100.0% |
| 2 | Nachingwea DC | 42,354,344 | 8,957,445 | 33,396,899 | 78.9% |
| 3 | Liwale DC | 61,629,366 | 20,255,000 | 41,374,366 | 67.1% |
| 4 | Morogoro DC | 41,134,773 | 14,438,300 | 26,696,473 | 64.9% |
| 5 | Mbinga DC | 74,253,235 | 31,298,217 | 42,955,018 | 57.8% |
| 6 | Kilosa DC | 29,203,720 | 25,137,032 | 4,066,688 | 13.9% |
| 7 | Songea DC | 24,249,467 | 23,088,947 | 1,160,520 | 4.8% |
| 8 | Korogwe DC | 29,201,404 | 28,495,250 | 706,154 | 2.4% |
| 9 | Kilombero DC | 28,232,045 | 28,029,800 | 202,245 | 0.7% |
| 10 | Namtumbo DC | 6,827,734 | 6,795,000 | 32,734 | 0.5% |
| 11 | Muheza DC | 4,133,330 | 4,129,596 | 3,734 | 0.1% |
| | **Total** | **369,451,463** | **190,624,587** | **178,826,876** | **48.4%** |

Hii inamaanisha kuwa baadhi ya shughuli za usimamizi wa misitu zilizokusudiwa hazikutekelezwa.

### 5.6.8 Mfuko wa Afya ya Jamii

Mfuko wa Afya ya Jamii (CHF) ulianzishwa mwaka 1997 ikiwa ni mmoja wa mifuko iliyoainishwa na Serikali kwa ajili ya kuhamasisha jamii katika uchangiaji wa huduma za afya Tanzania.

Ukusanyaji na utumiaji wa Fedha katika Mifuko umeelezwa zaidi katika Waraka Na. 2 wa mwaka 1997 uliotolewa na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii ambao ulielekeza kuwa fedha zitatumika kwa matumizi yaliyopitishwa yakiwemo ununuzi wa madawa, matengenezo madogo madogo ya majengo, mafuta na posho za watumishi kwa ajili ya safari za kwenda kununua madawa.

Katika mwaka huu wa ukaguzi, yafuatayo yalibainika katika usimamizi wa Mfuko wa Afya ya Jamii.

#### (a) Bakaa la fedha za Mfuko wa Afya ya Jamii Sh. 2,963,900,725

Katika kipindi hiki cha ukaguzi, nimepitia usimamizi wa Mfuko wa Afya ya Jamii katika Halmashauri thelathini na tatu (33) na kubaini kuwa Halmashauri hizo zilikuwa na bakaa la jumla ya Sh. 2,963,900,725 ambazo kwa kiasi kikubwa lilisababishwa na aidha Halmashauri nyingi kutofungua akaunti za benki zinazojitegemea kwa ajili ya Mfuko wa Afya pekee au kuchelewa kwa fedha toka Hazina. Pia Halmashauri hizo hazikutengeneza taarifa ya fedha kwa ajili ya Mfuko wa Afya ya Jamii kwa mwaka husika.
Orodha ya Halmashauri ambazo zilibaki na bakaa wakati wa kufunga mwaka imeonyeshwa kwenye **Kiambatisho (xxix)**

Ninashauri kwamba, Halmashauri zinatakiwa kutekeleza mpango wa Afya ya Jamii kwenye mwaka husika kwa ajili ya faida ya jamii inayohusika kuliko kukaa na bakaa kubwa la fedha benki. Vile vileHalmashauri zinatakiwa kuandaa hesabu za Mfuko wa Afya ya Jamii kila Mwaka.

**(b) Matumizi ya fedha za za Mfuko wa Afya ya Jamii yaliyofanywa bila kuzingatia Mwongozo uliowekwa Sh. 44,086,650**

Mwongozo wa shughuli za Mfuko wa Afya ya Jamii uliotolewa mwezi Juni 1999 unafafanua kwamba fedha za mfuko zitatumiwa kwa matumizi yanayohusiana na shughuli za afya tu. Manunuzi ya vifaa na huduma zinazohusiana na afya kama madawa, vifaa vya hospitalini, ukarabati wa vifaa vya afya, samani, vitendea kazi, sare za wauguzi, malipo ya posho ya muda wa kazi wa ziada kwa waganga na wauguzi, usafiri na posho za kujikimu watumishi wakiwa safari za kikazi kama zimeainishwa katika mpango.

Wakati wa ukaguzi tulibaini kuwa fedha za Mfuko wa Afya ya Jamii kiasi cha Sh. 44,086,650 katika Mamlaka nne (4) za Serikali za Mitaa ambazo ni Halmashauri ya Manispaa ya Songea, Halmashauri ya Manispaa ya Dodoma, Halmashauri ya wilaya Ulanga na Halmashauri ya wilaya Iramba zilitumika kwa shughuli nyingine ambazo si zile zilizoainishwa katika mwongozo wa shughuli za Mfuko wa Afya ya Jamii

Ninashauri kuwa Halmashauri zitumie michango ya fedha za Mfuko wa Afya ya Jamii kwa shughuli zilizokusudiwa na kupitishwa kwa kuzingatia Waraka Na. 2 wa mwaka 1997 uliotolewa na wizara ya Afya na ustawi wa jamii

**(c) Madai Yaliyopelekwa Mfuko wa Bima ya Afya ya Taifa (CHIF) Lakini Hayajalipwa Kiasi cha Shs.34,316,220**

Wakati wa kupitia utendaji wa Mfuko wa Afya ya Jamii tulibaini kuwa madai ya Mamlaka mbili za Serikali za Mitaa yaani Halmashauri ya wilaya ya Kilolo na Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro kiasi cha Sh. 34,316,220 yalipelekwa Mfuko wa Bima ya Afya ya Taifa (CHIF) ikiwa ni kutaka kurejeshewa gharama za huduma ya afya zilizotolewa kwa wanachama waliopo chini ya mfuko huo. Hata hivyo Halmashauri hizo zilikuwa bado hazijarejeshewa fedha hizo.

Vile vile kiasi cha Sh. 12,831,520 kilikusanywa na Vituo vya Afya na Zahanati katika Halimashauri za Wilaya ya Manyoni na Ukerewe lakini kiasi hicho cha fedha zilizokuanywa hakikuwasilishwa kwa mtunza fedha wa Halmashauri.

Ninazishauri Halmashauri husika kuhakikisha kuwa zinafuatilia madai yaliyopelekwa NHIF ili waweze kulipwa. Vilevile kiasi cha Sh. 12,831,520 kilichokusanywa na Vituo vya Afya na Zahanati kiwasilishwe kwa mtunza fedha wa Halmashauri, kikatiwe stakabadhi na kupelekwa benki.

### 5.6.9 Fedha Za MMES Ambazo Hazikutumika Sh. 724,673,833

Wizara ya fedha iligawa fedha kwa Mamlaka ya Serikali za mitaa kwa ajili ya Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari (MMES) kwa lengo la kuongeza ubora wa shule, upatikanaji wa shule na uboreshaji wa shule za sekondari.

Hata hivyo, Ukaguzi uliofanyika kuhusiana na utendaji na matumizi ya fedha za MMES umebaini kuwa Mamlaka za Serikali za Mitaa zipatazo kumi na moja (11)

zilikuwa na kiasi cha Sh. 3,632,457,408 na kati ya hizo kiasi cha Sh.2,907,783,575 zilitumika kwa shughuli mbalimbali za Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari (MMES) na kubakiza bakaa la Sh. 724,673,833 sawa na 20% ya fedha zote zilizopokelewa kama inavyoonyeshwa katika jedwali lifuatalo:

| Jina la Halmashauri | Bakaa la Fedha za MMES ambazo hazikutumika | | | |
|---|---|---|---|---|
| | Kiasi kilichokuwepo (Sh.) | Kiasi kilichotumika (Sh.) | Kiasi kilichobaki (Sh.) | % |
| Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi | 271,689,000 | 239,513,000 | 32,176,000 | 11.84% |
| Halmashauri ya Wilaya ya Bukoba | 223,144,000 | 183,266,066 | 39,877,934 | 17.87% |
| Halmashauri ya Wilaya ya Karagwe | 561,498,166.73 | 551,991,535.73 | 9,506,631.00 | 1.69% |
| Halmashauri ya Wilaya ya Ngara | 189,673,000.00 | 182,049,463.00 | 7,623,537.00 | 4.02% |
| Halmashauri ya Wilaya ya Missenyi | 163,269,189 | 156,507,356 | 6,761,833 | 4.14% |
| Halmashauri ya Wilaya ya Chato | 130,226,470.63 | 118,486,621.99 | 11,739,848.64 | 9.01% |
| Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa | 104,058,000 | 79,371,665 | 24,686,335 | 23.72% |
| Halmashauri ya Wilaya ya Liwale | 130,000,000 | 50,000,000.00 | 80,000,000 | 61.54% |
| Halmashauri ya Wilaya ya Nachingwea | 180,750,000 | 106,201,501.00 | 74,548,499 | 41.24% |
| Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro | 1,023,627,471.89 | 807,270,695.41 | 216,356,776.48 | 21.14% |
| Halmashauri ya Wilaya ya Kahama | 252,912,489.00 | 228,583,489.00 | 24,329,000.00 | 9.62% |
| Halmashauri ya Wilaya ya Karatu | 401,609,620.94 | 204,542,182.00 | 197,067,438.94 | 49.07% |
| **Jumla** | **3,632,457,408.19** | **2,907,783,575.13** | **724,673,833.06** | **19.95%** |

Kuwepo kwa Kiasi cha fedha kwenye akaunti ya benki ambacho hakijatumika inamaanisha kuwa shughuli zilizopangwa kufanywa hazikutekelezwa kikamilifu na hivyo kusababisha baadhi ya shughuli za MMES zilizokusudiwa kutokufanyika.

## 5.7 Usimamizi wa Matumizi

### 5.7.1 Malipo yenye Nyaraka Pungufu Sh. 5,692,624,802

Wakati wa ukaguzi wa kumbukumbu za matumizi katika sampuli iliochaguliwa, matumizi yenye ya Shs.5,692,624,802 yanayohusiana na Halmashauri 63 yalikuwa na nyaraka pungufu kinyume na Agizo Na. 5 (c) na 368 ya Memoranda ya fedha za Mamlaka ya Serikali za Mitaa ya mwaka 1997 ambayo inaagiza malipo yote yanayofanywa na Halmashauri yaambatanishwe na nyaraka sahihi. Halmashauri husika zimeorodheshwa katika **Kiambatanisho (xxx)**

Malipo yanayofanyika bila viambatisho yanakwaza mwawanda ya ukaguzi katika kuhakiki uhalali wa malipo husika.

Muhtasari wa malipo yenye nyaraka pungufu kwa miaka ya 2007/08, 2008/09, 2009/10 na 2010/11 ni kama ilivyoonyeshwa hapa chini:-

| Mwaka | Kiasi(Shs.) | Idadi ya Halmashauri |
|---|---|---|
| 2007/08 | 3,590,228,595 | 69 |
| 2008/09 | 2,526,117,587 | 33 |
| 2009/10 | 2,830,338,208 | 34 |
| 2010/11 | 5,668,730,107 | 63 |

Taarifa hiyo inaonyeshwa pia katika Chati Mstari hapa chini:




Chati mstari iliyopo juu inaonyesha kwamba, kutoka wastani wa Halmashauri hamsini (50) kwa miaka minne mfululizo, kiasi cha matumizi yenye nyaraka pungufu yalikuwa yakipungua kwa Sh.1.1bill kutoka Sh.3.6bill ilivyoripotiwa katika mwaka wa fedha 2007/08 hadi Sh.2.5 ilivyoripotiwa katika mwaka wa fedha 2008/09.

Pia kiasi hiki kiliongezeka kwa Sh.0.3bill na Sh.2.9 bill kutoka Sh.2.5bill ilivyoripotiwa katika mwaka wa fedha 2008/09 kwenda Sh.2.8bill na 5.7 katika mwaka 2009/10 na 2010/11 kwa mtiririko huo.

### 5.7.2 Matumizi yasiyokuwa na hati za malipo Sh. 1,080,519,637

Kwa mwaka wa fedha 2010/11, Halmashauri 32 zilifanya malipo yenye jumla ya Sh.1,080,519,637 ambayo hati za malipo pamoja na viambatanisho vyake havikupatikana kwa ajili ya ukaguzi, hivyo uhalali wa matumizi haya haukuweza kuthibitshwa kutokana na kukwazwa kwa mawanda ya ukaguzi. Halmashauri husika ni kama zinavyoonyeshwa katika **Kiambatisho (xxxi)**

Kutokuwepo kwa hati za malipo ni kinyume na Agizo Na.368 na 369 la Memoranda ya Fedha ya Mamlaka za Serikali za Mitaa,1997 ambayo kwa pamoja yanaelekeza kuwa hati za malipo pamoja na viambatisho vyake vinatakiwa kuweka vizuri na kutunzwa kwa muda usiopungua miaka mitano (5).

Kwa muhtasari idadi ya Halmashauri zilizokuwa na matumizi yasiyokuwa na hati za malipo kwa miaka ya fedha 2007/2008, 2008/2009, 2009/2010 na 2010/2011 imeoneshwa katika jedwali hapa chini:

| Mwaka | Kiasi (Shs.) | Idadi ya Halmashauri |
|---|---|---|
| 2007/08 | 1,370,245,729 | 45 |
| 2008/09 | 2,526,117,587 | 33 |
| 2009/10 | 2,830,338,208 | 34 |
| 2010/11 | 1, 080,519,637 | 32 |

Taarifa hii inaweza kuoneshwa katika chati mstari ifuatavyo:




Kutokana na chati mstari hapo juu inaweza kuelezewa kuwa, mapungufu haya yanahusu kwa wastani Halmashauri 36 kwa miaka minne mfululizo, kiasi cha kukosena kwa hati za malipo kimeongezeka kwa Shs.1.1bill. na Shs.0.3bill

kutoka Shs.1.4 kilichoripotiwa mwaka 2007/08 hadi 2008/09 na 2009/10 kwa mpangilio huo.

Hata hivyo kuanzia mwaka wa fedha 2009/10 hadi 2010/11, kiasi cha kukosekana kwa hati za malipo kilipungua kwa Shs.1.7bill kutoka Shs.2.8bill hadi Shs.1.1bill kwa mtiririko huo.

Kwa vile hili limekuwa ni tatizo linalojirudia katika Halmashauri nyingi kwa muda mrefu, napenda kuwakumbusha viongozi wa Serikali za Mitaa juu ya wajibu wao katika kuhakikisha kuwa, nyaraka za Halmashauri ikiwa ni pamoja na hati za malipo zinatunzwa vizuri na lazima ziwe zinapatikana kwa ajili ya ukaguzi zihitajikapo.

### 5.7.3 Kutooneka kwa stakabadhi za kukiri mapokezi kutoka kwa walipwaji Sh. 2,525,230,334

Malipo ya Sh. 2,525,230,334 kutoka Halmashauri 13 ambayo aidha yalilipwa moja kwa moja na Hazina ikiwa ni makato ya kisheria, au yalilipwa na Halmashauri hizo kwenda kwenye Taasisi mbalimbali kwa ajili ya huduma mbalimbali zilizotolewa na taasisi hizo lakini malipo hayo hayakuweza kuthibitika kama yamepokelewa na Taasisi husika kwa vile hazikuweza kukiri mapokezi hayo kwa kutoa stakabadhi/ risiti ya kukiri kupokea kiasi cha fedha kilicholipwa kinyume na Agizo Na. 5 (c) la Memoranda ya Fedha za Serikali za Mitaa la mwaka 1997.

Halmashauri hizo zimeonyeshwa katika jedwali hapa chini:

| Na. | Halmashauri | Kiasi (Sh) |
|---|---|---|
| 1. | Halmashauri ya Manispaa ya Arusha | 6,000,000 |
| 2. | Halmashauri ya Wilaya ya Meru | 12,719,450 |
| 3. | Halmashauri ya Wilaya ya Longido | 913,131,204.30 |
| 4. | Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji | 122,323,122 |
| 5. | Halmashauri ya Wilaya ya Kibondo | 199,070,173 |
| 6. | Halmashauri ya Wilaya ya Moshi | 1,541,987.24 |
| 7. | Halmashauri ya Wilaya ya Babati | 141,132,882.86 |
| 8. | Halmashauri ya Wilaya ya Hanang' | 9,603,775 |
| 9. | Halmashauri ya Wilaya ya Kiteto | 12, 879,000 |
| 10. | Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro | 1,048,131,740 |
| 11. | Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga | 54,797,000 |
| 12. | Halmashauri ya Manispaa ya Songea | 2,400,000 |
| 13. | Halmashauri ya Mji wa Korogwe | 1,500,000 |
| | **Jumla** | 2,525,230,334 |

Kukosekana kwa nyaraka za kukiri mapokezi kunakwaza mawanda ya ukaguzi katika kuthibitisha matumizi katika vifungu husika.

### 5.7.4 Matumizi yaliyofanywa kwa kutumia vifungu visivyohusika Sh.1,670,251,079

Kifungu Na. 43(5) cha Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, 1982 (Iliyorekebishwa 2000) inaeleza ya kuwa "endapo mamlaka ya Serikali za Mitaa itaidhinisha bajeti ya mwaka kwa ujumla, bajeti kama ilivyopitishwa itakuwa inaibana kisheria Mamlaka ya Serikali za Mitaa, ambayo itahakikisha kuwa matumizi yake yatalenga na hayatazidi makadirio ya vifungu husika kama ilivyoidhinishwa ". Kinyume na kifungu hicho cha sheria, matumizi ya jumla ya Sh.1,670,251,079 kutoka Halmashauri (22) yalilipwa kwa kutumia vifungu visivyohusika bila kibali cha kamati ya fedha kwa ajili ya uhamishaji. Halmashauri husika ni zifuatazo:

| S/N | Halmashauri | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|
| 1 | H/W Kondoa | 818,548,165 |
| 2 | H/W Kwimba | 557,897,542 |
| 3 | H/W Monduli | 50,674,010 |
| 4 | H/W Ngara | 47,790,275 |
| 5 | Jiji la Dar es Salaam | 38,528,640 |
| 6 | H/W Geita | 32,439,488 |
| 7 | Manispaa ya Songea | 29,868,790 |
| 8 | Jiji la Mwanza | 24,000,290 |
| 9 | Manispaa ya Singida | 13,955,120 |
| 10 | H/W Muleba | 10,000,000 |
| 11 | H/W Rombo | 8,155,000 |
| 12 | Tunduru | 6,413,200 |
| 13 | H/W Shinyanga | 5,146,782 |
| 14 | H/W Kahama | 5,044,000 |
| 15 | H/W Mvomero | 4,710,000 |
| 16 | Manispaa ya Bukoba | 4,646,000 |
| 17 | H/W Mbinga | 3,313,000 |
| 18 | H/W Missenyi | 3,046,000 |
| 19 | H/W Namtumbo | 2,448,875 |
| 20 | H/W Biharamulo | 1,968,502 |
| 21 | H/W Urambo | 1,335,000 |
| 22 | Manispaa ya Morogoro | 322,400 |
| | **Jumla** | **1,670,251,079** |

Matumizi yaliyofanywa nje ya vifungu vilivyoidhinishwa yanadhihirisha kwamba kazi ambazo zingegharimu sh.1,670,251,079 na ambazo ziliidhinishwa hazikufanyika.

### 5.7.5 Matumizi yaliyofanywa nje ya Bajeti iliyodhinishwa Sh. 549,421,946.

Katika mwaka wa fedha 2010/11, matumizi ya kiasi cha Shs.549, 421,946 yalifanyika nje ya bajeti iliyopitishwa bila ya kuomba idhini yoyote ambayo ni kinyume na kifungu Na. 10 (3) cha Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa Namba 9 ya mwaka 1982 (Iliyorekebishwa 2000).

Matumizi hayo yalifanywa na Halmashauri tisa (9) kama zilivyoorodheshwa hapa chini:-

| Na. | Halmashauri | Kiasi (Sh) |
|---|---|---|
| 1 | Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo | 12,719,945 |
| 2 | Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni | 204,207,523 |
| 3 | Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa | 236,995,838 |
| 4 | Halmashauri ya Wilaya ya Chato | 15,816,800 |
| 5 | Halmashauri ya Wilaya ya Rorya | 3,799,000 |
| 6 | Halmashauri ya Wilaya ya Nanyumbu | 10,000,000 |
| 7 | Halmashauri ya Wilaya ya Misungwi | 29,627,840 |
| 8 | Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo | 7,895,000 |
| 9 | Halmashauri ya Wilaya ya | 28,360,000 |
| | **Jumla** | **549,421,946** |

Hii ina maana kuwa kuna baadhi ya kazi zilizoko katika bajeti iliyoidhinishwa hazikuweza kutekelezwa kutokana na kutozingatia sheria ya matumizi.

### 5.7.6 Uhamisho wa ndani kutoka akaunti moja kwenda nyingine kwa njia ya mikopo ambayo haijarejeshwa Sh. 750,621,650

Ukaguzi wa kumbukumbu za nyaraka za malipo katika sampuli ya Halmashauri (20) ulifanyika na kubaini kwamba kulifanyika uhamisho wa ndani kwa ndani wa Sh. 750,621,650 kutoka akaunti moja kwenda nyingine kwa njia ya mikopo ndani ya halmashauri hizo ambayo ilikuwa haijarejeshwa hadi mwisho wa mwaka wa fedha wa 2010/2011 kinyume na agizo na.49 ya Memoranda ya fedha ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa ya mwaka 1997.

Mikopo ya aina hii inapelekea akaunti zilizokopesha kushindwa kutekeleza shughuli zake kama zilivyoidhinishwa. Halmashauri zinazohusika ni kama inavyoonyeshwa katika jedwali hapa chini:

| Na. | Halmashauri | Kiasi ( Sh.) |
|---|---|---|
| 1 | Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba | 190,561,470 |
| 2 | Halmashauri ya Wilaya ya Chato | 99,544,000 |
| 3 | Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro | 99,343,510 |
| 4 | Halmashauri ya Wilaya ya Rorya | 57,917,750 |
| 5 | Halmashauri ya Manispaa ya Dodoma | 47,040,000 |
| 6 | Halmashauri ya Wilaya ya Monduli | 42,067,962 |
| 7 | Halmashauri ya Wilaya ya Ulanga | 36,946,000 |

| | | |
|---|---|---|
| 8 | Halmashauri ya Mji ya Korogwe | 36,000,000 |
| 9 | Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga | 30,000,000 |
| 10 | Halmashauri ya Manispaa ya Bukoba | 26,897,067 |
| 11 | Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo | 20,704,000 |
| 12 | Halmashaur ya Wilaya ya Babati | 15,147,000 |
| 13 | Halmashauri ya Wilaya ya Muleba | 10,000,000 |
| 14 | Halmashauri ya Wilaya Mbarali | 7,878,200 |
| 15 | Halmashauri ya Wilaya ya Hanang' | 7,154,195 |
| 16 | Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe | 6,400,000 |
| 17 | Halmashauri ya Mji ya Njombe | 6,300,000 |
| 18 | Halmashauri ya Manispaa ya Arusha | 4,495,000 |
| 19 | Halmashauri ya Wilaya ya Moshi | 3,719,531 |
| 20 | Halmashauri ya Wilaya ya Simanjiro DC | 2,505,966 |
| | **Jumla** | **750,621,650** |

Uhamisho wa namna hii unasababisha kazi zinazohusiana na fedha zilizokopwa kutotekelezeka.

## 5.8 Madeni na Miadi Sh. 5,852,750,556

Halmashauri kwa Uwezo wake wa kisheria na kwa maingiliano ya kibiashara na Jamii; zinaweza kushitaki au kushtakiwa. Matokeo ya uhusiano huo katika mwaka wa fedha 2010/2011 Halmashauri 10 zimekuwa na kesi mbalimbali za kisheria za jumla ya Sh.5,852,750,556 ambazo karibu zote ni kesi za madai ambapo matokeo yake hayawezi kutabirika na vile vile kukadirika. Halmashauri zimeorodheshwa katika **Kiambatisho (xxxii)**

Menejimenti za Halmashauri zinashauriwa kuhakikisha kuwa zinajihusisha katika kufuatilia maendeleo ya kesi husika, kwa kuwa matokeo ya kutofuatilia mashauri mahakamani kunaweza kupelekea hasara kwa halmashauri kulipa fidia ambazo zingeweza kuepukwa.

## 5.9 Masuala Mengine

### 5.9.1 Ucheleweshaji wa kuwasilisha taarifa za utekelezaji wa miradi kwa mwaka 2010/2011

Kufuatia makubaliano kati ya TAMISEMI, Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali na Ofisi ya Bunge katika ukaguzi wa miradi iliyotekelezwa na Halmashauri, Katibu Mkuu wa OWM - TAMISEMI aliamua kutoa maelekezo kwa barua Kumb. Na.2/CA.26/215/01/1 ya tarehe 10 Novemba, 2010 ambayo inawataka Maafisa Masuuli wote kuandaa taarifa za utekelezaji wa mradi kwa kufuata mwongozo wa taarifa zinazopelekwa mbele ya Kamati ya Bunge ya hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC) na kuziwasilisha pamoja na hesabu za mwisho kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali kwa ajili ya ukaguzi kabla au tarehe 30 Septemba ya kila mwaka wa fedha.

Katika sampuli iliyochaguliwa, Halmashauri tano (5), ambazo ni Halmashauri ya Wilaya ya Kongwa, Halmashauri ya Wilaya ya Tabora, Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo, Halmashauri ya Wilaya ya Songea na Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa hazikuwasilisha taarifa za utekelezaji wa mradi ya maendeleo kinyume na maelekezo yaliyotolewa na Ofisi ya Waziri Mkuu-TAMISEMI.

Halmashauri kumi na tano (15) hazikuwasilisha taarifa za utekelezaji wa mradi ya maendeleo ndani ya tarehe ya kisheria (Septemba 30, 2011 au kabla ). Uchelewevu huu ni wa muda kati ya siku 67-108. Pia Halmashauri kumi na tano (15) ziliwasilisha taarifa za utekelezaji wa Mradi zisizokidhi viwango kulingana mwongozo wa Kamati ya Bunge ya hesabu za Serikali za Mitaa kama zilivyochambuliwa hapa chini:

Orodha ya Halmashauri (15) ambazo hazikuwasilisha taarifa za utekelezaji wa miradi yake ndani ya tarehe ya kisheria ni kama zifuatazo hapa chini:-

| Na. | Halmashauri | Tarehe ya uwasilishaji wa taarifa | Muda wa uchelewe-shaji (Siku) |
|---|---|---|---|
| 1 | Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino | 31/12/2011 | 90 |
| 2 | Halmashauri ya Wilaya ya Iramba | 16/12/2011 | 75 |
| 3 | Halmashauri ya Wilaya ya Chato | 23/12/2011 | 84 |
| 4 | Halmashauri ya Manispaa ya Songea | 18/01/2012 | 79 |
| 5 | Halmashauri ya Wilaya ya Urambo | 22/12/2011 | 83 |
| 6 | Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni | 22/12/2011 | 83 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 7 | Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu | 6/12/2011 | 67 |
| 8 | Halmashauri ya Wilaya ya Kibondo | 18/12/ 2011 | 79 |
| 9 | Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma | 24/11/2011 | 83 |
| 10 | Halmashauri ya Wilaya ya Nzega | 28/12/2011 | 89 |
| 11 | Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge | 28/11/2011 | 89 |
| 12 | Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali | 09/01/2012 | 100 |
| 13 | Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru | 17/01/2012 | 108 |
| 14 | Halmashauri ya Wilaya ya Singida | 16/12/2011 | 107 |
| 15 | Halmashauri ya Manispaa ya Singida | 09/01/2012 | 100 |

Orodha ya Halmashauri (15) ambazo ziliwasilisha taarifa za utekelezaji wa miradi zisizokidhi viwango

| Na. | Halmashauri |
|---|---|
| 1 | Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru |
| 2 | Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro |
| 3 | Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro |
| 4 | Halmashauri ya Wilaya ya Ulanga |
| 5 | Halmashauri ya Wilaya ya Kilombero |
| 6 | Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa |
| 7 | Halmashauri ya Wilaya ya Kibondo |
| 8 | Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma |
| 9 | Halmashauri ya Wilaya ya Iramba |
| 10 | Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni |
| 11 | Halmashauri ya Wilaya ya Singida |
| 12 | Halmashauri ya Manispaa ya Singida |
| 13 | Halmashauri ya Wilaya ya Igunga |
| 14 | Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge |
| 15 | Halmashauri ya Wilaya ya Urambo |

Ukaguzi hauwezi kuthibitisha usahihi wa taarifa ambazo hazikuweza kuletwa Ukaguzi na kukaguliwa. Aidha, pamoja na kukwaza mawanda ya Ukaguzi pia kutoletwa kwa taarifa hizi ni ukiukwaji wa maagizo yaliyotolewa na OWM – TAMISEMI.

### 5.9.2 Michango ya 20% isiyopelekwa kwenye Vijiji na Kata Sh.1,556,830,464

Kifungu cha 9 (e) cha Sheria ya Fedha ya Mamlaka za Serikali za Mitaa Na.9 ya 1982 inaeleza kuwa mapato ya Vijiji na Kata yatajumuisha mapato kutoka Serikali Kuu, Wilaya au kutoka kwa mtu mmoja mmoja au Taasisi kwa njia ya michango. Pia, Agizo Na. 91 la Memoranda ya Fedha ya Mamlaka za Serikali za Mitaa ya mwaka 1997 inaeleza kuwa Mkurugenzi atahakikisha kuwa kila Kijiji ndani ya eneo husika kinapokea fedha moja kwa moja au kwa kupitia Mamlaka husika.

Mwaka 2004 Serikali ilifuta baadhi ya Vyanzo vya mapato yatokanayo na kodi na kuamua kutoa fidia kwenye Halmashauri kwa kodi hizo zilizofutwa. Halmashauri ziliamuliwa kupeleka 20% ya ruzuku ya vyanzo vilivyofutwa kwenye kata na Vijiji kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli za Kata na Vijiji na kusaidia shughuli za maendeleo.

Ukaguzi ulibaini kuwa Halmashauri 50 hazikurejesha kwenye Vijiji na Kata Jumla ya Sh. 1,556,830,464 ikiwa ni fidia ya 20% kutokana na vyanzo vya mapato vilivyofutwa kama inavyooneshwa katika **kiambatisho (xxxiii)**

Kutokana na hali hiyo, jamii za kata/Vijijini hazikupata mgawo wao wa fedha za maendeleo na kwa hiyo basi, miradi mingi ya maendeleo haikutekelezwa kama ilivyokusudiwa.

Menejimenti za Halmashauri zinatakiwa kuhakikisha kuwa fedha za maendeleo kwa ajili ya Vijiji na Kata zinapelekwa kwa wakati kama ilivyoagizwa na Serikali.

### 5.9.3 Utekelezaji wa Kilimo Kwanza

"Kilimo Kwanza" ni mkakati wa Serikali unaokusudia kuhuisha Sekta ya Kilimo nchini. Muundo wa utekelezaji wa nguzo za "Kilimo Kwanza" umeainisha wadau mbalimbali zikiwemo Mamlaka za Serikali za Mitaa chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ili kutekeleza mkakati ya Kilimo Kwanza.

Tathmini ya utekelezaji wa "Kilimo Kwanza" imebaini masuala yafuatayo ambayo yanarudisha nyuma na kuzuia utekelezaji wa Kilimo Kwanza kwa ufanisi. Mchanganuo wa mambo mbalimbali yaliyobainika yameonyeshwa katika **Kiambatisho (xxxiv)**

Ili kuweza kufikia matarajio ya lengo la "Kilimo Kwanza", ninapendekeza yafuatayo:

- Kamati zinazohusika zinatakiwa kuhakikisha kuwa kuna ufuatiliaji wa karibu wa vocha za kilimo na kwamba hatua za kisheria zichukuliwa dhidi ya wale wanaosababisha hasara au upotevu.

- Uongozi wa Halmashauri unapaswa kuhakikisha kuwa mawakala wanaohusika na usambazaji wa pembejeo za kilimo wanafuata masharti ya mikataba.
- Halmashauri zinapaswa kushirikiana na Wizara ya Kilimo kuhakikisha kuwa pembejeo za kilimo zinatolewa kwa wakati na kwa kulingana na mahitaji ili kuchochea kilimo katika Halmashauri.

# SURA YA SITA

## 6.0 MAPITIO YA MIKATABA NA UZINGATIAJI WA TARATIBU ZA MANUNUZI

Sheria ya Manunuzi ya Umma Na. 21 ya mwaka 2004 inaelezea manunuzi kama mchakato unaohusisha kununua, kupanga, kukodi au kupata mali au kazi za ujenzi au huduma kwa taasisi inayonunua kwa kutumia fedha za umma na unahusisha majukumu yote yanayohusiana na kupata vifaa, shughuli za ujenzi au huduma ikijumuisha maelezo ya mahitaji, kuchagua na kuitisha wazabuni, kuandaa na hatimaye kutoa mikataba. Ikizingatiwa kwamba sehemu kubwa ya matumizi ya Serikali hutumika katika manunuzi ya vifaa na huduma, kuna haja ya kuimarisha nidhamu ya matumizi na kuwa na uwazi katika mchakato wa manunuzi ili kupata kiwango cha juu cha thamani ya fedha katika manunuzi yote yanayofanywa na Serikali.

## 6.1 Ufuataji wa Sheria na Kanuni za manunuzi

Kifungu cha 44(2) cha Sheria ya Manunuzi ya Umma Na. 21 ya mwaka 2004 na Kanuni ya 31 ya Kanuni za Manunuzi ya Umma (Vifaa, ujenzi na huduma zisizo za ushauri, kuuza mali za umma kwa Zabuni) za mwaka 2005, zinanitaka kueleza katika ripoti yangu kama taasisi inayokaguliwa imefuata matakwa ya sheria hii na kanuni zake. Kwa kuzingatia wajibu wa taasisi zinazofanya manunuzi ikijumuisha Halmashauri, ninachoweza kusema kwa ujumla ni kwamba kiwango cha ufuataji wa Sheria ya manunuzi ya Umma na Kanuni zake kutokana na Halmashauri zilizokaguliwa bado si cha kuridhisha kulingana na matakwa halisi ya Sheria hii.

## 6.2 Ufanisi wa Utendaji kazi wa Kitengo cha Usimamizi Manunuzi (PMU)

Kifungu cha 34 cha Sheria ya Manunuzi ya Umma Na. 21 ya mwaka 2004, na Kanuni ya 22 ya Kanuni za Bodi ya Zabuni ya Serikali za Mitaa za mwaka 2007 zimeainisha kwamba, kila taasisi inayofanya manunuzi, inatakiwa kuwa na Kitengo cha usimamizi wa manunuzi chenye wataalamu wa kutosha. Kitengo cha usimamizi manunuzi kitaundwa na wataalamu wa manunuzi pamoja na wataalamu wa fani mbalimbali na wakisaidiwa watumishi wa kutosha.

Tathmini ya utendaji wa kitengo cha Manunuzi ya Umma katika Halmashauri mbalimbali imeonyesha kushuka kwa ufanisi ikilinganishwa na hali ilivyokuwa katika miaka ya nyuma. Kwa mwaka huu, Halmashauri 35 zimeonekana kuwa na vitengo vya manunuzi ya umma visivyo fanya kazi ipasavyo, ikilinganishwa na Halmashauri 29 zilizotolewa taarifa mwaka uliopita.

Mapungufu yaliyobainika yanajumuisha wazabuni kutoa huduma kabla ya kusaini mikataba na Halmashauri, na kushindwa kuandaa na kuwasilisha taarifa za kila mwezi za manunuzi kwenye Bodi ya Zabuni ya Manunuzi kulingana na kifungu cha 35 (o) na (q) cha Sheria ya Manunuzi ya Umma Na. 21 ya mwaka 2004, na Kanuni ya 23 ya Kanuni za Bodi ya Zabuni ya Serikali za Mitaa za mwaka 2007. **Kiambatisho Na. xxxv**

Wakati wa Ukaguzi imebainika kuwa, sababu ya kutofuata Sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2004 na Kanuni zake za mwaka 2005 ni mapungufu ya uanzishwaji wa vitengo vya manunuzi ya umma au kuwa na vitengo vya manunuzi visivyofanya kazi vema katika Mamlaka za Serikali za Mitaa. Katika baadhi ya maeneo, Vitengo vya Manunuzi ya Umma vilivyopo havina watumishi wa Kutosha na waliopo hawana elimu na mafunzo ya kutosha juu ya manunuzi.

## 6.3 Mapitio ya Mikataba na Uzingatiaji wa Taratibu za Ununuzi katika Halmashauri

Sura hii inahusika na tathmini ya jumla ya uzingatiaji wa Sheria ya Manunuzi ya Umma Na.21 ya mwaka 2004 na Kanuni zake za mwaka 2005, pamoja na Memoranda ya Fedha za Serikali za Mitaa ya mwaka 1997. Pia, inahusika na menejimenti ya mikataba na uzingatiaji wa sheria za Manunuzi ambazo zimeonekana kuwa na umuhimu wa kuonekana katika taarifa hii na zilitolewa taarifa katika taarifa za ukaguzi kwa kila Halmashauri husika katika mwaka wa fedha 2010/2011. Mapitio yangu ya jumla ya uzingatiaji wa sheria tajwa hapo juu yalibaini mapungufu yafuatayo:

**a) Manunuzi ya bidhaa na huduma bila kupitishwa na Bodi ya Zabuni Sh.239,984,297**

Kanuni Na. 7 ya Kanuni za Bodi za manunuzi za Serikali za Mitaa (GN Na. 177) ya mwaka 2007 na Kifungu Na. 34 cha Sheria ya Manunuzi Namba 21 ya mwaka 2004 kinazitaka Halmashauri kuunda Bodi ya Zabuni. Bodi za Zabuni za Mamlaka ya Serikali za Mitaa ziliundwa ili kuhakikisha kwamba, thamani ya fedha na ubora wa bidhaa na huduma vinapatikana kwa halmashauri wakati wa kufanya manunuzi.

Hata hivyo, kinyume na sheria tajwa hapo juu, ukaguzi ulibaini kuwa katika mwaka wa fedha 2010/2011Halmashauri saba (7) zilifanya manunuzi bila ya kupata idhini ya Bodi ya Zabuni. Halmashauri husika na kiasi cha fedha kilichotumika ni kama inavyoonekana katika jedwali hapa chini:

| Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|
| 1 | H/W Mkuranga | 68,497,262 |
| 2 | H/W Chamwino | 34,720,000 |
| 3 | H/M Dodoma | 47,435,485 |
| 4 | H/M Kigoma/Ujiji | 15,807,500 |
| 5 | H/M Mtwara | 4,252,000 |
| 6 | H/W Songea | 25,271,600 |
| 7 | H/W Tunduru | 44, 000,450 |
| | **JUMLA** | **239,984,297** |

Mbali ya kutofuata Sheria ya Manunuzi ya Umma, pia thamani ya fedha katika manunuzi haya haikuweza kuthibitika.

**b) Manunuzi ya huduma kutoka kwa wazabuni wasiothibitishwa Sh.272,623,633**

Kanuni Na. 67 (3) ya Kanuni za manunuzi ya Umma za mwaka 2005 inasema kwamba isipokuwa pale ambapo wazabuni, wakandarasi au watoa huduma tayari wameainishwa (pre qualified), taasisi inayofanya manunuzi kwa kutumia zabuni zilizodhibitiwa (restricted tender) atahitajika kutafuta mzabuni kutoka kwenye orodha ya wazabuni waliopitishwa/waliothibitishwa, kwa mapana zaidi ili kuleta ushindani wa bei.

Hata hivyo, Ukaguzi umebaini kuwa malipo yenye jumla ya kiasi cha Sh.272,623,633 yanayohusu Halmashauri 19 yalilipwa kwa wauzaji mbalimbali wa bidhaa na huduma ambao hawakuwa katika orodha ya wazabuni waliopitishwa kwa ajili ya mwaka wa fedha 2010/11.

| Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|
| 1. | H/W Meru | 21,086,150 |
| 2. | H/W Bagamoyo | 3, 068,000 |
| 3. | H/W Mkuranga | 37,000,000 |
| 4. | H/W Rufiji/Utete | 2,700,000 |
| 5. | H/Mji Lindi | 1,012,200 |
| 6. | H/W Kilombero | 3,441,276 |
| 7. | H/W Morogoro | 1,924,875 |
| 8. | H/W Mvomero | 23,619,550 |
| 9. | H/M Mtwara | 4,252,000 |
| 10. | H/W Tandahimba | 6,646,000 |
| 11. | H/W Misungwi | 4,000,000 |
| 12. | H/W Sengerema | 64, 481,290 |
| 13. | H/W Mbinga | 35,315,000 |
| 14. | H/M Songea | 7,057,000 |
| 15. | H/W Kahama | 4, 339,500 |
| 16. | H/M Shinyanga | 12,505,000 |
| 17. | H/W Kishapu | 20,106,500 |
| 18. | H/W Kilindi | 18,969,292 |
| 19. | H/W Nzega | 1,100,000 |
| **Jumla** | | **272,623,633** |

Ubora wa vifaa vilivyonunuliwa kutoka kwa wauzaji wasiopitishwa haukuweza kuthibitika. Pia, Halmashauri hizi hazikuzingatia sheria za manunuzi za Umma, 2004 na kanuni zake za mwaka 2005.

### c) Manunuzi yaliyofanywa bila kuwa na ushindani Sh.397,571,968

Uhakiki wa kumbukumbu za manunuzi kwa mwaka wa fedha 2010/2011 ulibaini kuwa kiasi cha Sh.397,571,968 kililipwa na Halmashauri kwa ajili ya kununua vifaa, kazi za ujenzi na huduma mbalimbali bila kufuata utaratibu wa ushindani wa bei kinyume na kanuni ya 63 ya Kanuni za Manunuzi ya umma, za mwaka 2005. Kutokufuata kanuni za manunuzi zilizowekwa kunaleta mashaka kama kweli thamani ya fedha ilipatikana katika manunuzi haya na vifaa vilivyonunuliwa vina ubora.

Jedwali hapa chini linaonyesha kiasi kilicholipwa kwa kila Halmashauri bila kuwa na ushindani.

| Na. | Halmashauri | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|
| 1 | H/W Kondoa | 53,907,992 |
| 2 | H/W Muleba | 49,300,600 |
| 3 | H/W Hanang' | 44,000,000 |
| 4 | H/W Babati | 43,187,500 |
| 5 | H/W Missenyi | 40,125,423 |
| 6 | H/W Bahi | 34,897,000 |
| 7 | H/W Shinyanga | 23,180,670 |
| 8 | H/W Mufindi | 19,440,016 |
| 9 | H/W Meru | 19,169,575 |
| 10 | H/W Biharamulo | 16,470,000 |
| 11 | H/W Ngara | 12,142,250 |
| 12 | H/W Rombo | 10,650,000 |
| 13 | H/W Nanyumbu | 7,868,800 |
| 14 | H/ Mji Njombe | 7,000,000 |
| 15 | H/W Bukoba | 5,591,440 |
| 16 | H/M Musoma | 3,638,723 |
| 17 | H/W Liwale | 2,100,000 |
| 18 | H/W Kilombero | 1,750,000 |
| 19 | H/W Kibondo | 1,701,980 |
| 20 | H/W Mafia | 1,450,000 |
| | **Jumla** | **397,571,968** |

Uongozi wa Halmashauri husika unatakiwa kuhakikisha kwamba angalau nukuu za bei zinapatikana kutoka kwa wauzaji watatu tofauti wa mali na huduma kabla ya manunuzi kufanyika ili kuhakikisha kuwa sheria na kanuni za manunuzi zinafuatwa. Inapobidi kununua kutoka kwa muuzaji mmoja,

uthibitisho na uhalali wa kufanya hivyo ni lazima upatikane na utaratibu huo upate kibali kutoka katika mamlaka husika.

**d) Vifaa ambavyo havikuingizwa katika leja ya vifaa Sh.594,164,665**

Agizo Na. 207 la Memoranda ya Fedha za Serikali za Mitaa ya mwaka 1997, inataka kumbukumbu za mapokezi, vifaa vilivyotoka stoo na kiasi cha vifaa vinavyosalia katika stoo viandikwe katika kurasa tofauti za leja ya stoo ikionyesha taarifa zote za manunuzi kama; tarehe ya kununua, stakabadhi ya kutolea mali ghalani, idadi na kiasi kwa kila kifaa kilichonunuliwa. Pia inataka tarehe ya kutolea mali ghalani, kiasi kilichotolewa, namba ya hati ya kutolea mali na kiasi kilichobaki ghalani.

Hata hivyo, ukaguzi uliofanyika kuhusu udhibiti wa bidhaa ghalani umeonyesha kuwa halmashauri 22 hazikufuata matakwa ya Agizo hilo. Angalia jedwali hapa chini:

| Na. | Halmashauri | Kiasi (Sh.) |
|---:|---|---:|
| 1 | H/W Ngorongoro | 242,698,650 |
| 2 | H/M Arusha | 94,643,000 |
| 3 | H/W Monduli | 49,027,030 |
| 4 | H/W Meatu | 37,306,950 |
| 5 | H/W Kilindi | 33,485,800 |
| 6 | H/M Dodoma | 31,812,200 |
| 7 | H/W Mbozi | 27,530,000 |
| 8 | Jiji la Mbeya | 13,292,200 |
| 9 | H/W Shinyanga | 9,720,000 |
| 10 | H/W Longido | 9,094,960 |
| 11 | H/Mji Korogwe | 8,719,040 |
| 12 | H/W Mbinga | 6,785,000 |
| 13 | H/W Songea | 6,740,000 |
| 14 | H/M Shinyanga | 5,885,000 |
| 15 | H/M Mtwara | 4,252,000 |
| 16 | H/W Chamwino | 3,699,535 |
| 17 | H/Mji Njombe | 3,020,160 |
| 18 | H/W Arusha | 2,748,000 |

| | | |
|---|---|---|
| 19 | H/W Meru | 1,538,200 |
| 20 | H/W Mbulu | 805,940 |
| 21 | H/Mji Babati | 700,000 |
| 22 | H/W Simanjiro | 661,000 |
| **Jumla** | | **594,164,665** |

Kwa manunuzi haya ambayo hayakuingizwa katika leja ya vifaa, yamedhibiti mawanda ya ukaguzi katika kujihakikishia iwapo vifaa vilivyonunuliwa vimepokelewa na taarifa zake kuwekwa vema.

**e) Vifaa vilivyolipiwa lakini havikupokelewa Sh.833,707,405**

Kanuni ya 122(1) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma, 2005, inaitaka kila taasisi inayofanya manunuzi kupata taarifa ya mapokezi ya vifaa vilivyonunuliwa kulingana na mkataba ili kuwezesha taasisi husika kufanya malipo kwa mzabuni. Kinyume na kanuni hiyo, vifaa vyenye thamani ya Sh. 833,707,405 viliagizwa na kulipiwa lakini vilionekana kupokelewa pungufu au kutopokelewa kabisa na Halmashauri kumi na tatu (13) kama inavyoonyeshwa katika Jedwali lifuatalo:

| Na. | Halmashauri | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|
| 1 | H/M Kinondoni | 523,532,623 |
| 2 | H/W Masasi | 197,795,500 |
| 3 | H/W Ngorongoro | 26,310,181 |
| 4 | H/W Kilolo | 22,000,000 |
| 5 | H/Mji Njombe | 11,827,800 |
| 6 | H/W Bagamoyo | 11,410,000 |
| 7 | H/W Nkasi | 8,998,400 |
| 8 | H/W Handeni | 7,807,831 |
| 9 | H/W Chamwino | 7,644,300 |
| 10 | H/W Mbinga | 6,785,000 |
| 11 | H/M Sumbawanga | 5,975,170 |
| 12 | Jiji la Mbeya | 3,498,200 |
| 13 | H/W Monduli | 122,400 |
| **Jumla** | | **833,707,405** |

Kutofuatilia kwa umakini juu ya vifaa vilivyolipiwa kabla vinaweza kuleta hasara kwa rasilimali za Serikali kupitia kutopokelewa kwa vifaa.

**f) Mapungufu katika kutunza kumbukumbu za mikataba na miradi Sh.4,452,071,069**

Utunzaji bora wa nyaraka za mikataba na miradi ni muhimu kwa ajili ya kurahisisha upatikanaji wa nyaraka zinapohitajika ili kuhakikisha mikataba inafanyika na kufuatiliwa ipasavyo. Utaratibu mzuri wa kuhifadhi nyaraka pia utawezesha Halmashauri husika na wadau wengine kama vile wafadhili na wakaguzi kupata nyaraka na taarifa muhimu kwa urahisi zaidi.

Hata hivyo, mapitio ya mikataba mbalimbali katika kipindi cha ukaguzi yalibaini mikataba mingi ambayo haikuwa na nyaraka muhimu katika majalada husika kama vile; makadirio ya gharama ya ujenzi, Makadirio ya Mkandarasi, vyeti vya kuruhusu malipo kwa mkandarasi na manunuzi ambayo yalifanywa kinyume na mpango wa mwaka wa manunuzi.

Kiwango cha kufuata sheria na kanuni za manunuzi bado hakiridhishi. Pia kwa upande wa matumizi ya aina hii kuna ongezeko ambapo katika mwaka wa ukaguzi, kiasi cha Sh.4,452,071,069 kama inavyoonyeshwa katika **Kiambatanisho (xxxvi)** kilitumika ikilinganishwa na kiwango cha Sh.1,755,429,901 kilichotolewa taarifa katika ukaguzi uliopita kama inavyoonekana katika jedwali hapa chini:

| Mwaka | Idadi ya Halmashauri | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|
| 2009/10 | 10 | 1,755,429,901 |
| 2010/11 | 24 | 4,452,071,069 |

Uongozi wa Halmashauri husika kwa mara nyingine unakumbushwa kuimarisha taratibu za manunuzi ili kuhakikisha kwamba zinapata thamani ya fedha kwa mali na huduma zinazonunuliwa. Kulingana na Agizo Namba 281 la Memoranda ya Fedha za Serkali za Mitaa ya mwaka 1997, Serikali za mitaa kupitia Halmashauri husika zinatakiwa kuteua watumishi watakaohusika na usimamizi na utekelezaji wa mikataba.

## 6.4 Mapungufu Katika Kuhesabu Mali/Vifaa

Maagizo Na.241-242 ya Memoranda ya Fedha za Serikali za Mitaa, 1997 yanazitaka Halmashauri kuhesabu mali kila mwisho wa mwaka wa fedha ambayo inajumuisha mali zilizopo ghalani na mali nyinginezo za Halmashauri. Hata hivyo, ukaguzi wa sampuli 26 za Halmashauri umeonyesha kuwa, mazoezi ya kuhesabu mali hayakufanyika kitu ambacho ni kinyume na matakwa ya maagizo yaliyotajwa hapo juu. Aidha, Halmashauri nyingine zilijifanya kana kwamba zimehesabu mali lakini usahihi wa takwimu za taarifa za zoezi hilo hazikuweza kukubalika kutokana na kutopatikana kwa karatasi za kuhesabu mali zilizoshuhudiwa na Wakaguzi kulingana matakwa ya kifungu Na. 59 (4) cha Viwango vya Kimataifa vya Ukaguzi.

Zaidi ya hayo, wakati wa zoezi la kuhesabu mali iligundulika kuwa vifaa mbalimbali vilikuwa havikupangwa vizuri. Kulikuwa na uhaba wa vyumba vyenye rafu (shelves) katika maghala matokeo yake baadhi ya vitu vilikuwa vimewekwa sakafuni. Pia, kulikuwa hakuna kadi za kutambulisha mali katika baadhi ya maghala yaliyotembelewa. Kutokana na hali tajwa hapo juu ilikuwa ni vigumu kujua usahihi wa takwimu na taarifa za mali za Halmashauri 26 zenye thamani ya Sh.7,493,150,850 zilizoonyeshwa katika taarifa za fedha.

Uongozi wa Halmashauri unapaswa kufanya zoezi la kuhesabu mali kila inapofikia mwisho wa mwaka na angalau Maafisa watatu lazima wahudhurie

katika zoezi hilo na kwamba karatasi za kuhesabu mali zisainiwe na Maafisa wote wanaoshiriki katika zoezi hilo.

Zaidi ya hayo, Uongozi wa Halmashauri unatakiwa uhakikishe kuwa vifaa na mali zote ni vizuri vipangwe vyema kabla ya zoezi la kuhesabu mali halijaanza ili kurahisisha zoezi hilo na kupunguza uwezekano wa kutoonwa kwa baadhi ya vitu au upotevu wa fedha kutokana na mali iliyoharibika. Katika siku za baadaye, Uongozi wa Halmashauri unapaswa kuzingatia Maagizo Na. 241-243 ya Memoranda ya fedha za Serikali za Mitaa ya mwaka 1997 na kuwakaribisha wakaguzi wakati wa zoezi la kuhesabu mali.

Mapungufu yaliyobainika wakati wa zoezi la kuhesabu mali yalihusisha Halmashauri ishirini na sita (26) ni kama zilivyoonyeshwa katika jedwali hapa chini:

| Na. | Halmashauri | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|
| 1 | H/M Arusha | 483,349,000 |
| 2 | H/W Longido | 33,237,000 |
| 3 | H/M Kinondoni | 197,801,792 |
| 4 | H/W Bahi | 6,542,699 |
| 5 | H/W Kondoa | 667,117,147 |
| 6 | H/W Mpwapwa | 652,684,844 |
| 7 | H/W Kasulu | 311,703,542 |
| 8 | H/W Kibondo | 70,668,000 |
| 9 | H/W Nachingwea | 70,521,000 |
| 10 | H/W Babati | 64,130,000 |
| 11 | H/W Kiteto | 50,126,865 |
| 12 | H/W Mbozi | 42,385,500 |
| 13 | H/W Geita | 2,462,098,000 |
| 14 | H/Mji Mpanda | 1,007,596,265 |
| 15 | H/M Sumbawanga | 14,593,244 |
| 16 | H/W Bariadi | 131,578,334 |
| 17 | H/W Bukombe | 172,435,414 |
| 18 | H/W Kahama | 482,603,496 |
| 19 | H/W Shinyanga | 38,492,200 |
| 20 | H/M Shinyanga | 56,605,805 |
| 21 | H/W Kishapu | 9,322,455 |
| 22 | H/W Maswa | 114,533,948 |
| 23 | H/ Mji Korogwe | 21,282,051 |
| 24 | H/W Kilindi | 10,683,600 |
| 25 | H/W Tabora | 89,489,600 |
| 26 | H/W Urambo | 231,569,049 |
| | **JUMLA** | **7,493,150,850** |

## SURA YA SABA

## 7.0 KAGUZI MAALUM

### 7.1 Muhtasari wa masuala yaliyojitokeza katika kaguzi maalumu

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) anaruhusiwa kufanya ukaguzi maalum kutokana na maombi kutoka kwa mtu yeyote, Taasisi, Mamlaka ya Umma, Wizara, Idara, Wakala, Mamlaka ya Serikali za Mitaa na vyombo vingine vile vile. Sheria pia inampa CAG mamlaka ya kufanya ukaguzi maalum pale anapoona inafaa. Katika mwaka husika, kaguzi maalum nane (8) zilifanyika. Muhtasari wa masuala yaliyojitokeza katika kaguzi maalumu ni kama ifuatavyo:

### 7.1.1 Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa

Katika mwaka wa fedha 2010/2011, Ukaguzi Maalum ulifanyika katika Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa. Muhtasari wa matokeo ya ukaguzi huo ni kama ifuatavyo:

- Taratibu za zabuni katika ujenzi wa nyumba za watumishi zenye thamani ya Sh.127,443,334 hazikufuatwa.
- Mikataba mingi haikumalizika ndani ya muda uliokubaliwa kwa sababu ya uwezo mdogo wa wakandarasi na usimamizi usiojitosheleza.
- Malipo ya muda wa uangalizi Sh.11,796,685 yalifanyika mara mbili kwa Mkandarasi Kalumanyili Enterprises.
- Malipo ya muda wa uangalizi Sh.19,411,178 yalilipwa kabla muda wa uangalizi kuisha.
- Fidia ya kutokamilisha kazi za ujenzi kwa wakati Sh.42,600,318 haikutozwa katika miradi minne ambayo haikukamilika.

- Halmashauri ililipa zaidi kiasi cha Sh.19,963,010 kwa kazi ya kupaka rangi katika nyumba 10 za watumishi.
- Kutokukamilika kwa miradi ya umwagiliaji katika kijiji cha Lifua na Mkiu Sh.725,033,547.
- Malipo ya Sh.13,094,400 yalilipwa kwa kazi ambayo haikufanyika.
- Mhandisi Mkazi hakusimamia ipasavyo miradi ya Umwagiliaji katika kijiji cha Mkiu na Lifua.
- Miradi yenye thamani ya Sh.170,173,107 imekamilika lakini haitumiki.
- Malipo ya mishahara Sh.48,148,000 yalilipwa kwa watumishi zaidi ya viwango vya mshahara wananavyostahili.
- Wafanyakazi kukaa katika kituo kimoja kwa muda mrefu bila ya uhamisho, hali hii imesababisha utendaji kazi usio na ufanisi.

### 7.1.2 Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu

Ukaguzi Maalum ulifanyika katika Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu ukihusisha kipindi cha kuanzia tarehe 1 Julai, 2007 hadi tarehe 30 Oktoba, 2010. Muhtasari wa matokeo ya ukaguzi huo ni kama ifuatavyo:

- Mapato yenye jumla ya Sh.32,230,000 ya mwaka 2009/2010 hayakuwasilishwa na mawakala wa ukusanyaji mapato.
- Hati za malipo za Sh.1,171,735,534 za mwaka wa fedha 2009/2010 hazikuwasilishwa kwa ajili ya Ukaguzi.
- Malipo ya mishahara Sh.66,325,162 ililipwa kwa watumishi hewa (watumishi waliostaafu na kuacha kazi).
- Matumizi mabaya ya fedha za miradi ya maendeleo Sh.5,513,049,264 ambayo yalitokana kwa kughushi taarifa za benki, hundi, kuhamisha fedha bila idhini ya Mkuu wa Idara na benki kulipa malipo kwa walipwaji wasiojulikana.

- Fedha za miradi ya maendeleo ya mwaka 2009/2010 kiasi cha Sh.724,632,112 hazikuhamishwa kutoka Akaunti ya Maendeleo kwenda katika Kata na Vijiji husika kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo ndani ya Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu. Kiasi hiki kilihusisha miradi ya maji (NRWSSP) Sh.88,700,000, miradi ya afya (HBF) Sh.244,358,000, JRF Sh.338,372,112 na miradi ya UKIMWI (TACAIDS) Sh.53,202,000.
- Malipo ya thamani ya Sh.465,780,569 yalitolewa kwa ajili ya shughuli zisizotarajiwa. Malipo haya yalihusisha mradi wa maji (NRWSSP ) Sh.338,974,569 na Mfuko wa afya wa jamii (CHF) Sh.126, 806,000.
- Katika mwaka 2009/2010, Halmashauri ilipokea kiasi cha Sh.338,372,112 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya afya (HBF,HSDG na JRF). Halmashauri haikuhamisha fedha hizi kupeleka katika akaunti ya Kamati ya Ujenzi ya afya ya msingi badala yake iliingia mkataba na wakandarasi mbalimbali kinyume na miongozo na taratibu zinazosimamia fedha za miradi ya afya.
- Katika mwaka 2009/2010, malipo ya kiasi cha Sh.20,800,000 yalilipwa kwa walipwaji wasiojulikana.
- Fedha za mradi wa afya wa jamii (CHF) Sh.27,000,000 zilitolewa na Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga kwenda Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu mwaka 2007/2008 kupitia barua yenye Kumbukumbu namba 15/32008, fedha hizi hazikuingizwa katika akaunti ya mradi wa afya (CHF) kama ilivyoonyeshwa katika taarifa za benki. Hivyo, haikuweza kufahamika fedha hizo ziliwekwa akaunti gani.
- Fedha za mradi wa afya (CHF) Sh12,358,000 na fedha za UKIMWI (TACAIDS) Sh.66,700,000 zilihamisha kwenda kwenye akaunti mbalimbali za Halmashauri bila ya kuwa na idhini ya Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya.
- Hati za malipo ya Sh.221,805,777 zililipwa kwa walipwaji mbalimbali bila kuidhinishwa na Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya.

- Nyaraka za mikataba za Sh.4,258,312,634 hazikuonekana katika mafaili husika ya mikataba wakati wa ukaguzi.
- Katika mwaka 2007/2008, Halmashauri ilihamisha fedha za mradi wa LGCDG Sh.260,803,765 kwenda katika kata 20 kwa ajili ya ujenzi wa Maabara 21 katika shule za sekondari 21, Hata hivyo mpaka kipindi cha ukaguzi miradi hiyo ilikuwa haijakamilika.
- Ukaguzi wa leja za mafuta za mwaka 2008/2009 na 2009/2010 ulibaini kuwa mafuta yenye thamani ya Sh.42,198,300 yalitumika kwa ajili ya shughuli zisizojulikana.
- Makato ya mishahara yenye thamani ya Sh.281,954,806 ya mwaka 2009/2010 hayakulipwa kwenye taasisi husika kinyume na Agizo namba 309 la Memoranda ya Fedha za Serikali za Mitaa ya mwaka 1997.

### 7.1.3 Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema

Ufuatao ni muhtasari wa matokeo ya ukaguzi maalum na pamoja na masuala ambayo yanahitaji kuchukuliwa hatua:

- Jumla ya Sh.77,070,789 zilitolewa na Serikali Kuu kwa ajili ya mradi wa Maji Nyamazugo na kiasi hicho kilitakiwa kuhamishiwa kwenye akaunti ya Mamlaka ya Maji Sengerema. Hata hivyo kati ya Sh.77,070,789 zilizopokelewa ni Sh.73,691,564 ndizo zilikuwepo katika akaunti maalum ya maji na kutumika kwa malengo yaliyokusudiwa. Hivyo, tofauti ya kiasi cha Sh.3,379,225 hakikutolewa maelezo
- Jumla ya Sh.572,569,599 zililipwa kwa ajili ya shughuli zisizokuwa kwenye mpango na pia zisizoidhinishwa na mamlaka husika.
  Mikataba ya thamani ya Sh.164, 791,440 ilifanywa bila ya kuwepo na makisio ya mhandisi kinyume na kanuni ya 46 (8) ya Kanuni za manunuzi ya Umma, 2005 (G.N.97)
  Mkataba wa thamani ya Sh.142,748,440 uliingiwa bila ya kuwepo na dhamana (performance security bond) kinyume na Agizo Na. 294 na 295 la LAFM, 1997 na kifungu cha 53 cha Sheria ya Manunuzi ya Umma, 2004.
- Malipo ya Sh.1,119,955,370 yalifanywa kwa walipwaji mbalimbali bila viambatanisho na uchambuzi wa gharama kutoka kwa wakandarasi kinyume na kanuni ya Na.95 (4) ya Kanuni za Fedha za Umma, 2004
- Kulikuwa na makosa yanayohusiana na Sh.142,748,440 kwa ajili ya kuongezwa kwa bomba la maji la Nyampulukano Sengerema mjini.
- Daftari la kumbukumbu za mikataba halikuwa linatunzwa. Baadhi ya taarifa muhimu kwa ajili ya mikataba (kama mabadiliko ya kazi/bei, hati za malipo n.k.). Taarifa muhimu zilikuwa haziandikwi katika daftari la mikataba kinyume na Agizo la 282 la Memoranda ya Fedha ya Mamlaka za Serikali za Mitaa ya mwaka 1997
- Fidia ya kutomaliza kazi kwa wakati ya Sh.66,800,523 haikukatwa kutoka kwenye malipo ya wakandarasi wawili (M/S WEDECO LTD na M/S Gemen Engineering .LTD) waliochelewesha kazi.

- Malipo ya Sh.8,869,880 yalifanywa bila kukata kodi ya ongezeko la dhamani (VAT) kwenye mkataba wenye kumbukumbu WEDECO No. SDC/DED/DWE/WW/52/2007 /2008.
- Malipo ya Sh.14,175,610 yalilipwa bila kuidhinishwa na kinyume na kanunu 89 (2) ya Kanuni za Fedha za Umma ya 2001 (iliyorekebishwa 2004). Rejea mkataba No.SDC/DED/DWE/WW/52/2007/2008.
- Vifaa vya kuunganishia mabomba ya maji vya thamani ya Sh.1,595,000 vilibaki na vilikabidhiwa kwa Halmashauri ya Wilaya na mkandarasi M/S WEDECO baada ya kukamilika kwa mradi wa Nyamazugo lakini vifaa hivyo vilivyorudishwa havikuingizwa kwenye leja na pia havikuonekana wakati ukaguzi kinyume na Agizo namba 223 la Memoranda ya Fedha ya Mamlaka za Serikali za Mitaa ya mwaka 1997 na Kanuni Na. 198 ya Kanuni za Fedha za Umma, 2001.
- Halmasahuri iliingia Mkataba wenye thamani ya Sh.424,850,543 kwa ajili ya mradi wa utengenezaji mabomba ya maji katika mradi wa Nyamazugo bila kutangazwa katika magazeti kinyume kanuni Na. 80 (5) ya Kanuni za Manunuzi za Umma, 2005.
- Visima kumi na mbili vilichimbwa katika maeneo mbalimbali ndani ya wilaya kwa gharama ya Sh.139,555,884 lakini kati ya visima kumi na mbili (12) vilivyochimbwa, visima vitano (5) yenye thamani ya Sh.30,630,000 havikuwa vinatoa maji.
- Mkandarasi kwa ajili ya ujenzi wa mabweni mawili na vyoo katika shule ya Sekondari ya Nyampulikano alilipwa zaidi kiasi cha Sh.4,846,715 na pia kiasi cha Sh.403,132 kwa ajili ya ujenzi wa ofisi Afisa Elimu wa Wilaya.
- Kulikuwa na mabadiliko ya bei ambayo hayakuidhinishwa kiasi cha Sh.8,700,000 katika mkataba wa ujenzi wa mabweni mawili na vyoo katika shule ya Sekondari Nyampulikano kinyume na kanuni Na. 44 ya Kanuni za manunuzi ya Umma, 2005.
  Halmashauri iliingia kwenye mkataba wa Sh.36,871,000 na Kampuni ya ujenzi ya Budaga kwa kwa ajili ya uboreshaji wa barabara ya Kasomeko – Mwaloni. Hata hivyo, Sh.22, 871,250 zililipwa kama sehemu ya gharama ya mkataba kwa kutumia jina la Mtu binafsi Bwana Michael K. Budaga badala ya jina la biashara kinyume na kanuni Na. 94 (3) ya Kanuni za Fedha za Umma, 2001.

### 7.1.4 Ukarabati wa Miundo mbinu ya Umwagiliaji katika Vijiji vya Faru na Ndekombeka Kilema Pofo-Kata ya Kilema Kusini: Halmashauri ya Wilaya ya Moshi

Ukaguzi Maalum ulifanyika katika mradi wa PADEP wa Ukarabati wa Miundo mbinu ya Umwagiliaji katika Vijiji vya Faru na Ndekombeka Kilema Pofo – Kata ya Kilema Kusini katika Halmashauri ya Wilaya ya Moshi. Mapungufu yafuatayo yalibainika:

(i) Kiasi cha Sh.18,000,000 kililipwa badala ya Sh.17,000,000 ambacho ndiyo kilikuwa kimeidhinishwa na kamati ya mradi na hivyo kufanya kuwe na malipo zaidi ya Sh.1,000,000.

(ii) Malipo yalitolewa kabla ya kazi kukaguliwa na Afisa Umwagiliaji wa Wilaya. Ripoti ya tarehe 5/10/2011 ilionyesha kwamba mradi ulikuwa umetekelezwa kwa 49% sawa na Sh.8,303,030 na kubaki 51%, sawa na Sh.8,969,970 ambayo ilikuwa haijatekelezwa. Hii ina maana kwamba mkandarasi alilipwa kiasi chote kabla ya kumaliza kazi kinyume na mkataba.

(iii) Uchunguzi wa barua yenye kumbukumbu. AG/M.10/6/VOL.II/91 ya tarehe 30/5/2011 unaonyesha kuwa mradi huo ulikuwa ukamilike tarehe 28/12/2010. Pia ripoti ya 2009/2010 ya ukaguzi uliofanywa na mkaguzi kutoka Wizara ya Kilimo, Chakula na umwagiliaj- mradi ulitakiwa kukamilika kabla ya 30/6/2011. Ziara ya kutembelea mradi iliyofanyika tarehe 21/9/2011, wiki 35 baada ya tarehe ya kukamilika, alibainika kuwa mradi huo ulikuwa bado haujakamilika.

### 7.1.5 Kijiji cha Barabarani - Halmashauri ya Wilaya ya Monduli

Ufuatao ni muhtasari wa mambo yaliyojitokeza wakati wa ukaguzi maalum uliofanyika:

- Kulikuwa na makusanyo na malipo ambayo hayakuwa viambatisho – Sh.9,207,000 kwa mwaka 2005/2006 na Sh.10,029,880 kwa mwaka 2006/07.
- Vitabu vya risiti vya ukusanyaji mapato ambavyo vilikusanya Sh.2,054,000 havikupatikana na kuwasilishwa wakati wa ukaguzi.
- Vitabu vya stakabadhi ambavyo vilikusanya Sh.3,668,409 kwa mwaka wa fedha 2005/06 havikupatikana na kuwasilishwa wakati wa ukaguzi.
- Kulikuwa na makusanyo ya mapato ya Sh.818,000 ambayo yalikusanywa kwa kutumia hati za malipo badala ya kutumia risiti za mapato.
- Mapato ya kiasi cha Sh.12,087,000 yalikusanywa kwa kutumia risiti za mapato, lakini hatukuweza kupata vitabu vilivyokusanyia na wala nyaraka za benki hazikupatikana.
- Kulikuwa na upotevu wa mapato ya kijiji kwa kipindi cha mwaka 2004/05 na 2005/06 ya Shs.880, 000 yaliyotokana na kulipa nje ya mkataba.
- Kulikuwa na matumizi yaliyolipwa bila viambatisho ya Sh.10,357,030.
- Vitabu viwili vya risiti za ukusanyaji Mapato vyenye namba 42201-42250 na 24651 - 24700 havikupatikana wakati wa ukaguzi.
- Kulikuwa na ugawaji wa viwanja kwa kutumia vitabu vya stakabadhi visivyotambuliwa na Halmashauri ya Wilaya ya Monduli.

### 7.1.6 Halmashauri ya Wilaya ya Longido

Katika mwaka wa fedha 2010/2011, Ukaguzi Maalum ulifanyika katika Halmashauri ya Wilaya ya Longido. Muhtasari wa matokeo ya ukaguzi huo ni kama ifuatavyo:

- Fedha za Miradi ya Afya na Elimu zilitumika kimakosa katika kufidia upungufu wa bajeti kwa ajili ya kununua magari kwa kiwango cha Shs.65, 386,809 na hivyo kusababisha miradi husika isitekelezwe kama ilivyopangwa
- Halmashauri ilinunua vifaa vya thamani ya Sh.1,008,020,362 ambavyo havikuwa katika mpango wa mwaka wa manunuzi kinyume na Kifungu namba 45 cha Sheria ya Manunuzi ya Umma Na.21.
- Halmashauri iliingia mkataba na Mkandarasi kwa ajili ya kazi ya ujenzi bila kuleta dhamana ya ujenzi Sh.81,566,375 ambayo ni asilimia 10% ya bei ya mkataba.
- Kukosekana kwa uwazi katika mabadiliko ya bei za mikataba ya wakandarasi watatu yenye thamani ya Sh.99,524,294.
- Fidia ya kutokamilisha kazi ya ujenzi kwa wakati Sh.12,166,984 haikutozwa kinyume na kifungu namba 27.1 hadi 27.4 cha mkataba.
- Bei ya mkataba ya ujenzi wa jengo la ofisi Sh.81,343,000 ilibadilishwa bila idhini ya Bodi ya Zabuni ya wilaya.
- Malipo ya awali Sh.10,000,000 yalilipwa kwa Mkandarasi bila dhamana ya benki kinyume na Sheria za Manunuzi ya Umma na pia kinyume na kipengele Na.54.1 cha mikataba.
- Kazi za mikataba ya ujenzi yenye thamani ya Sh.10,556,000 ilikabidhiwa kwa Halmashauri bila kukamilika.
- Ukaguzi umebaini kukosekana kwa ushahidi wa kuhakiki ubora wa vifaa kwa ajili ya ujenzi wa jengo la ghorofa moja pamoja na kuwa kiasi cha Sh.10,450,000 kilikuwa kimewekwa kwenye mchanganua wa bei (BOQ) kwa kazi hiyo.
- Kazi za Kilimo (DADPS) za thamani ya Sh.124,887,200 zilitolewa kwa mkandarasi bila ya kupitishwa na Bodi ya Zabuni kinyume na Kanuni ya 19 (1) na (2) ya sheria ya Bodi ya Zabuni ya Serikali za Mitaa.
- Fidia ya kucheleweshа kumaliza kazi kiasi cha Sh.9,371,667 haikukatwa kutoka kwenye malipo ya mkandarasi aliyechelewesha ujenzi wa nyumba tatu (3) za wafanyakazi Longido na nyumba moja (1) ya wafanyakazi Matale.
- Jumla ya Sh.19,975,822 zilipelekwa kwa ajili ya ujenzi wa Hosteli Matale (A) lakini zilitumika kwa madhumuni na kazi nyingine isiyokuwa kwenye mpango.
- Kulikuwa na gharama za usafirishaji wa vifaa kutoka Arusha zilizokuwa zimeghushiwa. Vifaa hivyo vilinunuliwa kwa Sh.2,718,000 na kusafirishwa kwa Sh.4,500,000 lakini tulibaini kuwa gharama halisi ya usafiri wakati wa ukaguzi ilikuwa ni Sh.2,046,000.
- Malipo ya Sh.4,000,000 yalilipwa kwa Mhandisi wa Wilaya kwa hundi Na.213754 na vocha No 1/6 laakini hayakuwa na viambatanisho.
- Kulikuwa na ununuzi wa vifaa vya mabomba 257 kutoka kwa wauzaji mbalimbali kwa bei zaidi ya bei ya soko kwa kiasi cha Sh.22,260,000 wakati wa utekelezaji wa mradi wa maji katika kijiji cha Mundarara.

- Jumla ya Sh.8,685,000 zilizotumika katika kununua chakula cha wanafunzi. Hakuna ushahidi uliotolewa kuthibitisha mapokezi na matumizi ya fedha hizo.
- Kulikuwa na jumla ya Sh.270,460,200 ambazo zilikuwa ni kodi ya ongezeko la thamani (VAT) kutokana na mikataba iliyoingiwa kati ya Halmashauri na wakandarasi mbalimbali ambazo hazikuzilipwa kwenye Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA).

### 7.1.7 Halmashauri ya Wilaya ya Kilindi

Ukaguzi Maalum ulifanyika katika Halmashauri ya Wilaya ya Kilindi. Muhtasari wa matokeo ya ukaguzi huo ni kama ifuatavyo:

- Malipo ya Sh.835,355,000 yalilipwa kwa Mkandarasi MS Afriq kama gharama ya vifaa vilivyokuwepo eneo la ujenzi kinyume na miongozo ya manunuzi ambayo inataka mkandarasi alipwe kwa kazi iliyofanyika.
- Bei ya mkataba wa ujenzi wa jengo la ofisi ilibadilishwa kutoka Sh.1,509,378,195 hadi Sh.2,894,804,195 bila idhini ya Bodi ya Zabuni ya Wilaya.
- Halmashauri ililipa Sh.48,000,000 kwa ajili ya milango na madirisha ya 'aluminium' ambayo haikupelekwa kwenye eneo la ujenzi.
- Fidia ya kutokamilisha kazi ya ujenzi kwa wakati katika jengo la Utawala la Halmashauri Sh.109,900,000 haikutozwa kinyume na makubaliano ya Mkataba.
- Aina ya Bati zilizotumika katika ujenzi wa jengo la Utawala la Halmashauri zenye thamani ya Sh.44,250,000 zilikuwa si sawa na zile zilizoainishwa katika mkataba
- Malipo ya kazi ya usanifu ya kuchora jengo la Utawala la Halmashauri ya Sh.800,000 yalilipwa zaidi ya inavyostahili.
- Kiasi cha Sh.4,800,000 kililipwa kwa kampuni ya ushauri ya NEDCO kama kodi ya ongezeko la thamani. Hata hivyo, ukaguzi ulibaini kuwa kiasi hicho cha kodi hakikupelekwa kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania.
- Mkandarasi – Clear Vision hakulipa kodi ya ongezeko la thamani kiasi cha Sh.38,288,110 kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania.
- Matumizi ya Mafuta yenye thamani ya Sh.6,256,000 hayakuingizwa katika leja na matumizi yake hayakufahamika.
- Fidia ya kutokamilisha kazi ya ukarabati wa zahanati kwa wakati Sh.6,531,624 haikutozwa kinyume na makubaliano ya mkataba.
- Fedha za mradi wa maji (WSDP) Sh.22,800,00 zilipotea kwa njia ya kughushi taarifa za benki.
- Malipo yenye Mashaka ya Sh.2,370,000 yalilipwa kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya ujenzi wa choo cha shimo cha mfano.
- Halmashauri ilitoa mafuta ya gari yenye thamani ya Sh.1,783,600 kwa gari binafsi kinyume na taratibu na sheria za matumizi ya Serikali.
- Makato ya mishahara yenye thamani ya Sh.4,368,684 ya watumishi hewa yalilipwa kwa taasisi husika kinyume na Agizo namba 309 ya Memoranda ya Fedha za Serikali za Mitaa ya mwaka 1997.

- Vocha za malipo zenye thamani ya Sh.31,245,700 hazikuonekana wakati wa kipindi cha ukaguzi maalum.
- Hundi zilizolipwa zenye jumla ya Sh.27,186,000 hazikupatikana.

- Mafuta ya Sh.5,100,000 hayakuingizwa katika leja ya mafuta.
- Mafuta ya Sh.1,798,500 yaliagizwa na kulipiwa, lakini mapokezi yake hayakuthibitishwa.

### 7.1.8 Machinjio ya Vingunguti - Manispaa ya Ilala

Wakati wa ukaguzi, mafungufu mbali mbali yalibainika kama yanavyoainishwa hapa chini:

- Halmashauri inakusanya kodi ya aina tatu katika machinjio ya kisasa ya Vingunguti kama vile kodi kwa ajili ya kuchinja, ukaguzi wa nyama na kodi kwa ajili ya kusafirisha nyama. Kwa kuzingatia hayo, katika mwaka wa fedha 2009/2010 Halmashauri ya Manispaa ya Ilala iliweka makadirio ya kukusanya kiasi cha Sh.244,000,000 na Sh.290,000,000 kwa mwaka wa fedha 2010/2011 na kupelekea jumla ya makadirio kuwa Sh.534,000,000 kwa miaka miwili. Hata hivyo, Halmashauri iliweza kukusanya jumla ya Sh.221,488,650 kwa mwaka 2009/2010 na Sh.266,782,650 kwa mwaka 2010/2011 na kupelekea jumla ya kiasi cha Sh.488,271,300 ambacho ni sawa 91% ya fedha zilizokadiriwa kukusanywa kiasi cha Sh.534,000,000.
- Viwango vya kodi ambavyo vinatumiwa na Halmashauri katika kukusanya mapato havijahuishwa kwa muda mrefu.
  Hakuna utaratibu unaoeleweka ambao unamtaka mkusanya mapato katika eneo la Vingunguti kutayarisha taarifa za kila wiki na kila mwezi kwa ajili ya kuziwasilisha kwa Mhasibu wa Mapato au Mweka Hazina wa Manispaa.
- Halmashauri ya Manispaa ya Ilala haifuatilii au haifanyi usuluhisho baina ya taarifa za ng'ombe au mbuzi wanaoletwa Machinjioni kutoka Soko la Pugu kama ni sawa na taarifa za mifugo hiyo ilivyotolewa Pugu.
- Taarifa zilizopo zinazohusiana na Ng'ombe na Mbuzi waliopokelewa katika Machinjio ya Vingunguti hazionyeshi kumbu kumbu Na. ya vibali vilivyotolewa katika Soko la Vingunguti kwa ajili ya urahisi wa kufanya usuluhisho.
- Halmashauri ya Manispaa ya Ilala haitunzi taarifa zinazoonyesha Ng'ombe na Mbuzi waliopokelewa kutoka soko la Pugu pamoja na namba ya kibali cha Afya ya wanyama wanaosafirishwa au kuruhusiwa kusafiri.
- Kuanzia mwezi Julai 2009 hadi mwezi Oktoba 2010 (miezi 16), Halmashauri ya Manispaa haikuweza kuweka kumbukumbu ya Vibali vya Afya ya wanyama wanaosafirishwa kutoka katika soko la Pugu kwa ajili ya usuluhisho.
- Halmashauri ya Manispaa haitunzi regista inayotunza kumbu kumbu za Vibali kutoka katika Soko la Pugu na matokeo yake idadi kamili kwa siku ya ng'ombe na mbuzi inaopokelewa haikuweza kufahamika.

- Timu ya ukaguzi imebaini kuwepo kwa masoko yasiyo rasmi katika eneo la Vingunguti. Uwepo wa masoko ambayo siyo rasmi katika eneo hilo la soko kumetokana na wanyama kutoka mikoani ambao wanaletwa moja kwa moja katika Soko la Vingunguti bila kwanza kupitia katika soko kuu la Pugu kinyume na Sheria ya Afya ya Wanyama Na.19 ya mwaka 2008 sura ya 8(1)(b) na (e).
- Timu ya ukaguzi ilifuatilia zaidi hadi katika Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi kuulizia kama Machinjio ya Vingunguti yamesajiliwa. Majibu yalikuwa kwamba Machinjio hiyo ya Vingunguti haijasajiliwa. Imebainika kuwa uendeshaji wa Machinjio hayo unafanyika bila kusajiliwa ikiwa ni kinyume na sura 41(1) ya Sheria ya Tume ya Chakula na Dawa ya mwaka 2003.
- Timu ya ukaguzi imebaini kuwa kulikuwa na mapendekezo mengi yaliyotolewa kwa Manispaa ya Ilala na Wataalam wa Wizara jinsi ya kufanya mageuzi katika Machinjio ya Vingunguti ili yaweze kuwa na viwango vinavyokubalika . Kwa mfano:
  - Kuwe na udhibiti wa kuingia katika Manjinjio.
  - Mauzo ya nyama katika Machinjio yanatakiwa kusitishwa mara moja.
  - Maduka ya ngozi yanatakiwa yafanyiwe marekebisho au ukarabati.
  - Maduka ambayo hayakuanzishwa kisheria kwa ajili ya uuzaji wa mbuzi na kondoo katika eneo la Reli yasitishwe mara moja.

Wakati wa kuandika taarifa hii ya ukaguzi maalum wa Machinjio ya Vingunguti, Mapendekezo yote yaliyotolewa na timu ya ukaguzi hayakuweza kupata majibu kutoka kwa uongozi wa Halmshauri.

Hata hivyo, kuna Kaguzi nyingine maalum zinazoendelea katika Halmashauri saba (7) kati ya hizo tatu (3) zinahusu Halmashauri za wilaya za Muheza, Ruangwa na Kilwa. Nyingine mbili (2) ni Halmashauri ya Manispaa ya Temeke na Halmashauri ya Manispaa ya Dodoma. Kaguzi mbili (2) nyingine zinazoendelea ni zile zinazohusu Mfuko wa Jimbo, ambazo zinafanyika Halmashauri ya manispaa ya Musoma na Halmashauri ya wilaya ya Kilindi.

Zaidi ya hizi kaguzi maalum zinazoendelea, kutokana na ukaguzi uliokamilika wa 2010/11 nimefanya maamuzi ya kufanya ukaguzi maalum katika Halmashauri ya Wilaya ya Mvomero kwa kuanzia. Baadhi ya maeneo yatakayozingatiwa katika ukaguzi huu ni pamoja na ujenzi wa jengo la Ofisi, ujenzi wa nyumba ya Mkurugenzi na ujenzi wa majengo ya hospitali matokeo yake yatakuwa katika taarifa za ukaguzi ujao.

Nimatumaini yangu pia kuwa matokeo ya kaguzi maalum katika hizo nane (8) yataonyeshwa katika Ripoti ijayo pamoja na matokeo ya kaguzi nyingine zitakazofanyika ikiwa ni njia ya kuwezesha kuimarisha uwajibikaji katika Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Ofisi ya Ukaguzi itaendelea kupokea maombi kutoka pande zote kwa kuzingatia sheria zilizopo, lakini ieleweke kuwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu hana wajibu na hatalazimika kuyakubali maombi yote lakini atazingatia kila ombi kulingana na uzito wake.

## 7.2 Mafunzo yaliyopatikana kutokana na Kaguzi Maalum zilizofanyika katika mwaka huu

### 7.2.1 Mfumo wa Udhibiti wa Ndani

Imebainika kuwa, kuna udhaifu mkubwa katika Uongozi wa Halmashauri juu ya Uwekaji na Usimamiaji wa Mfumo thabiti wa Udhibiti wa Ndani (Internal Control System). Hali hii imepelekea hata mtu mmoja kukamilisha miamala (transactions) ya kibadhirifu bila kutambuliwa na mfumo uliokuwepo ikiwa ni pamoja na kufanya malipo bila hati za malipo wala hundi.

Mweka Hazina ndiye mwenye majukumu ya kuhakikisha anasimamia mwenendo wa Fedha za Halmashauri na udhibiti wake pamoja na kusimamia kitengo cha Fedha. Hali ambayo imekuwa tofauti kabisa katika Halmashauri zilizokaguliwa, mfano mzuri ni Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu ambapo Mweka Hazina hakuwa makini na alikosa uaminifu ambapo kwa kushirikiana na baadhi ya watumishi alichukua fedha za Halmashauri kinyume na utaratibu.

Udhaifu huu wa Mfumo wa Udhibiti wa Ndani uliwezesha kufichwa kwa ukweli wa hali halisi ya mwenendo wa taarifa za benki katika akaunti mbalimbali. Hali ambayo iliwafanya wakuu wa Idara kutumia taarifa hizo za benki ambazo zilighushiwa. Hali hii inaonesha kuwa mkazo wa ufuatiliaji wa taarifa za benki pamoja na ufanyikaji wa usuluhishi wa benki kuwa ni maeneo ambayo yanatakiwa kuangaliwa kwa umakini zaidi.

### 7.2.2 Ushiriki wa Watumishi wa Benki Katika Njama za Kibadhirifu

Katika ukaguzi maalum uliofanyika katika Halmashauri ya wilaya ya Kishapu imedhihirika kuwa watumishi wa benki wasio waaminifu wameweza kushirikiana na watumishi wa Halmashauri kufanya ubadhirifu. Kwa hali isiyo ya kawaida watumishi wa Benki waliweza kuruhusu kufanyika miamala mbalimbali ambayo ilikuwa ni kinyume na taratibu zilizowekwa kati ya Benki na Halmashauri pamoja na taratibu za ujumla kwa Taasisi za Fedha.

Hali inayoonesha kuwa, badala ya Benki kuwa ni sehemu ya udhibiti wa ubadhirifu lakini imekuwa ni njia ya kukamilika kwa uzandiki (deceit) wa watumishi wasio waaminifu akiwemo Mweka Hazina na watunza fedha. Ubadhirifu mwingi uliofanywa haungewezekana kufanyika bila kuwepo na ushirikiano kati ya watumishi wa Halmashauri na wale wa Benki. Hali hii iliwahi pia kuonekana katika halmashauri ya Rombo na Kilosa.

### 7.2.3 Muda wa wafanyakazi kukaa katika kituo kimoja cha kazi na madhara ya uhamisho wa mara kwa mara

Pamoja na nia nzuri ya kubadilisha vituo vya kazi kwa Watumishi wa Umma hasa Wakurugenzi Watendaji wa Halmashauri ili kuboresha huduma kwa Umma, mabadiliko hayo yakifanyika baada ya vipindi cha muda mfupi sana huathiri utendaji wa jumla wa kazi. Vile vile, baadhi ya Halmashauri zina wafanyakazi ambao wamekaa muda mrefu zaidi ya miaka 25 katika kituo kimoja na hivyo kukosa ufanisi katika kazi na kujiwekea mazingira ya kufanya kazi kwa mazoea.

### 7.2.4 Mapungufu katika manunuzi na mikataba

- Halmashauri zilikuwa zinafanya malipo kwa kutumia gharama za mkataba iliyorekebishwa bila kupata idhini ya Bodi ya Zabuni.

- Wahandisi wa Wilaya wameshindwa kusimamia ujenzi unaofanyika katika Halmashauri na kusababisha miradi mingi ya Halmashauri kuchelewa kukamilika na kazi kufanywa chini ya kiwango na Wakandarasi. Pia, fidia ya ucheleweshaji kazi haikutozwa kwa Wakandarasi ambao hawakumaliza kazi kwa wakati.

- Halmashauri iliingia mikataba na wakandarasi bila ya wakandarasi husika kuwa na dhamana ya kufanya kazi.

- Baadhi ya Wakandarasi walilipwa zaidi ya kiwango walichostahili kulipwa. Malipo hayo yalifanyika kutokana na uzembe wa Wahandisi wa Wilaya wakati kuandaa vyeti vinavyoonyesha kazi iliyofanyika.

- Kiasi kikubwa cha fedha kutokana na Kodi ya ongezeko la thamani (VAT) hakikulipwa kwa Mamlaka ya Kodi ya Mapato (TRA) na Wakandarasi ambao si waaminifu. Taarifa hiyo imethibitika baada ya kufuatilia taarifa za walipa kodi TRA. Ni wazi kwamba kiasi kisicholipwa itakuwa ni hasara kwa Serikali kama hakitabainishwa na TRA.

- Kumekuwa na udhaifu mkubwa kwa Viongozi wa Halmashauri katika kulinda na kusimamia nyaraka muhimu za fedha. Hali hii imesababisha wigo wa ukaguzi kuwa finyu, kwa kutokuonekana kwa nyaraka hizo wakati wa ukaguzi. Hii pia inaweza kuwa ni kiashiria cha kuwepo kwa ubadhirifu mkubwa wa fedha za serikali.

### 7.2.5 Upotevu wa Fedha za Halmashauri

Idadi ya Wanyama waliokuwa wanapokelewa katika Machinjio ya Vingunguti ni kubwa ikilinganishwa na idadi ya Mifugo iliyotoka katika Soko la Pugu sehemu ambayo Wanyama wanatakiwa kukaguliwa kabla ya kupelekwa kwenye Machinjio ya Vingunguti kwa ajili ya kuchinjwa. Hali hiyo

inasababishwa na Wanyama ambao wanapelekwa moja kwa moja kwenye Machinjio na kusababisha Halmashauri ya Manispaa kukosa maduhuli yatokanayo na ada ya kugagua wanyama. Hakuna uthibiti uliowekwa kudhibiti hali hii.

Kwa kumalizia, kunapokuwa na viashiria vya matumizi mabaya ya rasilimali za umma ni lazima Halmashauri zikachukue hatua mapema ili kuzuia madhara zaidi. Aidha,
kuna haja ya kuimarisha Mfumo wa Udhibiti wa Ndani ili kuzuia matumizi mabaya na kuhakikisha uwepo wa mgawanyo wa kazi ambao utasaidia kazi ya Afisa mmoja kuthibitishwa na Afisa mwingine.

## SURA YA NANE

### 8.0 HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

Wigo wa ukaguzi katika Mamlaka za Serikali umekuwa ukibadilika kwa haraka. Hii inatokana na ukweli kwamba Tanzania inafanya marekebisho mbalimbali ambayo yanalenga katika kupeleka Madaraka kwa wananchi (D by D). Ili kuhakikisha kwamba mageuzi ya kuaminika na endelevu yanafanyika, ni muhimu kwamba wadau wote wawe na uhakika kwamba Serikali za Mitaa zina uwezo wa kusimamia fedha na rasilimali nyingine za umma kwa ufanisi. Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi (NAO) kwa kupitia ukaguzi wake wa kila mwaka inafanya juhudi kutimiza wajibu wake kwa uwezo iliyopewa kutoa uthibitisho huo.

Kama nilivyo ainisha katika sura iliyotangulia kwamba, Ripoti hii ni muhtasari wa yale yaliyo tolewa taarifa katika ripoti ya ukaguzi iliyopelekwa kwa kila Halmashauri. Taarifa hizi za kila Halmashauri zina mapendekezo juu ya kila suala ambalo linahitaji maboresho. Maafisa Masuuli wa Serikali za Mitaa wanatakiwa kuandaa majibu kutokana na matokeo ya ripoti ya ukaguzi na mapendekezo yaliyotolewa na kuwasilisha kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali kama ilivyoelekezwa kwenye kifungu cha 40 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma Namba 11 ya 2008 na Kanuni za 86 na 94 za Kanuni za Ukaguzi wa Umma, 2009.

Baada ya kuwasilisha yaliyojiri kutokana na matokeo ya ukaguzi kwa mwaka 2010/2011 kwenye Mamlaka ya Serikali za Mitaa katika sura zilizotangulia, sasa napenda kutoa hitimisho na mapendekezo yafuatayo, na ambayo kama yatatekelezwa yataimarisha usimamizi wa fedha ndani ya Mamlaka za Serikali za Mitaa nchini.

### 8.1 Hati za Ukaguzi za Mamlaka za Serikali za Mitaa

Kwa mwaka wa fedha 2010/2011, idadi ya hati zinazoridhisha zimeongezeka kwa 5% kutoka mwaka 2009/10 kwenda 2010/11, hati zenye mashaka zimepungua kwa 6% kutoka mwaka 2009/10 hadi 2010/11. Pia, hati zisizoridhisha zimeongezeka kwa 1% toka mwaka 2009/10 kwenda 2010/11.

### 8.2 Ufuatiliaji wa Mapendekezo ya Ukaguzi kwa Miaka ya Nyuma

Kulikuwa na masuala muhimu yaliyotolewa taarifa katika ripoti yangu ya ukaguzi ya mwaka uliopita pamoja na ripoti ya LAAC ambayo aidha yalikuwa yametekelezwa sehemu tu au hayakutekelezwa kabisa kama yalivyoonyeshwa kwenye taarifa hii katika sura ya tatu (3) ya taarifa hii.

Mamlaka za Serikali za Mitaa ziongeze juhudi zaidi ili kuhakikisha kwamba mapendekezo ya ukaguzi kwa miaka ya nyuma yanatekelezwa kwa wakati ili kuleta ufanisi katika utendaji wa Serikali za Mitaa na kwa lengo la kuongeza udhibiti na uwajibikaji kwa mali za umma.

## 8.3 Usimamizi wa Mapato

Kuna udhaifu katika udhibiti wa ndani na taratibu za kiuhasibu katika kuhakikisha ukusanyaji sahihi wa mapato na uingizaji wa hesabu sahihi katika vitabu vya Halmashauri kuhusiana na makusanyo ya Halmashauri yatokanayo na vyanzo vya ndani.

Nimebainisha kwamba karibu Halmashauri zote chini ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa hazifanya juhudi za kutosha katika kukusanya mapato yaliyo chini ya mamlaka zao na kwa upande mwingine hakuna ubunifu katika kugundua fursa nyingine za makusanyo ambazo zinaweza kuongeza uwezo wa Halmashauri kimapato na hivyo kuondoa ukwasi na kupunguza kiwango cha kuwa tegemezi. Kama ilivyoripotiwa katika ripoti za ukaguzi za miaka ya nyuma, Serikali za Mitaa bado zinategemea zaidi ruzuku kutoka Serikali Kuu. Matumizi ya kawaida yanategemea ruzuku hiyo kwa zaidi ya 90%, ambapo katika hali ya kawaida kwa kiasi kikubwa ilitakiwa kulipwa kwa kutumia vyanzo vya mapato vya ndani.

Serikali za Mitaa zinapaswa kuhakikisha kuwa mapato yanakadiriwa vizuri, yanakusanywa kwa wakati na kwa usahihi na kutunza kumbukumbu katika vitabu vya hesabu, mikataba ya kukusanya mapato inasimamiwa vizuri. Halmashauri kuongeza wigo wa ukusanyaji wa mapato na kuboresha usimamizi wa mapato ili kuepuka mwanya kwa mapato kuvujwa na matumizi mabaya ya fedha za umma. Pia, hatua stahiki zichukuliwe kwa wale ambao ni sehemu ya usimamizi wa mapato ya Halmashauri watakao patikana kuhusika na uvujaji wa mapato.

## 8.4 Usimamizi wa Matumizi

- Eneo hili limetawaliwa na sifa ya kukosekana kwa hati za malipo, hati za matumizi zenye viambatanisho pungufu. Hili ni tatizo la mara kwa mara katika idadi kubwa ya Halmashauri zetu na limekuwepo kwa kipindi cha muda mrefu. Napenda kuwakumbusha Maafisa Masuuli kuhusu wajibu wao wa usimamizi wa Halmashauri katika kuhakikisha kuwa wanawajibika juu ya utunzaji wa nyaraka za Halmashauri ikiwa ni pamoja na hati za malipo na kuhakikisha zinapatikana wakati zinapohitajika kwa ajili ya ukaguzi. Hii inahusisha kuimarisha zaidi udhibiti wa ndani katika utunzwaji mzuri wa nyaraka.

- Maafisa Masuuli wahakikishe kuwa sheria husika zinafutwa kwa kuhakikisha kuwepo kwa mifumo ya usimamizi wa matumizi ya rasilimali, kuhakikisha zinatumika katika namna bora, ufanisi, uwazi na kuweka kumbukumbu za kutosha pia kutoa taarifa zinapohitajika.

## 8.5 Kuboresha Usimamizi Wa Rasilimali Watu na Udhibiti wa Mishahara

- Inapendekezwa kwamba, Menejimenti za Halmashauri zinapaswa kuhakikisha kuwa kunakuwepo na mfumo wa tathmini ya upimaji wa utendaji (OPRAS) ili kurahisisha ufuatiliaji wa maendeleo ya mfanyakazi

na kutathmini, kugundua na kuweka kumbukumbu za uwezo na mapungufu katika utendaji wa wafanyakazi wake ili kuwezesha kuchukuliwa kwa hatua zaidi kwa ajili ya kuboresha ikiwa ni pamoja na mafunzo, kupandishwa vyeo, uhamisho, na kuondolewa kwenye utumishi kwa wasiofaa.

- Serikali za Mitaa kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI na Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma wanapaswa kuhakikisha kuwepo kwa mfumo endelevu wa ufuatiliaji wa viwango vya wafanyakazi na kuchukua hatua muafaka kwa wakati kwa kujaza nafasi wazi ili kuboresha utoaji wa huduma katika sekta ya umma. Aidha, Imeonekana kuwepo kwa mabadiliko ya mara kwa mara na yanayotokea baada ya muda mfupi yanayowahusisha Wakurugenzi wa Halmashauri na Wakuu wa Idara, pia kuwepo watumishi wanaokaimu nafasi ya wakuu wa Idara kwa muda mrefu hasa Idara ya Fedha na Idara ya Ukaguzi wa Ndani. Haya yote yamechangia kupunguza uwajibikaji na hivyo kuathiri utendaji.

- Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI inatakiwa kuhakikisha kuwa utaratibu wa uhamisho wa Wakurugenzi na Wakuu wa Idara usiwe ni mara kwa mara sana kiasi cha kuharibu mipango endelevu ya Halmashauri. Nafasi yoyote iliyo wazi ni ijazwe kwa haraka iwezekanavyo kwa kuthibitisha wale ambao wanakaimu nafasi hizo kama wana sifa au kwa njia ya kuwapandisha vyeo maafisa wengine wenye uwezo na sifa. Aidha, Maafisa Masuuli kila mwaka waandae orodha ya wafanyakazi ambao wamefanya kazi katika Halmashauri zao kwa kipindi cha muda mrefu na kuweka gharama zao katika bajeti kwa ajili ya kuhamishwa na kuwasilisha Ofisi ya Waziri Mkuu-TAMISEMI kwa ajili ya ufuatiliaji. Hii itasaidia kuondokana na tabia ya "kufanya kazi kwa mazoea".

- Maafisa Masuuli kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma wanapaswa kusafisha na kuondoa rekodi batili ya wanaolipwa mishahara wakati hawako katika utumishi wa umma.

- Changamoto ya kukopa kuliko viwango vinavyoruhusiwa kwa wafanyakazi wa Halmashauri bado ni sugu. Kukopa kwa kupindukia si tu uvunjaji wa sheria halali lakini pia kunaondoa motisha kwa wafanyakazi kufanya kazi kwa ufanisi. Halmashauri lazima zipewe maelekezo ya kuhakikisha kwamba maombi yote mikopo yanapitishwa na Maafisa Masuuli na kwamba kila mwezi makato yasizidi 2/3 ya mshahara wa mfanyakazi kwa mwezi. Menejimenti zisaidie kuwa na utaratibu wa kuhakikisha kwamba ufahamu unakuwepo kati ya wafanyakazi juu ya kukopa kupita kiasi.

- Mfanyakazi yeyote ambaye kwa njia moja au nyingine amechangia matumizi mabaya lazima aadhibiwe ipasavyo na si kumuhamishia kituo kingine cha kufanya kazi, hali ambayo ni ya kawaida katika Serikali za

Mitaa na imesababisha matatizo katika utendaji wa Serikali za Mitaa zilizokaguliwa. Hatua zitakazochukuliwa zinapaswa kuwa sawa na athari zilizosababishwa na mfanyakazi huyo na kwa mujibu wa sheria na kanuni za utumishi zilizopo.

## 8.6 Uzingatiwaji wa Sheria ya Manunuzi ya Umma

Kulingana na Ripoti ya Ukaguzi uliofanywa na PPRA kwa manunuzi ya mwaka wa fedha 2010/2011 kiasi cha 41% ya matumizi yote ya serikali kama ikilinganishwa na 52% ya mwaka uliopita. Hii inaonyessha bado sehemu kubwa ya rasilimali za Serikali za Mitaa zinatumika kwa njia ya ununuzi wa bidhaa, kazi za ujenzi na ununuzi wa huduma ya ushauri ili kutoa huduma kwa umma ndani ya serikali za Mitaa. Hivyo basi, kila Halmashauri inapaswa kuangalia taratibu zilivyoelezwa katika Sheria ya Ununuzi wa Umma ya mwaka 2004 na kanuni zake za mwaka 2005 na Kanuni za Bodi za Zabuni za Mamlaka za Serikali za Mitaa za mwaka 2007, ili kuepuka matumizi mabaya ya fedha za umma, na mgongano wa maslahi, vitendo vya rushwa na upotevu katika manunuzi.

Ili Serikali za Mitaa ziweze kupata thamani ya fedha katika suala la bei, ubora wa huduma/vifaa na kwa kuzingatia viwango na vigezo vilivyowekwa Maafisa Masuuli wanatakiwa kuzingatia mahitajio ya sheria.

Katika kuhakikisha uzingatiaji wa sheria ya manunuzi na kanuni zake nina mapendekezo yafuatayo:

- Mamlaka ya Serikali za Mitaa kwa kushirikiana na PPRA na OWM - TAMISEMI wanapaswa kuendelea kufanya mafunzo ya mara kwa mara kwa wafanyakazi katika vitengo vya manunuzi (PMU), wajumbe wa Bodi ya Zabuni ya Halmashauri, Wakuu wa Idara, Maafisa wa Masuuli na madiwani ili kuongeza maarifa yao kuhusu sheria ya manunuzi na majukumu waliyonayo katika kusimamia manunuzi ya umma .
- Juhudi za ziada zinahitajika kwa taasisi za serikali husika ili kuhakikisha kwamba Taasisi za Umma zinatumia mfumo wa manunuzi wa vifaa vinavyotumika mara kwa mara (CUIS) ambao ulianza katika mwaka wa fedha uliopita. Inategemewa kuwa matumizi sahihi ya mfumo huu yatapunguza gharama za manunuzi na hivyo kuongeza tija zaidi katika manunuzi yanayofanywa na Serikali.
- Halmashauri zinatakiwa kutumia nyaraka za zabuni na vigezo kwa ajili ya uchambuzi wa zabuni kama zilivyotolewa na Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA).

- Mwenyekiti wa Halmashauri asiwe mtiaji saini kwenye mikataba, ingawa Agizo Na. 280 la Memoranda ya Fedha ya Mamlaka za Serikali za Mitaa ya mwaka 1997 linasema kuwa mikataba yote itawekwa saini na Mwenyekiti wa Halmashauri na Mkurugenzi. Memoranda ya Fedha ya Mamlaka za Serikali za Mitaa ya mwaka 1997 inapingana na kifungu cha 33 (h) cha

Sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2004 ambapo majukumu ya kusaini mikataba ya manunuzi imekabidhiwa kwa Afisa Masuuuli ambaye ameelezewa katika kifugu cha 33 cha Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa Namba 9 ya mwaka 1982 (iliyorekebishwa mwaka 2000) kuwa ni Mkurugenzi wa Halmashauri.

## 8.7 Kuboresha Uhasibu na mifumo ya Udhibiti wa Ndani

Udhaifu katika uhasibu na mifumo ya udhibiti wa ndani ni kati ya mambo yaliyoonekana wakati wa ukaguzi ambapo inaweza kuathiri uwezo wa kurekodi, na utoaji wa taarifa za fedha. Kama juhudi za makusudi huzitachukuliwa inaweza kusababisha kukosekana kwa taarifa muhimu za fedha zinapohitajika. Baadhi ya masuala ya kuzingatia katika eneo hili ni pamoja na yafuatayo:

- **Kuimarisha Utayarishaji wa Taarifa za Fedha**
  Taarifa za fedha za Halmashauri ni sehemu muhimu ya uwajibikaji kwa ajili ya utoaji taarifa za rasilimali za Halmashauri. Malengo ya kutoa taarifa ni pamoja na kusaidia katika kuongoza na kutoa maamuzi na kuwezesha watumiaji wengine kama vile Bunge, vyombo vya fedha, wawekezaji, wafanyakazi, walipa kodi na Jumuiya za Kiraia kupata taarifa muhimu za Halmashauri.

  Idadi ya makosa katika taarifa za fedha na rasimu ya taarifa za fedha zilizowasilishwa kwa ajili ya ukaguzi ilikuwa haikubaliki. Idadi ya marekebisho katika hesabu hizo imeongezeka kwa kiasi kikubwa, marekebisho yaliyohitajika kwa kiasi kikubwa yameongeza wingi wa kazi zisizo za lazima kwa upande wa menejimenti za halmashauri na pia timu za ukaguzi kuhusiana na hesabu za mwaka wa fedha 2010/2011.

  Kwa hiyo, kuna haja ya kuboresha michakato yote inayohusiana na utayarishaji wa taarifa za fedha katika Mamlaka ya serikali za mitaa. Hii ni pamoja kuwa na ratiba ya maandalizi ya hesabu za mwaka na kuanzisha michakato ndani ya halmashauri itakayo angalia ubora wa hesabu zilizotengenezwa na kabla ya kuwasilishwa kwa ajili ya ukaguzi. Aidha, Ofisi ya Waziri Mkuu-TAMISEMI inapaswa kutoa mafunzo mara kwa mara ili kujenga uwezo wa wafanyakazi wa kushiriki katika maandalizi ya Taarifa za Fedha na kwamba programu mpya (toleo la 9.05) iliyo katika mfumo funganifu wa usimamizi wa fedha (IFMS) ifundishwe kwa wahasibu na kabla ya kuanza kutumika kwa ukamilifu.

**Uhuru wa Vitengo vya Ukaguzi wa Ndani**

Ukaguzi wa ndani ni chanzo muhimu cha ushauri wa kujitegemea na lengo ni kushauri juu ya mambo yanayoweza kuathiri utekelezaji wa kazi za Halmashauri.

Ukaguzi wa ndani una jukumu la kutathmini uimara wa mfumo wa usimamizi wa fedha na ambao ni msingi wa utayarishaji wa taarifa sahihi za fedha. Kazi za ukaguzi wa ndani zinakuwa zimeimarika kama kitengo cha ukaguzi wa ndani hakitajihusisha na utekelezaji wa kazi za halmashauri ambazo kitengo hicho kinazikagua. Hii itasaidia kukifanya kitengo cha ukaguzi wa ndani kufanya kazi zake kwa malengo bila upendeleo na kutokuwa na mgongano wa kimaslahi. Uhuru wa wakaguzi wa ndani utaimarika kama Wakaguzi hawa watawajibika kwa Mkurugenzi wa Halmashauri juu ya masuala ya Utawala na kwa kamati ya ukaguzi juu ya masuala ya kiukaguzi.

Hivyo, ninapendekeza kwamba, menejimenti za Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa kushirikiana na OWM - TAMISEMI na Idara ya Mkaguzi Mkuu wa Ndani chini ya Wizara ya Fedha waimarishe utendaji wa vitengo vya ukaguzi wa ndani kwa kuongezeza rasilimali fedha na watu katika vitengo vya Ukaguzi wa Ndani. Aidha, wakaguzi wa ndani wapatiwe vifaa, maarifa na stadi za kuwawezesha kupanua wigo wa ukaguzi na kuboresha utendaji wao. Pia, mfumo wa uwajibikaji upitiwe upya ili Wakaguzi wa ndani waweze kuwajibika kwa Mkurugenzi wa Halmashauri juu ya masuala ya Utawala na kwa kamati ya ukaguzi juu ya masuala ya kiukaguzi.

- **Mfumo wa Udhibiti wa Vihatarishi**

  Serikali za Mitaa zinahitajika kufuatilia mara kwa mara vihatarishi vinavyokabili mfumo wa usimamizi wa Serikali za Mitaa na utaratibu wa kutoa huduma kwa jamii yake. Halmashauri zikishirikiana na Kamati za ukaguzi zinatakiwa kuwa na ufahamu kwamba wakaguzi wa nje wanakagua juu ya umadhubuti wa udhibiti wa vihatarishi katika halmashauri lakini hii haimanishi kwamba ukaguzi huu ni toshelevu na hivyo kuondoa jukumu la menejementi za halmashauri kufanya mapitio yake katika eneo linalohusiana na mfumo wa udhibiti wa vihatarishi.

  Halmashauri zinapaswa kuhakikisha kuwa zinakuwa na mipango ya udhibiti wa vihatarishi na taarifa kuhusiana na utekelezaji wa mipango hiyo zinaandaliwa mara kwa mara. Kutokana na kukosekana kwa mipango madhubuti, Halmashauri zinakuwa haziko katika nafasi nzuri ya kudhibiti athari ya vihatarishi vinapotokea na hivyo kuathiri utoaji huduma. Kamati za Ukaguzi ni muhimu kwani zina jukumu la kufuatilia na kutathmini shughuli za Halmashauri kuhusiana na udhibiti wa vihatarishi. Jukumu hili la kamati za Ukaguzi linaweza kutekelezwa vizuri kwa kuwa na Ukaguzi wa ndani ulio madhubuti.

- **Kamati za Ukaguzi**

  Katika utekelezaji wa IPSASs kuna mabadiliko muhimu katika utoaji wa taarifa za fedha. Kamati za Ukaguzi zipewe fursa ya kutosha katika kupitia taarifa za fedha zisizokaguliwa kabla ya kuwasilishwa kwa wakaguzi wa nje. Aidha, mafunzo yanapaswa kutolewa kwa wanakamati ili wanakamati hao wawe na nafasi nzuri ya kutoa changamoto kwa uongozi wa Halmashauri

ulioandaa taarifa za fedha. Kuna haja ya kuboresha wigo na ufanisi wa Kamati za Ukaguzi na kuongeza uwazi zaidi katika majukumu waliopewa.

Kwa ujumla, masuala haya ya udhibiti wa vihatarishi yanahitaji usimamizi wa makini kwa sababu yanaashiria hatari kubwa ambazo zinaweza kuzuia Serikali za Mitaa kufikia malengo yake.

Halmashauri kwa kushirikiana na Idara ya Mkaguzi Mkuu wa Ndani na Ofisi ya Waziri Mkuu-TAMISEMI ni muhimu kuweka mpango thabiti wa kushughulikia maswala ya udhibiti wa ndani na mfumo wa utawala katika Halmashauri

## 8.8 Taarifa za Utekelezaji wa Miradi Zilizoandaliwa Kulingana na Mfumo Unaohitajika na Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC)

Taarifa za utekelezaji wa miradi ambazo zinaandaliwa kulingana na muundo unaohitajika na LAAC zinatakiwa ziwasilishwe Ofisi ya Ukaguzi kabla ya tarehe 30 Septemba kila mwaka zikiwa pamoja na taarifa ya fedha ya mwaka. Hii itawawezesha wakaguzi kufanya tathmini kuhusu taarifa za fedha zilizowasilishwa na taarifa nyingine kwa mwaka husika. Pia kutoa fursa kwa wakaguzi kukagua uwepo na thamani ya fedha kwa miradi mbalimbali iliyotolewa taarifa ya kutekelezwa.

## 8.9 Matumizi ya Fedha za Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo (CDCF)

CDCF unakutoa fedha kwa ajili ya jamii ili kutumika katika maeneo ya kipaumbele kama maji, elimu, miundombinu, afya au kilimo. CDCF unaweza pia kutoa fursa kwa wananchi kuwa na nguvu zaidi katika kuamua vipaumbele vyao na kugawa fedha na rasilimali kufikia vipaumbele hivyo.

Halmashauri zinapaswa kuwa makini ili kuhakikisha kwamba mifumo yote ya uwajibikaji kwa Fedha za Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo inatekelezwa kwa mujibu wa Sheria Namba 16 ya Fedha za Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo ya 2009 na kusimamia rasilimali za umma. Kutokana na kutokuwepo kwa uwasilishaji wa taarifa ya kiasi kilichopokelewa na kutumiwa na Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo (CDCF), Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI inapaswa kutekeleza masharti ya Sheria ya CDCF kwa kuhakikisha kuwa hakuna utoaji wa fedha nyingine kwa Halmashauri kwa mwaka unaofuata hadi taarifa ya fedha zinazohitajika kwa mujibu wa sheria zitakapowasilishwa.

## 8.10 Uimarishaji wa Usimamizi wa Mradi

Usimamizi wa miradi unahusisha uwepo wa miundombinu, michakato na vifaa ambavyo kwa pamoja hujulisha muda wa kufanya mradi, gharama za mradi na ubora na kisha kuhakikisha malengo hayo yanafikiwa.

Matokeo ya usimamizi wa miradi yanaonyesha kwamba usimamizi na utekelezaji wa miradi haukuwa mzuri kwani baadhi ya miradi ilitekelezwa katika viwango visivyostahili, pia kulikuwa na ucheleweshaji wa kukamilisha

miradi ndani ya muda uliopangwa na vile vile baadhi ya miradi iliyokamilika haitumiki.

Kama kuna usimamizi duni wa miradi, gharama za ziada zinaweza kuongezeka katika utekelezaji wa miradi hiyo. Hivyo:

- Uongozi wa Halmashauri unatakiwa kuimarisha Usimamizi na Tathmini (M & E), utaratibu ambao utahakikisha kwamba ufuatiliaji unaimarika na changamoto zilizobainika zinatatuliwa kwa haraka ili kuwepo na utekelezaji mzuri wa miradi iliyopangwa na matumizi mazuri ya miradi hiyo itakapokamilika kwa wakati muafaka.

- Taarifa juu ya fedha zilizopelekwa Serikali za Mitaa lazima itolewe Halmashauri na taasisi husika (mfano Hazina). Taarifa hii ipelekwe Halmashauri mara tu fedha hizo zinapotumwa. Taarifa hii lazima iwe na ufafanuzi wa wazi juu ya lengo la fedha zilizotumwa. Utoaji wa fedha zilizoidhinishwa kwa wakati, ni muhimu ili kuhakikisha kwamba shughuli zilizopangwa zinatekelezwa kwa wakati muafaka.

## 8.11 Utendaji wa Mifuko Mbalimbali ya Fedha Usioridhisha

Kwa miaka kadhaa sasa uwajibikaji katika Mfuko wa Wanawake na Vijana na pia Mfuko wa Afya wa Jamii (CHF) haujawa wa uwazi kama inavyotakiwa na Agizo Na.84 (iii) la Memoranda ya Fedha za Mamlaka za Serikali za Mitaa ya mwaka 1997 na maelekezo kutoka kwenye Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC). Kutokuwepo na uwazi kunazuia mkaguzi kutoa uhakika wa kama fedha hizi zinatumika kwa kazi na malengo ya kuanzishwa kwa mifuko hiyo.

Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI inashauriwa kutoa muongozo kwa Halmashauri jinsi ya kuandaa taarifa na ripoti za fedha ili kuwa na utaratibu wa uwajibikaji unaolenga kutathmini kufikiwa malengo yalionzisha mifuko hii. Tangu kuanzishwa kwa mifuko hii Halmashauri hazijaweza kutayarisha taarifa ya hali ya kifedha, taarifa ya utendaji ya fedha na mtiririko wa fedha kwa ajili ya ukaguzi. Hatua ya kuandaa hesabu na ripoti za mifuko hii itakuwa ni ya msingi kwa ajili ya ukaguzi ili kutoa uhakika wa uendeshaji wa mifuko hii.

## 8.12 Uboreshaji Katika Udhibiti wa Usimamizi wa Fedha

Ili Mamlaka za Serikali za Mitaa ziweze kuleta maendeleo yaliyokusudiwa katika usimamizi, uwajibikaji na udhibiti wa fedha katika sekta ya umma, Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI inashauriwa kuhakikisha kuwa Maafisa Masuuli wanawajibika katika kuhakikisha kuwa masharti ya sheria yanazingatiwa. Kuwajibika huku ni kwa maana ya kudhibiti ubora, usimamizi na udhibiti wa ukusanyaji na matumizi ya rasilimali za umma.

Katika suala hili, napendekeza kwamba Waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa asimamie kikamilifu utekelezaji wa Kanuni za Fedha za Serikali za

Mitaa za adhabu na tozo (surcharge and Penalties) za mwaka 2010 juu ya Maafisa Masuuli na Maafisa wengine wote yasiozingatia sheria.

## 8.13 Hitimisho Kuhusu Kaguzi Maalum

### 8.13.1 Ushirikishwaji wa Watumishi wa benki katika Udanganyifu

Katika kaguzi maalum tumebaini kuwa baadhi ya wafanyakazi wa Benki wasio waaminifu walishirikiana na watumishi wa Halmashauri katika kufanya ubadhilifu wa fedha za Halmashauri. Katika hali isiyo ya kawaida, wafanyakazi wa Benki waliruhusu malipo yasiyo halali kufanyika kinyume na taratibu zilizopo na pia kinyume na miongozo na taratibu za taasisi za fedha. Hali hii inaonyesha kuwa mbali ya kuwa benki ni sehemu ya udhibiti wa matumizi mabaya ya fedha, benki imekuwa njia ya kufanikisha udanganyifu wa wafanyakazi wa Halmashauri wasio waaminifu. Ubadhirifu uliofanyika usingeweza kutekelezeka kama kusingekuwepo na kula njama kati ya wafanyakazi wa Benki na watumishi wa Halmashauri.

### 8.13.2 Usimamizi Miradi ya Maendeleo

Halmashauri zinapaswa kuongeza juhudi katika usimamizi na utekelezaji wa miradi kwa kutumia rasilimali fedha zinazopata kwa mujibu wa mipango iliyopitishwa. Pia, Halmashauri zinapaswa kupeleka kwa wakati fedha zinazotolewa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi katika ngazi za chini kama vile kwenye kata na vijiji ili kuepuka kuwa na salio kubwa la fedha za miradi ifikapo mwisho wa mwaka jambo ambalo linakwamisha maendeleo yaliyokusudiwa.

Kuna uhamasishaji hafifu na mwamko mdogo wa wananchi katika kujitolea na kuchangia katika miradi yao ya maendeleo. Ofisi ya Waziri Mkuu-TAMISEMI kama Wizara mama wanapaswa kutoa maelekezo juu ya uhamasishaji wa jamii kwa kueleza wazi majukumu ya Halmashauri katika ngazi zote na Madiwani juu ya uhamasishaji. Hii itasaidia miradi ya maendeleo kukamilika kwa wakati pamoja na kupunguza uwezekano wa kuongezeka kwa gharama kwa kutokana na kuchelewa kwa kukamilisha miradi ya maendeleo.

## 8.14 Utekelezaji wa "Kilimo Kwanza"

Ili kufikia matarajio ya "Kilimo Kwanza" napendekeza yafuatayo:

- Kamati zinazohusika zinatakiwa kuhakikisha ufuatiliaji wa karibu wa vocha za kilimo na kwamba hatua za kisheria zinachukuliwa dhidi ya wale waliosababisha upotevu na hasara kwa pembejeo hizo za kilimo.
- Uongozi wa Halmashauri unapaswa kuhakikisha kuwa mawakala waliopewa wajibu wa usambazaji wa pembejeo za kilimo wana mikataba halali na wanazingatia kwa ukamilifu vipengele vilivyo katika mikataba husika.

• Halmashauri zinapaswa kushirikiana na Wizara ya Kilimo kuhakikisha kuwa pembejeo za kilimo zinatolewa kutokana na mahitaji na kwa wakati ili kuchochea maendeleo ya kilimo ndani ya Halmashauri.

## 8.15 Haja ya kuwa na mwongozo sahihi juu ya uendeshaji wa akaunti sita (6) za Benki katika Halmashauri

Serikali imefanya uamuzi sahihi wa kupunguza idadi ya akaunti za benki za Serikali za Mitaa kutoka wastani wa akaunti 33 hadi 6 kwa kila Halmashauri. Inatarajiwa kwamba, hii itapunguza gharama za uendeshaji na kuimarisha usimamizi wa fedha ndani ya Serikali za Mitaa kwa:

a. Kuwa na akaunti chache za benki zinazoweza kusimamiwa vizuri ikiwa ni pamoja na kufanya usuluhisho wa benki angalau mara moja kila mwezi.
b. Kuondoa akaunti za benki ambazo zilikuwa hazifanyi kazi na hivyo kupunguza changamoto ya kuwa na fedha benki ambazo zilikuwa hazijafanyiwa kazi iliyokusudiwa.
c. Kuondoa matumizi mabaya ya fedha za halmashauri ambazo zilikuwa zinakuwepo benki kwa muda mrefu bila kutekeleza kazi zilizokusudiwa.

Ili kuleta matokeo mazuri ya mabadiliko hayo, nina mapendekezo yafuatayo ambayo yanazingatia matarajio ya wadau wa Serikali za Mitaa:

- Kuna haja ya kuimarisha matumizi ya fedha kwa kuwa na daftari la kudhibiti matumizi ya fedha kwa kila kasma au mfumo wowote mwingine ambao utadhibiti na kuimarisha matumizi ya fedha ambapo miradi tofauti itatumia akaunti moja ya benki.
- OWM – TAMISEMI itengeneze mfumo thabiti wa namba wa kutambulisha kila kasma na ambao utaboresha otoaji wa kila taarifa inayohitajika kama taarifa za kila sku, kila wiki, kila mwezi, kila baada ya miezi mitatu na taarifa mwaka.
- Jambo lingine la kuzingatia ni mabadiliko katika mfumo funganifu wa usimamizi wa fedha (IFMS). Mfumo huu unabadilika kutoka katika toleo la 7.35 na kwenda katika toleo la 9.05, hivyo ni muhimu katika kutekeleza matumizi ya akaunti 6 za benki halmashauri zikazingatia uwepo wa mfumo mpya (toleo la 9.05) ambao utaendeshwa na kudhibitiwa na OWM – TAMISEMI. Hii itasaidia kufanya kwa urahisi usuluhisho wa benki kwa fedha za kasma mbalimbali ambazo ziko katika akaunti moja ya benki.

## VIAMBATISHO

## Kiambatisho (i)

## Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha

| Na. | Halmashauri | Jumla ya matumizi | Jumla ya Makosa | | % ya Upotoshwaji | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Malipo pungufu | Malipo zaidi | % ya Malipo funguf u | % ya Malipo zaidi |
| 1 | H/M Arusha | 27,446,538,646 | 690,085,425 | - | 2.51 | 0.00 |
| 2 | H/W Karatu | 15,617,993,613 | 325,637,434 | 13,926,700 | 2.09 | 0.09 |
| 3 | H/W Meru | 21,643,889,164 | 2,619,313,310 | 12,991,740 | 12.10 | 0.06 |
| 4 | H/W Mkuranga | 16,612,853,723 | 453,790,563 | - | 2.73 | 0.00 |
| 5 | H/W Rufiji/Utete | 18,141,703,472 | 35,591,187 | 6,187,500 | 0.20 | 0.03 |
| 6 | H/M Temeke | 49,298,746,483 | 67,978,937 | 3,861,000 | 0.14 | 0.01 |
| 7 | H/W Bahi | 12,056,173,205 | 353,442,837 | 2,306,300,327 | 2.93 | 19.13 |
| 8 | H/W Dodoma | 26,689,607,120 | 793,682,851 | 998,281,645 | 2.97 | 3.74 |
| 9 | H/W Kondoa | 26,965,085,496 | 1,756,611,483 | 11,444,021,076 | 6.51 | 42.44 |
| 10 | H/W Kongwa | 16,608,913,306 | 447,749,553 | 253,868,733 | 2.70 | 1.53 |
| 11 | H/W Mpwapwa | 17,563,630,000 | 531,454,497 | 9,966,520,409 | 3.03 | 56.75 |
| 12 | H/W Muleba | 23,234,751,055 | 381,445,566 | 1,902,716,573 | 1.64 | 8.19 |
| 13 | H/W Missenyi | 12,222,708,630 | - | 104,067,561 | 0.00 | 0.85 |
| 14 | H/W Kasulu | 31,758,657,783 | 441,516,278 | 294,239,764 | 1.39 | 0.93 |
| 15 | H/W Kibondo | 22,709,622,145 | 1,084,612,000 | 1,039,042,779 | 4.78 | 4.58 |
| 16 | H/W Kigoma | 28,407,321,746 | - | 1,005,450,844 | 0.00 | 3.54 |
| 17 | H/MKigoma/Ujiji | 13,632,157,456 | 688,554,480 | 420,212,000 | 5.05 | 3.08 |
| 18 | H/W Moshi | 36,586,596,389 | 2,703,979,166 | 1,782,414,553 | 7.39 | 4.87 |
| 19 | H/W Mwanga | 16,720,495,448 | 2,461,725,845 | 2,094,850,571 | 14.72 | 12.53 |
| 20 | H/W Rombo | 22,114,334,929 | 5,332,225,813 | 3,351,633,203 | 24.11 | 15.16 |
| 21 | H/W Kiteto | 9,382,992,479 | 5,793,000 | 73,872,800 | 0.06 | 0.79 |
| 22 | H/Mji Babati | 8,952,577,153 | 1,187,793,630 | 181,447,014 | 13.27 | 2.03 |
| 23 | H/W Babati | 15,588,324,000 | 5,078,643,000 | 270,095,812 | 32.58 | 1.73 |
| 24 | H/W Musoma | 22,457,424,523 | - | 1,727,334,858 | 0.00 | 7.69 |
| 25 | H/W Tarime | 18,922,487,024 | 218,089,842 | - | 1.15 | 0.00 |
| 26 | H/W Chunya | 15,708,175,542 | 8,816,920,987 | 120,000,000 | 56.13 | 0.76 |
| 27 | H/W Ileje | 9,744,546,854 | 653,515,119 | 14,053,148 | 6.71 | 0.14 |
| 28 | H/W Kyela | 14,785,066,103 | 9,059,361,838 | - | 61.27 | 0.00 |
| 29 | H/W Mbarali | 14,282,523,546 | 458,600,570 | - | 3.21 | 0.00 |
| 30 | H/W Rungwe | 30,163,014,004 | 196,385,053 | 1,332,000 | 0.65 | 0.00 |
| 31 | H/W Kilombero | 20,496,923,880 | 55,442,729,673 | 5,679,291,696 | 270.49 | 27.71 |
| 32 | H/W Kilosa | 34,417,131,546 | 8,892,058,858 | 19,434,128,719 | 25.84 | 56.47 |
| 33 | H/W Morogoro | 18,003,402,091 | 5,835,609,709 | 1,835,424,605 | 32.41 | 10.19 |
| 34 | H/MMorogoro | 23,750,506,374 | 9,082,615,653 | 2,005,194,841 | 38.24 | 8.44 |
| 35 | H/W Mvomero | 21,745,728,763 | 5,881,248,320 | 4,011,470,237 | 27.05 | 18.45 |
| 36 | Jiji la Mwanza | 46,982,085,879 | 4,627,419,269 | - | 9.85 | 0.00 |
| 37 | H/W Ukerewe | 11,237,985,118 | 1,191,188,161 | 1,380,411,123 | 10.60 | 12.28 |
| 38 | H/W Mpanda | 29,764,071,905 | 5,611,533,000 | 172,156,000 | 18.85 | 0.58 |
| 39 | H/W Nkasi | 19,527,687,505 | 1,509,314,479 | - | 7.73 | 0.00 |
| 40 | H/MSumbawanga | 15,109,312,448 | 5,008,376,562 | - | 33.15 | 0.00 |
| 41 | H/M Songea | 15,641,202,150 | 633,109,812 | 175,476,101 | 4.05 | 1.12 |
| 42 | H/W Songea | 15,617,921,145 | 13,206,937,207 | 12,988,826,391 | 84.56 | 83.17 |
| 43 | H/W Namtumbo | 10,924,986,686 | 1,057,392,298 | 3,687,751,493 | 9.68 | 33.76 |
| 44 | H/W Iramba | 23,998,741,000 | 3,838,466,380 | 188,133,749 | 15.99 | 0.78 |
| 45 | H/W Manyoni | 15,581,502,506 | 121,919,058 | 11,237,768,848 | 0.78 | 72.12 |
| 46 | H/W Singida | 21,414,179,000 | 2,659,394,000 | 233,610,536 | 12.42 | 1.09 |
| 47 | H/M Singida | 13,030,427,864 | 91,605,205 | 1,059,873,799 | 0.70 | 8.13 |
| 48 | H/W Handeni | 17,537,186,205 | 561,498,936 | - | 3.20 | 0.00 |
| 49 | H/W Korogwe | 14,199,389,727 | 1,561,932,870 | - | 11.00 | 0.00 |
| 50 | H/Mji Korogwe | 7,478,605,257 | 493,294,119 | 51,397,342 | 6.60 | 0.69 |
| 51 | H/W Lushoto | 30,101,790,317 | 1,806,107,419 | - | 6.00 | 0.00 |
| 52 | H/W Muheza | 17,309,581,098 | 368,690,286 | 1,934,583 | 2.13 | 0.01 |
| 53 | H/W Pangani | 7,945,127,496 | 250,081,299 | 4,141,027,576 | 3.15 | 52.12 |
| 54 | Jiji la Tanga | 24,655,852,635 | 5,670,846,106 | - | 23.00 | 0.00 |
| 55 | H/W Mkinga | 9,459,567,325 | 378,382,693 | - | 4.00 | 0.00 |
| 56 | H/W Igunga | 18,970,317,361 | 213,330,000 | 9,320,511,904 | 1.12 | 49.13 |
| 57 | H/W Nzega | 22,058,857,391 | 77,009,632 | 584,784,466 | 0.35 | 2.65 |
| 58 | H/W Sikonge | 9,851,317,268 | 2,303,116,701 | 81,411,604 | 23.38 | 0.83 |
| 59 | H/W Tabora | 16,419,148,832 | 1,783,929,861 | - | 10.86 | 0.00 |
| 60 | H/W Urambo | 21,933,029,693 | 61,150,422 | 1,308,130,307 | 0.28 | 5.96 |
| | **Jumla** | **1,191,182,477,501** | **187,064,788,252** | **118,967,438,529** | **15.70** | **9.99** |

# Kiambatisho (ii)

**Mwelekeo wa Hati za Ukaguzi zilizotolewa katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa kwa Miaka 2007/08, 2008/09, 2009/10 and 2010/11**

| Mkoa | Halmashauri | 2007/08 | 2008/09 | 2009/10 | 2010/11 |
|---|---|---|---|---|---|
| ARUSHA | | | | | |
| 1 | Arusha H/M | Hati yenye shaka | Hati yenye shaka | Hati yenye shaka | Hati Isiyoridhisha |
| 2 | Karatu H/W | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati yenye shaka |
| 3 | Monduli H/W | Hati yenye shaka | Hati yenye shaka | Hati yenye shaka | Hati yenye shaka |
| 4 | Ngorongoro H/W | Hati yenye shaka | Hati yenye shaka | Hati yenye shaka | Hati yenye shaka |
| 5 | Meru H/W | Hati yenye shaka | Hati yenye shaka | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 6 | Longido H/W | Hati yenye shaka | Hati yenye shaka | Hati yenye shaka | Hati yenye shaka |
| 7 | Arusha H/W | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati yenye shaka |
| COAST | | | | | |
| 8 | Bagamoyo H/W | Hati Inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati Inayoridhisha | Hati yenye shaka |
| 9 | Kibaha H/W | Hati yenye shaka | Hati yenye shaka | Hati yenye shaka | Hati Inayoridhisha |
| 10 | Kibaha H/MJI | Hati Inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati yenye shaka | Hati Inayoridhisha |
| 11 | Kisarawe H/W | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 12 | Mafia H/W | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati Inayoridhisha |
| 13 | Mkuranga H/W | Hati yenye shaka | Hati Inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati Inayoridhisha |
| 14 | Rufiji/Utete H/W | Hati yenye shaka | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati yenye shaka |
| DSM | | | | | |
| 15 | Dar es Salaam H/JIJI | Hati Inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati yenye shaka | Hati yenye shaka |
| 16 | Ilala H/M | Hati yenye shaka | Hati yenye shaka | Hati Inayoridhisha | Hati yenye shaka |
| 17 | Kinondoni H/M | Hati Inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati Inayoridhisha | Hati yenye shaka |
| 18 | Temeke H/M | Hati yenye shaka | Hati Inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati yenye shaka |
| DODOMA | | | | | |
| 19 | Bahi H/W | Hati yenye shaka | Hati yenye shaka | Hati Inayoridhisha | Hati yenye shaka |
| 20 | Chamwino H/W | Hati yenye shaka | Hati yenye shaka | Hati yenye shaka | Hati Inayoridhisha |
| 21 | Dodoma H/M | Hati yenye shaka | Hati Inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati yenye shaka |
| 22 | Kondoa H/W | Hati Inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati Inayoridhisha | Hati yenye shaka |
| 23 | Kongwa H/W | Hati Inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati Inayoridhisha | Hati yenye shaka |
| 24 | Mpwapwa H/W | Hati Inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati Inayoridhisha | Hati yenye shaka |
| IRINGA | | | | | |
| 25 | Iringa H/W | Hati yenye shaka | Hati yenye shaka | Hati Inayoridhisha | Hati yenye shaka |
| 26 | Iringa H/M | Hati yenye shaka | Hati Inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati Inayoridhisha |
| 27 | Ludewa H/W | Hati yenye shaka | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati yenye shaka |
| 28 | Makete H/W | Hati yenye shaka | Hati yenye shaka | Hati yenye shaka | Hati yenye shaka |
| 29 | Mufindi H/W | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 30 | Njombe H/W | Hati yenye | Hati yenye | Hati | Hati |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | shaka | shaka | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 31 | Njombe H/MJI | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati Inayoridhisha |
| 32 | Kilolo H/W | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati yenye shaka |
| KAGERA | | | | | |
| 33 | Biharamulo H/W | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 34 | Bukoba H/W | Hati yenye shaka | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 35 | Bukoba H/M | Hati yenye shaka | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 36 | Karagwe H/W | Hati Inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 37 | Muleba H/W | Hati yenye shaka | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 38 | Ngara H/W | Hati yenye shaka | Hati yenye shaka | Hati Inayoridhisha | Hati yenye shaka |
| 39 | Missenyi H/W | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 40 | Chato H/W | Hati Inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati yenye shaka | Hati yenye shaka |
| KIGOMA | | | | | |
| 41 | Kasulu H/W | Hati yenye shaka | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati yenye shaka |
| 42 | Kibondo H/W | Hati Inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati Inayoridhisha | Hati yenye shaka |
| 43 | Kigoma H/W | Hati Inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 44 | Kigoma/Ujiji H/M | Hati yenye shaka | Hati yenye shaka | Hati Inayoridhisha | Hati yenye shaka |
| KLM | | | | | |
| 45 | Hai H/W | Hati yenye shaka | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 46 | Moshi H/W | Hati yenye shaka | Hati yenye shaka | Hati yenye shaka | Hati yenye shaka |
| 47 | Moshi H/M | Hati Inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati yenye shaka | Hati Inayoridhisha |
| 48 | Siha H/W | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 49 | Mwanga H/W | Hati yenye shaka | Hati yenye shaka | Hati Isiyoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 50 | Rombo H/W | Hati Inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati Isiyoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 51 | Same H/W | Hati Inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| LINDI | | | | | |
| 52 | Kilwa H/W | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Isiyoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 53 | Lindi H/W | Hati yenye shaka | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 54 | Lindi H/MJI | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati Inayoridhisha |
| 55 | Liwale H/W | Hati yenye shaka | Hati Inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati yenye shaka |
| 56 | Nachingwea H/W | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 57 | Ruangwa H/W | Hati yenye shaka | Hati Inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati Inayoridhisha |
| MANYARA | | | | | |
| 58 | Babati H/W | Hati yenye shaka | Hati Inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati yenye shaka |
| 59 | Hanang' H/W | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati Inayoridhisha |
| 60 | Kiteto H/W | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati yenye shaka |
| 61 | Mbulu H/W | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati yenye shaka |
| 62 | Simanjiro H/W | Hati yenye shaka | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 63 | Babati H/MJI | Hati yenye shaka | Hati Inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati Inayoridhisha |
| MARA | | | | | |
| 64 | Musoma H/W | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati Inayoridhisha |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 65 | Bunda H/W | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati Inayoridhisha |
| 66 | Musoma H/M | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati yenye shaka |
| 67 | Serengeti H/W | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 68 | Tarime H/W | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati Inayoridhisha |
| 69 | Rorya H/W | Hati Inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati yenye shaka | Hati Inayoridhisha |
| MBEYA | | | | | |
| 70 | Chunya H/W | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati yenye shaka |
| 71 | Ileje H/W | Hati yenye shaka | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 72 | Kyela H/W | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 73 | Mbarali H/W | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati Inayoridhisha |
| 74 | Mbeya H/W | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati Inayoridhisha |
| 75 | Mbeya H/JIJI | Hati Inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati yenye shaka | Hati Inayoridhisha |
| 76 | Mbozi H/W | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati yenye shaka |
| 77 | Rungwe H/W | Hati yenye shaka | Hati yenye shaka | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| MOROGORO | | | | | |
| 78 | Kilombero H/W | Hati yenye shaka | Hati yenye shaka | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 79 | Kilosa H/W | Hati yenye shaka | Hati Isiyoridhisha | Hati yenye shaka | Hati yenye shaka |
| 80 | Morogoro H/W | Hati yenye shaka | Hati yenye shaka | Hati yenye shaka | Hati Isiyoridhisha |
| 81 | Morogoro H/M | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati yenye shaka |
| 82 | Ulanga H/W | Hati Inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 83 | Mvomero H/W | Hati yenye shaka | Hati yenye shaka | Hati yenye shaka | Hati yenye shaka |
| MTWARA | | | | | |
| 84 | Masasi H/MJI | - | - | Hati yenye shaka | Hati Inayoridhisha |
| 85 | Masasi H/W | Hati yenye shaka | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 86 | Mtwara H/W | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati Inayoridhisha |
| 87 | Mtwara H/M | Hati yenye shaka | Hati yenye shaka | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 88 | Newala H/W | Hati Inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 89 | Tandahimba H/W | Hati yenye shaka | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 90 | Nanyumbu H/W | Hati yenye shaka | Hati yenye shaka | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| MWANZA | | | | | |
| 91 | Geita H/W | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati yenye shaka |
| 92 | Kwimba H/W | Hati yenye shaka | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati yenye shaka |
| 93 | Magu H/W | Hati yenye shaka | Hati Inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati yenye shaka |
| 94 | Misungwi H/W | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati Isiyoridhisha |
| 95 | Mwanza H/JIJI | Hati yenye shaka | Hati yenye shaka | Hati yenye shaka | Hati yenye shaka |
| 96 | Sengerema H/W | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati yenye shaka |
| 97 | Ukerewe H/W | Hati yenye shaka | Hati yenye shaka | Hati yenye shaka | Hati Inayoridhisha |
| RUKWA | | | | | |
| 98 | Mpanda H/W | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati Inayoridhisha |
| 99 | Mpanda H/MJI | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati yenye shaka |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 100 | Nkasi H/W | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati yenye shaka |
| 101 | Sumbawanga H/W | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati Inayoridhisha |
| 102 | Sumbawanga H/M | Hati Inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati yenye shaka | Hati Inayoridhisha |
| RUVUMA | | | | | |
| 103 | Mbinga H/W | Hati Inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati yenye shaka | Hati Inayoridhisha |
| 104 | Songea H/M | Hati yenye shaka | Hati Inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati yenye shaka |
| 105 | Songea H/W | Hati Inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati Inayoridhisha | Hati Isiyoridhisha |
| 106 | Tunduru H/W | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati yenye shaka |
| 107 | Namtumbo H/W | Hati yenye shaka | Hati yenye shaka | Hati yenye shaka | Hati yenye shaka |
| SHINYANGA | | | | | |
| 108 | Bariadi H/W | Hati yenye shaka | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 109 | Bukombe H/W | Hati yenye shaka | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati yenye shaka |
| 110 | Kahama H/W | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati Inayoridhisha |
| 111 | Meatu H/W | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati Inayoridhisha |
| 112 | Shinyanga H/W | Hati yenye shaka | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 113 | Shinyanga H/M | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 114 | Kishapu H/W | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Isiyoridhisha | Hati yenye shaka |
| 115 | Maswa H/W | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| SINGIDA | | | | | |
| 116 | Iramba H/W | Hati yenye shaka | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 117 | Manyoni H/W | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati yenye shaka |
| 118 | Singida H/W | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati Inayoridhisha |
| 119 | Singida H/M | Hati yenye shaka | Hati Inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati yenye shaka |
| TANGA | | | | | |
| 120 | Handeni H/W | Hati Inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati Inayoridhisha | Hati yenye shaka |
| 121 | Korogwe H/W | Hati yenye shaka | Hati yenye shaka | Hati yenye shaka | Hati Inayoridhisha |
| 122 | Korogwe H/MJI | Hati yenye shaka | Hati yenye shaka | Hati yenye shaka | Hati yenye shaka |
| 123 | Lushoto H/W | Hati yenye shaka | Hati yenye shaka | Hati yenye shaka | Hati Inayoridhisha |
| 124 | Muheza H/W | Hati yenye shaka | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 125 | Pangani H/W | Hati Inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati yenye shaka | Hati yenye shaka |
| 126 | Tanga H/JIJI | Hati Inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati yenye shaka | Hati Inayoridhisha |
| 127 | Kilindi H/W | Hati yenye shaka | Hati Inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati Isiyoridhisha |
| 128 | Mkinga H/W | Hati Inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati yenye shaka | Hati Inayoridhisha |
| TABORA | | | | | |
| 129 | Igunga H/W | Hati yenye shaka | Hati yenye shaka | Hati yenye shaka | Hati Inayoridhisha |
| 130 | Nzega H/W | Hati yenye shaka | Hati Inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati Inayoridhisha |
| 131 | Sikonge H/W | Hati Inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati yenye shaka | Hati yenye shaka |
| 132 | Tabora H/W | Hati yenye shaka | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati yenye shaka |
| 133 | Urambo H/W | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati yenye shaka |

## Kiambatisho (iii)

**Orodha ya Halmashauri zilizoongeza ufanisi kwa kupata Hati inayoridhisha kutoka katika Hati Isiyoridhisha**

| S/N | Name Of The Council | 2009/2010 | 2010/2011 |
|---|---|---|---|
| 1 | Kibaha H/W | Hati yenye shaka | Hati Inayoridhisha |
| 2 | Kibaha H/MJI | Hati yenye shaka | Hati Inayoridhisha |
| 3 | Mafia H/W | Hati yenye shaka | Hati Inayoridhisha |
| 4 | Mkuranga H/W | Hati yenye shaka | Hati Inayoridhisha |
| 5 | Chamwino H/W | Hati yenye shaka | Hati Inayoridhisha |
| 6 | Iringa H/M | Hati yenye shaka | Hati Inayoridhisha |
| 7 | Njombe H/MJI | Hati yenye shaka | Hati Inayoridhisha |
| 8 | Moshi H/M | Hati yenye shaka | Hati Inayoridhisha |
| 9 | Mwanga H/W | Hati Isiyoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 10 | Rombo H/W | Hati Isiyoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 11 | Kilwa H/W | Hati Isiyoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 12 | Lindi H/MJI | Hati yenye shaka | Hati Inayoridhisha |
| 13 | Ruangwa H/W | Hati yenye shaka | Hati Inayoridhisha |
| 14 | Hanang' H/W | Hati yenye shaka | Hati Inayoridhisha |
| 15 | Babati H/MJI | Hati yenye shaka | Hati Inayoridhisha |
| 16 | Musoma H/W | Hati yenye shaka | Hati Inayoridhisha |
| 17 | Bunda H/W | Hati yenye shaka | Hati Inayoridhisha |
| 18 | Tarime H/W | Hati yenye shaka | Hati Inayoridhisha |
| 19 | Rorya H/W | Hati yenye shaka | Hati Inayoridhisha |
| 20 | Mbarali H/W | Hati yenye shaka | Hati Inayoridhisha |
| 21 | Mbeya H/JIJI | Hati yenye shaka | Hati Inayoridhisha |
